

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Thelathini na Nne - Tarehe 1 Juni, 2016**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Katibu!

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge wa Kambi ya Upinzani Walitoka Nje)*

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango, kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Bajeti, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**MHE. DAVID E. SILINDE - NAIBU MSEMaji MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:** Maswali.

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mbunge wa Muheza sasa aulize swali lake.

Na. 275

**Kuidhinisha Halmashauri ya Mji - Muheza**

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB** aliuliza:-

Mji mdogo wa Wilaya ya Muheza ulianzishwa mwaka 2007 na ulihusisha Kata tatu za Muheza Mjini, Mbaramo, Majengo na Masuguru; na tangu wakati huo, umekuwa ukihudumia wananchi wake na taratibu za mapendekezo ya kuidhinisha uanzishwaji wa Halmashauri ya Mji wa Muheza tangu tarehe 10/01/2016.

Je, ni kwa nini Serikali imechelewa kuiuadhiinisha Muheza kuwa Halmashauri ya Mji huku ikijua kuna ongezeko kubwa la watu na Kata zimeongezeka hadi kufikia sita?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mapendekezo ya kupandisha hadhi Mamlaka ya Mji Mdogo wa Muheza, kuwa Halmashauri ya Mji wa Muheza, yalifanyika na kupitishwa katika vikao vyote vya kisheria, vikiwemo Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya na Mkoa. Maombi haya tayari yamepokelewa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI baada ya kupitishwa na RCC. Hatua itakayofuata ni kwenda kufanya uhakiki wa vigezo vinavyozingatiwa katika kuanzisha Halmashauri za Miji nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Adadi Rajab, swali la nyongeza.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, maombi ya kuanzisha Mji huo sasa hivi ni miaka tisa, tangu mwaka 2007. Nataka Mheshimiwa Waziri anihakikishie; ni lini, wataalam wake wa kwenda kuhakiki watafika Muheza?

Swali la pili, Jimbo la Muheza linaweza kuwa ni kubwa kuliko Majimbo yote hapa mjengoni, lina kata 37, vijiji 135, vitongoji 530 unafikiria ni lini Jimbo hilo linaweza kugawiwa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumbukumbu halali tulizokuwa nazo, ni kwamba kikao cha RCC kilikaa Novemba 2013; na mchakato huu maana yake ulienda kuja katika Ofisi ya Rais, lakini kipindi hicho ikiwa Ofisi ya Waziri Mkuu. Ndiyo maana hapa juzi juzi Waziri wangu mwenye dhamana, Mheshimiwa George Simbachawene, aliwaambia wataalam wetu kuleta *analysis* ya kila Halmashauri na kila Mkoa. Nadhani wameomba na wanaangalia iko katika *status* gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo haya ya Jimbo lako Mheshimiwa Adadi, ni kwamba wataalamu wetu katika kipindi hiki cha hivi sasa, bajeti wanayoshughulika nayo ni kwamba maeneo ya kipaumbele cha kwanza, itakuwa kuja kwako Muheza lakini hali kadhalika kwenda katika Mji huu wa Mombo ambapo maeneo haya maombi yao yote yameletwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Adadi Rajab usiwe na mashaka, hata ndugu yangu hapa Mheshimiwa Profesa Maji Marefu mambo yenu yote yakiwa yako jikoni yanaendelea kufanyiwa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kugawanya Kata ili Jimbo la Muheza kuwa katika Majimbo mawili, naomba niseme kwamba kwa sababu jambo hili haliko kwetu, TAMISEMI, liko katika Tume ya Taifa ya Uchaguzi; ambapo ikiona kama inafaa kwa vigezo, basi labda Jimbo hili linawezekana litaweza kugawa kama Majimbo mengine yalivyogawiwa.

Kwa hiyo, nina imani Tume ya Taifa ya Uchaguzi, wataangalia kufanya *analysis*, kuangalia ukubwa wa Jimbo hili, kwa sababu kuna Kata 37 na vijiji zaidi ya 135 wataangalia kwamba katika uchaguzi ujao, inawezekana saa nyingine wao watakavyoona inatosha, watafanya maamuzi sahihi katika eneo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, na mimi niulize swali moja dogo tu. Kwa kuwa vijiji vya Chipogolo, Mima, Pwaga, Kibakwe, Berege, Mbori na Chunyu vina idadi ya watu wengi sana, ni *trading centers* ambazo ni kubwa sana na kuna wafanyabiashara wengi.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubaliana nami kwamba sasa ipo haja kwenda kufanya utafiti kuona kwamba vinaweza kupewa hadhi ya kuwa Miji Midogo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikiri wazi kuwa juzi nilikwenda pale Mpwapwa, katika kuangalia ule mfumo wa maji kama vijana wa sekondari ya Mpwapwa wanapata maji na kuangalia huduma ya afya kama wanatumia mifumo ya *electronic* katika Hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Wilaya ile ina Majimbo mawili, Jimbo la Kibakwe na Jimbo la Mpwapwa, lakini jiografia yake ni kubwa zaidi; na kwa sababu najua utaratibu wa kuomba maeneo hayo sasa kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo, maana yake mchakato wake unaanza katika ngazi za chini, kuanzia ngazi za vijiji, katika mikutano ya Baraza la Madiwani, halikadhalika katika WDC na Baraza la Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtakavyoona kuwa hiyo nafasi inatosha, basi nadhani mchakato hiyo itaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI itafanya tathmini kuangalia kwamba, basi kama kuna hadhi ya kuipa mamlaka ya Miji Midogo hatutasita kufanya hivyo. Kuhusu kuangalia kama vile vigezo vitakuwa vimefikiwa.

Kwa hiyo, kwa kushirikiana na Mheshimiwa George Simbachawene ambaye ni Waziri wa Nchi yuko eneo hilo, halikadhalika Mheshimiwa Lubeleje ambaye ni Mbunge wa Mpwapwa aliyeleta *concern* hii, nadhani tunaweza kufanya mchakato huo, basi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, haitasita ikiona kwamba pale mahitaji yanayotakiwa yaweze kufanyiwa hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Venance Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wilaya ya Kilolo inafanana kabisa na matatizo ambayo yako hapo, na ni katika

Majimbo makubwa, takriban lina kilometa za mraba takribani 21,000; na kwa kuzingatia hilo, Serikali iliamua kutoa Mji Mdogo wa Ilula, sasa ni muda mrefu.

Je, haioni sasa ni muda muafaka wa kupewa hadhi ya kuwa Halmashauri kamili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika kumbukumbu zangu pale kuna barua ya tarehe 2 Juni, 2015 imetoka Kilolo iliyokuwa ikiomba uanzishaji wa Halmashauri hii. Katika maeneo ambayo Ofisi ya Rais, TAMISEMI itaenda kufanya uhakiki, eneo la Kilolo litakuwa mojawapo. Kwa hiyo, tufanye subira katika hilo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ina Majimbo mawili; Mlalo na Lushoto, na tunalo ombi katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI la kupata Halmashauri ya Mlalo.

Je, ni lini sasa Serikali itatupatia Jimbo la Mlalo Halmashauri kamili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika kumbukumbu zetu, namshukuru Mheshimiwa Mbunge alishawahi kufika mpaka ofisini na katika kufanya rejea katika *documents* zetu, tumeona kwamba kuna vitu fulani vilikuwa bado havijakidhi vigezo kule Mlalo; na maelekezo tuliyoyatoa ni kwamba, wafanye ule mchakato kuangalia vile vigezo viweze kukamilika, halafu maombi yale yawasilishwe rasmi katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ilimradi eneo hilo sasa wataalam watakapokuja kufanya uhakiki; ikionekana eneo hilo sasa linatosha kuanzisha Halmashauri mpya, basi hakuna shaka, Ofisi ya Rais, TAMISEMI haitosita kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshatoa maelekezo katika suala zima la Mlalo na Mheshimiwa Shangazi amekuwa akilifuatilia kwa ukaribu sana suala hili. Sasa naomba nitoe msukumo katika maeneo husika, ule mchakato na vile vigezo mwanzo vilikuwa havijakamilika vizuri, tuweze kuvikamilisha na maombi hayo sasa yawasilishwe katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ufanisi wa hali ya juu katika maeneo hayo.

Na. 276

### **Fedha Za TASAF Kutowafikia Walengwa**

**MHE. AMINA S. MOLLEL (K.n.y. MHE. SABREENA H. SUNGURA)** aliuliza:-

Kumekuwa na tatizo kubwa la mgawanyo wa fedha za TASAF ambapo wananchi wengi wasio na uwezo, wamekuwa hawapati fedha hizo.

Je, Serikali imejipangaje kutatua kero hii kwa wananchi ambao hawapati fedha hizo hususan katika Mkoa wa Kigoma?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utambuzi wa kaya za walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini, ulianza mwezi Novemba, 2013 na hadi sasa umeshaandikisha kaya 1,100,000 katika Halmashauri 159 za Tanzania Bara, pamoja na Wilaya zote za Unguja na Pemba. Kaya hizi zinapata ruzuku kwa utaratibu wa uhaulishaji fedha baada ya kutimiza masharti ya kupeleka watoto shule na kliniki na pia kushiriki katika kazi za kutoa ajira ya muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaanza ulipanga kufikia asilimia 70 ya Miji, Mitaa na Shehia za Halmashauri ambavyo ndivyo vilivyofikiwa kutokana na mchakato wa kuvipanga, kutokana na viwango vya umaskini katika kila Halmashauri. Baada ya jamii kutambua kaya maskini na kuzipitisha kwenye mikutano ya hadhara iliyosimamiwa na viongozi wa Vijiji, Mitaa na Shehia. Kaya zilizotambuliwa zilijaziwa dodoso ili kukusanya taarifa zaidi za kaya na hatimaye Kaya hizo ziliandikishwa kwenye daftari la walengwa na kuanza kupokea ruzuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa TASAF kwa kushirikiana na Halmashauri ilifanya kila jitihada kuhakikisha kwamba kaya zinatambuliwa na kuandikishwa kwenye mpango ni kaya maskini sana kwenye baadhi ya maeneo Kigoma ikiwa ni mojawapo, baadhi ya jamii na viongozi walifanya udanganyifu na kuingiza majina ya kaya ambazo siyo maskini sana na kuziacha kaya zinazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuona changamoto hizo, TASAF imefanya mapitio ya orodha ya kaya zilizoandikishwa na kufanya ukaguzi wa

nyumba kwa nyumba na kuziondoa kwenye mpango wa kaya zote ambazo siyo maskini. Zoezi hili ni endelevu na ni la kudumu. Kaya zote ambazo siyo maskini na ziliingizwa kwa makosa au kwa makusudi katika orodha ya kaya maskini zitaondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka kufikia tarehe 30 Mei, 2016 maeneo yote 161 ya utekelezaji ambayo ni Halmashauri 159 za Tanzania Bara, Unguja na Pemba, zimeshaondoa Kaya ambazo hazistahili kuwemo kwenye orodha ya walengwa. Jumla ya kaya 25,446 zimeshaondolewa kwenye mpango kwa sababu mbalimbali ikiwemo vifo, kukosa vigezo vya kaya maskini na kuondolewa kwa Wajumbe wa Kamati za Mpango na viongozi wa Vijiji na Mtaa na Shehia katika orodha ya kaya maskini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina Mollel, swali la nyongeza.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na nina maswali mawili ya nyongeza.

Moja, kwa kuwa zoezi hili limeleta malalamiko na kwa kuwa baadhi ya waliochangia utaratibu huu kwenda vibaya na kuandikisha kaya ambazo hazikustahili kupata mgao huu wa TASAF; je, Serikali inawachukulia hatua gani watumishi ambao wamefanya makosa haya na kuwakosesha haki yao ya msingi wale waliostahili kupata mgawanyo huu wa TASAF?

Swali la pili, kwa kuwa baadhi ya walionufaika wanadai kwamba kiasi hiki ni kidogo; je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuongeza kiasi cha fedha ili kiwanufaishe walengwa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa niaba ya Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutambua kwamba kumetokea udanganyifu kama nilivyosema katika jibu langu la msingi na kwamba takribani kaya 25,446 ni zile ambazo hazikuwa zinakidhi vigezo vilivyoelezwa vya kiwango cha umaskini, lakini wakawekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tumechukua hatua mbalimbali za kinidhamu hasa kwa watumishi wale ambao ni wa Halmashauri, kwa sababu kwa kiasi kikubwa zoezi hili linafanywa kwa ushirikiano kati ya Wizara hii na Wizara ya TAMISEMI kwa maana ya watumishi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa wale viongozi wa kuchaguliwa, tutaona hatua nzuri zinazofaa kwao, kwa sababu udanganyifu huu umefanywa mahali pengine ni kwa makusudi na mahali pengine siyo kwa makusudi, ni kwa kukosa vielelezo vya kutosha juu ya hao wanaotakiwa kunufaika na utaratibu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kiasi hiki anachodai Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kidogo na je, hatuoni haja ya kuongeza? Msingi wa kiwango hiki ni kwamba lengo letu ni kuzisaidia, *not permanently* kaya hizi maskini ili ziweze ku-*gain* mahali ambapo sasa zinaweza zikajiendesha zenyewe. Vigezo vinavyotumika kama nilivyosema, kwanza kabisa unaangalia kama familia hiyo ina watoto, lakini cha pili, ni kwamba je, hata kama ina watoto je, watoto hao wanaenda shule au wanaenda kliniki?

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana katika mpango huu, baadhi ya maeneo wameamua kuzisaidia hizi familia kuwalipia CHF yaani Mfuko wa Afya ya Jamii ili waweze kuwa na uhakika wa kupata matibabu. Hili tunalitia moyo sana, kwa sababu moja kati ya vitu vinavyoumiza familia masikini ni kutokupata matibabu stahiki. Sasa hili la shule na lishe ni jambo ambalo tumeweka kama vigezo. Sasa kama haya nia yake ni kuikuza familia itoke pale na ifike mahali ambapo itajitegemea, ikiwa ni pamoja na shughuli nyingine za kiuchumi, basi fedha hizi kwa kiwango tulichopanga, tumezingatia hali ya kutosha kwake na hivyo watajenga uwezo kidogo kidogo na baadaye wataweza kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito tu kwa watu wanaonufaika na mpango huu kuwa na dhamira ya kujenga kujitegemea na siyo kuendelea kusaidiwa ili baada ya programu hii kuisha, wawe wameshajenga huo uwezo. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nsanzugwako.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWAKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Naomba niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, muuliza swali msingi wake ulikuwa ni udanganyifu mkubwa uliotokea katika Mkoa wa Kigoma hasa katika Mfuko huu wa TASAF, sasa nilikuwa naomba Waziri anipe *comfort* hapa kwamba je, haoni kwamba kuna haja ya kufanya uhakiki maalum kwa Mkoa wa Kigoma kama ambavyo Mheshimiwa Sabreena alijielekeza kwenye swali lake?

Mheshimiwa Naibu Spika, udanganyifu kwa Mkoa wa Kigoma ulikuwa ni mkubwa sana katika Wilaya ya Kasulu na Kibondo katika Mfuko huu wa TASAF. (Makofi)



**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ni kweli kwamba msingi wa swali ilikuwa hasa ni kujua udanganyifu uliotokea Kigoma; na tunapojibu swali hapa kwa sababu linagusa karibu programu hii ambayo ni ya Wilaya ambapo tumeanza kwa Tanzania Bara karibu Wilaya 151, ni dhahiri kwamba tungepata maswali mengi na ndiyo maana tumekuja na jibu la jumla kwamba yale yaliyotokea Kigoma yametokea pia na maeneo mengine; na udanganyifu umekuwepo na hatua hizo hizo zitakazochukuliwa Kigoma ndizo zitakazochukuliwa na huko sehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa tu ni kwamba kwa utafiti tuliofanya Kigoma ni kwamba kaya ambazo zinaonekana zimefanyiwa udanganyifu ni takribani kaya 1,020 na hizo tumeshaziondoa kwenye orodha na wale watumishi waliofanya udanganyifu huo wanaendelea kuchukuliwa hatua, lakini pia kuna wale wengine ambao ni wa kuchaguliwa maana unavyojua lile zoezi linashirikisha wale Wenyevidi wa Vijiji pale, Mtaa na nini na nini. Sasa unamkuta Mwenyekiti wa Kijiji au Mwenyekiti wa Kitongoji amemweka mke wake au unamkuta mwingine ni mtumishi, ni mwalimu naye yupo kwenye mpango huu. Hao wote tumewaondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama ni kuchua hatua za kinidhamu dhidi yao pamoja na ile *benefit of doubt* ya watu kutokufahamu; wengine wamefanya siyo kwa makusudi, lakini kwa wale waliofanya makusudi kusema ukweli hatua zitachukuliwa na kazi hiyo kwa maana ya Mkoa wa Kigoma, tumeifanya vizuri labda tu hapa tuendeleo kuchukua hatua ili jambo hili lisijrudie tena. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Abdallah Chikota.

Na. 277

### **Ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Mtwara**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA (K.n.y. MHE. HAWA A. GHASIA)** aliuliza:-

Uwanja wa Ndege wa Mtwara ulijengwa mwaka 1965.

(a) Je, ni lini uwanja huo utafanyiwa ukarabati mkubwa ili kuwezesha ndege kuruka na kutua bila matatizo?

(b) Je, ni lini uwanja huo utawekewa taa ili ndege ziweze kutua wakati wote?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeendelea kufanya matengenezo ya mara kwa mara ya Kiwanja cha Ndege cha Mtwara. Ikiwa ni mpango wa muda mfupi, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania inafanya tathmini ya uchakavu wa matabaka ya lami ya njia ya kuruka na kutua ndege ili kubaini ukarabati stahiki unatakiwa na mahitaji ya fedha ya kufanya ukarabati huo. Katika kutekeleza jukumu hili, shilingi milioni 290 zimetengwa na mamlaka katika mwaka 2015/2016 na kazi hiyo ya tathmini inatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2016. Aidha, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imetenga shilingi bilioni kumikwa ajili ya ukarabati wa kiwanja hiki.

Katika mpango wa muda mrefu, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege katika mwaka wa fedha 2015/2016 ilitenga fedha kiasi cha shilingi milioni 600 kwa ajili ya kuandaa mpango kabambe kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa kiwanja hicho kutoka Daraja III(C) la sasa kwenda daraja IV(E) ili kiweze kuhudumia ndege kubwa zaidi na hivyo kuwa kitovu cha usafiri wa anga kwa Ukanda wa Kusini. Ukarabati na upanuzi wa kiwanja utahusisha miundombinu yote ya kiwanja ikiwemo taa na mitambo ya kuongozea ndege pamoja na majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hiyo ya uandaaji wa mpango kabambe wa usanifu wa awali inatarajiwa kukamilika Julai, 2016. Kukamilika kwa mpango huu kutaiwezesha Serikali kutafuta fedha za ukarabati na upanuzi wa kiwanja ikiwemo ufungaji wa taa za kuongoza ndege wakati wa kutua na kuruka nyakati za usiku.

(b) Ikiwa ni mpango wa muda mfupi, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeingia makubaliano na Kampuni ya *British Gas (BG)* kwa ajili ya kutumia taa zake ambazo ni za kuhamisha (*portable airfield ground lighting*) kwa ajili ya kuongozea ndege pale ambapo ndege itatakiwa kutua usiku.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nimuulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba miundombinu ya kiwanja cha ndege ni pamoja na barabara inayoingia uwanjani na barabara hii sasa imechakaa. Sasa nataka kuuliza kwamba Serikali ina mpango gani wa ukarabati wa barabara inayoingia uwanja wa ndege wa Mtwara kutoka Magomeni Mjini Mtwara hadi uwanja wa ndege?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, amesema kwamba kuna *master plan* ambayo inaandaliwa; sasa nilitaka kuuliza kwamba kwa kuwa Serikali ina mpango gani wa kutwaa eneo la ardhi kwa sababu sehemu kubwa ya uwanja huo wa ndege imepakana na eneo la Jeshi; sasa kwa vyovyote vile watahitaji eneo la kijiji cha Naliendele; wamejiandaa je kutwaa eneo hili ili kuepusha migogoro ya wananchi wa Naliendele hapo baadaye? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukarabati wa barabara, ni sehemu ya mpango ambao nimeueleza katika swali langu la msingi. Tunapoongelea kukarabati uwanja huu ni kurekebisha njia za barabara za kurukia na kutua ndege pamoja na maingiliano na nyumba vilevile za abiria. Kwa hiyo, ni mpango wote, unaunganisha kila kitu ikiwa ni pamoja na barabara zinazoingilia uwanja huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, namwomba Mheshimiwa Mbunge asubiri kwanza tupate taarifa kamili ya mpango kabambe huo ambao unakamilika mwezi Julai kama nilivyosema katika jibu langu la nyongeza, baada ya hapo ndiyo masuala ya kutwaa ardhi na mipango mingine ya kutekeleza mpango huo yatafuatia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ...

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Dau.

**NAIBU SPIKA:** Hapana. Mheshimiwa mama hapo, aliyekaa. *(Kicheko)*

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipati nafasi hii. Nami naomba niulize swali linalofanana na swali na msingi. Kwa jina naitwa Zaynabu Matitu Vulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi niulize swali linalofanana na swali la msingi. Kwa kuwa Mafia ina uwanja wa ndege; na kwa kuwa Mafia ni eneo ambalo linapokea watalii wengi sana.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka taa ili wasafiri hao waweze kutumia ndege wakati wowote na kuweza kuunganisha na ndege zao kwa ajili ya safari zao za Kimataifa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, uwekaji wa taa katika kiwanja cha ndege cha Mafia utafanyika pale mahitaji yatakapojitokeza. Kwa sasa hatuna ndege zinazotua usiku. Needs hiyo itakapojitokeza, wataalam watafanya mpango huo na taa hizo zitawekwa. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea.

**MBUNGE FULANI:** Aaaaaaahhhh!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi, sasa aulize Swali Lake.

Na. 278

### **Barabara ya Ulinzi Kati ya Tanzania na Msumbiji**

**MHE. JEROME D. BWANAUSI** aliuliza:-

Barabara ya ulinzi kati ya Tanzania na Msumbiji ni muhimu sana kwa ulinzi na kiuchumi.

Je, ni lini barabara hiyo itajengwa hasa ikizingatiwa kuwa imekuwa ikiahidiwa kwa miaka mitano sasa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mangamba – Madimba – Tangazo – Kitaya – Mnongodi – Mapili hadi Mitemaupinde ni barabara ya ulinzi

inayounganisha Wilaya za Mtwara Vijijini, Newala na Nanyumbu. Barabara hii inayoambaa na mpaka wa Tanzania na Msumbiji ilikuwa inatumiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa ajili ya ulinzi wa mpakani. Kipande cha barabara hii kati ya Mangamba – Madimba – Tangazo – Kitaya hadi Mnongodi chenye urefu wa kilometa 108 kinahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS). Sehemu inayobaki yenye urefu wa kilometa 250 haiko chini ya milki ya mamlaka yoyote, hivyo imekuwa pori baada ya kukosa matengenezo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania, imefanya na kukamilisha usanifu wa kipande cha barabara chenye urefu wa kilometa 120 kati ya Mapili na Mtemaupinde pamoja na daraja la Lukwamba na usanifu kukamilika mwaka 2007. Kwa kuanzia Serikali ilianza kazi ya ujenzi wa daraja hili mwaka 2013 na kazi zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na ufunguzi wa sehemu Mapili hadi Mitemaupinde na hadi sasa jumla ya kilometa 25 zimefunguliwa. Aidha, Wizara yangu imetenga fedha katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 kwa ajili ya kuendelea kuifungua barabara hii na barabara nyingine za ulinzi zilizopo katika Mkoa jirani wa Ruvuma. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bwanausi, swali la nyongeza.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali na naomba niulize maswali mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini swali langu la kwanza; kwa kuwa Serikali imeamua kuifanyia kazi barabara hiyo ya ulinzi; na kwakuwa kuna vijiji kumi vya ulinzi ambavyo vipo katika Jimbo la Lulindi na hakuna daraja pale, daraja lake la Mto Myesi Mbagala lilichukuliwa na maji wakati wa mafuriko 2012.

Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuwaagiza watu wa TANROADS Mkoa wa Mtwara walifanyie tathmini daraja hilo ili liweze kujengwa wakati huu barabara hii ikitengenezwa? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kwamba, kwa kuwa aliyekuwa Waziri wa Ujenzi ambaye sasa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Pombe Magufuli aliahidi kusaidia ujenzi wa madaraja matatu ambayo yalizolewa na maji katika mafuriko ya mwaka 2013 na 2014; madaraja ya Mto Mwiche katika kijiji cha Shaurimoyo, Nakalola na Nanjota na tayari lile la Nanjota limeanza kufanyiwa kazi; je, Mheshimiwa Waziri atalithibitisha vipi Bunge hili kwamba yale madaraja ya Shaurimoyo pamoja na Nakalola sasa litaingia kwenye mpango wa kujengwa? (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikujulishe kwamba nilikuwepo katika hilo eneo. Nilikwenda na Mheshimiwa Mbunge, niliwaona wale watu jinsi wanavyopata shida kwa sababu zile kata zote zilikuwa zimekatwa kabisa, hakukuwa na mawasiliano; na kwa kweli tuliagiza angalau daraja moja liunganishwe kwa haraka ili watu waanze kupata sehemu ya mawasiliano waweze kwenda Masasi kujipatia huduma zao za kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, madaraja hayo mengine mawili yametengewa bajeti na nawaagiza TANROADS watoe kipaumbele ili Kata zile zote ambazo zilikuwa zimetengwa ziweze kupata huduma kwa urahisi zaidi kama ilivyokuwa awali. Kwa kutegemea hilo daraja moja tu haitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu daraja la ulinzi, naomba nalo likafanyiwe tathmini kama ambavyo mwakilishi wa wananchi wa kule ameomba na ninafahamu kuna vijiji vingi ambavyo vipo katika ule mpaka, barabara ilikuwa ni ya Jeshi, lakini kwa sasa kuna makazi mengi na watu wanalima sana kule. Kwa hiyo, naomba vilevile pamoja na daraja hili katika barabara ile ya ulinzi walifanyie tathmini halafu waje na taarifa ambayo itatusaidia kufanya maamuzi ya nini kifanyike. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma Kasheku.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa swali la msingi lililoulizwa linafanana kabisa na matatizo yaliyopo kwenye Jimbo la Geita Vijijini ambapo mwaka 2013 Mheshimiwa Rais Mstaafu alipokuja kule tulimweleza kuhusiana na barabara mbadala ya kilometa 75 kuanzia Bugulula, Senga, Sungusila mpaka kwenda kuungana na Sengerema Mwamitiro kwamba ipande kutoka kwenye hadhi ya Halmshauri kwenda kwenye hadhi ya TANROADS na Mheshimiwa Rais Mstaafu alimwomba Mheshimiwa Rais wa sasa ambaye alikuwa Waziri kwamba atusaidie na akatuambia tufuate taratibu za Serikali na akatupa kuanzia shilingi milioni 400 tukaanza kukarabati ile barabara; na taratibu zote zimeshakamilika tumepeleka kuomba...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, uliza swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Swali langu la msingi, Waziri wa Ujenzi anatoa kauli gani kuhusu kuipandisha barabara hii kuwa ya TANROAD angalau kwa kiasi cha changarawe? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema ahadi ilitolewa na viongozi wetu na kwa maana hiyo, viongozi wetu walionesha dhamira ya kuitengeza hii barabara. Na mimi namhakikishia, sisi ambao tumekabidhiwa dhamana ya kutekeleza dhamira za viongozi wetu, tutalishughulikia hili. Kuhusu matengenezo *Regional Manager* wa Geita afanyie tathmini, apeleke taarifa makao makuu ili maamuzi sahihi yaweze kufanyika kwa haraka. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lililoulizwa Na. 278, linafanana na barabara ya Mzani – Nyakahula – Mrusagamba – Mrugalama iliyopo Wilaya ya Ngara, Kagera. Pia kuna barabara ya Karagwe kupitia pori la Kimisi, Tubenako Ngara ambazo Mheshimiwa Rais aliahidi zitajengwa. Je, ni lini Serikali itakamilisha barabara hizo kwa kiwango cha lami? (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nilijibu awali, dhamira yetu ni kutekeleza ahadi zote ambazo viongozi wetu walizitoa katika nyakati mbalimbali, kuanzia awamu ya nne na awamu ya tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Oliva kwamba barabara hizo alizoziongelea, maadam zilitolewa ahadi, nasi tutazichukua ili tuweze kuzishughulikia kwa namna ambavyo uwezo wa kifedha utakavyokuwa unatujaa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nami naomba kuuliza maswali madogo mawili. Swali langu la kwanza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issaay, ni swali moja la nyongeza.



**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nashukuru. Naomba kuuliza, ni kwa nini Wizara ya Ujenzi haijaweza kupitisha barabara mpya za Halmashauri ya Mji wa Mbulu na kwa kuwa mji wetu wa Mbulu ni mji mkongwe kuliko miji yote Tanzania? Naomba kauli ya Wizara kuhusu barabara hizi mpya kwa kuwa sasa magari yameongezeka sana katika Wilaya zetu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tuna barabara ambayo ni ya lami kwa pale Mbulu Mjini. Vilevile Mheshimiwa Mbunge atakuwa anafahamu kwamba katika bajeti ambayo tunashukuru sana mliipitisha hapa Bungeni, kuna bajeti ya kutekeleza baadhi ya barabara ambazo ziko ndani ya Wilaya ya Mbulu; na ninamhakikishia kwamba tutatoa kipaumbele ili fedha zile zilizotengwa kwa ajili ya kujenga barabara za Wilaya ya Mbulu na Wilaya nyingine tutazitekeleza kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyotujalia nguvu za kifedha.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea. Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga sasa aulize swali lake.

Na. 279

### **Mbuga za Hifadhi ya Wembere**

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU** aliuliza:-

Mbuga ya Hifadhi ya Wembere ni mbuga iliyotelekezwa na Serikali na kupoteza sifa za kuendelea kuwa hifadhi na sasa inatumika na wafugaji kulisha mifugo na wakulima kulima alizeti na mpunga kwenye eneo hilo.

Je, ni kwa nini Serikali isibadilishe matumizi ya mbuga hiyo badala yake ipimwe na kutumika kwa wafugaji na wakulima na kuondoa migogoro inayoendelea kati ya wakulima na wafugaji ambayo wakati mwingine inasababisha mauaji na uharibifu wa mali?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga kama ifuatavyo:-



Mheshimiwa Naibu Spika, Mbuga ya Wembere ipo ndani ya mipaka ya mikoa ya Tabora na Singida. Umuhimu wa eneo hili ni pamoja na kuwa chanzo cha maji yanayokwenda katika maziwa Eyasi na Kitangire. Mbuga hiyo pia ni maarufu kwa aina (*species*) za mimea na wanyamapori mbalimbali na muhimu kwa mazalia ya ndege mbalimbali wenye sifa za Kitaifa na Kimataifa. Eneo hilo linatambuliwa Kimataifa kama mahsusi kwa kundi muhimu la uhifadhi wa ndege duniani tangu mwaka 2001.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa eneo hilo linakabiliwa na changamoto ya uvamizi kwa shughuli za kilimo na ufugaji kama alivyobainisha Mheshimiwa Mbunge, bado Serikali haijaitelekeza mbuga hiyo na kinyume chake eneo hilo linatumika kwa shughuli za uwindaji wa kitalii ambapo linaliingizia Taifa fedha za kigeni na kutoa ajira kwa wananchi waishio kando ya eneo hilo. Kwa mfano, katika kipindi cha mwaka 2013/2014 hadi 2015/2016 Serikali imepata kiasi cha dola za Kimarekani 142,450 kutokana na shughuli za uwindaji katika vitalu vilivyoko ndani ya eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu kiikolojia wa eneo hilo Kitaifa na Kimataifa Wizara yangu itaendeleza majadiliano na Serikali ya Mkoa wa Tabora na Singida ili kuona uwezekano wa kupandisha hadhi eneo hilo ili kuwa na uhifadhi endelevu wa bioanuai zilizopo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kafumu, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Namshukuru Naibu Waziri kwa majibu ambayo hayatoshelezi.

Kwa kuwa mimi nimezaliwa na kukulia katika mbuga hii, ni mashahidi kwamba mbuga hii ilitelezwa, kwa hiyo, wananchi wengi wakulima na wafugaji walihamia katika mbuga hii. Matokeo yake wanyama na hao ndege anaosema wametoweka; kama wamebaki ni sehemu ndogo sana; na kwa kuwa eneo hili mwaka 2014 lilisababisha mauji ya wakulima watano kutokana na mgogoro wa wakulima: kwa nini Serikali isikubali ombi hili? Swali la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa sasa hivi nchi inakabiliwa na migogoro ya wafugaji na wakulima, sisi sote ni mashahidi; na kwa kuwa mwaka 2011 Serikali hii ilifanya tathmini ya mbuga zile ambazo zimepoteza sifa na Wembere ilikuwa ni mojawapo; kwa nini Serikali isilitazame upya jambo hili na kuitenga mbuga hii ili wananchi wanaoishi kwenye eneo hilo waweze kulima na kufuga bila kugombana; lakini pia wanaweza kubakiza eneo dogo kwa ajili ya hawa ndege hawa anaowasema? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, naona kulikuwa na ushauri hapo na swali, kwa hiyo, wewe jielekeze kwenye maswali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili la Wembere hivi sasa ninavyozungumza, limegawanywa katika vitalu vinne; Kitalu kinachoitwa *Wembere Open Area Central One*, kitalu kinachoitwa *Wembere Central Area Two*, *Wembere Game Controlled Area* upande wa Kusini, lakini pia upande wa Kaskazini kuna *Wembere Open Area*, vyote hivi vikiwa ni vitalu vinavyopaswa kuendesha shughuli za uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, mojawapo ya kitalu, kwa mfano, hiki cha upande wa Kaskazini, *Wembere Open Area* hakijawahi hata kupata mwekezaji kwenye shughuli hizo za uwindaji. Lakini vipo vitalu ambavyo vinafanyakazi, kwa mfano kile cha *Open Area Central One*, kinatumika na ndiyo hicho ambacho nimesema ni mojawapo ya vitalu vinavyoingizia fedha Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tunazungumzia mazingira halisi ambayo Mheshimiwa Mbunge anatoka, wakati huo huo tunachokizungumzia ni suala la utaalim vilevile, basi nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba arejee azma ya Serikali tuliyoitangaza hapo awali, kwamba sasa tunataka kufanya zoezi Shirikishi; yeye pamoja na wananchi kwenye eneo linalohusika kwenye maeneo hayo ya Wembere pamoja na timu ya wataalam ambayo tayari tumeshasema baada ya Bunge hili tunakwenda kwenye maeneo hayo kuhakiki, twende tukaoneshane.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuchanganye utaalim na maoni ya wananchi ili tuweze kufikia muafaka sasa kujua kama kuna eneo ambalo ni sehemu ya eneo hili ambalo litaonekana halifai kuendelezwa tena kwa shughuli hii ambayo sasa hivi inaendeshwa kwa mujibu wa sheria, basi itakuwa hivyo. Kwa sasa hivi tutaendana na sheria kama ilivyo mpaka hapo mabadiliko yatakapofanyika baada ya zoezi lile la Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuulizwa swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo yaliyoko katika swali namba 279 yanafanana sana na hali halisi iliyoko Urambo katika Kata ya Nsenda ambako wakulima wa Lunyeta na Kangeme walichomewa mahindi yao kutokana na mgogoro wa mipaka kama ulivyoielezwa katika suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mgogoro huu umewaacha wakulima bila kujua hatima yao na kusababisha usumbufu sana wa kupata chakula; na Serikali ilikiri kwamba ilifanya makosa kuwachomea wakulima ambao walikuwa wamelima katika eneo hilo, je, Serikali iko tayari sasa kufuatana na mimi kwenda kuangalia hali halisi ili kutafuta ufumbuzi wa kudumu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tunazo sheria, lakini ni kweli pia kwamba kuwa na sheria ni sehemu moja au ni jambo moja, lakini utekelezaji wa sheria ni jambo lingine. Inawezekana kabisa kwamba mahali pengine utekelezaji wa sheria unaweza kuwa ni utekelezaji wa sheria unaovunja sheria. Sasa pale ambapo tayari kuna sheria na sheria zinatakiwa kusimamiwa, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa sheria, lakini tunatoa wito kwanza kwa watu wote ambao wanatekeleza sheria, hasa zile sheria ambazo ziko chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, waweze kutekeleza sheria hizo bila kukiuka sheria zenyewe, lakini bila kufanya mambo ambayo yanakwenda kinyume cha kanuni na taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa suala mahsusi ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliuliza, linalohisiana na eneo alilolitaja, napenda kumuahidi kwamba nikitoka hapa nitakwenda kulifuatilia zaidi na mimi nilifahamu kwa sababu ni mahsusi ili niweze kuona kama tunaweza kupata suluhisho katika kipindi hiki ambacho tuko Bungeni; lakini kama itabidi kwenda kuangalia, basi mara tu baada ya kumaliza Bunge la Bajeti, nitaweza kuandamana naye kwenda kuona kuna nini ili tuweze kupata ufumbuzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mponda.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Migogoro ya ardhi ambayo inajitokeza kati ya hifadhi na wananchi nayo yanajitokeza katika Pori Tengefu la Bonde la Kilombero. Tumeiomba Serikali, naomba niwaulize hapa Serikali, ni lini sasa mtarudisha ardhi ile ya *Buffer Zone* katika Pori Tengefu la Kilombero? (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza niseme kwamba *Buffer Zone* tafsiri yake ya moja kwa moja isiyohitaji utaalam mwingi sana ni eneo ambalo linapaswa kuwa siyo la yeyote kati ya pande mbili zinazopakana. Eneo hilo kwa mujibu wa kanuni na taratibu, linapaswa kuwa ni eneo ambalo shughuli za uhifadhi zinakuwa *mild*, lakini pia shughuli za matumizi ya kibinadamu na zenyewe zinakuwa *mild* kwa maana ya

kwamba siyo eneo ambalo linatumika moja kwa moja kwa asilimia mia moja na pande zote mbili zinazopakana. Kwa hiyo, kusema kwamba lirudishwe kwa wananchi, pengine inaweza kuwa siyo sahihi sana kwa sababu halijawahi kuwa kwa asilimia mia moja upande wa hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotangulia kusema na ninarudia tena, mazoezi haya yote ya kupitia hifadhi baada ya hifadhi; iwe hifadhi ya misitu, iwe hifadhi ya wanyamapori au hifadhi nyingine yoyote ile chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii; maeneo yote hayo yameorodheshwa kama sehemu ya migogoro ya ardhi na yameorodheshwa hivyo na Wizara ya Ardhi. Pia tunakwenda kufanya *team work* miongoni mwa Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ardhi yenyewe, TAMISEMI, eneo ambalo sasa Mheshimiwa Mbunge atashirikiana na Serikali ya Wilaya pale, lakini pia Wizara ya Nishati na Madini, pale patakapokuwa panahusika na mambo ya madini; lakini pia masuala ya maji kwa sababu tunahusika pia. Kwa kutunza misitu tunatunza pia vyanzo vya maji, basi pale itakapobidi kwamba kuna chanzo cha maji tunataka kukifanya kiwe endelevu, kukilinda, basi na Wizara ya Maji itahusika. Kwa kuanzia ni Wizara hizo tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba wananchi wote na kupitia swali hili la Mheshimiwa Mbunge, wawe wavumilivu katika kipindi hiki ambacho ni kipindi cha mpito ambapo Serikali sasa inakwenda kutafuta majibu ya kudumu kwenye migogoro hii ya mipaka na hifadhi na migogoro ya ardhi kwa ujumla.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martha Mlata, swali fupi.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa swali fupi, nilikuwa namwomba Naibu Waziri, kwa swali lile la Wembere, kwa sababu alisema watakwenda kuzungumza pamoja na wananchi, lakini sheria bado inatekelezwa ile ile. Mimi nilikuwa naomba tu aniahidi kwamba yuko tayari kuongozana na mimi twende Wembere akashuhudie kipindi hiki kabla hatujamaliza Bunge la Bajeti? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martha Mlata, nadhani wakati wa bajeti, Mawaziri wanapaswa kuwepo humu ndani. Kwa hiyo, nadhani ombi lako, mkimaliza tu bajeti utaongea na Mheshimiwa Waziri atakujibu. Nadhani hatakataa kuambatana nawe. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, lakini nikumbushe tu, maswali mafupi na Mawaziri mtusaidie majibu ambayo yanakwenda kwenye swali lililoulizwa. Maelezo mengi yanatupoteza hata kufuatilia jibu.

Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa, Mheshimiwa Munira Mustafa Khatib, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 280

**Mpango Maalum wa Kuwapeleka Jeshi la Kujenga Taifa Vijana  
Wanaomaliza Kidato cha Nne Nchini**

**MHE. SUBIRA K. MGALU (K.n.y. MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB)** aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko kubwa la vijana wanaomaliza kidato cha nne kutokana na ongezeko la shule za kata nchini, vijana hawa wamekuwa wakizagaa mitaani bila kujua la kufanya na matokeo yake kujiingiza kwenye vitendo hatarishi kama dawa za kulevya, uvutaji wa bangi, wizi, udokozi na kadhalika.

Je, ni kwa nini Serikali isianzishe mpango maalum wa kuwapeleka Jeshi la Kujenga Taifa vijana wanaomaliza kidato cha nne nchini ili wakimaliza mafunzo waweze kujiajiri wenyewe pamoja na kuwa wazalendo?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu uliopo hivi sasa, wa vijana kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa ni ule wa vijana kujitolea ambao ni wenye elimu kuanzia shule ya msingi hadi vyuo vikuu na ule wa mujibu wa sheria ambao ni kwa vijana waliomaliza kidato cha sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango maalum anaoushauri Mheshimiwa Mbunge wa kuwachukua vijana wote wanaomaliza kidato cha nne kwa sasa hautawezekana kutokana na uwezo mdogo wa kifedha. Hivi sasa uwezo wa JKT kuchukua vijana wa kujitolea ni ni kati ya vijana 5,000 hadi vijana 7,000 kwa mwaka kutokana na bajeti inayotolewa. Hata hivyo, ushauri huu ni mzuri na Serikali itafanya maandalizi ya kambi nyingi zaidi na kutenga bajeti kubwa zaidi kwa ajili ya uendeshaji kadiri uwezo wa kifedha utakavyoruhusu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa Wanaochaguliwa kwenda JKT kwa sifa za chuo kikuu na *form six* ni wachache kwa baadhi ya maeneo hasa Mkoa wa Pwani; je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kwamba nafasi hizi zichukuliwe na vijana wanaomaliza kidato cha nne ili kuweza kukabili ongezeko la vijana hao? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa vijana hawa wanaokwenda JKT baada kuhitimu, wengi wao wakirejea katika maeneo wanakosa ajira wakati wanakuwa na ujuzi, lakini wanashindwa kujiajiri kutokana na kutokuwa na mitaji ya kutosha; je, Wizara ipo tayari kufanya tathmini ili kuweza kuwawezesha hasa vijana ambao wameonesha vipaji katika makambi hayo? Ahsante. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ulinzi na Jshi la Kujenga Taifa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nieleze tu kwamba wale vijana wanaokwenda kwa mujibu wa sheria ni wengi kuliko uwezo wa Serikali wa kuwachukua kwa sasa, yaani wanaomaliza *form six* kabla ya kwenda kujiunga na vyuo idadi yao ni kubwa mno kiasi cha kwamba kwa uwezo wa sasa hatuwezi kuwachukua wote, ndiyo maana baadhi tu wanachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, siyo sahihi kwamba wanaokwenda ni wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili; na hii niseme kabla sijaingia kwenye swali la pili, kwamba Serikali inaendelea kujipanga kuongeza kambi, kuongeza majengo ndani ya makambi ili hatimaye tuweze kuchukua vijana wote wanaomaliza *form six* kabla ya kwenda kujiunga na vyuo waweze kupita katika Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, ni kweli kwamba kwa wale wanaokwenda kwa kujitolea ambao idadi yao ni kubwa, ni zaidi ya vijana 5,000 kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, siyo wote wanaopata nafasi ya kuajiriwa ndani ya vyombo vya ulinzi na usalama. Kwa kiwango kikubwa kama tulivyosema wakati wa bajeti yangu, takriban asilimia 71 ya vijana hao, wanapata ajira kwenye vyombo vya ulinzi na usalama, lakini asilimia iliyobaki wanalazimika kurudi nyumbani kwa sababu hakuna uwezo wa kuwaajiri wote.

Kwa hiyo, nakubalina na wazo la Mheshimiwa Mbunge kwamba ni lazima sasa tufanye utaratibu wa kuwawezesha vijana hawa ili wanaporudi waweze kujitegemea, kujiajiri wao wenyewe. Utaratibu huu umeshaanza kupangwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ili vijana hawa waweze kupatiwa mitaji na kwa kuwa wana ujuzi fulani wanaotokanao JKT waweze kujiajiri wao wenyewe.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu, swali fupi la nyongeza.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Hivi karibuni JKT wametangaza nafasi za vijana wanaomaliza *form six* na wametangaza nafasi 1,500 mpaka 2,000. Nimemsikia Mheshimiwa Waziri anasema uwezo wao ni kati ya 5,000 mpaka 7,000. Nataka kufahamu, sasa ni mpango upi mwingine wa Wizara hii kuhakikisha kwamba hao zaidi ya 20,000, ambao hawajapa nafasi wanakwenda?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nieleweke kwamba kuna vijana wanaojiunga na JKT wa aina mbili. Kuna vijana tunaowaita wanajiunga kwa mujibu wa sheria, ni wale ambao wamemaliza *form six* kabla ya kujiunga na vyuo vikuu. Vijana hawa idadi yao tuliyoichukuwa mwaka huu ni 14,000 na sio wote ambao tunaweza kuwachukuwa kwa sababu waliohitimu *form six* ni wengi zaidi ya hapo, kwa hiyo, tunaendelea kujenga uwezo ili tuweze kuwachukuwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale vijana 5,000 mpaka 7,000 niliozungumzia, hao ni vijana wanaoingia kwa kujitolea, ambapo idadi yao ndiyo hiyo. Kwa hiyo, niseme tu kwamba hawa wa mujibu wa Sheria, idadi yao ni kubwa zaidi ni 14,000 na wanakaribia kuanza ndani ya wiki moja ili waweze kupata mafunzo hayo ya Jeshi la Kujenga Taifa.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea, Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo, sasa aulize swali lake.

Na. 281

### **Wafanyabiashara Kutozwa Kodi Mara Mbili**

**MHE. MATTAR ALI SALUM** aliuliza:-

Wafanyabiashara wanaotoa bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara hutozwa kodi Zanzibar na wanapofika Tanzania Bara hutozwa kodi tena; vilevile, wafanyabiashara wanaotoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar, hutozwa kodi tena Zanzibar. Hali hii husababisha wafanyabiashara kushindwa kuendelea na biashara kwani wanatozwa kodi mara mbili:-

(a) Je, Serikali inatambua uwepo wa utaratibu wa kutozwa kodi mara mbili kwa wafanyabiashara?



(b) Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi na wa kudumu kutatua suala la wafanyabiashara kutozwa kodi mara mbili?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uwepo wa utaratibu wa kutozwa kodi mara mbili kwa wafanyabiashara wanoingiza bidhaa za nje Tanzania Bara kupitia Zanzibar kwa sababu Tanzania Bara inatumia mfumo ujulikanao kama *Import Export Commodity Database*, ambao hautumiki kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Import Export Commodity Database* ni mfumo unaoweka kumbukumbu ya bei ya bidhaa mbalimbali zilizoingizwa nchini kutoka mataifa mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbukumbu ya bei za bidhaa mbalimbali zilizopo kwenye mfumo wa *Import Export Commodity Database* hutumiwa kama msingi wakati wa kufanya tathmini ya kodi ya bidhaa zinazoingizwa nchini pale thamani ya bidhaa husika inapoonekana kuwa hailingani na hali halisi. Hivyo basi, tofauti ya kodi inayotokana na kutotumika kwa mfumo wa *Import Export Commodity Database* kuthamini kiwango cha kodi kwa upande wa Zanzibar hukusanywa Tanzania Bara ili kuweka mazingira sawa ya ushindani kibiashara kwa bidhaa zote zinazoingia Tanzania Bara.

Mpango wa muda mfupi, muda mrefu na wa kudumu wa kutatua changamoto ya wafanyabiashara kutozwa kodi mara mbili, ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuridhia matumizi ya mfumo ya uthaminishaji wa kodi inayotumika ndani ya Idara ya Forodha ili kuondoa tofauti zilizopo za ukadiriaji wa kodi kati ya sehemu mbili za nchi yetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mattar Salum, swali la nyongeza.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kero hii inalalamikiwa sana na wafanyabiashara wetu na hufikia hatua kupoteza wafanyabiashara hawa kuendelea na biashara. Je, ni lini Wizara hii itaanza utatuzi wa kero hii kwa wafanyabiashara wote?



Swali la pili, Wizara itamaliza lini kero hii ya kutatua suala hili la kodi ya wafanyabiashara wanaotoka Zanzibar? (Makofi)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, utofauti huu unatokana na tatizo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutokutumia mfumo nilioutaja kwenye jibu langu la swali la msingi. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kuishawishi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kujiunga na mifumo inayotumika ndani ya Idara ya Forodha ili kuondoa changamoto hii inayowakumba wafanyabiashara wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niliambie Bunge lako Tukufu kwamba, progress ni nzuri na kwa kuanzia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika bajeti yake ya mwaka 2016/2017 imeridhia kutumia mfumo wa *Import Export Commodity Database* kwa bidhaa ya magari yatakayoingia Zanzibar ili kuweza kuondoa changamoto hii. Kwa hiyo, naona huu ni mwanzo mzuri. Tunaendelea kuishawishi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iweze kujiunga moja kwa moja kwa bidhaa zote zinazolingizwa Zanzibar na hatimaye kuletwa Tanzania Bara.

**NAIBU SPIKA:** Swali fupi, Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa Wilaya ya Lushoto ina Mjimbo matatu na Ofisi ya TRA ni moja tu kwa Majimbo yote matatu; je, ni lini Serikali itaipandisha hadhi Ofisi ya TRA, Lushoto na kutoa *TIN Number*, *Motor Vehicle* na *License* za udereva ili wananchi wasipate taabu ya kwenda mpaka Tanga Mjini? (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunajua Wilaya ya Lushoto ina Majimbo matatu na tuna Ofisi moja ya TRA.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimiwa Mbunge atakumbuka ndani ya wiki mbili zilizopita, nilijibu kuhusu ufunguzi wa Ofisi za TRA, lakini kwa kuwa tuna Ofisi ya TRA Lushoto, kinachohitajika ni kupandishwa hadhi; namuomba Mheshimiwa Mbunge tuonane ili tuweze kukaa pamoja na tuone ni jinsi gani sasa tutaweza kuipandisha hadhi ofisi hii ili huduma hizi muhimu ziweze kupatikana kwa ajili ya wafanyabiashara wetu. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Kibamba, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Sixtus Mapunda.

Na. 282

**Kuboresha Maslahi na Kujenga Kituo cha Polisi**

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA (K.n.y. MHE. JOHN J. MNYIKA)** aliuliza:-

Askari Polisi wa Kituo cha Polisi Wilaya ya Kimara wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu kwani kituo ni kidogo na maslahi yao yamekuwa duni:-

(a) Je, ni wapi na lini kituo kipya kitajengwa ili kuboresha huduma na usalama Jimboni Kibamba?

(b) Je, hatua gani zimechukuliwa kuboresha maslahi ya Askari hao ikiwa ni pamoja na kuwaongezea motisha?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA (K.n.y. NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Kibamba, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kipolisi Kimara ilianzishwa kufuatia kuundwa kwa Kanda Maalum ya Polisi Dar es Salaam chini ya Mpango wa Maboresho ya Jeshi la Polisi ya mwaka 2006 kwa lengo la kuboresha ufanisi na kuongeza huduma za ulinzi na usalama kwa wananchi. Kutokana na uhaba wa rasilimali fedha, huduma za polisi zilianza kutolewa katika jengo la kituo kidogo cha Polisi Mbezi Luis.

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo hilo halikidhi hadhi ya kuwa Kituo cha Polisi Wilaya na pia lipo kwenye hifadhi ya barabara kuu ya Morogoro. Serikali itajenga kituo kipya eneo la Luguruni muda wowote kuanzia sasa. Aidha, hali ya vitendea kazi imezidi kuboreshwa ambapo hivi karibuni Wilaya ya Kimara imepatiwa gari lingine lenye namba PT 3696 *Toyota Land Cruiser* kuimarisha ulinzi wa eneo hilo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha maslahi ya kuongeza motisha kwa askari wa Jeshi la Polisi, hivi karibuni Serikali imeongeza posho ya chakula, yaani *Ration Allowance* toka shilingi 180,000 hadi kufikia shilingi 300,000 kwa mwezi, kupandisha viwango vya mishahara sambamba na kuendelea kutoa huduma ya Bima ya Afya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sixtus Mapunda, swali la nyongeza.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kibamba na Ubungo katika ujumla wake ni Mji unaokua kwa kasi sana na ongezeko kubwa la watu linalohatarisha usalama wa mali na raia kitu ambacho Kituo cha Kibamba kinapochelewa kujengwa kinahatarisha usalama wa eneo hili. Serikali haioni umuhimu wa kulichukulia hili jambo katika udharura wake ili kituo kijengwe kwa haraka?

Pili, kwa kuwa tatizo la maslahi ya askari wa Kibamba na maeneo mengine hayatofautiani na yale ya Mbinga, Nyasa, Songea Vijijini, Namtumbo Tunduru na Madaba; haoni kuna ulazima sasa kwa Serikali kuboresha maslahi ya watumishi katika maeneo niliyoyataja ikihusisha fedha maalum kwa ajili ya *operation* za ulinzi na usalama pamoja na kuboresha makazi yao hususan maeneo ya kulala ili kusitiri utu wao? (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Muungano na Mazingira kwa niaba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA (K.n.y. NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza kuhusu Serikali haioni udharura wa kujenga? Kama nilivyosema ni kwamba Serikali inatambua sana umuhimu wa kuboresha hicho Kituo cha Polisi cha Kibamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba, tayari tumewaongezea gari la pili kwa kuzingatia umuhimu huo huo na nikasema kwamba wakati wowote ule, Serikali inatafuta fedha sasa hivi kwa ajili ya kuanza kujenga vituo vya polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukijibu hapa mara kwa mara kwamba sasa hivi tuna mpango kabambe wa kujenga nyumba za watumishi 4,136, ambazo zitaenda sambamba na ujenzi wa vituo vya polisi. Kwa hiyo, namuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tayari imeshachukuwa udharura wa suala hili na tutahakikisha kwamba tunajenga haraka sana iwezekanavyo ili kuweza kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo hayo ambayo yametajwa na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge na concern ya Wabunge wengi sana ni kusikia maslahi ya Polisi wetu, Askari wetu; Serikali imekuwa ikifanya jitihada nyingi sana za kuhakikisha kwamba maslahi ya polisi yameimarishwa. La kwanza, askari ambao hawana nyumba tumekuwa tukiwapatia *allowances* za pango za nyumba ili waweze kulipia gharama hizo ambazo ni asilimia 15 ya mishahara yao kwa ajili ya kulipia pango.

Mheshimiwa Naibu Spika la pili, tumekuwa tukiwalipia kwa mfano, utalaam maalum, *professional allowances*. Mtu ana utalaam maalum; ni askari, lakini dereva. Tunamlipa vilevile posho ya asilimia 15 ya mshahara wake, lakini vilevile kwa mfano, unakuwa Polisi umeajiriwa leo, lakini wewe labda ni *Doctor of Medicine*, tayari umeshakuwa daktari, lakini umeajiriwa polisi na una cheo cha chini, unapewa mshahara sawa na wa daktari kama kawaida bila kujali cheo chako. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kuna *hardship allowance* kwa wale ambao wanafanya kazi ngumu mnawajua ninyi, *FFU*, ambao kila mwezi nao tunawapa *allowances* ya shilingi 100,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bima ya Afya, askari anapomaliza tu mafunzo yake anakatiwa Bima ya Afya asilimia 100 na Serikali. Pia kuna suala lingine ambalo tumekuwa tukiwadhamini; wanapotaka mikopo kwenye taasisi za fedha pamoja na SACCOS, yote haya yamekuwa yakifanywa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la mwisho ambapo Serikali imeboresha maslahi ya Polisi kuyapandisha kuyatoa kwa maana ya *ration allowance* ilikuwa shilingi 180,000 sasa ni shilingi 300,000. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wanaweza kuona jinsi Serikali ambavyo inazidi kuboresha maslahi ya askari wetu ili wajisikie kwamba wanafanya kazi nzuri ya ulinzi wa Taifa lao.

Sasa ameuliza, mambo mengine ya kupata fedha kwa ajili ya ulinzi...

**NAIBU SPIKA:** Naomba ufupishe kidogo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani majibu yaliojibiwa kwa niaba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tumeridhika nayo. (Makofi)

Mheshimiwa Ally Saleh Ally, Mbunge wa Malindi, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Edward Mwalongo.

Na. 283

**Wastaafu wa Jeshi la Polisi Kutolipwa  
Haki zao kwa Wakati**

**MHE. EDWARD F. MWALONGO (K.n.y. MHE. ALLY SALEH ALLY)** aliuliza:-

Wapo askari polisi kadhaa ambao wamestaafu kwa zaidi ya miaka 20 sasa na wametumikia nchi kwa uadilifu na uzalendo, lakini hawajalipwa stahili zao; Serikali kwa mara ya mwisho iliwasiliana nao kupitia barua CAB/336/394/01/70 ya tarehe 28 Julai, 2015:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali haijawajibu barua yao zaidi ya miezi sita?

(b) Je, ni kwa nini suala hili halimalizwi kwa miaka yote ili wahusika wapate haki zao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA  
(K.n.y. NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wizari ya Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Saleh Ally, Mbunge wa Malindi lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, (a) siyo kweli kwamba wastaafu hawa hawajajibiwa kwa zaidi ya miezi sita, bali kumbukumbu zinaonyesha kuwa Jeshi la Polisi limeshawaandikia barua ya kuwajibu askari hao tangu tarehe 12/10/2015 yenye kumbukumbu namba PHQ/C.10/8A/VOL.9/90.

Mheshimiwa Naibu Spika, (b) suala hili halina utata wowote kwani wastaafu hawa hawana wanachodai Jeshi la Polisi kwani haki zao walishalipwa kulingana na mikataba yao, kwani walikuwa chini ya mkataba wa bakishishi (*gratuity*) ambao ulikuwa ni uchaguzi wao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwalongo, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba niulize swali dogo tu la nyongeza kwa maslahi ya Polisi wa Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi limekuwa likijishughulisha sana na kusaidia polisi, lakini hali ya polisi katika Mkoa wa Njombe ni mbaya sana. Mkoa huu umeanza mwaka 2012 na mpaka leo hawana nyumba hapa moja.

Je, Mheshimiwa Waziri atanihakikishia kwamba katika nyumba hizo 4,136 zipo zitakazo jengwa katika Mkoa wa Njombe? (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, kwa niaba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA (K.n.y. NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uanzishwaji wa mikoa mipya ikiwemo Njombe, Geita, Simiyu na Mkoa mpya wa Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba, Wizara yangu itahakikisha kwamba katika huu mpango kabambe tunaouzungumza mikoa mipya itapewa kipaumbele na nimhakikishie kwamba Njombe, makazi ya askari wetu pamoja na vituo vyetu vitaimarishwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani tuendeleo na matangazo kwa sababu muda wetu umekwisha, halafu Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwa anajibu kwa niaba ya Wizara ambayo ni ya watu wengine.

Waheshimiwa Wabunge, kuna matangazo ya wageni hapa, halafu nitaleta kwenu matangazo mengine. Tangazo la kwanza ni wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ambao ni wageni waliopo Jukwaa la Spika.

Kundi la kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango, wakiongozwa na Ndugu Dorothy Mwanyika ambaye ni Kaimu Katibu Mkuu Hazina; yupo pia Ndugu James Dotto ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Hazina; yupo Ndugu Amina Shaban - Naibu Katibu Mkuu, Hazina; yupo pia Ndugu Florence Mwanri - Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango; tunao pia Manaiibu Katibu Watendaji kutoka Tume ya Mipango, Makamishna kutoka Wizarani, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, Wakurugenzi na watumishi wengine wa Wizara, wote wasimame kwa pamoja, karibuni sana. (Makofi)

Kundi lingine ni wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango kutoka Mahakama, ambao ni Mheshimiwa Hussein Katanga - Mtendaji Mkuu wa Mahakama; Mheshimiwa Jaji Ferdinand Wambali - Mkuu wa Chuo cha Mahakama Lushoto; Mheshimiwa Katarina Revokati - Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania; Ndugu Mathias Mwangu - Mkurugenzi wa Mipango, Bajeti na Uratibu. (Makofi)

Pia tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge na kundi la kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu ambaye ni msaidizi wake anayetoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Busoro Pazi. (Makofi)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Josephine Genzabuke ambao ni Waheshimiwa Madiwani kutoka Kasulu Kibondo, ambao ni Mheshimiwa Asia Kasebo, Mheshimiwa Agnes Kanyamagenge na Mheshimiwa Jane Rulanyaga, karibuni sana. (Makofi)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Joseph Selasini ambaye ni mwanae anayesoma Mkoani Morogoro, ambaye ni Ndugu Erick Temba, karibu sana. (Makofi)

Mgeni wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambaye ni Ndugu yake kutoka Dodoma ambaye anaitwa Ndugu Leah Mwamoto, karibu sana. (Makofi)

Tunao pia wageni sita wa Mheshimiwa Mary Chatanda ambao ni watoto wake kutoka Mkoani Dar es Salaam, wamekuja kujifunza Bunge linavyoendeshwa; Ndugu Mohamed Jaffer, Ndugu Mohamed S. Mohamed, Ndugu Arif Khalifan, Ndugu Benjamin Bariki, Ndugu Jacklin Nyenza na Ndugu Moses Edward, karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 90 na walimu saba kutoka Shule ya Awali na Msingi ya Moga ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wanafunzi 73 kutoka Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohana (St. John's) kilichopo Mjini Dodoma. Sijawaona lakini nadhani labda wako getini. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, yapo matangazo mengine, tangazo mojawapo linatoka Sekretarieti ya Bunge Sports Club kwamba Wabunge wote mnatangaziwa leo saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Msekwa kutakuwa na Mkutano wa Bunge Sports Club utakaowashirikisha Wabunge na watumishi kwa ajili ya kufanya uchaguzi wa viongozi wa Bunge Sports Club. Nafasi zitakazogombewa ni Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Meneja wa Timu na Wajumbe wengine watano. Wabunge na watumishi wanaombwa kuhudhuria ili kukamilisha zoezi hilo kwa wakati. (Makofi)

Tangazo lingine ni la ibada; imeandikwa Ibada ya Misa. Nadhani ni tangazo la Misa Takatifu Kanisa Katoliki. Mheshimiwa Joseph Selasini, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mtakatifu Thomas Moore anawatangazia Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wakatoliki na wasio Wakatoliki kwamba leo tarehe 1 mwezi wa sita, saa 7.00 mchana baada ya kuahirishwa shughuli za Bunge, kutakuwa



na Misa Takatifu kwa Wakaristu wote. Mnakaribishwa, hajataja ukumbi, lakini nadhani baada ya kutoka hapa saa 7.00 pengine atakuwa maeneo ambayo tutaweza kumuona, pengine itakuwa rahisi waumini hawa Katoliki wakisogea sehemu zile za Ukumbi wa Pius Msekwa ili waweze kumuona Mwenyekiti wao.

Waheshimiwa Wabunge, tumepata taarifa na wengi wenu pengine mmeshazisikia; kuna mauaji mengine ya kutisha yametokea eneo la Tanga. Tunazo taarifa kwamba Naibu Waziri ametumwa hilo eneo ili akapate kuzungumza na Kamati za Ulinzi na Usalama kuhusu hayo maeneo ambayo mauaji yametokea na atulettee taarifa.

Sasa kwa sababu Waziri Mkuu yuko hapa na pia Waziri anayehusika na mambo ya Bunge, tunaomba Serikali itulettee hiyo taarifa kwa sababu mauaji yamekuwa yakitokea na mara nyingi tumekuwa tukiwasihi Serikali mtulettee, nadhani bado mnazitafuta. Tunaomba mfanye haraka mtulettee hizo taarifa kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wanahitaji kujua nini kinaendelea maana mauaji yanatokea maeneo mengi ya nchi. (Makofi)

Kwa hiyo, ni vizuri mtulettee taarifa iliyo kamili ili tuweze kujiridhisha kwamba Serikali inachukua hatua stahiki dhidi ya hawa watu wanaoua watu wasio na hatia. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo tunaendelea. Katibu!

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mwongozo wa Spika! Mwongozo!

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Katibu, naomba ukae. Mheshimiwa Martha Mlata.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Natumia Kanuni ya 68 (7), naomba nisisome ili tuokoe muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiti chako kimekuwa ni shahidi kwamba baadhi ya Mawaziri wanaojibu maswali hapo mbele wamekuwa wakitumia muda mwingi sana kujibu maswali, wanazunguka, hata wakati mwingine jibu lenyewe linalokuja wala siyo sahihi. Wakati huo wanatumia muda mwingi wa Waheshimiwa Wabunge hawa ili waweze kuuliza maswali mengine ya nyongeza, kwa hiyo, wanapoteza sana muda.



Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, tufanyaje ili wawe na majibu mafupi na Waheshimiwa Wabunge wengine waweze kupata nafasi ya kuuliza maswali na majibu yao yawe sahihi? Huwezi ukaulizwa kuhusu taa za *airport* unasema hakuna umuhimu kwa sasa na wakati watu wanahitaji kusafiri usiku na mchana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa Mwongozo na Mheshimiwa Martha Mlata, lakini kwa sababu mwongozo wake una sehemu mbili; sehemu ya kwanza ni majibu kuwa marefu, lakini sehemu ya pili ni majibu kwamba yametolewa kuhusu taa kwa namna ambavyo Mheshimiwa Martha Mlata ameelezea; kwa sababu hiyo itanitaka nikangalie Taarifa Rasmi za Bunge, nione swali lililoulizwa na jibu lililotolewa, mwongozo huo nitautoa hapo baadaye. (Makofi)

Mheshimiwa Kangi Lugola!

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mwongozo!

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naomba Mwongozo chini ya Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na haya uliyoyatolea maelezo hivi punde juu ya mauaji yanayotokea katika nchi yetu, nimelazimika niombe Mwongozo huu kwa sababu mauaji haya ambayo ni ya kupangwa yaani *organized crime* yaliyoanza kujitokeza katika Mkoa wa Mwanza na maeneo mengine; mambo haya Waheshimiwa Wabunge tumewahi kuiuliza Serikali kuhusu namna gani itaweza kukabiliana na wimbi hili ambalo limejitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kutuambia kwamba Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani sasa amekwenda Tanga kushughulikia jambo hili na wakati huo huo mambo ambayo yametokea Mwanza na maeneo mengine tulishaitaka Serikali ijaribu kutuambia nini kinaendelea na wana mikakati gani juu ya kukabiliana na mambo haya ambayo tunaamini ni sehemu ya ugaidi; kwa sababu wale waliofanya mauaji Tanga jana waliweza kunyang'anya vyakula wakarudi navyo kwenye Mapango ya Amboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ni dalili tosha kwamba haya mauaji ni ugaidi kwa sababu magaidi, ishara mojawapo ni kuvizia watu na kuwanyang'anya vyakula ama kwa kuwaua na kurudi sehemu zao waendeleo kufanya mauaji. Sasa tutaendelea katika hii hali ya kuambiwa kwamba sasa Naibu Waziri amekwenda Tanga na matokeo yake pia atakaporudi wanaendelea kukaa kimya halafu mauaji yanaendelea kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako, kwa nini kauli hizi za kusema wanafanyia kazi na matokeo yake hawaji hapa Bungeni, wanaingia mitini wanakuwa wa kutoa kauli tu?

Naomba Mwongozo, tabia hii ya Serikali kutoleta mrejesho Bungeni wa namna ambavyo wamefanyia kazi itaisha lini na mapema iwezekanavyo? (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Naona Mheshimiwa Waziri anataka kusimama, ngoja atoe maelezo halafu nitatoa Mwongozo.

Mheshimiwa Jenista Mhagama!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE WALEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu concern kubwa ya Waheshimiwa Wabunge lakini na hata Watanzania wote kwenye tatizo hili ambalo limekuwa likijitokeza mara kadhaa sasa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, umesema vyema, Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa maelekezo tayari ndani ya Serikali, Mawaziri wanaohusika na Naibu Waziri wetu wa Mambo ya Ndani alishakwenda Mwanza na toka jana yuko kule Tanga. Siyo kwamba ni jambo jepesi la kusimama tu kama Serikali na kutoa taarifa kwa mambo haya yanayotokea bila kuyafuatilia kwa undani na kujua nini ambacho kimejiri na nini ambacho Serikali inaweza kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile siyo sahihi, kwa mauaji hayo jinsi yalivyotokea, kuanza kusema tu ni mauaji ambayo yanashabihiana na suala la kigaidi, hapana. Mauaji yamekuwa yakitokea, tumekuwa tukikamata majambazi mbalimbali ambao wamekuwa wakifanya mambo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachoweza kulihakikishia Bunge lako Tukufu, Serikali tuachiwe tufanye kazi hiyo kama tulivyoanza kuifanya. Pale tutakapona kwamba tumeweza kujidhihirishia na kupata taarifa za kina kwa maagizo ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa akitupa tuyafanyie kazi, basi tutaweza kutoa taarifa ambayo itaeleweka kwa Watanzania wote na siyo kutoa taarifa ambayo haijakamilika na inaweza ikapotosha umma mzima na nchi nzima ya Tanzania bila kuwa na sababu ya msingi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wawe wavumilivu, wajue kwamba tunalifahamu na Serikali inajali kabisa suala hilo na ndiyo maana hata Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani amekuwa akikimbia kila eneo ambalo tatizo limekuwa likitokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumemsikia Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. Pia niliombwa Mwongozo na Mheshimiwa Kangi Lugola kuhusu mauaji yanayoendelea hapa nchini na ametaja maeneo ya mifano.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka wakati nikitoa maelezo baada ya kutoa tangazo, nimeionba Serikali kwamba itulettee taarifa kamili kuhusu hayo mauaji ya maeneo mbalimbali ambayo yote Waheshimiwa Wabunge tumeyasikia na mengine yametokea katika maeneo yetu ambayo tunawawakilisha wananchi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hiyo, Mheshimiwa Kangi Lugola na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla tuvute subira wakati Serikali inatayarisha hiyo taarifa mahsusi kwa ajili ya haya mauaji na namna pia wakati watakapoleta hiyo taarifa naamini watatujulisha namna gani wanajipanga ili haya mambo yasiendeleo kutokea kwa sababu sisi Wabunge lakini pia na wananchi tunatishwa na mambo haya.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea. Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

#### **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

##### **Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2016 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments*) Bill 2016)**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**NAIBU SPIKA:** Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

##### **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2016 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 2*) Bill 2016)**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Miswada ya Sheria miwili imesomwa kwa mara ya kwanza leo tarehe 01, Juni, 2016 ambayo ni Muswada

wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2016 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill 2016*) na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2016 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments No. 2) Bill 2016*). Baada ya hatua hiyo, Miswada hiyo sasa itapelekwa kwenye Kamati husika ili kujadiliwa.

Aidha, Waheshimiwa Wabunge mmewekewa nakala ya Miswada hiyo wenye visanduku vyenu vya nyaraka (*pigeonholes*). Hivyo mnaombwa mkaichukue ili muweze kuipitia na kujiandaa kutoa maoni yenu na kujitayarisha kwa ajili ya mjadala wa sheria hizi.

Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2016/2017 – Wizara ya Fedha na Mipango**

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Fedha na Mipango.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuanza hotuba yangu kwa kumshukuru Mungu kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2016/2017. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii adhimu kuwapongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushindi mkubwa walioupata katika Uchaguzi Mkuu wa tarehe 25 Oktoba, 2015. (*Makofi*)

Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa kwa kuchaguliwa na wananchi wa Jimbo la Ruagwa kwa kura nyingi kuwa Mbunge wao na hivyo kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa pamoja nawaombea afya njema viongozi wetu

hawa na hekima kutoka kwa Mungu katika kutekeleza majukumu yao chini ya kaulimbiu ya Hapa Kazi Tu kwa manufaa ya wananchi wote na hasa maskini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kulingoza Bunge letu Tukufu kwa busara na hekima. Aidha, nakupongeza pia wewe kwa kuteuliwa kuwa Mbunge na kuchaguliwa kuwa Naibu Spika na hivyo kumsaidia Mheshimiwa Spika kuendesha vyema shughuli za Bunge. Nawaombea Mungu awape afya na hekima ya kuendesha Bunge hili kwa manufaa ya Taifa kwa ujumla. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wa kuchaguliwa kuwakilisha wananchi wa Majimbo yenu na wote walioteuliwa kuwakilisha makundi maalum katika jamii yetu. Aidha, nawapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kumsaidia katika kuwaletia maendeleo Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani zangu pia za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuniamini na kuiteua kuwa Waziri wa Fedha na Mipango. Ninamwahidi Mheshimiwa Rais na Watanzania wote kwamba nitatekeleza jukumu hili kwa bidii na uadilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimshukuru Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Mbunge wa Kondo, kwa ushirikiano anaonipa kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi. Aidha, nawashukuru viongozi wa Wizara wakiongozwa na Dkt. Servacius Likwelile, Naibu Makatibu Wakuu, Dorothy Mwanyika, James Dotto na Amina Shaaban kwa hali yao ya kujituma katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

Vilevile napenda kuwashukuru Profesa Benno Ndulu - Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania; Alphayo Kidata - Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania; Bwana Lawrence Mafuru – Msajili wa Hazina; kwa kunisaidia kutekeleza majukumu yangu na kuongoza taasisi muhimu.

Aidha, nawashukuru Makamishna, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi, Wakuu wa Vitengo na wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kazi nzuri na ushirikiano wao mkubwa wanaonipatia kutekeleza majukumu ya kila siku. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo kwa

ushirikiano wao waliotupatia wakati wa kujadili mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaahidi kwamba tutaendelea kushirikiana na Kamati hii kwa lengo la kuleta ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Nawashukuru pia viongozi wa Mahakama lakini pia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri wanazozifanya kuendelea kusimamia mihimili hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuifikisha Tanzania kuwa nchi yenye kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Ili kufikia azma hii, ni muhimu kuwekeza katika viwanda kama ilivyosisitizwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wakati alipokuwa akizindua Bunge la Kumi na Moja, tarehe 20 Novemba, 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa anawasilisha hotuba yake katika Bunge lako Tukufu tarehe 25 Aprili, 2016, alielezea mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Tano na napenda kunukuu: "Malengo ya Serikali ya Kufikia kipato cha kati na kufanyika mapinduzi makubwa ya viwanda, yanategemea sana utulivu wa uchumi." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imejipanga kuchukua hatua madhubuti zinazolenga kujenga Taifa linalojitegemea kwa kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Moja ya hatua hizo ni kusimamia na kufuatilia kwa ukamilifu utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/2017 mpaka 2020/2021 ambao unajikita katika kujenga msingi wa uchumi wa viwanda na maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili mpango huu uweze kutekelezwa kwa ufanisi, ni dhahiri kuwa tutahitaji rasilimali za kutosha hususan rasilimali fedha. Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na wadau wengine, inalo jukumu la kuimarisha ukusanyaji wa mapato lakini pia kupanua wigo wa vyanzo vipya vya mapato na kusimamia kwa ufanisi matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato, Wizara itajielekeza kwanza, kusimamia matumizi ya vifaa na mifumo ya kielektroniki ili kuongeza ufanisi na kudhibiti upotevu wa mapato; lakini pia kurasimisha sekta isiyo rasmi kuingia katika mfumo wa kodi na hivyo kupanua wigo wa kodi; na kuimarisha ufuatiliaji wa mapato yanayokusanywa na taasisi na mamlaka mbalimbali. Tunalenga pia kuimarisha ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi na kuboresha usimamizi wake chini ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kuchukua hatua za kudhibiti na kupunguza misamaha ya kodi isiyo na tija na kuendelea kuimarisha usimamizi na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara bandarini na maeneo ya mipakani. Mikakati mingine ni kama inavyoonyeshwa katika kitabu cha hotuba yangu ukurasa wa saba hadi wa kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nieleze kidogo mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka huu wa fedha tunaomalizia 2015/2016.

Katika mwaka 2015/2016 majukumu ya Wizara yaliendelea kutekelezwa kupitia mafungu tisa ya kibajeti na taasisi na mashirika 35 yaliyo chini yake. Mafungu hayo ni Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango, Fungu 21 – Hazina, Fungu 22 - Deni la Taifa, Fungu 23 - Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha, Fungu 13 - Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu, Fungu 7 – Ofisi ya Msajili wa Hazina, Fungu 66 – Tume ya Mipango na Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu changu cha hotuba kuanzia ukurasa wa 12 mpaka wa 85 tumeeleza kwa kina mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya 2015/2016 kwa mafungu yote na taasisi na mashirika, lakini pia tumeelezea mafanikio, changamoto na hatua za kukabiliana na changamoto. Naomba maelezo hayo kama nilivyoyaeleza yapokelewe katika kumbukumbu rasmi za Bunge na yanukuliwe hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nieleze kwa kifupi malengo na mpango wa bajeti kwa mwaka 2016/2017. Kwanza ni majukumu ya Wizara; la kwanza, ni kubuni na kusimamia utekelezaji wa sera za uchumi kwa ujumla. Katika mwaka 2016/2017 Wizara imejipanga kuendelea kuimarisha Sera ya Fedha ili iendane na Sera ya Bajeti kwa lengo la kudhibiti na kupunguza mfumuko wa bei pamoja na tofauti kati ya riba za amana na zile za mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa uratibu wa mipango ya maendeleo, katika mwaka 2016/2017 Wizara imepanga kuendelea kuwaelimisha wadau mbalimbali kuhusu wajibu wao katika kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa miaka mitano, kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/2017 - 2017/2018, kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuchapisha, kusambaza na kuelimisha wadau mbalimbali kuhusu mwongozo wa usimamizi wa uwekezaji wa umma na shughuli hii inalenga kuimarisha taratibu za uibuaji, utekelezaji na usimamizi wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha kuwa miradi iliyoibuliwa inatekelezwa kikamilifu na kwa mafanikio makubwa.



Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu pia itaratibu mikakati ya kupunguza umaskini. Katika mwaka 2016/2017 Wizara imepanga kuandaa Mpango wa Kitaifa wa ufuatiliaji na tathmini wa jitihada za kuondoa umasikini ikiwemo viashiria vya kupima utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu. Mpango huu utasaidia kufuatilia utekelezaji wa programu za kuondoa umaskini katika sekta mbalimbali, kuibua changamoto na kurekebisha kasoro kila mwaka, kuandaa taarifa ya hali ya umaskini na maendeleo ya watu, kuanzisha Kituo cha Utunzaji na Utoaji Taarifa Mbalimbali kuhusu Programu za Kuondoa Umaskini na Maendeleo ya Watu, kuandaa mwongozo wa namna ya kuibua na kutumia fursa za kiuchumi katika maeneo yanayowazunguka wananchi katika Halmashauri, lakini pia kufanya tafiti mbalimbali kuhusu umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu pia itasimamia ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato katika mwaka 2016/2017, pamoja na mambo mengine Wizara imepanga kuendelea na mfumo wa dirisha moja la kielektroniki kati ya Mamlaka ya Bandari Tanzania na Mamlaka ya Mapato; kuendelea kudhibiti mizigo yote inayoingia kutoka bandari kavu zote; kuendelea kuimarisha mapato kwenye ushuru wa forodha na bidhaa; kuendelea kusimamia matumizi ya mashine za kielektroniki (*electronic fiscal devices*); kushughulikia kwa haraka rufaa za pingamizi za kodi; kufanya kaguzi kwa kuzingatia viashiria hatarishi vya uvujaji wa mapato ya Serikali; kusimamia misamaha ya kodi ili kuhakikisha inatolewa tu kwa wale wanaostahili na inatumika ipasavyo na pia kuendelea kutoa elimu ya walipa kodi kuhusu umuhimu wa kulipa kodi kwa maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa misaada na mikopo katika mwaka 2016/2017 Serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kupata fedha za nje za kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaelekeza fedha za nje katika kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo itakayochochea ukuaji wa uchumi sambamba na kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuimarisha usimamizi wa matumizi ya Serikali. Hata hivyo, azma ya Serikali ni kupunguza na hatimaye kuondokana na utegemezi wa kibajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo tumekubaliana kuwaleta washauri elekezi wa Kimataifa ili waweze kufanya tathmini ya ushirikiano wetu pamoja na namna ya kuendesha majadiliano. Lengo ni kuboresha ushirikiano wa maendeleo na kushauriana na Serikali juu ya njia nzuri zaidi ya kupokea fedha za nje ili ziweze kuwekezwa kwenye miradi ya maendeleo yenye kuleta ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa mwaka 2016/2017 imepanga pamoja na mambo mengine kuendelea kuandaa na kusimamia



utekelezaji wa bajeti ya Serikali inayojumuisha matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo, kuendelea kupitia mfumo wa uwasilishaji wa bajeti za Wizara, Idara za Serikali, Mikoa na Halmashauri na kuhakikisha kuwa Sera na Mipango ya Kitaifa na ile ya kisekta vyote vinaingizwa ipasavyo katika bajeti ya Serikali na kutengewa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kufanya tathmini ya bajeti ya Serikali kwa lengo la kuhakikisha kuwa inazingatia mahitaji ya makundi yote ya jamii; kuendelea kuimarisha mfumo ya kompyuta ya uandaaji bajeti ili kukidhi mahitaji ya taarifa mbalimbali zinazohitajika na kuendelea kujenga uwezo wa Wizara, Idara za Serikali Mikoa na Idara katika uandaaji wa bajeti ya muda wa kati. Usimamiaji wake na utoaji taarifa za utekelezaji ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji na tathmini kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017 Wizara yangu imepanga kuandaa na kukamilisha programu ya usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za Umma Awamu ya Tano kwa miaka mitano yaani 2017/2018 mpaka 2021/2022. Pia kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Serikali wa kada zinazohusiana na usimamizi wa fedha za umma, kufanya tathmini ya utekelezaji wa programu kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ili kupima mafanikio ya utekelezaji wa programu ya nne na kusimamia na kuratibu zoezi la upimaji wa mfumo ya fedha yaani *Public Expenditure and Financial Accountability* katika mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingine ambayo tutafanya ni kusimamia malipo. Katika mwaka 2016/2017 Wizara imepanga kuendelea kutoa udhamini wa masomo kwa Wahasibu, Wakaguzi, Wagavi na Wataalam wa Kompyuta kutoka Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ambao wako vyuoni; pia kusimamia mfumo wa *TISS* katika Halmashauri 58 zilizopo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Arusha, Tanga, Morogoro na Dodoma. Wizara imepanga kuendelea kusimamia, kuimarisha na kuboresha uendeshaji na uunganishaji wa mtandao wa malipo wa Serikali.

Aidha, Wizara imepanga kuunganisha mfumo wa malipo wa *EFT* katika Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kuunganisha Mfumo wa Uwasilishaji Mapato wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*Tanzania Revenue Gateway System*) na Mfumo wa Hazina (*The Treasury Revenue Accounting System*) kwa lengo la kupata taarifa za mapato ya kodi kutoka *TRA* kielektroniki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imepanga pia kufuatilia utekelezaji wa miongozo ya ukaguzi wa ndani, kukagua mfumo wa kuandaa bajeti, kufanya ukaguzi maalum kadiri ya mahitaji ya mlipaji Mkuu wa Serikali na wadau wengine na kuendelea kutoa mafunzo na kufanya ufuatiliaji wa miongozo

mbalimbali inayotolewa na Wizara kwa wakaguzi wa ndani wote na wadau mbalimbali wanaotumia miongozo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingine ambayo tutafanya katika mwaka ujao wa fedha ni kuendelea kulipa madeni mbalimbali yaliyokopwa na Serikali ili kugharamia miradi ya maendeleo nchini, pamoja na kuwasilisha michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Aidha, kwa kuwa malipo ya fidia kwa wafanyakazi waliokuwa wakipata ajali mahali pa kazi yalikuwa hayashughulikiwi ipasavyo na Mifuko iliyopo ya Hifadhi ya Jamii ambayo mingi ni ya pensheni, Serikali ilianzisha Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi na Wizara kwa mwaka 2016/2017 imepanga kuanza kuwasilisha mchango wa mwajiri kwenye Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi ili watumishi wa umma wakipata ajali mahali pa kazi waweze kulipwa na mfuko huo kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usimamizi wa mali za Serikali, katika mwaka 2016/2017 Wizara chini ya jukumu lake la kusimamia mali za Serikali imepanga kufanya uthamini wa ardhi na majengo ili kuwa na taarifa sahihi za mali za Serikali; kuendelea kuondosha mali chakavu, sinzia na zile zilizokwisha muda wake na kufanya uhakiki wa mali za watu binafsi zilizo chini ya ungalizi wa Serikali na zile zinazotokana na utaifishwaji kwa lengo la kuepuka ulipaji wa fidia usiokuwa wa lazima.

Aidha, Wizara itahakiki mali katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali ili kutoa ushauri wa kupunguza hasara zinazotokana na matumizi yasiyo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ununuzi wa umma, katika mwaka 2016/2017 Wizara kupitia Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini imepanga kutekeleza yafuatayo:-

- Kufanya mapitio ya Kanuni za Ununuzi wa Umma; kuandaa mwongozo wa utekelezaji wa shughuli za ununuzi wa Umma nchini; na
- Kuwajengea uwezo wadau mbalimbali wa ununuzi nchini juu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma na kukamilisha tathmini ya ufanisi wa Mfumo wa Ununuzi wa Umma Nchini.

Aidha, Wizara yangu imepanga kutekeleza Mpango wa Mafunzo wa Maafisa Ununuzi na Ugavi walioko katika Serikali Kuu na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kuwajengea uwezo juu ya usimamizi wa mikataba ya ununuzi; kutoa mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa Malipo wa EPICO9 kwa baadhi ya Maafisa, ununuzi na ugavi Serikalini pamoja na kuendelea kuhakiki taarifa za Maafisa

Ununuzi na Ugavi na kuziweka katika daftari la Maafisa Ununuzi na Ugavi Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingine zilizopangwa kufanywa na Wizara katika mwaka 2016/2017 ni pamoja na kukamilisha mfumo wa manunuzi kwa njia ya mtandao na kuanza kuutumia kwa majaribio kwa kwenye robo ya pili ya mwaka ujao wa fedha 2016/2017 kwa manunuzi ya dawa na vifaa tiba, pamoja na manunuzi ya bidhaa mtambuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuongeza uwezo wa watumiaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma kwa kufanya mafunzo kwa wanataaluma na wadau wengine ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti juu ya taaluma ya Ununuzi na Ugavi, utakaopelekea kutoa ushauri kwa Serikali kwenye maeneo ya taratibu na Sera za Ununuzi na Ugavi na kuongeza kiwango cha ufaulu wa watahiniwa toka kiwango cha sasa cha asilimia 42.8 hadi kufikia asilimia 50 kwa kuboresha mazingira ya kujifunzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017 Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini imepanga kuendelea na ununuzi wa magari kwa pamoja, kuongeza uwezo wa Wakala wa Kuhifadhi Mafuta kufikia wastani wa lita 50,000 kila Mkoa katika Mikoa ya Iringa, Kigoma, Mbeya, Morogoro na Mwanza, kuanza ujenzi wa ofisi, ghala na kisima cha mafuta katika Mikoa ya Geita, Katavi, Njombe na Simiyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini utaendelea na kazi ya kufunga mfumo wa udhibiti na usimamizi wa mafuta ya magari na mitambo katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa, Mbeya, Mwanza, Morogoro, Ruvuma, Singida na Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Ukaguzi wa Hesabu za Serikali katika mwaka 2016/2017 Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imelenga kuendelea kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2015/2016. Ukaguzi utaelekezwa katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ukaguzi utahusisha sekta ya mafuta na gesi na pia ukaguzi katika sekta ya madini utaimarishwa. Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi itaendelea kuimarisha uwezo wa kitaalamu kwa wakaguzi wake na kuendelea na ujenzi wa majengo ya Ofisi ya Taifa ukaguzi ili kuongeza uhuru wa wakaguzi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na tija zaidi ili kukidhi matakwa ya viwango vya Kimataifa vya taasisi za ukaguzi pamoja na Maazimio ya Kimataifa ya Lima na Mexico ambayo Tanzania imeyaridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usimamizi wa mashirika na taasisi za umma; K atika mwaka 2016/2017 Wizara yangu kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina, itaendelea kufanya uhakiki wa mali za taasisi na mashirika za umma zilizolingizwa katika daftari la mali; kufuatilia na kuhakiki mali za mashirika yaliyobinafsishwa ili kubaini mali ambazo hazikuingizwa kwenye orodha ambazo hivi sasa zinamilikiwa kinyume na sheria ili zirejeshwe Serikalini, kufanya utafiti wa taasisi ambazo zina vyanzo binafsi vya mapato kwa lengo la kuangalia uwezekano wa kuziondoa kwenye utegemezi wa ruzuku ya Serikali na kukamilisha maandalizi ya mfumo wa tathmini na ufuatiliaji kwa taasisi na mashirika ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017 shilingi trilion 1.14 zimetengwa kwa ajili ya kulipa mchango wa mwajiri kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Aidha, Wizara itaendelea kuboresha kumbukumbu za wastaafu ikiwa ni pamoja na kulipa pensheni kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu udhibiti wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi, katika mwaka 2016/2017, Wizara imepanga kuendelea kupokea na kuchambua taarifa za miamala shuku zinazohusu utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi. Lakini pia kuendelea kuwasilisha taarifa za intelegensia kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria kwa ajili ya uchunguzi; kukamilisha zoezi la kutathmini mianya na viashiria vya fedha haramu na ufadhili wa ugaidi nchini; kuendelea na utekelezaji wa mikakati ya kitaifa na kimataifa ya udhibiti wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi; na kuendelea na ukaguzi wa taasisi mbalimbali za fedha na zisizo za fedha ili kubaini kama sheria na miongozo ya kudhibiti utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili ugaidi inafuatwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017 Wizara kupitia Tume ya Pamoja ya Fedha imepanga kuendelea kufanya stadi ya uwekezaji katika mambo ya muungano. Stadi hii inalenga kubaini ushiriki wa pande mbili za Muungano katika uwekezaji kwa mambo ya Muungano. Aidha, Wizara inakusudia kufanya mapitio ya stadi zilizofanywa na Tume kuhusu mfumo bora wa kodi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni pamoja na uchambuzi wa masuala ya fedha yanayohusu mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha ujao, Wizara itaendelea kupokea na kuchambua miradi ya ubia kwa lengo la kuiidhinisha; kutoa ushauri kwa Wizara na Taasisi za Serikali katika kuchagua miradi bora ya ubia; kuziwezesha taasisi zenye miradi ya ubia kuajiri washauri elekezi pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa wadau mbalimbali kuhusu sera, sheria na kanuni za miradi ya ubia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka ujao wa fedha, Wizara yangu itaendelea kusimamia na kuratibu taasisi na mashirika ya umma yaliyoko chini ya Wizara, mipango na malengo ya bajeti kwa mwaka 2016/2017 kwa upande wa mashirika na taasisi za umma zilizo chini ya Wizara, ni kama inavyooneshwa katika kitabu cha hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 97 mpaka ukurasa 121.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nieleze makadirio ya mapato ya Wizara kwa mwaka 2016/2017. Kwanza makadirio ya mapato, katika mwaka 2016/2017 Wizara inakadiria kukusanya maduhuli kiasi cha shilingi bilioni 449.699 kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mauzo ya nyaraka za zabuni, kodi za pango, mauzo ya leseni za minada na mishahara isiyolipwa, gawio, marejesho ya mikopo na michango kutoka katika taasisi na mashirika ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kueleza mbele ya Bunge lako Tukufu, maombi ya fedha kwa matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango na taasisi zake, kwa mwaka ujao wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya fedha na mipango kwa mwaka 2016/2017 kupitia mafungu yote tisa ya kibajeti, inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 8,716,493,400,510 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 45.45 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi trilioni 8 na bilioni 671.04 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Kwa upande wa fedha za Maendeleo, Wizara ya Fedha na Mipango inaomba kuidhinishiwa shilingi 791,998,424,264 kati ya fedha hizo shilingi 723,150,000,000 ni fedha za ndani. Na shilingi 68,848,424,268 ni fedha za nje, mchanganuo kwa kila fungu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 50 Wizara ya Fedha na Mipango, katika mwaka ujao wa fedha fungu hili Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya Kawaida - shilingi 50,716,878,000 kati ya hizo mishahara shilingi 6,984,801,000, Matumizi Mengineyo ni shilingi 43,732,077,000; na

(b) Miradi ya Maendeleo, shilingi 26,035,591,500 na kati ya hizo, fedha z ndani ni shilingi 9,000,000,000 na fedha za nje Shilingi 17,035,591,500.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 21 - Hazina, katika kwa mwaka 2016/17, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya Kawaida shilingi 411,279,240,510 na kati ya fedha hizo, mishahara ya fungu hili ni Shilingi 4,474,752,000; matumizi mengineyo

shilingi 406,804,488,510 ambazo ni kwa ajili ya matumizi ya idara, taasisi zilizo chini ya fungu hili, pamoja na matumizi maalum; na

(b) Miradi ya maendeleo shilingi 740,155,523,400 na kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni shilingi 699,500,000,000, fedha za nje ni shilingi 40,655,523,400.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 22 - Deni la Taifa, katika fungu hili kwa mwaka 2016/17, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya Kawaida shilingi 8,009,341,187,000 kati ya hizo mishahara shilingi 9,340,716,000, matumizi Mengineyo ni shilingi 8,000,471,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali katika fungu hili kwa mwaka 2016/2017, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya Kawaida - shilingi 45,585,865,000, kati ya hizo mishahara ni shilingi 6,784,116,000 na Matumizi Mengineyo ni shilingi 38,801,749,000; na

(b) Kwa upande wa miradi ya maendeleo kwa fungu hili tunaomba shilingi 4,493,750,000 ambazo kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni shilingi bilioni mbili na fedha za nje ni shilingi 2,493,750,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 7 - Ofisi ya Msajili wa Hazina, katika mwaka ujao wa fedha, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya Kawaida shilingi 160,181,000,000 kati ya hizo mishahara ni shilingi 1,974,355,000, matumizi mengineyo s hilingi 158,206,645,000; na

(b) Miradi ya Maendeleo jumla shilingi 3,228,540,000 na kati ya hizo fedha za ndani ni shilingi 650,000,000 na fedha za nje shilingi 2,578,540,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 10 ni Tume ya Pamoja ya Fedha na katika fungu hili kwa mwaka 2016/2017, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya Kawaida shilingi 1,374,270,000 kati ya hizo mishahara shilingi 464,472,000 na matumizi mengine ni shilingi 909,798,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 13 ni Kitengo cha Udhhibiti wa Fedha Haramu, katika fungu hili kwa mwaka ujao wa fedha, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kwa Matumizi ya Kawaida shilingi 1,603,081,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Katika fungu hili kwa mwaka 2016/2017, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya Kawaida shilingi 32,373,096,000 kati ya hizo mishahara ni shilingi 13,870,774,000, Matumizi Mengineyo ni shilingi 18,502,322,000; na

(b) Kwa upande wa miradi ya maendeleo kwa fungu hili, fedha za nje ni shilingi 12,285,427,368 fedha za ndani ni shilingi 8,000,000,000 na fedha za nje ni shilingi 4,285,427,368.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 66 Tume ya Mipango, kwa mwaka wa fedha ujao 2016/2017 Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya kawaida shilingi 4,038,783,000 na kati ya fedha hizo mishahara ni shilingi 1,560,492,000 matumizi mengineyo shilingi 2,478,291,000. Kwa upande wa miradi ya maendeleo tunaomba shilingi 5,799,592,000 ambayo kati ya hizo fedha za ndani ni shilingi 4,000,000,000 na fedha za nje ni shilingi 1,799,592,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maombi ya fedha kwa mafungu tisa niliyoyataja ambayo yako katika aya ya 190 ya kitabu cha hotuba yangu, nichukue fursa hii pia kuwasilisha maombi ya fedha kwa mwaka 2016/2017 kwa ajili ya Mfuko wa Mahakama - Fungu 40 na Mfuko wa Bunge - Fungu 42.

Maombi haya ni kwa mujibu ya marekebisho yaliyofanyika kwenye kifungu cha 59(3) cha Sheria ya Utawala wa Mahakama, Sura 237 na kifungu cha 29(3) cha Sheria ya Utawala wa Bunge, Sura 115, kupitia Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015. Sheria hizi zinampa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kuwasilisha Bungeni maombi ya fedha za matumizi ya Mifuko hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia sheria hii, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishhe jumla ya shilingi 230,693,160,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mafungu haya mawili. Kati ya hizo, shilingi 176,931,426,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 53,761,734,000/= ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mafungu yote mawili. Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:-



Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 40 - Mfuko wa Mahakama, Katika fungu hili kwa mwaka 2016/2017, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya Kawaida shilingi 84,865,309,000 kati ya hizo mishahara ni shilinigi 50,345,775,000; matumizi mengineyo shilingi 34,519,534,000; na

(b) Miradi ya maendeleo shilingi 46,761,734,000; na kati ya fedha hizo fedha za ndani ni shilingi 24,000,000,000 na fedha za nje ni shilingi 22,761,734,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 42 - Mfuko wa Bunge, katika fungu hili kwa mwaka ujao wa fedha 2016/2017 Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Jumla ya matumizi ya kawaida, shilingi 92,066,117,000 kati ya hizo mishahara shilingi 23,798,609,000 na matumizi mengineyo shilingi 68,267,508,000 kwa upande wa miradi ya maendeleo fedha za ndani ni shilingi bilioni saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kuzishukuru nchi na mashirika mbali mbali ya kimataifa ambayo kwa namna moja au nyingine yamesaidia katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara. Napenda kuzishukuru nchi za Finland, Uingereza kupitia shirika la *DFID*, Canada, Denmark kupitia shirika lake ya *DANIDA*, Ireland, Japan kupitia *JICA*, Marekani, Norway, Sweden, Uholanzi na Ujerumani. Pia taasisi mbalimbali za Kimataifa ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia, *Global Fund*, Umoja wa Ulaya na mashirika ya Umoja wa Mataifa ya *UNFPA* na *UNDP*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru sana wafanyakazi na wananchi wote ambao wameendelea kulipa kodi kwa hiyari na pia kushiriki katika ujenzi wa Taifa letu. Ni imani yangu kuwa juhudi hizi zinazochukuliwa na Serikali yetu na wananchi zitatuwezesha kufikia malengo yetu ya kukuza uchumi na kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara [www.mof.go.tz](http://www.mof.go.tz).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO MHE. DKT. PHILIP I. MPANGO (MB.),  
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWAKA WA  
FEDHA 2016/2017 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

- 1. Mheshimiwa Spika,** kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2016/17.
- 2. Mheshimiwa Spika,** naomba kuanza hotuba yangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2016/17.
- 3. Mheshimiwa Spika,** napenda kutumia fursa hii adhimu kuwapongeza kwa dhati kabisa Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushindi mkubwa waliopata katika uchaguzi mkuu wa tarehe 25 Oktoba, 2015 na kuwawezesha kuongoza Taifa letu na Serikali ya Awamu ya Tano. Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Kassim M. Majaliwa kwa kuchaguliwa na wananchi wa Jimbo la Ruangwa kwa kura nyingi kuwa mbunge wao na hivyo kutoa fursa kwa yeye kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa pamoja, nawaomba afya njema na hekima kutoka kwa Mungu katika kutekeleza majukumu yao chini ya kaulimbiu ya “Hapa Kazi Tu” kwa manufaa ya wananchi wote na hasa masikini.
- 4. Mheshimiwa Spika,** naomba nikupongeze wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara na hekima. Aidha, nampongeza pia Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu kwa kuteuliwa kuwa mbunge na kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika na hivyo kukusaidia kuendesha vyema shughuli za Bunge. Nawaomba kwa Mungu awape afya na hekima ya kuendesha Bunge hili kwa manufaa ya Taifa kwa ujumla.
- 5. Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kuwakilisha wananchi wa majimbo yenu na wote walioteuliwa kuwakilisha makundi maalum katika jamii yetu. Aidha, nawapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri wote wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kumsaidia katika kuwaletea maendeleo Watanzania.

**6. Mheshimiwa Spika,** naomba pia nitoe shukrani zangu za dhiti kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuniamini na kuiteua kuwa Waziri wa Fedha na Mipango. Hivyo, kwa mara nyingine, ninamuahidi Mheshimiwa Rais na Watanzania kwa ujumla kwamba nitatekeleza jukumu hili kwa bidii, weledi na uadilifu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji – Mbunge wa Kondo, kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango. Nawapongeza pia Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali Dkt. Servacius Beda Likwelile, Naibu Makatibu Wakuu Ndugu Dorothy S. Mwanyika, Ndugu James Doto na Ndugu Amina Kh. Shaaban kwa kuteuliwa kwao katika nafasi hizo na ninawashukuru kwa kusimamia vyema kazi za kila siku za Wizara yangu. Pia napenda kuwashukuru Prof. Benno Ndulu, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Alphayo Kidata, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, Bw. Lawrence Mafuru – Msajili wa Hazina na Dkt. Albina Chuwa – Mtendaji Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa kunisaidia kutekeleza majukumu yangu vizuri na kuongoza taasisi muhimu wanazosimamia kwa weledi mkubwa. Aidha, nawashukuru Makamishna, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi, Wakuu wa Vitengo na wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kazi nzuri na ushirikiano wao mkubwa wanaonipatia.

**7. Mheshimiwa Spika,** napenda kutumia fursa hii, kuwashukuru Wenyevidi wa Bunge wote, kwa kuendesha majadiliano ya bajeti kwa mwaka 2016/17 kwa umakini. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini kwa kuchaguliwa kuongoza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti. Pia, natoa shukrani nyingi kwa Kamati yake kwa ushauri na mapendekezo ambayo yamesaidia sana kuboresha mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2016/17. Ninaahidi kwa dhiti kabisa kwamba tutaendelea kushirikiana na Kamati hii ili kuhakikisha Tanzania inafikia dhamira yake ya kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

**8. Mheshimiwa Spika,** hotuba yangu itajikita katika maeneo makuu matatu ambayo ni: Kwanza, ni Mwelekeo wa Majukumu ya Wizara katika Kujenga Msingi wa Uchumi Imara. Pili, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2015/16 na tatu, Malengo na Maombi ya Fedha kwa mwaka 2016/17.

## 2.0 MWELEKEO KATIKA KUJENGA MSINGI WA UCHUMI IMARA

**9. Mheshimiwa Spika,** azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuifikisha Tanzania kuwa nchi yenye kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Ili kufikia azma hii, ni muhimu kuwekeza katika viwanda kama ilivyosisitizwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wakati akizindua Bunge la 11 tarehe 20 Novemba, 2015.

**10. Mheshimiwa Spika**, wakati Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim M. Majaliwa (Mb), alipokuwa anawasilisha hotuba yake katika Bunge lako Tukufu mnamo tarehe 25 Aprili, 2016, alielezea mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Tano yenye falsafa ya HAPA KAZI TU nanukuu **“Malengo ya Serikali ya Kufikia kipato cha kati na kufanyika mapinduzi makubwa ya viwanda yanategemea sana utulivu wa uchumi”**, mwisho wa kunukuu.

**11. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imejipanga kuchukua hatua madhubuti zinazolenga kujenga Taifa linalojitegemea kwa kukuza uchumi na kupunguza umasikini. Moja ya hatua hizo ni kusimamia na kufuatilia kwa ukamilifu utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21. Mpango huu unajikita katika kujenga msingi wa uchumi wa viwanda na maendeleo ya watu.

**12. Mheshimiwa Spika**, ili mpango huu uweze kutekelezwa kwa ufanisi na kupata matokeo tarajiwa, ni dhahiri kuwa tutahitaji rasilimali za kutosha, hususan rasilimali fedha. Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na wadau wengine inalo jukumu la kuimarisha ukusanyaji wa mapato ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa rasilimali fedha. Aidha, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015- 2020 imeweka bayana majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango ya kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato, kupanua wigo wa vyanzo vipya vya mapato na kusimamia kwa ufanisi matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozombalimbali.

**13. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato, Wizara itajielekeza katika maeneo yafuatayo:- Kusimamia kikamilifu matumizi ya vifaa na mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato ili kuongeza ufanisi na kudhibiti upotevu wa mapato; Kurasimisha sekta isiyo rasmi kuingia katika mfumo wa kodi na hivyo kupanua wigo wa kodi na; Kuimarisha ufuatiliaji wa mapato yanayokusanywa na taasisi na mamlaka mbalimbali za Serikali ili kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Tunalenga pia kuimarisha ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi na kuboresha usimamizi wake chini ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kutokana na uzoefu na mifumo ya ukusanyaji iliyopo nchi nzima; Kuendelea kuchukua hatua za kudhibiti na kupunguza misamaha ya kodi isiyo na tija; na Kuendelea kuimarisha usimamizi na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara bandarini na maeneo ya mipakani ili kuhakikisha kwamba kodi stahiki zinakusanywa.

**14. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi, hatua ambazo zitachukuliwa ni pamoja na kuendelea kusimamia kikamilifu matumizi ya vifaa na mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato ili kuongeza ufanisi na kudhibiti upotevu wa mapato. Napenda

kutumia fursa hii kuaagiza kuwa, kuanzia mwaka ujao wa fedha ni lazima mfumo wa kieletroniki utumike katika utoaji wa risiti kwa tozo, faini, ada na malipo mengine yote ya Serikali kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wakala wote wa Serikali. Hii itahusisha pia malipo ya faini mahakamani, fainiza usalama barabarani, viingilio kwenye mbuga za wanyama, na vibali vya kuvuna maliasili. Maafisa Masuuli wote wanaelekezwa kusimamia utekelezaji wa agizo hili. Aidha, Serikali imeamua kufanya uthamini wa majengo kwa mkupuo ili kuongeza mapato yatokanayo na kodi ya majengo na usimamizi wake kuwa chini ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kuanzia mwaka ujao 2016/17.

**15. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kutambua mchango mkubwa wa sekta binafsi katika kukuza uchumi. Hivyo, Serikali itatoa fursa kwa sekta hii kushiriki kikamilifu katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa ushirikiano na Serikali. Kwa kutambua mchango mkubwa na umuhimu wa sekta binafsi katika kukuza uchumi, Serikali imedhamiria kushughulikia vikwazo mbalimbali kwa ufanyaji biashara na uwekezaji kwa nguvu zaidi.

**16. Mheshimiwa Spika,** Wizara itazingatia sheria, kanuni, taratibu, miongozo na kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya kudhibiti matumizi ya fedha za umma. Hii ni pamoja na kudhibiti matumizi ya Serikali yasiyo ya lazima kama vile safari za nje zisizo na tija, sherehe, warsha, semina, ununuzi wa magari na samani. Aidha, Wizara itaimarisha mfumo wa ununuzi wa pamoja wa bidhaa mtambuka Serikalini ili kupata bidhaa bora na thamani halisi ya bidhaa husika.

**17. Mheshimiwa Spika,** Wizara itaimarisha Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali kwa kumuongezea wataalam wenye weledi na taaluma mbalimbali ili kumwezesha kupata thamani halisi ya miradi, mifumo na programu mbalimbali za maendeleo. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia jukumu lake la msingi la kufanya kaguzi za ndani ili kuhakikisha kwamba kila taasisi inatumia rasilmali za umma kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo.

**18. Mheshimiwa Spika,** ili kuhakikisha uchumi unaendelea kuwa katika hali ya utulivu na kukua kwa kasi, uimara na uwezeshwaji wa sekta ya fedha unahitajika. Hivyo, mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Tano ni kudhibiti mfumuko wa bei ili uendelee kubaki kwenye tarakimu moja na hivyo kuzuia kasi ya kupanda kwa gharama za maisha; kudhibiti nakisi ya bajeti ili iendelee kushuka na kufikia kiwango kisichozidi asilimia 3 ya Pato la Taifa; Kusimamia deni la Taifa ili liendelee kuwa himilivu; kuhakikisha thamani ya shilingi ya Tanzania inatengamaa; Kuongeza thamani na mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi, kudhibiti matumizi ya fedha za kigeni na kuepuka kuagiza bidhaa zisizo za lazima kutoka nje ya nchi; na kuendelea

kuwa na mikakati itakayoweza kuwa na akiba ya fedha za kigeni zinazotosheleza kuagiza bidhaa na huduma nje bila ya matatizo.

**19. Mheshimiwa Spika**, sambamba na mikakati niliyoitaja hapo juu, majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango yatakatika kutekelezwa ili kufikia azma ya kujenga msingi wa uchumi imara na Taifa linalojitegemea ni pamoja na:-

- i. Kutoa dira na mwongozo wa uchumi wa Taifa;
- ii. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali;
- iii. Kusimamia Deni la Taifa;
- iv. Kufuatilia utekelezaji wa mipango ya kupunguza umaskini katika sekta mbalimbali;
- v. Kusimamia mali ya Serikali;
- vi. Kusimamia taasisi na mashirika ya umma;
- vii. Kusimamia Sera ya Ubia kati ya Serikali na sekta binafsi;
- viii. Kusimamia ulipaji wa mafao na pensheni kwa wastaafu;
- ix. Kudhibiti biashara ya fedha haramu pamoja na ufadhili wa ugaidi;
- x. Kuandaa, kusimamia na kutoa taarifa ya utekelezaji wa mipango ya kitaifa ya maendeleo; na
- xi. Kusimamia sera, sheria, kanuni na taratibu za uhasibu, ukaguzi wa ndani na ununuzi wa umma.

### 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2015/16

**20. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16, majukumu ya Wizara yaliendelea kutekelezwa kupitia mafungu tisa ya kibajeti na taasisi na mashirika 35 yaliyo chini yake (**Jedwali na.1**). Mafungu hayo ni Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango; Fungu 21 – Hazina; Fungu 22 - Deni la Taifa; Fungu 23 - Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali; Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha; Fungu 13 - Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu; Fungu 7 – Ofisi ya Msajili wa Hazina; Fungu 66 – Tume ya Mipango na Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

**21. Mheshimiwa Spika**, ili kufikia lengo kuu la kusimamia utekelezaji wa sera za uchumi jumla, Wizara katika mwaka 2015/16, pamoja na mambo mengine ilipanga kutekeleza yafuatayo:

- i. Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla;
- ii. Kuratibu Mipango ya Maendeleo ya Taifa;
- iii. Kuratibu Mikakati ya kupunguza Umaskini;
- iv. Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali;
- v. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali;
- vi. Kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za umma;



- vii. Kusimamia, kuimarisha na kuboresha uendeshaji na uunganishaji wa mtandao wa malipo ya Serikali;
- viii. Kuendelea kulipa madeni ya ndani na nje kwa wakati;
- ix. Kusimamia Mali ya Serikali;
- x. Kusimamia Ununuzi wa Umma;
- xi. Kukagua hesabu za Serikali;
- xii. Kuimarisha usimamizi wa mashirika na taasisi za umma;
- xiii. Kuendelea kuboresha huduma za pensheni kwa wastaafu na malipo ya mirathi;
- xiv. Kudhibiti fedha haramu na ufadhili wa ugaidi;
- xv. Kuishauri Serikali katika masuala ya fedha za Jamhuri ya Muungano yanayohusu matumizi ya kawaida katika Serikali zote mbili.
- xvi. Kupokea na kuchambua miradi ya ubia kati ya Serikali na sekta binafsi; na
- xvii. Kusimamia na kuratibu taasisi na mashirika ya umma chini ya Wizara;

### 3.1 Mapato kwa mwaka 2015/16

**22. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16, Wizara ilikadiria kukusanya maduhuli ya **shilingi bilioni 145.06** kutoka vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mauzo ya nyaraka za zabuni, kodi za pango, mauzo ya leseni za minada, gawio, marejesho ya mikopo na michango kutoka katika taasisi na mashirika ya umma. Hadi kufikia Machi, 2016 maduhuli yaliyokusanywa yalifikia **shilingi bilioni 129.92** sawa na asilimia 90 ya makadirio.

### 3.2 Matumizi ya Kawaida kwa mwaka 2015/16

**23. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16, Wizara ya Fedha na Mipango kwa mafungu yote Tisa iliidhinishwa matumizi ya kawaida jumla ya **shilingi 7,317,624,478,770 (bilioni 7,317.62)**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 49,810,799,642 (bilioni 49.81)** ni kwa ajili ya mishahara na **shilingi 7,267,813,679,128 (bilioni 7,267.81)** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ambapo kati ya hizo **shilingi 6,381,430,000,000 (bilioni 6,381.43)** ni Deni la Taifa. Hadi kufikia Machi, 2016 jumla ya **shilingi 4,612,762,849,799 (bilioni 4,612.76)** zilikuwa zimepokelewa na kutumika. Kati ya hizo, mishahara ni **shilingi 29,675,454,380 (bilioni 29.67)**, sawa na asilimia 60 ya fedha zilizoidhinishwa; na matumizi mengineyo ni **shilingi 4,583,087,395,419 (bilioni 4,583.1)**, sawa na asilimia 63 ya fedha iliyoidhinishwa (Jedwali Na.2).

### 3.3 Matumizi kwa Miradi ya Maendeleo mwaka 2015/16

**24. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa matumizi ya maendeleo, jumla ya **shilingi 1,031,758,764,000 (bilioni 1,031.76)** ziliidhinishwa kwa mafungu yote tisa ya Wizara. Kati ya fedha hizo, **shilingi 658,637,200,000 (bilioni 658.64)** ni fedha za ndani na **shilingi 373,121,564,000 (bilioni 373.12)** ni fedha za nje. Hadi



Machi, 2016, Wizara ilipokea na kutumia jumla ya **shilingi 21,806,498,320 (bilioni 21.81)**. Kati ya hizo fedha za nje ni **shilingi 19,128,298,320 (bilioni 19.13)** na fedha za ndani ni **shilingi 2,678,200,000 (bilioni 2.68)** (Jedwali Na.3).

### **3.4 UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2015/16:**

**25. Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza mapato na matumizi ya Wizara napenda sasa kuchukua fursa hii kuelezea kwa kina utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2015/16.

#### **3.4.1 Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla**

**26. Mheshimiwa Spika**, Wizara imesimamia utekelezaji wa Sera na Mikakati ya uchumi jumla zikiwemo Sera za Kibajeti na zile za Kifedha (Fiscal and Monetary policies) ili kuhakikisha kuwa uchumi wetu unaendelea kukua na hivyo kunufaisha wananchi walio wengi zaidi. Sera ya bajeti inalenga, pamoja na mambo mengine, kudhibiti na kupunguza mfumuko wa bei na hivyo kupunguza gharama za maisha ya wananchi.

#### **3.4.2 Uratibu wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa**

**27. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuratibu uandaaji na ufuatiliaji wa mipango ya maendeleo nchini sambamba na kusimamia uchumi. Ili kutekeleza majukumu hayo, Wizara imekamilisha uandaaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) na tayari umeidhinishwa na Bunge lako tukufu. Aidha, Wizara imeandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17. Mpango huu ni wa kwanza katika kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Mwaka 2016/17 – 2020/21.

**28. Mheshimiwa Spika**, mikakati maalum iliyozingatiwa katika Mpango wa Mwaka 2016/17 ni pamoja na:- Kuendelea kuandaa mazingira wezeshi kwa ushiriki wa sekta binafsi katika kugharamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo, hususan miradi ya viwanda; kushawishi sekta binafsi za ndani na nje ya nchi kushiriki katika kuibua na kutekeleza miradi ya maendeleo; Kutoa mwongozo kwa sekta binafsi kushiriki katika miradi kwa njia ya ubia na sekta ya umma na; Kuweka mikakati ya kuvutia uwekezaji wa kigeni wa moja kwa moja.

**29. Mheshimiwa Spika**, katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2015/16, Wizara imefanya uchambuzi wa maandiko ya miradi na taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kwa kila robo mwaka; na kufuatilia

utekelezaji wa baadhi ya miradi ya Kitaifa ya kinkakati. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Overseas Development Institute (ODI) iliendesha na kukamilisha tafiti kuhusu aina ya viwanda vitakavyopewa kipaumbele kwa kuzingatia fursa za Tanzania, kubaini malengo ya maendeleo ya viwanda kwa miaka 5 (2016/17 – 2020/21); maendeleo ya sayansi na teknolojia; na kubaini vyanzo vya mapato kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango. Tafiti hizo zimetumika kuboresha maandalizi ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21).

### 3.4.3 Uratibu wa Mikakati ya Kupunguza Umaskini

**30. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2015/16, Wizara iliendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa MKUKUTA-II ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya mikakati huo ambao baada ya kuongezewa muda wa mwaka mmoja wa utekelezaji, unafikia ukomo wake mwezi Juni, 2016. Matokeo ya tathmini hiyo yameainishwa katika Taarifa ya Utekelezaji wa MKUKUTA-II kwa kipindi cha Miaka Mitano (2010-2015). Taarifa hii ilisambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge wakati nilipowasilisha mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Pili (2016/17 - 2020/21) kwenye semina ya Waheshimiwa Wabunge mwezi Februari, 2016. Tathmini hiyo imetoa mchango mkubwa katika kubainisha vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo Awamu ya Pili ambao umejumuisha masuala ya kupambana na umaskini.

**31. Mheshimiwa Spika**, kwa ufupi, mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa MKUKUTA-II ni pamoja na kukua kwa pato la wastani la Mtanzania kutoka shilingi 770,464.3 mwaka 2010 kufikia shilingi 1,918,928 mwaka 2015; kuongezeka kwa kasi ya kupungua kwa umaskini wa kipato ambapo kati ya mwaka 2007 na 2012 umasikini ulipungua kwa asilimia 6.2, kutoka asilimia 34.4 hadi asilimia 28.2, ikilinganishwa na kupungua kwa kiwango cha asilimia 4.6 katika kipindi cha miaka 15, yaani kutoka asilimia 39 mwaka 1992 hadi kufikia 34.4 mwaka 2007.

**32. Mheshimiwa Spika**, umri wa mtanzania wa kuishi umeongezeka kutoka miaka 51 mwaka 2001 hadi miaka 61 mwaka 2012. Mafanikio hayo kwa pamoja yamechangia kupandisha Kipimo cha Maendeleo ya Binadamu (Human Development Index - HDI) kutoka asilimia 48.8 mwaka 2014 hadi asilimia 52 mwaka 2015.

### 3.4.4 Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali

#### (a) Mapato ya Ndani

**33. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16, Sera za Mapato zililenga kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya **shilingi bilioni 13,999.52**

(ikijumuisha mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa). Hadi kufikia Machi, 2016 jumla ya makusanyo ya ndani (ikijumuisha mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa) yalikuwa **shilingi bilioni 10,346.55** sawa na **asilimia 74** ya makadirio ya mwaka.

**34. Mheshimiwa Spika,** ili kuboresha ukusanyaji wa mapato ya kodi, Wizara imeingia mikataba ya kiutendaji na Mamlaka ya Mapato Tanzania kuanzia ngazi ya juu mpaka wasimamizi wa chini; kupitia TRA, Wizara imeendelea kuimarisha matumizi ya mashine za kielektroniki (EFD) ikiwa ni pamoja na kuanza kutoa mashine hizo bure kwa wafanyabiashara na kupiga marufuku Taasisi, Wakala wa Serikali, na Mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya biashara na wazabuni ambao hawatumii mashine hizo; kuboresha matumizi ya mfumo wa TANCIS pamoja na Mfumo Mmoja wa Ukadiriaji wa Thamani za Bidhaa; Kuwatambua walipa kodi kupitia taffiti mbalimbali na hatimaye kuwasajili; na Kutekeleza utaratibu wa ulipaji kodi kwa kutumia vitalu vya kodi.

**35. Mheshimiwa Spika,** hatua nyingine zilizochukuliwa ni pamoja na: kuwatambua na kuwasajili wajasiriamali walio kwenye sekta isiyo rasmi na kufuatilia mwenendo wa malipo yao; Kutekeleza mkakati wa ulipaji kodi kwa hiari; Kufanya utafiti kuhusu kodi za pango za majengo ambazo zinatoa mwelekeo wa kodi za mapato kutoka kwa wenye majengo ya biashara; Kutumia mifumo ya TEHAMA katika kusajili na malipo ya kodi; na uwasilishaji kwa njia ya kielektroniki wa Ritani za kodi ya ongezeko la thamani na miamala ya forodha. Aidha, Serikali ilikamilisha Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi ya mwaka 2015 yenye lengo la kuhakikisha kuwa matumizi ya mapato yatokanayo na mafuta na gesi yatasimamiwa ipasavyo kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

**36. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi Wizara imesimamia na kuhimiza utumiaji wa mfumo wa kielektroniki katika utoaji wa risiti kwa tozo, faini, ada na malipo mengine yote ya Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa na mawakala wote wa Serikali. Aidha, Wizara imeendelea kuhimiza uongezaji wa kufanya uthamini wa majengo mijini ili kuhakikisha ulipaji wa viwango stahiki; na kusimamia kwa karibu zaidi mashirika ya umma na wakala wa serikali ili kuhakikisha Serikali inapata gawio stahiki, matumizi yasiyo na tija yanaondolewa na mapato ya ziada yanachangia mfuko mkuu wa Serikali.

#### **(b) Misaada na Mikopo**

**37. Mheshimiwa Spika,** Wizara ililenga kuendeleza ushirikiano na wadau mbalimbali wakiwemo Washirika wa Maendeleo katika kutekeleza mipango ya maendeleo. Katika mwaka 2015/16, Washirika wa Maendeleo waliahidi

kuchangia bajeti ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi bilioni 2,322.5** ambapo misaada ya Kibajeti ni **shilingi bilioni 660**, Mifuko ya ksekta ni **shilingi bilioni 199** na miradi ya Maendeleo ni **shilingi bilioni 1,463**.

**38. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi, 2016 kiasi cha **shilingi bilioni 1,064.89** sawa na **asilimia 46** kimepokelewa. Kati ya kiasi hicho, Misaada ya kibajeti ni **shilingi bilioni 169.6** (sawa na asilimia 26 ya ahadi), Mifuko ya ksekta ni **shilingi bilioni 243.96** (sawa na asilimia 123 ya ahadi) na Miradi ya Maendeleo **shilingi bilioni 651.32** (sawa na asilimia 46 ya ahadi).

**39. Mheshimiwa Spika**, kupungua kwa misaada toka nje kunatokana na kujiondoa kwa baadhi ya Washirika wa Maendeleo wanaochangia kupitia Misaada na mikopo ya kibajeti na baadhi ya Washirika wa Maendeleo kupunguza ahadi zao. Wafadhili wanaochangia kupitia misaada ya kibajeti walipunguza michango yao kutoka **shilingi bilioni 660** mpaka **shilingi bilioni 399** katikati ya mwaka wa fedha 2015/16 na wengine kuhusisha utoaji wa fedha na masharti ambayo hayakuwemo katika makubaliano ya awali. Katika kushughulikia changamoto hizi, Serikali inaendelea na mazungumzo na Washirika wa Maendeleo ili kuhakikisha kwamba fedha zilizohidiwa zinatolewa kwa wakati.

#### **3.4.5. Uandaaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali**

**40. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu la Uandaaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, Wizara imeratibu uandaaji wa Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa Mwaka 2016/17 pamoja na Kitabu cha Taarifa ya Hali ya uchumi kwa mwaka 2015 na; kufanya marekebisha ya takwimu za Bajeti ya Mafungu mbalimbali kwenye mfumo wa IFMS na kuchapisha vitabu vya bajeti ya mwaka wa fedha 2015/16 (Juzuu Na. II, III & IV). Aidha, Wizara iliandaa, kuchapisha na kusambaza kitabu cha tafsiri rahisi ya Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2015/16 yaani "Citizens Budget"; na kuendesha mafunzo ya wakufunzi wa kitaifa wa Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015 na kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali kwa Mikoa 26, Halmashauri 182, pamoja na Wizara zote nchini.

**41. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha usimamizi wa bajeti hasa kwenye miradi ya maendeleo unazingatiwa, Wizara ilifanya ufuatiliaji wa fedha za Mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu; mapato na matumizi ya VETA; fedha za „Skills Development Levy kwa Mamlaka ya Elimu Tanzania. Aidha, Wizara ilihakiki madeni ya Shirika la Habari Tanzania (TBC), Kampuni ya magazeti Tanzania (TSN), Kampuni ya Simu (TTCL) yanayodaiwa katika Taasisi mbalimbali za Serikali na Shirika la kudhibiti nzige wa jangwani na nzige wekundu.

Wizara pia ilifanya ufuatiliaji wa fedha za SDL zilizotolewa kwenye mradi wa "Support Skills Development Project" kwa Wizara ya Kazi.

### **3.4.6. Usimamizi na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha za Umma**

**42. Mheshimiwa Spika,** katika kudhibiti matumizi ya fedha za umma, Wizara kupitia Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali imeendelea kufanya ukaguzi maalum katika Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali. Jukumu hilo limetekelezwa kwa kufanya uhakiki wa madai ya walimu na watumishi wasio walimu wa Serikali, watoa huduma ya chakula katika shule za msingi na sekondari za Serikali, madai ya Wakandarasi, Washauri, madai ya fidia, mirahaba na gharama za usimamizi wakati wa utekelezaji wa miradi ya barabara.

**43. Mheshimiwa Spika,** kaguzi nyingine zilizofanyika ni pamoja na ukaguzi maalum kuhusu matumizi ya fedha za umma katika kampuni ya Reli Tanzania (TRL), Ukaguzi maalum katika Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili (MOI), ukaguzi wa ununuzi na wa mikataba katika sekta ya umma, na Ukaguzi maalum wa kuthibitisha deni la ujenzi wa Jengo la Hospitali ya MOI (MOI Phase III). Matokeo ya kazi hizi yameiwezesha serikali kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 482.28 iwapo madeni hayo yangelipwa bila kuhakikiwa. Wizara imeendelea kutoa mapendekezo mbalimbali yanayotokana na matokeo ya kazi za ukaguzi maalum na kuwasilisha kwa Maafisa Masuuli kwa ajili ya kuchukua hatua stahiki.

**44. Mheshimiwa Spika,** Wizara pia inaendelea kufanya ukaguzi wa mfumo wa malipo ya mishahara katika taasisi za Serikali; na ukaguzi wa kiufundi katika miradi kumi ya maendeleo katika mikoa ya Mbeya na Iringa. Miradi hii inahusisha majengo, barabara, maji na umwagiliaji. Miradi hiyo ni; nyumba 6,064 za watumishi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, ujenzi wa hifadhi ya nyayo za kale huko Ngorongoro, mfumo wa maduhuli wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), na jengo la ofisi za kanda ya ziwa ya Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA). Wizara pia imefanya ufuatiliaji wa mapendekezo yaliyotolewa kwenye taarifa za ukaguzi wa ndani pamoja na ufuatiliaji wa mapendekezo ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali.

**45. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma imetoa mafunzo ya muda mfupi juu ya usimamizi wa fedha za umma na maboresho kwa watumishi wa kada za uhasibu, ugavi, ukaguzi, na mfumo ya TEHAMA kwa lengo la kuboresha utendaji; na imeratibu na kusimamia zoezi la Upimaji wa Mifumo ya Fedha (Public Expenditure and Financial Accountability - PEFA) katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Wizara imeratibu na kusimamia Mpango Maalum wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

pamoja na; Kuratibu na Kusimamia Maboresho ya Usimamizi wa Fedha kwa Upande wa Zanzibar hasa Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mamlaka ya Mapato Zanzibar na Wizara ya Fedha ya Zanzibar.

### **3.4.7. Usimamizi wa Malipo**

**46. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kudhamini mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 238 wa kada ya uhasibu, ugavi, uchumi na kompyuta kutoka kwenye wizara, Idara za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Manispaa, Halmashauri za miji; na Watumishi wapatao 650 wa kada ya uhasibu wamepatiwa mafunzo ya kutayarisha hesabu kwa kutumia viwango vya kimataifa vya Uhasibu (IPSAS Accrual). Aidha, Mfuko wa Bunge umeunganishwa kwenye Mtandao wa Malipo wa kieletroniki wa TISS pamoja na EFT; Malipo ya Mirathi (Death Gratuity) yameunganishwa kwenye mfumo wa "Electronic Fund Transfer". Mfumo huu umewezesha malipo kuingizwa kwenye akaunti za benki za warithi moja kwa moja na hivyo kuharakisha malipo. Wizara imeendelea kusimamia uendeshaji mtandao wa malipo wa Serikali (Integrated Financial Management System – IFMS) kwa kutoa ushauri wa kitaalamu na kuziwezesha Idara/Wizara za Serikali pamoja na Mikoa kutumia mtandao kwa ufanisi. Pia kutatua matatizo ya kiufundi pale yanapotokea.

### **3.4.8. Deni la Taifa**

**47. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kusimamia Deni la Taifa kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada SURA 134. Aidha, msisitizo umewekwa kukopa mikopo yenye masharti nafuu ambayo inakopwa kwa uangalifu na kutumika kwenye miradi yenye vichocheo vya ukuaji wa uchumi, ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, ujenzi wa mitambo ya kufua umeme na ujenzi wa viwanja vya ndege.

**48. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2015/16, Serikali ilitenga shilingi bilioni 504.57 kwa ajili ya kulipa riba ya deni la nje. Hadi Machi, 2016 shilingi bilioni 414.66 sawa na asilimia 82 zilitumika kwa ajili hiyo. Aidha, Serikali ilitenga shilingi bilioni 899.89 kwa ajili ya kulipa riba ya deni la ndani. Hadi Machi, 2016 shilingi bilioni 547.88 sawa na asilimia 61 zilitumika kwa ajili hiyo.

**49. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2015/16 Serikali ilitenga pia shilingi bilioni 421.20 kwa ajili ya kulipa mtaji wa deni la nje. Hadi Machi, 2016 shilingi bilioni 395.90 sawa na asilimia 94 zilitumika kwa ajili hiyo. Aidha, Serikali ilitenga shilingi trilioni 2.7 kwa ajili ya kulipa mtaji wa deni la ndani. Hadi Machi, 2016 shilingi trilioni 1.86 sawa na asilimia 69 zilitumika kwa ajili hiyo.



### 3.4.9. Usimamizi wa Mali ya Serikali

**50. Mheshimiwa Spika,** katika jukumu la usimamizi wa mali ya Serikali, Wizara imefanya uthamini wa ardhi, majengo na mali nyingine za Serikali ambapo taasisi kumi zinaendelea kufanyiwa uthamini; Kuondosha mali chakavu katika Wizara na Idara za Serikali ambapo jumla ya shilingi bilioni 2.06 zilikusanywa kutokana na mauzo ya magari na vifaa chakavu; na vibali vya uondoshaji wa mali chakavu vilivyokuwa na thamani ya shilingi bilioni 1.68 vilitolewa kwa mamlaka na taasisi mbalimbali za Serikali.

### 3.4.10. Ununuzi wa Umma

**51. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2015/16 Wizara imepitia Sheria ya Ununuzi wa Umma Na.7 ya Mwaka 2011 na kupendekeza marekebisho ya sheria hiyo; Kukamilisha uandaaji wa Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma na mkakati wa utekelezaji wake; Kuanza kutekeleza mpango wa mahitaji ya mafunzo wa maafisa ununuzi na ugavi kwa kuwajengea uwezo wa namna ya kupunguza vihatarishi katika ununuzi wa umma; Kuhakiki taarifa za maafisa ununuzi na ugavi na kuziweka katika daftari la maafisa ununuzi na ugavi Serikalini pamoja na kukamilisha maandalizi ya kufanya tathmini ya ufanisi wa mfumo wa ununuzi wa umma nchini.

**52. Mheshimiwa Spika,** katika usimamizi wa ununuzi wa umma, Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma imefanya uchunguzi katika zabuni 26 zinazohusu manunuzi yaliyofanywa na taasisi mbalimbali za umma. Kati ya hizo, taarifa za uchunguzi wa zabuni 18 zimekamiliika na kuwasilishwa kwenye mamlaka husika, na zabuni 8 zilizobaki bado zinaendelea kufanyiwa uchunguzi. Aidha, Wizara imefanya ukaguzi wa taratibu za utoaji wa zabuni na utekelezaji wa miradi na mikataba itokanayo na ununuzi wa umma kwa taasisi 126, zikiwemo Wizara na Idara zinazojitegemea 23, mashirika ya umma 36 na Serikali za Mitaa 67. Ukaguzi huu umehusisha jumla ya mikataba 5,206 yenye thamani ya shilingi bilioni 420.01. Maeneo yaliyobainika kuwa na upungufu kwa ukaguzi uliofanyika ni katika usimamizi wa mikataba, utunzaji wa nyaraka, utumiaji wa mfumo wa uwasilishaji wa taarifa za ununuzi kwa njia ya kieletroniki pamoja na kushughulikia malalamiko ya wazabuni.

**53. Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya kaguzi katika miradi ya ujenzi 385 inayotekelezwa na taasisi 126. Miradi hiyo imejumuisha barabara, madaraja, majengo, ukarabati wa reli, ununuzi wa vifaa pamoja na huduma za Washauri Waelekezi. Maeneo yaliyobainika kuwa na upungufu ni pamoja na ukosefu wa michoro na usanifu (design and drawings), malipo ya ziada kwa kazi ambazo hazikufanyika, kuzidisha vipimo vya kazi husika, kutoteua wasimamizi wa miradi, kutoandaa taarifa za utekelezaji wa



miradi na kutoambatanisha hati za malipo na vipimo halisi (payment certificates and measurement sheets) ili kuthibitisha uhalali wa malipo husika.

**54. Mheshimiwa Spika,** Wizara imezifungia jumla ya kampuni 21 (pamoja na wakurugenzi wake), kushiriki katika zabuni zinazohusu manunuzi ya umma kwa kipindi cha mwaka mmoja. Asilimia 90 ya kampuni zilizofungwa (kampuni 19) ilisababishwa na kutotimiza masharti ya mkataba katika utekelezaji wa miradi husika na asilimia 10 iliyobaki (kampuni 2) zilifungwa kutokana na kuwasilisha nyaraka zisizo halali wakati wa mchakato wa zabuni.

**55. Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza matumizi ya TEHAMA katika usimamizi wa ununuzi nchini, Wizara imeendelea kupokea taarifa za manunuzi kutoka kwa taasisi nunuzi 388, kati ya 475 zilizounganishwa kwenye mfumo wa utunzaji wa taarifa za manunuzi, yaani „Procurement Management Information System . Aidha Wizara imeufanyia maboresho mfumo huu ili kurahisisha zaidi shughuli za ununuzi nchini, ikiwa ni pamoja na kuwawezesha wakaguzi wa ndani wa taasisi zote za umma kuutumia mfumo katika kutoa taarifa za utekelezaji wa sheria ya manunuzi kwenye taasisizao.

**56. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Mamlaka ya Rufaa za Zabuni za Umma iliendelea kusikiliza na kutatua mashauri yanayotokana na ununuzi wa umma. Hadi Machi, 2016 jumla ya mashauri 30 yalipokelewa. Kati ya hayo, mashauri 18 walalamikaji walishinda, mashauri 11 Serikali ilishinda na lalamiko moja lilifutwa na mlalamikaji.

**57. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha huduma ya ununuzi Serikalini, Wizara kupitia Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini iliendelea na utaratibu wa kununua magari kwa pamoja kwa lengo la kupunguza gharama. Hadi Machi, 2016 Serikali imefanikiwa kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 16.61 kwa kununua magari 551 kwa kutumia utaratibu huu. Aidha, Wizara imeongeza uwezo wa Wakala wa kuhifadhi mafuta kwa kujenga kituo kipywa katika Wilaya ya Ileje mkoani Mbeya chenye ujazo wa lita 50,000. Wizara imetoa mafunzo kwa taasisi 11 katika mkoa wa Dar Es Salaam kuhusu namna ya kutumia mfumo wa udhibiti wa usimamizi wa mafuta ya magari na mpaka sasa taasisi tatu ambazo ni PPRA, PSPTB na GPSA zimeanza kutumia mfumo huu.

**58. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi imesajili jumla ya Wataalamu 1,735 wa fani ya ununuzi na ugavi kati ya wataalam 1,250 iliyokusudia kusajili kwa mwaka 2015/16. Hadi kufikia Machi, 2016 jumla ya wataalam waliosajiliwa na Bodi katika ngazi mbalimbali imefikia 5,187. Aidha, Bodi iliendesha mitihani ya taaluma ya ununuzi na ugavi katika ngazi mbalimbali ambapo kwa mwaka 2015/16, jumla ya watahiniwa 1,651

walifanya mitihani na watahiniwa 707 sawa na asilimia 42.8 walifaulu. Vilevile, Bodi ilizindua mitaala mipya ya mafunzo ya taaluma ya ununuzi na ugavi ambapo itaanza kufundishwa mwaka 2016/17.

**59. Mheshimiwa Spika,** majukumu mengine yaliyotekelezwa na Bodi ni pamoja na:- Kufanya ukaguzi wa wanataaluma wenye sifa za kufanya kazi za ununuzi na ugavi kwa mujibu wa matakwa ya Sheria kwenye taasisi 50 katika mikoa ya Mwanza, Mbeya na Lindi; na kukamilisha marekebisho ya Kanuni Na.GN.364 na GN.365 za mwaka 2009 ili ziendane na marekebisho ya sheria Na. 23 ya mwaka 2007 ili kuleta ufanisi katika utendaji kazi wa Bodi.

**60. Mheshimiwa Spika,** Bodi imefanikiwa kusajiliwa na taasisi ya kimataifa ya "International Federation of Purchasing and Supply Management" na kupata – "Global Standards Certification". Hili limefanikiwa baada ya uchambuzi uliofanywa wa mitaala ya Bodi kuonekana imekidhi vigezo vya usajili huo wa kimataifa. Hii inafanya wataalamu wanaofanya mitihani ya Bodi na kufaulu kupata sifa ya kukubalika kimataifa, hivyo kuwa na nafasi kubwa ya ushindani katika soko la ajira ndani na nje ya nchi.

### **3.4.11. Ukaguzi wa Hesabu za Serikali**

**61. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Ofisi ya Mdhidhi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ilifanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2014/15 kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Wizara ilifanya ukaguzi wa hesabu za Wizara na Idara za Serikali zinazojitegemea 63, mikoa 25 ya Tanzania Bara; Wakala za Serikali 32, Mifuko maalum na Taasisi nyingine za Serikali 45, Balozi 34 za Tanzania nje ya nchi, na hivyo kufanya jumla ya Taasisi zote zilizokaguliwa chini ya Serikali Kuu kufikia 199. Ukaguzi mwingine ulifanyika kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa 164 na Mashirika ya Umma 102 kati ya Mashirika 186.

**62. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa miradi ya maendeleo, jumla ya ripoti 799 za ukaguzi zimetolewa. Miradi hii ni ile inayofadhiliwa na Benki ya Dunia, na ile inayogharamiwa kwa fedha za maendeleo za ndani. Aidha, katika ukaguzi wa ufanisi, jumla ya ripoti 11 zimetolewa katika kipindi kilichoishia Machi, 2016. Kwa ujumla, ukaguzi uliofanyika katika mwaka wa fedha 2014/15 umewezesha kutolewa Ripoti kuu 5 ambazo zimewasilishwa kwenye Bunge lako hili tukufu, tarehe 25 Aprili, 2016. Ripoti hizo ni muhtasari wa jumla ya ripoti 1,275 zilizotolewa kwa kipindi cha mwaka 2014/15.

**63. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeendelea kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti za ukaguzi wa fedha zilizotolewa miaka iliyopita. Katika kipindi hicho kulikuwa na mapendekezo 99 yaliyotolewa kwa Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa, na Mashirika

ya Umma. Kati ya hayo, yaliyotekelezwa ni 35 sawa na asilimia 35. Aidha, utekelezaji wa mapendekezo 11 bado haujaanza na wa mapendekezo 53 unaendelea. Kwa ujumla, Mashirika ya Umma yametekeleza mapendekezo yote yaliyotolewa. Aidha, Serikali Kuu imeonesha juhudi nzuri katika utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kwa kuwa ni asilimia mbili tu ya mapendekezo ndiyo yaliyokuwa hayajatekelezwa. Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeonekana kutotekeleza mapendekezo hayo kwa kiwango cha asilimia 63. Kwa upande wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kwenye ripoti za ukaguzi wa ufanisi, kati ya mapendekezo 113 yaliyotolewa mapendekezo 29 yalitekelezwa, 68 yapo kwenye hatua za utekelezaji; na 16 hayajatekelezwa.

**64. Mheshimiwa Spika,** matokeo ya ukaguzi uliofanyika katika mwaka 2014/15 umeonesha kuwa, kati ya taasisi 1,264 zilizokaguliwa, hati safi zilizotolewa ni 1,065; hati zenye shaka 194; hati zisizoridhisha 4; na hati mbaya 2. Aidha, kati ya hati safi 1065 zilizotolewa, hati 739 zilihusu miradi ya maendeleo. Vilevile, hati zenye shaka 60 zilitolewa kwenye miradi ya maendeleo. Hakuna miradi iliyopata hati zisizoridhisha au hati mbaya. Serikali Kuu ilipata jumla ya hati safi 180, hati zenye shaka 18, hati isiyoridhisha moja, na haikupata hati mbaya. Mamlaka za Serikali za Mitaa zilipata hati safi 47, hati zenye shaka 113, hati zisizoridhisha 3 na hati mbaya moja. Aidha, Mashirika ya Umma yalipata hati safi 99, hati zenye shaka 3, na hakuna hati isiyoridhisha wala hati mbaya.

### 3.4.12. Usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma

**65. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ina jukumu la kusimamia rasilimali za Serikali kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali kwa ujumla. Rasilimali hizi ni pamoja na uwekezaji wa Serikali katika hisa za Mashirika ya Umma na ya Binafsi. Aidha, katika kutekeleza jukumu hili, Wizara husimamia utendaji wa Mashirika na Taasisi za Umma na kutoa ushauri kwa Serikali juu ya uwekezaji wake na nini kifanyike ili kuimarisha uendeshaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma yanayosimamiwa na Wizara yapatayo 216.

**66. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza jukumu hili, Wizara kwa mwaka 2015/16 imekamilisha Taarifa ya uwekezaji wa Serikali kwenye Mashirika na Taasisi za Umma na kuiwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali - CAG; Kukirejesha kwenye umiliki wa Serikali Kiwanda cha General Tyre kwa kununua hisa za mbia; Kukamilisha uhakiki wa madai wa waliokuwa watumishi kwenye mashirika yaliyobinafsishwa; Kufanya Ukaguzi wa Kimenejimenti kwenye Taasisi nne ambazo ni Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere – Kivukoni, Shirika la Elimu - Kibaha, Bodi ya Kahawa Tanzania na Chuo cha Ubaharia – Dar Es Salaam ambapo taarifa ya kaguzi hizo zimeandaliwa.

**67. Mheshimiwa Spika,** Wizara pia ilifanya uperembaji (Monitoring and Evaluation) kwenye Taasisi na Mashirika ya Umma 55 yaliyobinafsishwa kwa lengo la kukagua ufanisi na kuhakiki utekelezaji wa masharti kulingana na mikataba ya ununuzi kwa mujibu wa agizo la Mheshimiwa Rais wakati wa ufunguzi wa Bunge la 11. Baadhi ya mashirika hayo ni Mwanza Textile, Shinyanga Meat, Ilemela Fisheries, Manawa Ginneries, Blanket Manufacturing, Mtwara Cashewnut Factory, Likombe Cashewnut, Newala I Cashewnut Factory, Newala II Cashewnut Factory, Mtama Cashewnut Factory, Mufindi Pyrethrum Factory, TTA Dabaga, Mufindi Tea Company, Ludodolelo Pyrethrum Factory na Mahenye Farm.

### **3.4.13. Mafao ya Wastaafu na Mirathi**

**68. Mheshimiwa Spika,** Dhana ya msingi ya sekta ya hifadhi ya jamii imejikita katika kuhakikisha kuwa wananchi wanawezeshwa kuishi maisha yenye staha kwa kupata huduma za msingi katika vipindi vya uzee, kifo, maradhi, ukosefu wa kazi, uzazi na hali nyingine itakayosababisha mtu asiweze kufanya shughuli za kujiongezea kipato. Serikali kwa kutambua mchango mkubwa uliotolewa na wastaafu katika ujenzi wa Taifa imeendelea kuboresha huduma ya malipo kwa wastaafu, kwa kulipa pensheni moja kwa moja kwenye akaunti zao kwa kutumia mfumo wa TEHAMA wa Benki Kuu ya Tanzania uitwao TACH kuanzia mwezi Mei, 2015. Aidha kumbukumbu za wastaafu zimeendelea kuhifadhiwa kwenye mfumo wa TEHAMA unaoitwa SAPERION ambapo hadi Machi, 2016 kumbukumbu za wastaafu 66,666 zilikuwa zimewekwa kwenye mfumo huo.

**69. Mheshimiwa Spika,** Kwa kutambua umuhimu huo wa hifadhi ya jamii kwa watumishi wa Umma na kwa kuzingatia sheria na kanuni za mifuko ya hifadhi ya jamii, Wizara hadi Machi, 2016 iliwasilisha mchango wa mwajiri kiasi cha shilingi bilioni 274.0.

### **3.4.14. Udhibiti wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi**

**70. Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2015/16 Wizara kupitia Kitengo cha Kudhibiti Utakasishaji wa Fedha Haramu imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Udhibiti wa Utakasishaji wa Fedha Haramu. Hadi kufikia Machi, 2016 Wizara imepokea na kuchambua taarifa 164 za miamala shuku inayohusu fedha haramu na ufadhili wa ugaidi. Kati ya hizo, taarifa 52 za kiintelijensia ziliwasilishwa kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria kwa uchunguzi. Aidha, Wizara ilikagua watoa taarifa mbalimbali ikiwa ni pamoja na benki 17 na kampuni ya masoko ya hisa moja.

**71. Mheshimiwa Spika,** Wizara pia ilisaini hati za makubaliano (Memorandum of Understanding) na wadau wa ndani na nje ya nchi ikiwemo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Kitengo cha Kudhibiti Utakasishaji wa Fedha Haramu cha Zimbabwe na hivyo kufanya idadi ya hati za makubaliano na vitengo mbalimbali kuwa kumi; Kutoa elimu na mafunzo kwa wadau mbalimbali wakiwemo watoa taarifa za jinsi ya kutumia mfumo maalum wa uchambuzi wa taarifa wa kompyuta kwa ajili ya kurahisisha uwasilishaji wa taarifa za miamala shuku na uchambuzi; na Kuratibu na kusimamia zoezi la Kitaifa la kutathmini viashiria hatarishi vya fedha haramu na ufadhili wa ugaidi.

### **3.4.15. Tume ya Pamoja ya Fedha**

**72. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2015/16 Wizara kupitia Tume ya Pamoja ya Fedha imekamilisha Ripoti ya Stadi kuhusu Mwenendo wa Uchumi na Mapato ya Muungano ambayo lengo lake ni kuiwezesha Tume kushauri na kupendekeza namna bora ya kuboresha vyanzo vya mapato ya muungano kwa kuzingatia mwenendo wa uchumi. Ripoti ya stadi hiyo imewasilishwa katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

### **3.4.16. Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi**

**73. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2015/16, Wizara imeendelea kupokea na kuchambua miradi ya ubia kwa lengo la kuiidhinisha kwa mujibu wa Sheria. Wizara kupitia kitengo chake cha ubia kati ya sekta ya umma na sekta Binafsi imechambua na kuidhinisha mradi wa kufua umeme wa Kinyerezi III. Aidha, upembuzi yakinifu wa mradi wa barabara ya tozo kati ya Dar es Salaam na Chalinze unaendelea kufanyika. Kadhalika, Serikali ipo katika hatua ya mwisho kumpata mshauri elekezi kwa ajili ya mradi wa kuzalisha madawa muhimu na utengenezaji wa vifaa tiba chini ya Bohari Kuu ya Madawa (MSD). Vilevile, Wizara kupitia kitengo chake cha ubia inafanya uchambuzi wa maandiko ya mradi wa daraja la Kigamboni kwa lengo la kuidhinisha Mradi huo tayari kwa kuandaliwa mkataba wa uendeshaji.

**74. Mheshimiwa Spika,** Sambamba na uchambuzi wa miradi, katika mwaka 2015/16 mafunzo mbalimbali yalitolewa kwa makundi sita yakiwemo watunga sera; Maofisa waandamizi Serikali Kuu na Serikali za Mitaa; Taasisi Binafsi; Mashirika ya Umma; Taasisi za Serikali; na taasisi za fedha kutegemea na mahitaji na majukumu ya kila kundi. Jumla ya wadau 217 walipatiwa mafunzo kuhusu Sera, Sheria na Kanuni za Miradi ya Ubia.

### 3.5. USIMAMIZI NA URATIBU WA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA CHINI YA WIZARA

**75. Mheshimiwa Spika,** Naomba sasa uniruhusu kueleza utekelezaji wa majukumu ya taasisi zilizo chini ya Wizara kwa mwaka 2015/16 kama ifuatavyo:-

#### 3.5.1. Huduma za Kibenki

##### (i) Benki Kuu ya Tanzania – BoT

**76. Mheshimiwa Spika,** Jukumu la msingi la Benki Kuu ni kuandaa na kutekeleza sera ya fedha inayolenga kuwa na kiwango kidogo cha mfumuko wa bei kwa ajili ya ukuaji endelevu wa uchumi wa Taifa. Ili kufanikisha azma hii, Benki Kuu inadhibiti ongezeko la ujazi wa fedha kwa kutumia nyenzo mbalimbali ambazo ni: Kuuza dhamana na hati fungani za Serikali; Kukopa au kukopesha mabengi kwa muda mfupi; Kuuza fedha za kigeni katika soko la jumla la mabengi; Kurekebisha riba inayotowza kwa mabengi na Serikali yanapokopa toka Benki Kuu; na Kuagiza mabengi kisheria yaweke sehemu ya amana za wateja wake Benki Kuu. Lengo ni kudumisha utulivu wa uchumi mpana na kuongeza ufanisi katika shughuli za uzalishaji kwa ajili ya ukuaji mzuri na endelevu wa uchumi.

**77. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi kilichoishia Machi, 2016 mfumuko wa bei umeshuka hadi kufikia asilimia 5.4 ikilinganishwa na asilimia 6.8 mwezi Disemba, 2015. Aidha, wastani wa mfumuko wa bei usiojumisha vyakula na nishati, ambao hupima kwa usahihi zaidi utekelezaji wa sera ya fedha, umeendelea kubaki katika kiwango cha chini cha asilimia 2.8 mwezi Machi, 2016. Hii inatokana na hatua mbalimbali thabiti za kisera zilizochukuliwa na Benki Kuu ya Tanzania katika kudhibiti ujazi wa fedha na ukwasi katika uchumi.

**78. Mheshimiwa Spika,** Ongezeko la fedha taslimu ambacho ni kipimo bora cha ukwasi kwenye uchumi katika kipindi kilichoishia Machi, 2016 ulikua kwa wastani wa asilimia 12.1 uliokuwa ndani ya lengo la asilimia 17.1. Sekta ya fedha imeendelea kuchangia ukuaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi kwa kasi nzuri ya kutoa mikopo kwa wakati na kwa kiwango cha kutosha. Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 24.0 katika mwaka ulioishia mwezi Februari, 2016, ikilinganishwa na makadirio ya asilimia 19.3 kwa mwaka 2015/16. Mikopo mingi kwa sekta binafsi ilielekezwa kwenye shughuli za biashara iliyokuwa na asilimia 19.4 ya jumla ya mikopo yote, shughuli binafsi asilimia 17.6, uzalishaji viwandani asilimia 11.1, shughuli za kilimo asilimia 7.8 na uchukuzi na mawasiliano asilimia 7.8.



**79. Mheshimiwa Spika,** Benki Kuu ina jukumu pia la kusimamia huduma za kibenki ambapo sekta hii imeendelea kukua ikichangiwa na uanzishwaji wa taasisi mpya za kifedha ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania. Hadi kufikia Machi, 2016, kulikuwa na jumla ya benki na taasisi za fedha zinazosimamiwa na Benki Kuu zipatazo 63 zenye matawi 725 nchini kote. Kiwango cha mitaji ikilinganishwa na mali iliyowekezwa kilikuwa asilimia 18.11 ikilinganishwa na kiwango cha chini kinachotakiwa kisheria cha asilimia 12.0. Kiwango cha mali inayoweza kubadilishwa kuwa fedha taslimu ikilinganishwa na kiwango cha amana zinazoweza kuhitajika katika muda mfupi kilifikia asilimia 36.84 ikilinganishwa na kiwango cha chini kinachohitajika kisheria cha asilimia 20.

**80. Mheshimiwa Spika,** Upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wananchi wasiofikiwa na mabenki umeendelea kuongezeka kutokana na ubunifu wa mipango ya utoaji wa huduma za malipo ya rejareja kupitia simu za mikononi, pamoja na huduma za uwakala wa mabenki. Ubunifu huu umechangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la amana za watu binafsi ambazo zimefikia shilingi trilioni 18.2 mwezi Machi, 2016 kutoka shilingi trilioni 15.6 mwezi Machi, 2015.

**81. Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Mifumo ya Malipo Nchini (National Payment Systems Act, 2015) imekamiliwa na kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali sheria na kanuni zinazohusu utoaji wa leseni na kuridhia uanzishwaji wa mifumo ya malipo nchini, pamoja na kanuni zake. Pia maboresho katika mfumo mpya wa malipo kwa kutumia hundi (Tanzania Automated Clearing System) ulioanza kutumika mwishoni mwa mwezi Aprili, 2015, umeongeza ufanisi mkubwa na kupunguza muda wa kusubiria malipo ya hundi kutoka siku tatu mpaka saba hadi kufikia siku moja.

## **(ii) Benki ya Maendeleo ya Kilimo –TADB**

**82. Mheshimiwa Spika,** Benki ya Maendeleo ya Kilimo ilipata leseni ya kujiendesha kama taasisi ya fedha ya kimaendeleo kutoka Benki Kuu ya Tanzania tarehe 4 Agosti 2015 na kuzinduliwa Rasmi na Rais wa Awamu ya Nne Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 8 Agosti, 2015. Madhumuni makuu ya kuanzishwa benki hii ni kusaidia upatikanaji, utoshelezi na usalama wa chakula endelevu nchini na kusaidia katika kuleta mapinduzi ya kilimo kutoka kilimo cha kujikimu kwenda kilimo cha biashara ili kuchangia kwenye ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini.

**83. Mheshimiwa Spika,** Serikali hadi sasa imeipatia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania mtaji wa shilingi bilioni 60. Aidha, katika hatua za awali, benki imeainisha minyororo 14 ya thamani ya mazao ya kilimo katika sekta ndogo ndogo nane itakayopewa kipaumbele katika kutoa mikopo



kwa kuanzia. Sekta hizo ni za uzalishaji wa nafaka; mifugo; ufugaji wa samaki, kilimo cha matunda, maua, mbogamboga, na viungo; mazao ya viwanda hasa miwa na korosho; mbegu za uzalishaji mafuta ya kula; na mazao ya misitu hasa ufugaji wa nyuki na mazao yake.

**84. Mheshimiwa Spika**, Benki imevijengea uwezo vikundi vipatavyo 89 vyenye jumla ya Wakulima 21,526 kwa ajili ya kuviandaa kuweza kuandika andiko la mkopo na kuweza kukopa. Hadi kufikia Machi, 2016, jumla ya vikundi nane mkoani Iringa vyenye wakulima 857 ndivyo vilivyoweza kukamilisha taratibu za ukopaji ambapo viliweza kupatiwa mkopo wa zaidi ya shilingi bilioni moja. Aidha, kwa sasa benki inaendelea na uchambuzi wa maombi mapya ya mikopo ambapo hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Machi, 2016 benki imechambua maombi kutoka vikundi 51 vya wakulima yenye jumla ya shilingi bilioni 39.

**(iii) Benki ya Maendeleo TIB – TIB DFI**

**85. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi, 2016 Benki ya Maendeleo TIB imefadhili miradi mikubwa ya maendeleo hasa katika sekta ya miundombinu na viwanda. Miradi hii ni pamoja na mradi wa TPDC wa kuchakata na usafirishaji gesi asilia hadi kwenye mitambo ya TANESCO ya kufua umeme ya Kinyerezi/Dar es Salaam; Ujenzi wa njia ya umeme kutoka Somanga Fungu hadi Kinyerezi; Mradi wa kuchakata gesi asilia wa kampuni ya Wentworth; Mradi wa maboti katika kuimarisha usimamizi wa uchimbaji gesi katika bahari ya Hindi; na Kiwanda cha kusindika kahawa laini (instant coffee) mjini Bukoba na Shirika la Reli Tanzania.

**86. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka ulioishia Disemba, 2015 Benki ilipata faida ya shilingi bilioni 9.2 ikilinganishwa na shilingi bilioni 10.4 zilizopatikana mwaka 2014. Kupungua kwa faida kumetokana na mgawanyo wa rasilimali (assets) za kibiashara katika TIB Development Bank na kampuni yake tanzu ya TIB Corporate Bank. Waraka mizania uliongezeka kwa asilimia 32 hadi kufikia shilingi bilioni 689.0 Disemba, 2015, ikilinganishwa na shilingi bilioni 413.0 Disemba, 2014.

**(iv) Benki ya Biashara TIB – TIB CBL**

**87. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wake wa kwanza wa kiutendaji, Benki ya Biashara TIB imepata faida ghafi (iliyokaguliwa) ya shilingi bilioni 5.3. Faida hii imetokana na mfumo imara na uadilifu wa uhibiti wa gharama za uendeshaji ambao kwa mjumuisho umeleta ufanisi mkubwa na kufanya matumizi ya benki kuwa madogo. Benki pia imeweza kupata mapato katika ubadilishaji fedha za kigeni kiasi cha shilingi bilioni 1.9. Mafanikio mengine yaliyopatikana katika mwaka 2015 ni pamoja na: kupatikana kwa leseni ya uendeshaji biashara ambayo imetolewa na Benki Kuu Julai, 2015; kuanzisha mfumo wa ulipaji kwa kutumia hundi na kuingia katika mfumo wa kitaifa wa

kibenki wa kupitisha hundi kwa haraka (Cheque Truncation) ikiwa ni pamoja na mfumo wa kisasa wa kuweka na kutoa pesa kupitia simu za mkononi (mobile banking) ambavyo vitaifanya benki kuwa ya ushindani na ufanisi kibiashara; na uanzishwaji wa kitengo cha wateja wa hadhi (Premier Customers) katika matawi ya benki na kuhamisha matawi mengine ili kuweza kuwafikia wateja kwa njia bora zaidi.

**(v) Benki ya Posta Tanzania – TPB**

**88. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2015/16, Benki ya Posta iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kibiashara kwa kusambaza huduma zake kwa wananchi. Hadi kufikia Machi, 2016 amana za wateja Benki ya Posta ziliongezeka na kufikia shilingi bilioni 312.5 ikilinganishwa na shilingi bilioni 240 Disemba, 2014. Thamani ya mikopo inayotolewa kwa wateja iliongezeka na kufikia shilingi bilioni 254.36 ikilinganishwa na shilingi bilioni 196 Disemba, 2014. Pato ghafi lililozalishwa na benki liliongezeka na kufikia shilingi bilioni 73.95 Disemba, 2015 ikilinganishwa na shilingi bilioni 52.77 Disemba, 2014.

**89. Mheshimiwa Spika,** Mwaka 2015 benki ilianza kutoa huduma kwa vikundi, hii ikiwa ni huduma mpya sokoni. Vikundi hivi ni pamoja na vikundi vya kuweka na kukopa vijijini. Hadi Machi, 2016 benki ilikuwa na wateja 2,617 na amana za thamani ya shilingi milioni 373. Aidha, benki ilianzisha utoaji huduma kwa VICOBA ambapo hadi Machi, 2016 benki ilikuwa na wateja 26,276 na amana zenye thamani ya shilingi bilioni tatu. Benki ilitoa huduma kwa vikundi visivyo rasmi na kufikisha wateja 1,000 sambamba na amana za thamani ya shilingi milioni 880. Akaunti maalum kwa mashabiki wa timu za Simba, Yanga na Mbeya City zilikuwa na wateja 16,000 na amana zenye thamani ya shilingi bilioni moja.

**(vi) Benki ya Twiga - Twiga Bancorp**

**90. Mheshimiwa Spika,** Benki ya Twiga imeendelea kutoa huduma mbalimbali za kibenki kupitia matawi yake matano na matawi madogo manne ambapo hadi Machi, 2016 amana za wateja ziliongezeka na kufikia shilingi bilioni 94.2 ikilinganishwa na shilingi bilioni 63.5 Juni, 2015 ikiwa ni ongezeko la asilimia 30. Aidha, mikopo iliyotolewa kwa wateja ilifikia shilingi bilioni 42.6 ikilinganishwa na shilingi bilioni 36.3 Juni, 2015 ikiwa ni ongezeko la asilimia 17. Vile vile, benki imewekeza kiasi cha shilingi bilioni 36.4 kwenye Dhamana za Serikali na Amana katika benki nyingine ikilinganishwa na shilingi bilioni 14.6 kama ilivyokuwa Juni, 2015 sawa na ongezeko la asilimia 149.

**91. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2016 Benki imepanga kuongeza amana za wateja kutoka shilingi bilioni 94.2 hadi kufikia shilingi bilioni 146.9; Kuwekeza kiasi cha

shilingi bilioni 61.6 katika Dhamana za Serikali na Amana za muda maalumu kwenye mabenki ifikapo tarehe 31 Disemba, 2016 ikilinganishwa na Dhamana pamoja na Amana zenye thamani ya shilingi bilioni 39 kama ilivyokuwa kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Disemba, 2015 ambalo ni ongezeko la shilingi bilioni 22.6 au asilimia 58.

### **3.5.2. Mifuko ya Hifadhi za Jamii**

#### **(i) Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma – PSPF**

**92. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2015 hadi Machi, 2016 Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma umesajili jumla ya wanachama 465,198 ikilinganishwa na wanachama 429,759 waliokuwa wamesajiliwa hadi mwezi Juni, 2015. Aidha, katika kipindi hicho, kiasi cha shilingi bilioni 677.18 kilikusanywa kutoka kwenye vyanzo vyake ikiwemo shilingi bilioni 458.57 kutokana na michango ya wanachama, shilingi bilioni 83.25 kutoka Serikalini kwa ajili ya kulipia “Pre July, 1999”, shilingi bilioni 21.3 mapato kutokana na uwekezaji katika vitega uchumi mbalimbali, shilingi bilioni 80.31 kutokana na vitega uchumi vilivyo komaa, shilingi bilioni 32.26 kutokana na marudisho ya mikopo kutoka kwa wanachama na shilingi bilioni 1.49 ni mapato kutokana na vyanzo vingine mbalimbali.

#### **(ii) Mfuko wa Mafao ya Kustaafu – GEPP**

**93. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016 Mfuko wa GEPP umesajili jumla ya wanachama 15,643. Katika kipindi hicho Makusanyo ya michango kutoka kwa wanachama yalifikia shilingi bilioni 44.48 sawa na asilimia 67 ya malengo ya mwaka mzima. Aidha, mapato ya vitega uchumi yameongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 21.41 sawa na asilimia 61 ya lengo. Vile vile, Thamani ya Mfuko ilifikia shilingi bilioni 384.5.

#### **(iii) Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma – PPF**

**94. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2015 hadi Machi, 2016 Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma umesajili wanachama 49,828 na kufanya idadi ya wanachama kuongezeka na kufikia wanachama 242,530. Aidha, katika kipindi hicho kiasi cha shilingi bilioni 395.7 zilikusanywa ikiwa ni michango ya wanachama na mapato yatokanayo na uwekezaji. Thamani ya Mfuko imeongezeka kufikia shilingi trilioni 2.27 ikiwa ni ongezeko la asilimia 8.9 ikilinganishwa na thamani ya Mfuko ya shilingi trilioni 2.08 iliyokuwa Juni, 2015. Ongezeko hilo lilitokana na kiasi cha uwekezaji katika makundi ya uwekezaji, kuongezeka kwa thamani ya hisa za kampuni ambazo Mfuko umewezeza, ukusanyaji wa michango na mapato yatokanayo na uwekezaji.

### 3.5.3. Rufani za Kodi

**95. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2015 hadi Machi, 2016 Bodi ya Rufani za Kodi (TRAB) imesajili jumla ya kesi 167 ambapo kiasi cha kodi kinachobishaniwa ilikuwa shilingi bilioni 379.84 na Dola za Kimarekani milioni 26.72. Jumla ya rufaa 141 zimesikilizwa na kutolewa maamuzi. Aidha, katika kipindi hicho Baraza la Rufani za Kodi (TRAT) limesajili kesi 46. Kati ya hizo kesi 31 zenye kiasi cha fedha shilingi 7,878,419,937 na Dola za Kimarekani 43,503,018 zilisikilizwa na kutolewa maamuzi.

### 3.5.4. Huduma za Bima

#### (i) Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima – TIRA

**96. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima imeandaa Sera ya Bima ya Taifa ambayo iko katika hatua za mwisho kukamilishwa. Lengo kuu la sera hii ni kupanua wigo wa shughuli za bima nchini ili wananchi walio wengi waweze kunufaika na huduma za bima. Aidha, Mamlaka imefungua ofisi yake ya kanda mkoani Dodoma inayohudumia mikoa ya Morogoro, Dodoma, Singida na Tabora hivyo kufanya Mamlaka kufikisha ofisi za kanda tano ikiwa ni pamoja na Zanzibar, Arusha, Mwanza na Mbeya. Mamlaka pia imeendelea kupokea na kuyatolea ufumbuzi malalamiko ya wateja wa Bima ili kukuza imani kwa Wananchi kuhusu huduma za Bima kupitia Baraza la usuluhishi la Bima.

#### (ii) Shirika la Bima la Taifa – NIC

**97. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Julai 2015 hadi Machi, 2016 utendaji wa Shirika la Bima la Taifa kibiashara uliendelea kuimarika ambapo Shirika limekusanya mapato ya shilingi bilioni 34.17. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 28.32 ni mapato yaliyotokana na ada za bima, shilingi bilioni 4.68 ni mapato yatokanayo na vitega uchumi, na shilingi bilioni 1.17 ni mapato yanayotokana na deni la mauzo ya nyumba. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya taasisi 15 za Serikali zilijwekea bima kupitia Shirika la Bima la Taifa. Taasisi hizo ni Mamlaka ya Bandari Tanzania; Benki Kuu ya Tanzania; Chuo Kikuu Cha Dar Es Salaam; Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania; Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro; Shirika la Bima la Zanzibar; Mamlaka ya Kudhibiti Chakula na Dawa; Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania; Ofisi ya Mdhidhi na Mkaguzi Mkuu wa Serikali; Mamlaka ya Usimamizi na Udhidhi wa Sekta ya Hifadhi ya Jami; Mfuko wa Pensheni wa PSPF; Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar Es Salaam; Chuo cha Taifa Cha Usafirishaji; Taasisi ya Saratani Ocean Road; na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima.

**98. Mheshimiwa Spika,** Shirika lilisaini mkataba wa kujiunga katika mfumo wa Bima unaoziunganisha kampuni za Bima za nchi wanachama wa jumuiya ya COMESA unaojulikana kama “Intersurty Agreement” mwezi Machi, 2015. Makubaliano hayo yanaziwezesha nchi kuwa washiriki rasmi katika mpango wa himaya moja ya forodha kwa ukanda huu wa Afrika. Kwa kujiunga na mfumo huu, NIC itakuwa kampuni pekee yenye kubeba dhamana ya utoaji wa bima kwa mizigo yote itakayopita Tanzania kwa kupitia mpango wa “Regional Customs Transit Guarantee Scheme – RCTG”.

Mpango huu umeliwezesha shirika kujiongeza mapato na kufaidika kupitia mfumo wa usafirishaji wa njia ya kati ujulikanao kama “Central Corridor” ambapo katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi, 2016 Shirika lilikusanya shilingi bilioni 1.52.

### **3.5.5. Mitaji na Dhamana**

#### **(i) Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana – CMSA**

**99. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi kilichoishia Machi, 2016 kumekuwa na maendeleo ya kuridhisha katika masoko ya mitaji na uanzishwaji wa soko la bidhaa nchini. Idadi ya makampuni yaliyorodheshwa kwenye Soko la Mitaji la Dar es Salaam iliongezeka kutoka 21 hadi 23 kufuatia kuorodheshwa kwa Benki ya Walimu ambayo iliongeza idadi ya wawekezaji katika soko hilo kutoka 200,000 hadi 435,000.

**100. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ilitoa idhini ya kuuzwa kwa hatifungani kwa wawekezaji wadogo wadogo. Toleo la kwanza lililofanywa na Benki ya Exim, ambapo jumla ya shilingi bilioni 19.97 zilikusanywa ikilinganishwa na lengo la shilingi bilioni 10 na kupata wawekezaji 512. Hii inaonesha uhitaji uliokuwepo kwa wawekezaji wadogo wadogo katika fursa zinazopatikana katika uwekezaji wa hatifungani. Vile vile, Mamlaka iliidhinisha matumizi ya simu za mikononi kwenye ushiriki katika masoko ya mitaji kwa lengo la kuwawezesha Watanzania waishio vijijini na mijini kushiriki katika uuzaji na ununuzi wa hisa, hatifungani za kampuni na vipande vya uwekezaji wa pamoja kwa kutumia teknolojia hiyo.

**101. Mheshimiwa Spika,** maandalizi ya uanzishwaji wa Soko la Bidhaa (Commodity Exchange) nchini yamefikia hatua ya kuridhisha. Baadhi ya masuala ambayo yameshafanyika hadi sasa ni pamoja na kutungwa kwa Sheria ya Masoko ya Bidhaa; Kuandaliwa kwa taratibu za ushiriki katika soko la bidhaa ambazo zitawezesha kutoa leseni na kuainisha taratibu za ushiriki katika Soko la Bidhaa la Tanzania; na kusajiliwa kwa Kampuni ya Soko la Bidhaa. Kufanikiwa kwa ukusanyaji wa mitaji na uorodheshwaji wa makampuni hayo kuliwezesha kuanzishwa kwa dirisha la kukuza ujasiriamali “Enterprise Growth Market” (EGM) katika Soko la Hisa la Dar es

Salaam. Hadi Machi, 2016 makampuni matano yalikuwa yemeorodheshwa kwenye dirisha hilo.

**(ii) Soko la Hisa la Dar Es Salaam – DSE**

**102. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi kilichoishia Machi, 2016 Soko limeweza kuorodhesha Hatifungani zenye thamani ya shilingi bilioni 783. Aidha, kwa upande wa hisa za makampuni, soko liliorodhesha hisa milioni 61.8 zenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 31. Idadi ya kampuni zilizoorodheshwa sokoni zimepanda mpaka kufikia kampuni 23 ikilinganishwa na kampuni 21 zilizokuwa zimeorodheshwa Julai, 2015. Ongezeko hili limewezesha pia kuongezeka kwa idadi ya wawekezaji kutoka 263,281 mwezi Julai 2015 hadi 464,000 mwezi Machi, 2016. Vile vile, katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi, 2016 hisa zenye thamani ya shilingi bilioni 632 ziliuzwa na hatifungani za Serikali zenye thamani ya shilingi bilioni 208 ziliuzwa katika soko la upili.

**3.5.6. Dhamana za Uwekezaji Tanzania**

**(i) Taasisi ya Huduma za Fedha na Mikopo Tanzania - UTT MFI**

**103. Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Huduma za Fedha na Mikopo Tanzania (UTT MFI) imejikita katika kutoa huduma za kifedha na mikopo kwa wataanzania wenye kipato cha chini na cha kati. Hadi kufikia Machi, 2016 jumla ya mikopo ya shilingi bilioni 11.5 ilitolewa kwa wananchi 16,951 kati ya hao wanawake ni 13,561 na wanaume ni 3,390.

**(ii) Kampuni ya Usimamizi wa Rasilimali za Uwekezaji - UTT AMIS**

**104. Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Usimamizi wa Rasilimali za Uwekezaji na Huduma kwa Wawekezaji (UTT AMIS) ikiwa kama Meneja wa Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja ilijikita zaidi katika kuimarisha, kuboresha na kukuza Mifuko mitano ya uwekezaji inayoisimamia ili iweze kutimiza malengo yake. Mifuko hiyo ni Mfuko wa Umoja, Mfuko wa Wekeza Maisha, Mfuko wa Watoto, Mfuko wa Jikimu na Mfuko wa Ukwasi. Hadi kufikia Machi, 2016 mifuko hii ilikuwa na jumla ya thamani ya shilingi bilioni 256 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 237 mwezi Disemba, 2015. Aidha, UTT AMIS iliendelea kutoa elimu kwa umma kwa njia ya magazeti, radio na luninga kwa lengo la kuhamasisha tabia ya kujiwekea akiba na dhana nzima ya uwekezaji.



**(iii) Taasisi ya Miradi na Maendeleo ya Miundombinu - UTT PID**

**105. Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Miradi na Maendeleo ya Miundombinu (UTT PID) imeweza kutekeleza majukumu yake yanayohusu kuibua na kutekeleza miradi kwa kukamilisha upatikanaji wa viwanja vilivyopimwa kwa bei nafuu kwa wananchi katika sehemu za Sengerema, Mapinga, Kilwa, Lindi, Morogoro na Bukoba; kusaini makubaliano kati ya Taasisi na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu uendelezaji wa viwanja vya balozi mbalimbali zilizopo nchi za nje; na kusaini mkataba wa kusimamia uendeshaji wa soko la kimataifa lililopo Mwanjelwa mkoani Mbeya. Aidha, Taasisi ipo katika hatua za awali za kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba za mfano za askari wa Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT).

**3.5.7. Taasisi za Mafunzo**

**(i) Chuo cha Usimamizi wa Fedha – IFM**

**106. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Usimamizi wa Fedha- IFM kimeendelea kutoa mafunzo katika matawi yake yaliyoko Dar es Salaam na Mwanza katika fani za Usimamizi wa fedha, uhasibu, benki, bima, kodi, hifadhi za jamii, teknolojia ya mawasiliano ya habari, na sayansi ya komputa. Katika mwaka 2015/16, Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 7,977 kati yao wanawake 3,042 sawa na asilimia 38.13 na wanaume 4935 sawa na asilimia 61.87. Aidha, wanafunzi 3,840 walihitimu masomo katika kozi mbalimbali.

**(ii) Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini – IRDP**

**107. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa masomo 2015/16, Chuo kilidahili jumla ya wanafunzi 4,622 katika kozi mbalimbali 17 zinazoendeshwa na Chuo. Kati ya wanafunzi waliodahiliwa, wanawake ni 2,362 sawa na asilimia 51 ya wanafunzi wote waliodahiliwa na wanaume ni 2,260 sawa na asilimia 49 ya wanafunzi waliodahiliwa. Aidha, Chuo kupitia Programu ya Kuboresha Elimu ya Msingi inayofadhiliwa na UKAID kimeendelea na uendeshaji mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kupanga na kusimamia mipango ya maendeleo ya sekta ya elimu ya msingi kwa Maafisa Elimu wa Wilaya katika mikoa saba ambayo ni Tabora, Dodoma, Simiyu, Shinyanga, Mara, Lindi, na Kigoma.



**(iii) Taasisi ya Uhasibu Arusha – IAA**

**108. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2015/16, Taasisi ya Uhasibu Arusha (IAA) imeendelea kutoa elimu katika nyanja za uhasibu, ugavi, usimamizi wa kodi, benki, utawala wa biashara, teknolojia ya habari na sayansi ya kompyuta katika ngazi mbalimbali. Aidha, Chuo kinatoa mafunzo ya uhasibu na usimamizi wa fedha katika ngazi ya stahada ya uzamili. Vilevile, Chuo kinatoa mafunzo ya shahada za uzamili (Masters Degree) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha “Coventry” cha Uingereza na Galgotias University, India. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: idadi ya wahitimu kuongezeka kutoka 1,367 mwaka 2014/15 mpaka 1,547 mwaka 2015/16. Hali kadhalika udahili wa wanafunzi uliongezeka kutoka wanafunzi 3,393 mwaka 2014/15 hadi wanafunzi 3645 mwaka 2015/16; Kuanza kutoa mafunzo katika Kampasi mpya ya Mwanza kwa ngazi ya Stahada na Stahada ya Uzamili; na kuanza kufundisha kwa kutumia mtandao ikiwa ni hatua muhimu ya kuanzisha kituo cha Elimu masafa (E- Learning Centre).

**(iv) Taasisi ya Uhasibu Tanzania – TIA**

**109. Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) imeendelea kutoa mafunzo kuanzia ngazi ya cheti, diploma na shahada katika fani za uhasibu, uhasibu wa Serikali, ununuzi na ugavi, rasilimali watu, uongozi wa biashara, masoko na mahusiano ya umma kupitia matawi sita katika mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Singida, Mtwara, Mwanza na Kigoma. Katika mwaka wa masomo 2015/16, Taasisi ilidahili wanafunzi 7,473 katika kozi zake mbalimbali na hivyo kuifanya idadi ya wanachuo wote kufikia 14,758.

**(v) Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika – EASTC**

**110. Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika, kiliendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu ya Shahada ya uzamili, Shahada, Stahada na Cheti cha Takwimu Rasmi kwa nchi wanachama 18 ikiwemo Tanzania ambapo katika mwaka wa masomo 2015/16, jumla ya wanafunzi 421 walisajiliwa. Aidha, Chuo kilianza rasmi kozi ya Shahada ya Uzamili katika Takwimu za Kilimo kwa ushirikiano na Chuo cha Kilimo cha Sokoine (SUA) ambapo jumla ya wanafunzi watano walidahiliwa na kuanza masomo. Kadhalika, katika jitihada zake za kutambulika kimataifa katika kutoa huduma ya takwimu rasmi, kimeweza kupata hadhi ya kuwa Mwangalizi katika mikutano ya takwimu ngazi ya Umoja wa Mataifa (UN STACOM) kutokana na mchango wake katika ufundishaji wa takwimu rasmi kwa nchi zinazotumia lugha ya kiingereza barani Afrika.

### 3.5.8. Taasisi za Kitaalam na Huduma Nyinginezo

#### (i) Mamlaka ya Mapato Tanzania – TRA

**111. Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha mwaka 2015/16 Mamlaka ya Mapato Tanzania ilipanga kukusanya mapato ya kodi ya shilingi bilioni 12,362.96 ikiwa ni ongezeko la asilimia 24.8 ukilinganisha na makusanyo halisi katika mwaka wa fedha 2014/15. Kati ya kiasi kilichotarajiwa kukusanywa, shilingi bilioni 499.98 zilitarajiwa kupatikana kutokana na marekebisho ya mfumo wa kodi kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2015. Mapato ya kodi yalitaraajiwa kuchangia asilimia 88 ya mapato ya ndani, wakati asilimia 12 iliyobaki ilitarajiwa kuchangiwa na mapato yasiyo ya kodi yakiwemo makusanyo ya Serikali za mitaa. Kwa upande wa Zanzibar, Mamlaka ya Mapato ilitarajiwa kukusanya mapato ya kodi ya shilingi bilioni 178.56 ikiwa ni ongezeko la asilimia 24 ukilinganisha na makusanyo halisi katika mwaka 2014/15. Hadi kufikia Machi, 2016 mapato halisi ya kodi kwa Tanzania Bara yalifikia shilingi bilioni 9,251.87 sawa na asilimia 100.2 ukilinganisha na lengo la kukusanya shilingi bilioni 9,234.99 (**Jedwali Na.4**). Makusanyo hayo ni ongezeko la asilimia 25.5 ukilinganisha na makusanyo yaliyofikiwa katika kipindi kama hiki katika mwaka wa fedha 2014/15.

**112. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Zanzibar, hadi kufikia Machi, 2016 makusanyo halisi yalifika shilingi bilioni 121.1 ikilinganishwa na lengo la kukusanya shilingi bilioni 132.25. (**Jedwali Na.5**). Makusanyo hayo ni sawa na asilimia 91.5 ya lengo na ni ongezeko la asilimia 13.3 ukilinganisha na makusanyo yaliyofikiwa katika kipindi cha mwaka 2014/15.

#### (ii) Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)

**113. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2015/16, Ofisi ya Taifa ya Takwimu iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kukusanya, kuchambua, kutunza na kuwasilisha takwimu zilizohitajika katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2015 hadi Machi, 2016 Ofisi ya Taifa ya Takwimu imetayarisha na kusambaza takwimu za Pato la Taifa za robo ya pili, robo ya tatu na robo ya nne ya mwaka 2014 na sasa imekamiliisha majumuisho ya takwimu za Pato la Taifa kwa mwaka 2015. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imeendelea kufanya uchambuzi wa kina wa taarifa na takwimu mbalimbali zilizotokana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 na kutoa machapisho yafuatayo: Taarifa za Vifo Nchini; Taarifa za Kazi na Ajira Nchini; Taarifa za Ndoa na Uzazi; Taarifa za Uhamiaji na Ukuaji wa Miji; Taarifa za Elimu na Kujua Kusoma na Kuandika; na Taarifa za Kijinsia.

**114. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16 kazi ya uhakiki wa mipaka ya kiutawala zimekamiliwa katika maeneo ya Msitu wa Hifadhi ya Taifa wa Kazimzumbwi, Sikonge mkoani Tabora na Manyoni mkoani Singida. Vile

vile uhakiki kwa wilaya za Gairo, Chemba na Wete zimekamiliika. Kazi ya uhakiki wa mipaka ya kiutawala inafanyika kwa lengo la kuboresha kanza ya kijiografia inayotokana na Sensa ya Watu na Makazi. Aidha, kazi ya kuhakiki mipaka ya utawala katika ngazi ya vijiji na mitaa imefanyika katika wilaya za Bagamoyo kwa mkoa wa Pwani na Kiteto katika mkoa wa Manyara. Kazi hii inalenga maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022.

### **(iii) Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha – SELF Microfinance Fund**

**115. Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa SELF ambao ni mwendelezo wa mradi wa SELF uliofikia ukomo wake Juni, 2015 unalenga kukuza na kupanua upatikanaji wa mikopo nafuu kwa wananchi hususani wa vijijini. Mfuko huu kwa kushirikiana na asasi 59 umeendelea kutoa mikopo kwa wajasiriamali ambapo hadi kufikia Machi, 2016, mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 5.76 ilikopeshwa kwa wajasiriamali wadogo wadogo 4,189 kati yao 2,279 (asilimia 54.4) ni wanawake na wanaume ni 1,910 (asilimia 45.6). Mikopo ililenga maeneo mbalimbali ikiwemo mikopo ya biashara ndogo ndogo, ufugaji, uvuvi, usindikaji, madini, viwanda vodogo vidogo, huduma mbalimbali za kibiashara pamoja na pembejeo za kilimo. Aidha, urejeshaji wa mikopo katika Mfuko wa SELF umefikia kiwango cha asilimia 90.

### **(iv) Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi – NBAA**

**116. Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi imeendelea kusimamia matumizi ya viwango vya kimataifa vya utayarishaji na ukaguzi wa taarifa za fedha katika Serikali Kuu na Idara zake, Sekta Binafsi pamoja na Mashirika Binafsi (NGOs). Hadi Machi, 2016 Bodi ilitekeleza majukumu yafuatayo:- Kusimamia utumiaji wa viwango vya kimataifa vya utayarishaji na ukaguzi wa taarifa za hesabu nchini; kuhariri mitaala pamoja na silabi ya taaluma ya uhasibu; kuendeleza taaluma ya uhasibu; kufanya usajili wa wahasibu na kutunza takwimu; pamoja na kusimamia ubora wa ukaguzi wa hesabu.

### **(v) Bodi ya Michezo ya Kubahatisha - Gaming Board**

**117. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2015/16, Bodi iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia na kuratibu sekta ya michezo ya kubahatisha nchini. Katika kutekeleza majukumu hayo, Bodi iliendelea kutoa leseni mbalimbali za michezo ya kubahatisha. Aidha, katika kipindi hicho Bodi ilifanya kaguzi za mara kwa mara kwa waendeshaji wa michezo ya kubahatisha nchini ili kuhakikisha kuwa michezo hiyo inaendeshwa kwa kuzingatia matakwa ya sheria ya michezo hiyo pamoja na sheria zingine za nchi.

**118. Mheshimiwa Spika,** Bodi pia iliendelea kukusanya kodi itokanayo na michezo ya kubahatisha nchini; yaani “gaming tax”. Hadi kufikia Machi, 2016 makusanyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 18.19, sawa na asilimia 86 ya lengo la mwaka la kukusanya shilingi bilioni 19.01. Makusanyo ya mwaka 2015/16 yanatarajiwa kukua kwa asilimia 79 ikilinganishwa na mwaka 2014/15. Aidha, Bodi inatarajia kuchangia kiasi cha shilingi bilioni 1.44 katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria. Hii ikiwa ni ongezeko la zaidi ya asilimia 95 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi milioni 734.39 zilizopelekwa mfuko Mkuu wa Serikali mwaka 2014/15.

### **3.5.9. Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Mwaka 2015/16**

**119. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2015/16, Wizara ilipanga kutekeleza miradi ifuatayo: Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Ujenzi wa Kituo cha Elimu cha Uhasibu; Ujenzi wa Maktaba ya Kisasa ya Chuo cha Uhasibu Arusha; Kujenga uwezo wa kiutendaji kwa Wizara, Idara za Serikali Zinazojitegemea na Mikoa; Maboresho ya Usimamizi wa Kodi; Mpango Kabambe wa Kuimarisha na Kuboresha Takwimu Tanzania; Uwezeshaji wa Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi; Mradi wa Uwezeshaji Wajasiriamali Wadogo; Mpango wa Taifa wa Kuongeza Kipato; na Mpango Kabambe wa Kutathmini Umaskini (Poverty Monitoring Master Plan).

**120. Mheshimiwa Spika,** Miradi mingine iliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na: Social Policy Analysis and Development; Pro-Poor Growth; Uratibu wa Miradi ya Maendeleo; na Population Planning.

**121. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi, 2016 miradi iliyopata fedha ni miwili tu ambayo ni: Programu ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP) na Mpango Kabambe wa Kuimarisha na Kuboresha Takwimu Tanzania (TSMP). Shughuli zilizofanyika chini ya mradi wa PFMRP ni pamoja na: kufanya tathmini ya mafunzo yaliyoendeshwa chini ya programu ya maboresho kwa kipindi cha mwaka 2012/13 hadi 2014/15; kufanya tathmini ya utekelezaji wa programu ya PFMRP kwa kipindi cha miaka miwili na nusu ya utekelezaji; kuendesha mafunzo ya result based management kwa maafisa 63 kutoka Ofisi mbalimbali za Serikali; kutekeleza mpango kazi wa kuwianisha mifumo ya usimamizi wa fedha;

**122. Mheshimiwa Spika,** shughuli nyingine zilizotekelezwa chini ya programu hii ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wakaguzi 74 juu ya namna ya kutumia software kufuatilia hoja za kiukaguzi zinazotolewa na Mdhidhi na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ambazo hazijafanywa kazi; kukamilisha uandaji wa Sera ya Usimamizi wa Mali ya Serikali; ufuatiliaji wa Kamati za Ukaguzi 60 katika Wizara, Idara Zinazojitegemea na Mikoa ili kuhakikisha zinazingatia miongozo ya ukaguzi; Kuwajengea uwezo Wakuu wa Idara

50 kutoka kwenye Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu usimamizi wa vihatarishi; na kuhakiki na kuhisha kanzidata ya taarifa za watumishi wa kada za ununuzi na ugavi katika mikoa ya Geita, Katavi, Manyara, Njombe na Simiyu.

**123. Mheshimiwa Spika,** katika Mpango Kabambe wa Kuimarisha na Kuboresha Takwimu Tanzania (TSMP), shughuli zilizofanyika ni pamoja na: kufanya utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Utafiti wa Viashiria vya Malaria wa 2015/16 (Tanzania Demographic and Health Survey and Malaria Indicator Survey); Kufanya Utafiti na kutoa Matokeo ya Tathmini ya Utoaji wa Huduma za Afya Tanzania, 2014/15 (Tanzania Service Provision Assessment Survey 2014-15; na kufanya utafiti wa kufuatilia hali ya umaskini katika Kaya (National Panel Survey) wa mwaka 2014/15.

### **3.6. MAFANIKIO NA CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI**

#### **3.6.1 MAFANIKIO**

**124. Mheshimiwa Spika,** Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2015/16 ni pamoja na: Kuongezeka kwa makusanyo ya mapato ya ndani; Kuendelea kutengemaa na kukua kwa uchumi kwa asilimia 7.0 mwaka 2015; Kuendelea kupungua kwa mfumuko wa bei na kufikia asilimia 5.4 Machi, 2016; Utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kupitia mapato ya ndani kama vile usambazaji wa umeme vijijini, Kinyerezi II pamoja na miradi ya umeme yenye vyanzo vya mapato ikijumuisha mfuko wa barabara, mfuko wa maji vijijini na Mamlaka ya Elimu; Kufanikisha uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 kwa kutumia fedha za ndani; Kupunguza malimbikizo ya madai ya watumishi, wazabuni na wakandarasi yaliyohakikiwa; Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaonufaika na mikopo ya elimu ya juu; na Kuanza utekelezaji wa elimu msingi bila malipo kwa kutenga shilingi bilioni 18.8 kila mwezi.

#### **3.6.2 CHANGAMOTO**

**125. Mheshimiwa Spika,** panapo mafanikio, changamoto nazo hazikosekani. Hivyo, utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2015/16 ulikabiliwa na changamoto za ukwepaji wa kodi unaohusisha wafanyabiasha na watumishi wasio waadilifu; Mwitikio hasi kwenye matumizi ya mashine ya kielektroniki (EFDs); Ukwepaji kodi kwa kampuni za kimataifa unaotokana na na kampuni hizo kutumia bei kubwa kuliko za soko kwenye biashara baina ya kampuni tanzu na kampuni mama (Transfer Pricing); Uwepo wa sekta kubwa isiyo rasmi ambayo hailipi kodi; na Kuwepo kwa taasisi nyingi zinazokusanya maduhuli kunakosababisha kuwa na idadi kubwa ya kodi zinazolalamikiwa na wafanya biashara.

**126. Mheshimiwa Spika,** changamoto nyingine ni pamoja na uwepo wa malalamiko ya utozaji kodi mara mbili kwa bidhaa zinazopitia Zanzibar kutokana na mfumo wa mgawanyo wa mapato unaopelekea kuwa na mifumo tofauti ya ukokotoaji kodi kwa bidhaa zinapoingia Zanzibar; Uvujaji wa mapato kutokana na kuwa na sheria ambazo hazijalenga zaidi mienendo ya biashara za sekta mpya kama mafuta na gesi; Kuwepo kwa bandari bubu na njia za panya zinazoingiza bidhaa nchini bila kulipiwa kodi. Kupungua kwa fedha za misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo kutokana na kuibuka kwa masharti mapya yanayoambatana na utoaji wa fedha hizo nje ya makubaliano ya awali; na ufanisi duni wa baadhi ya mashirika (kama vile ATCL, TRL, na TAZARA) unaolazimu kuendelea kupata ruzuku ya mishahara na uendeshaji kutoka Serikalini.

### **3.6.3 HATUA ZA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO**

**127. Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na changamoto za utekelezaji wa bajeti kama ziliyobainishwa hapo juu, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo: Kusimamia dhana ya kulipa kodi kwa hiari kwa wafanyabiashara na uwajibikaji kwa watumishi wasio waadilifu; Kuendelea kutoa elimu juu ya umuhimu na faida za kulipa kodi kwa kutumia mitandao ya kielektroniki; na Kuendelea na utekelezaji wa programu mbalimbali za kurasimisha shughuli za sekta isiyo rasmi ikiwa ni pamoja na kufanya uthamini wa mkupuo wa majengo ili kufanikisha ukusanyaji wa kodi ya majengo.

**128. Mheshimiwa Spika,** hatua nyingine zilizochukuliwa ni pamoja na kuboresha Sheria ya Kodi (2004) kwa kuanzisha sheria ya kodi inayojitegemea ambayo itasimamia shughuli za uchimbaji madini, gesi na mafuta; Mamlaka ya Mapato Tanzania kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kupambana na biashara za bandari bubu na njia za panya; Kuendelea na majadiliano baina ya Serikali na Wahisani ili kuhakikisha kwamba fedha za misaada na mikopo zinapatikana kama ilivyohidiwa na kwa wakati; na Serikali inakusudia kufanya marekebisho makubwa kwa Mashirika ya Umma ili yaweze kujiendesha kibiashara bila kutegemea ruzuku ya Serikali.

## **4.0 MALENGO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2016/17**

**129. Mheshimiwa Spika,** Baada ya kuelezea utekelezaji wa mjukumu ya Wizara kwa kina kwa mwaka 2015/2016, naomba sasa nieleze malengo ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2016/17.



#### **4.1 MAJUKUMU YA WIZARA**

##### **4.1.1 Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla**

**130. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 Wizara imepanga kuendelea kuimarisha Sera ya fedha ili iendane na sera ya bajeti kwa lengo la kudhibiti na kupunguza mfumuko wa bei pamoja na tofauti kati ya riba za amana na zile za mikopo.

##### **4.1.2 Uratibu wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa**

**131. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 Wizara chini ya uratibu wa mipango ya maendeleo imepanga kuendelea kuwaelimisha wadau mbalimbali kuhusu wajibu wao katika kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2020/21); Kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2017/18; Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na; Kuchapisha, kusambambaza na kuelimisha wadau mbalimbali kuhusu Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma (PIM – OM). Shughuli hii inalenga kuimarisha taratibu za uibuaji, utekelezaji na usimamizi wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha kuwa miradi inayoibuliwa inatekelezwa kikamilifu na kwa mafanikio makubwa.

##### **4.1.3 Uratibu wa Mikakati ya Kupunguza Umaskini**

**132. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa mwaka 2016/17 imepanga kuandaa mpango wa kitaifa wa ufuatiliaji na tathmini wa jitihada za kuondoa umaskini, ikiwemo viashiria vya kupima utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu. Mpango huu utasaidia kufuatilia utekelezaji wa programu za kuondoa umaskini katika sekta mbalimbali, kuibua changamoto na kurekebisha kasoro kila mwaka; Kuandaa taarifa ya Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu; Kuanzisha kituo cha utunzaji na utoaji wa taarifa mbalimbali kuhusu programu za kuondoa umaskini na maendeleo ya watu; Kuandaa mwongozo wa namna ya kuibua na kutumia fursa za kiuchumi katika maeneo yanayowazunguka wananchi katika halmashauri mbalimbali nchini. Hatua hii itaongeza ushiriki wa wananchi hususani vijijini katika miradi ya uzalishaji na kuongeza kipato; na kufanya tafiti mbalimbali kuhusu masuala ya kuondoa umaskini hususan namna bora na endelevu ya kuboresha jitihada za Serikali katika kuinua hali ya maisha ya wataanzania walio chini ya mstari wa umaskini na kuongeza kasi katika kuleta maendeleo ya binadamu.

##### **4.1.4 Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali** **(a) Mapato ya Ndani**

**133. Mheshimiwa Spika**, ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato, katika mwaka 2016/17 Wizara pamoja na mambo mengine imepanga kuendelea na mfumo wa dirisha



moja la kielektroniki kati ya Mamlaka ya Bandari Tanzania na Mamlaka ya Mapato; kuendelea kudhibiti mizigo yote inayoingia kutoka bandari kavu zote; kuendelea kuimarisha mapato kwenye ushuru wa forodha na bidhaa; kuendelea kusimamia matumizi ya mashine za kielektroniki (EFDs); kushughulikia kwa haraka rufaa za pingamizi na kodi; kufanya kaguzi kwa kuzingatia viashiria hatarishi vya uvujaji wa mapato ya Serikali; kusimamia misamaha ya kodi ili kuhakikisha inatolewa tu kwa wale wanaostahili na inatumika ipasavyo na; kuendelea kutoa elimu ya walipa kodi kuhusu umuhimu wa kulipa kodi kwa maendeleo ya nchi.

**(b) Misaada na Mikopo**

**134. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2016/17 Serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kupata fedha za nje za kugharamia miradi ya maendeleo. Serikali itaelekeza fedha za nje katika kutelekeza miradi mikubwa ya maendeleo itakayochochea ukuaji wa uchumi sambamba na kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuimarisha usimamizi wa matumizi ya Serikali. Hata hivyo, azma ya Serikali ni kupunguza na hatimaye kuondokana na utegemezi wa kibajeti.

**135. Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo tumekubaliana kuwaleta Washauri Elekezi wa kimataifa ili waweze kufanya tathmini ya ushirikiano wetu pamoja na namna ya kuendesha majadiliano. Lengo ni kuboresha ushirikiano wa maendeleo na kushauriana na Serikali juu ya njia nzuri ya kupokea fedha za nje ili ziweze kuwekezwa kwenye miradi ya maendeleo yenye kuleta ufanisi zaidi.

**4.1.5 Uandaaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali**

**136. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa mwaka 2016/17 imepanga pamoja na mambo mengine kuendelea kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali inayojumuisha matumizi ya kawaida na maendeleo; Kuendelea kupitia mfumo wa uwasilishaji wa bajeti za Wizara, Idara za Serikali, Mikoa na Halmashauri na kuhakikisha kuwa Sera na Mipango ya Kitaifa na ile ya Kisekta vyote vimeingizwa ipasavyo katika Bajeti ya Serikali na kutengewa fedha; Kufanya tathmini ya Bajeti ya Serikali kwa lengo la kuhakikisha kuwa inazingatia mahitaji ya makundi yote ya jamii; Kuendelea kuimarisha mfumo ya Kompyuta ya uandaaji bajeti ili kukidhi mahitaji ya taarifa mbalimbali zinazohitajika na; Kuendelea kujenga uwezo wa Wizara, Idara za Serikali, Mikoa na Idara katika uandaaji wa bajeti ya muda wa kati, usimamiaji wake na utoaji taarifa za utekelezaji ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji na tathmini kwa wakati.

#### 4.1.6 Usimamizi na Udhhibiti wa Matumizi ya Fedha za Umma

**137. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Wizara imepanga kuandaa na kukamilisha Mpango wa Programu wa Awamu ya Tano wa Miaka Mitano 2017/2018 - 2021/22; Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Serikali wa kada zinazohusiana na usimamizi wa fedha za umma; Kufanya tathmini ya utekelezaji wa programu kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ili kupima mafanikio ya utekelezaji wa Programu ya Awamu ya Nne na; Kusimamia na Kuratibu zoezi la Upimaji wa Mifumo ya Fedha - *Public Expenditure and Financial Accountability* katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

#### 4.1.7 Usimamizi wa Malipo

**138. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Wizara imepanga kuendelea kutoa udhamini wa masomo kwa wahasibu, wakaguzi, wagavi na wataalamu wa kompyuta kutoka Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ambao wapo vyuoni; Kusimamia Mfumo wa TISS katika Halmashauri zipatazo 58 zilizopo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Arusha, Tanga, Morogoro na Dodoma. Wizara imepanga kuendelea kusimamia, kuimarisha na kuboresha uendeshaji na uunganishaji wa mtandao wa malipo wa Serikali. Aidha, Wizara imepanga kuunganisha Mfumo wa Malipo wa EFT katika Wizara ya Fedha na Mipango, Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi; Kuunganisha mfumo wa uwasilishaji mapato wa Mamlaka ya mapato Tanzania - Tanzania Revenue Gateway System (RGS) na mfumo wa Hazina - Treasury Revenue Accounting System kwa lengo la kupata taarifa za mapato ya kodi kutoka TRA kielektroniki.

**139. Mheshimiwa Spika,** Wizara imepanga pia kufuatilia utekelezaji wa Miongozo ya ukaguzi wa ndani; kukagua mfumo wa kuandaa bajeti; Kufanya ukaguzi maalum kadiri ya mahitaji ya Mlipaji Mkuu wa Serikali na wadau wengine; na kuendelea kutoa mafunzo na kufanya ufuatiliaji wa miongozo mbalimbali ambayo imetolewa na Wizara kwa wakaguzi wa ndani wote na wadau mbalimbali wanaotumia miongozo hiyo.

#### 4.1.8 Deni la Taifa

**140. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa mwaka 2016/17 imepanga kuendelea kulipa madeni mbalimbali yaliyokopwa na Serikali ili kugharamia miradi ya maendeleo nchini pamoja na kuwasilisha michango ya Serikali kwenye mifuko ya hifadhi za jamii. Aidha, kwa kuwa malipo ya fidia kwa wafanyakazi waliokuwa wakipata ajali mahala pa kazi yalikuwa hayashughulikiwi ipasavyo na waajiri na mifuko iliyopo ya Hifadhi ya Jamii ambayo mingi ni ya Pensheni, Serikali ilianzisha Mfuko wa Fidha kwa Wafanyakazi na Wizara kwa mwaka 2016/17 imepanga kuanza kuwasilisha

mchango wa mwajiri kwenye Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ili watumishi wa umma wakipata ajali mahala pa kazi waweze kulipwa na Mfuko huu kwa wakati na pia kupata malipo yenye staha.

#### **4.1.9 Usimamizi wa Mali ya Serikali**

**141. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Wizara chini ya jukumu lake la kusimamia mali ya Serikali imepanga kufanya uthamini wa ardhi na majengo ili kuwa na taarifa sahihi za mali ya Serikali; Kuendelea kuondosha mali chakavu, sinzia na zilizokwisha muda wake; na Kufanya uhakiki wa mali za watu binafsi zilizo chini ya uangalizi wa Serikali na zile zinazotokana na utaiifishwaji kwa lengo la kuepuka ulipaji wa fidia usiokuwa wa lazima. Aidha, Wizara itahakiki mali katika Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali ili kutoa ushauri wa kupunguza hasara zinazotokana na matumizi yasiyo sahihi.

#### **4.1.10 Ununuzi wa Umma**

**142. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo: Kufanya mapitio ya kanuni za ununuzi wa umma; Kuandaa mwongozo wa utekelezaji wa shughuli za ununuzi wa umma nchini; Kuwajengea uwezo wadau mbalimbali wa ununuzi nchini juu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma na kukamilisha tathmini ya ufanisi wa mfumo wa ununuzi wa umma nchini. Aidha, Wizara imepanga kutekeleza mpango wa mahitaji ya mafunzo wa maafisa ununuzi na ugavi walioko katika Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuwajengea uwezo juu ya usimamizi wa mikataba ya ununuzi; Kutoa mafunzo ya matumizi ya mfumo wa malipo wa EPICOR 9 kwa baadhi ya maafisa ununuzi na ugavi Serikalini pamoja na kuendelea kuhakiki taarifa za maafisa ununuzi na ugavi na kuziweka katika daftari la maafisa ununuzi na ugavi Serikalini.

**143. Mheshimiwa Spika,** kazi nyingine zilizopangwa kufanywa na Wizara kwa mwaka 2016/17 ni pamoja na kukamilisha mfumo wa manunuzi kwa njia ya mtandao na kuanza kuutumia kwa majaribio kwenye robo ya pili ya mwaka 2016/17 kwa manunuzi ya madawa na vifaa tiba pamoja na manunuzi ya bidhaa mtambuka; Kuongeza uwezo wa watumiaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma kwa kufanya mafunzo kwa wanataaluma na wadau wengine ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti juu ya taaluma ya ununuzi na ugavi utakaopelekea kutoa ushauri kwa Serikali kwenye maeneo ya taratibu na sera za ununuzi na ugavi na; Kuongeza kiwango cha ufaulu wa watahiniwa toka kiwango cha sasa cha asilimia 42.8 hadi kufikia asilimia 50 kwa kuboresha mazingira ya kujifunzia.

**144. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Wizara kupitia Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini imepanga kuendelea na ununuzi wa magari kwa pamoja; Kuongeza uwezo wa Wakala wa kuhifadhi mafuta kufikia wastani wa lita 50,000 kila mkoa katika mikoa ya Iringa, Kigoma, Mbeya, Morogoro na Mwanza; Kuanza ujenzi wa ofisi, ghala na kisima cha mafuta katika mikoa ya Geita, Katavi, Njombe na Simiyu. Aidha, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini utaendelea na kazi ya kufunga mfumo wa udhibiti na usimamizi wa mafuta ya magari na mitambo katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa, Mbeya, Mwanza, Morogoro, Ruvuma, Singida na Tanga.

#### **4.1.11 Ukaguzi wa Hesabu za Serikali**

**145. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imelenga kuendelea kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2015/16. Ukaguzi utaelekezwa katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma. Aidha, ukaguzi utahusisha Sekta ya mafuta na gesi na pia ukaguzi katika sekta ya madini utaimarishwa ipasavyo. Wizara itaendelea kuimarisha uwezo wa kitaalam kwa Wakaguzi wake, na kuendelea na ujenzi wa majengo ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ili kuimarisha uhuru wa wakaguzi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na tija zaidi ili kukidhi matakwa ya viwango vya kimataifa vya taasisi za ukaguzi pamoja na maazimio ya kimataifa ya Lima na Mexico ambayo Tanzania imeyaridhia.

#### **4.1.12 Usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma**

**146. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Wizara kupitia Msajili wa Hazina, itaendelea kufanya uhakiki wa mali za taasisi na mashirika za umma zilizolingizwa katika daftari la mali; Kufuatilia na kuhakiki mali za mashirika yaliyobinafsishwa ili kubaini mali ambazo hazikuingizwa kwenye orodha ambazo hivi sasa zinamilikiwa kinyume na sheria ili zirejeshwe Serikalini; Kufanya utafiti wa taasisi ambazo zina vyanzo binafsi vya mapato kwa lengo la kuangalia uwezekano wa kuziondoa kwenye utegemezi wa ruzuku ya Serikali; na kukamilisha maandalizi ya mfumo wa tathmini na ufuatiliaji kwa taasisi na mashirika ya umma.

#### **4.1.13 Mafao ya Wastaafu na Mirathi**

**147. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2016/17 shilingi trilioni 1.14 zimetengwa kwa ajili ya kulipa mchango wa mwajiri kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Aidha, Wizara itaendelea kuboresha kumbukumbu za wastaafu ikiwa ni pamoja na kulipa pensheni kwa wakati.

#### **4.1.14 Udhibiti wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi**

**148. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Wizara imepanga kuendelea kupokea na kuchambua taarifa za miamala shuku zinazohusu utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi; Kuendelea kuwasilisha taarifa za intelijensia kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria kwa ajili ya uchunguzi; Kukamilisha zoezi la kutathmini mianya na viashiria vya fedha haramu na ufadhili wa ugaidi nchini; Kuendelea na utekelezaji wa mikakati ya kitaifa na kimataifa ya udhibiti wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi; na kuendelea na ukaguzi wa taasisi mbalimbali za fedha na zisizo za fedha ili kubaini kama sheria na miongozo ya kudhibiti utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili ugaidi inafuatwa ipasavyo.

#### **4.1.15 Tume ya Pamoja ya Fedha**

**149. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2016/17 Wizara kupitia Tume ya Pamoja ya Fedha imepanga kuendelea kufanya stadi ya uwekezaji katika mambo ya muungano. Stadi hii inalenga kubaini ushiriki wa pande mbili za muungano katika uwekezaji kwa mambo ya muungano. Aidha, Wizara inakusudia kufanya mapitio ya stadi zilizofanywa na Tume kuhusu mfumo bora wa kodi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni pamoja na uchambuzi wa masuala ya fedha yanayohusu mambo ya muungano.

#### **4.1.16 Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi**

**150. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Wizara itaendelea kupokea na kuchambua miradi ya ubia kwa lengo la kuiidhinisha; Kutoa ushauri kwa Wizara na Taasisi za Serikali katika kuchagua miradi bora ya ubia; Kuziwezesha taasisi zenye miradi ya ubia kuajiri washauri elekezi pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa wadau mbalimbali kuhusu sera, sheria na kanuni za miradi ya ubia.

### **4.2 USIMAMIZI NA URATIBU WA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA CHINI YA WIZARA**

#### **4.2.1 Huduma za Kibenki**

##### **(i) Benki Kuu ya Tanzania – BoT**

**151. Mheshimiwa Spika,** ili kufikia malengo ya uchumi mpana ambayo Serikali imejiwekea, Benki Kuu ya Tanzania katika mwaka wa fedha 2016/17 imeweka malengo yafuatayo:- Ukuaji wa wastani wa fedha taslim usiozidi asilimia 13; Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi wa asilimia 14.8; Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 20.5; na kuwa na akiba ya fedha za

kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 4.

**(ii) Benki ya Maendeleo ya Kilimo –TADB**

**152. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2016/17, Benki imepanga kuendelea kutoa mikopo kwa angalau minyororo 14 ya thamani (agricultural value chains) itakayofanyiwa tathmini yakinifu kama iliyoanishwa kwenye mpango kazi wa kwanza wa 2016-2020; Kufanya maandalizi ya kutoa mikopo ya kuendeleza miradi ya Kilimo cha umwagiliaji; Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Benki, mabenki mengine na wadau mbali mbali wa Kilimo hususan wale watakaoshiriki katika hatua mbalimbali za mchakato wa kutoa mikopo; Kuitangaza benki na huduma zake kwa wananchi ili waweze kuzielewa shughuli zake na jinsi benki itakavyowahudumia; Kufungua Ofisi za kikanda katika kanda sita katika Kipindi cha miaka mitano ya kwanza kulingana na ukuaji wa biashara na upanuzi wa huduma mikoani; Kusimamia utoaji na usimamizi wa fedha kwenye uendeshaji wa miradi ya Kilimo mbalimbali nchini; na kuratibu upatikanaji wa dhamana mbalimbali kwa ajili ya mikopo kwa wakulima ili mabenki yaweze kuelekeza nguvu zao kuwakopesha wakulima wengi zaidi.

**(iii) Benki ya Maendeleo TIB – TIB DFI**

**153. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2016/17 Benki ya Maendeleo TIB imepanga kuongeza utoaji mikopo katika sekta mbalimbali hadi kufikia shilingi bilioni 726.9, kutoka shilingi bilioni 538.7 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 35; Waraka mizania unategemewa kukua kufikia shilingi bilioni 872.2 Disemba, 2016, kutoka shilingi bilioni 689.0 mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 27. Faida kabla ya kodi inategemea kufikia shilingi bilioni 13.1 ifikapo Disemba, 2016, kutoka shilingi bilioni 9.2 Disemba, 2015 ambalo ni ongezeko la asilimia 42. Aidha, ili kugharimia ukuaji huo, benki imepanga kukopa fedha za muda mrefu na wa kati kufikia shilingi bilioni 325.0 ikijumuisha shilingi bilioni 100 zinazotazamiwa kutokana na Hati Fungani (Corporate Bond). Benki imepanga kukusanya amana za wateja kufikia shilingi bilioni 301.5 mwaka 2016/17.

**(iv) Benki ya Biashara TIB – TIB CBL**

**154. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2016/17 Benki ya Biashara TIB imepanga kuongeza utoaji mikopo ya muda mfupi na wa kati kama mitaji ya uwendeshaji (working capital) katika sekta mbalimbali hadi kufikia shilingi bilioni 176.5, kutoka shilingi bilioni 114.4 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 54.3; Waraka mizania unategemewa kukua kufikia shilingi bilioni 348.8 Disemba, 2016, kutoka shilingi bilioni 219.1 Disemba, 2015 sawa na ongezeko la

asilimia 59.2. Faida kabla ya kodi inategemea kufikia shilingi bilioni 8.8 ifikapo Disemba, 2016 kutoka shilingi bilioni 5.3 Disemba, 2015 ambalo ni ongezeko la asilimia 70. Aidha, ili kugharimia ukuaji huo, benki ya TIB CBL imepanga kukusanya amana za wateja kufikia shilingi bilioni 298.0 kwa mwaka 2016.

**(v) Benki ya Posta Tanzania – TPB**

**155. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016, Benki imejipanga kufikia malengo yafuatayo kibiashara; Kuongeza mapato ya Benki na kufikia shilingi bilioni 89.1; Kupata faida kabla ya kodi ya shilingi bilioni 12.6; Kukuza amana za benki na kufikia shilingi bilioni 382.59; Kuongeza thamani ya mikopo hususan kwa wananchi wa kipato cha chini na kufikia shilingi bilioni 334.504; Kukuza thamani ya mtaji mpaka kufikia shilingi bilioni 51.1; na kuongeza idadi ya wateja wapya wa benki hadi kufikia wateja milioni moja na laki moja.

**(vi) Twiga Bancorp**

**156. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2016, benki imeweka lengo la kukusanya na kukuza amana za wateja kufikia shilingi bilioni 146.9 kutoka shilingi bilioni 86.3 za Disemba, 2015 hii ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 60.6 au asilimia 71. Aidha, kutokana na shughuli mbalimbali za kibiashara benki inatarajia kukusanya mapato ya jumla ya shilingi bilioni 14.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 11.2 zilizokusanywa mwaka 2015, hii ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 3.5 au asilimia 31 ikilinganishwa na mapato yaliyokusanywa mwaka wa 2015.

**157. Mheshimiwa Spika,** benki kwa kushirikiana na mawakala wa ukusanyaji madeni imejiweka lengo la kukusanya madeni ya shilingi bilioni tano kutoka kwa wateja wa mikopo ambao wamekuwa sugu. Aidha, benki imejiweka lengo la kutoa mikopo kwa wateja mbalimbali itakayofikia shilingi bilioni 70 kutoka shilingi bilioni 37.4 ilivyokuwa Disemba, 2015 hii ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 32.6 au asilimia 88.

**158. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa uwekezaji, benki imeweka lengo la kuwekeza kiasi cha shilingi bilioni 61.6 katika Dhamana za Serikali na Amana za muda maalumu kwenye mabanki ikilinganishwa na Dhamana pamoja na Amana zenye thamani ya shilingi bilioni 39 zilizowekezwa hadi Disemba, 2015. Hili ni ongezeko la shilingi bilioni 22.6 au asilimia 58.



## 4.2.2 Mifuko ya Hifadhi za Jamii

### (i) Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma – PSPF

**159. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2016/17 Mfuko unatarajia kusajili wanachama 30,000 na kuongeza idadi ya wanachama hadi kufikia 476,190 Juni, 2017. Aidha, Mfuko unatarajia kukusanya shilingi bilioni 803.22 kutokana na michango ya wanachama, shilingi bilioni 90.48 mapato kutokana na vitega uchumi mbalimbali, shilingi bilioni 510.92 kutokana na vitega uchumi vilivyo koma na shilingi bilioni 173.64 kutokana na deni la michango kwa Serikali kabla ya Julai, 1999. Mfuko unatarajia kuwekeza shilingi bilioni 554.40 kwenye vitega uchumi, shilingi bilioni 1,040.15 zitatumika kulipa mafao, shilingi bilioni 2.99 zitapewa kwa SSRA kama ada ya mwaka na shilingi bilioni 49.07 zitakuwa gharama za uendeshaji. Mafanikio ya malengo haya yataongeza thamani ya Mfuko kutoka shilingi trilioni 1.46 zinazokadiriwa mwezi Juni, 2016 hadi kufikia shilingi trilioni 1.55 ifikapo Juni, 2017.

### (ii) Mfuko wa Mafao ya Kustaafu – GEPF

**160. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Mfuko utaendelea na jitihada zake za kupanua wigo wa wanachama na hivyo kusajili wanachama zaidi kupitia mpango wa hiari wa kujiwekea akiba ya uzeeni na mpango wa lazima. Mfuko pia utaboresha huduma kwa wanachama kwa kuwekeza zaidi katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, kukuza mapato yatokanayo na uwekezaji kwa kuwekeza katika maeneo salama na yenye kuleta mapato zaidi. Hadi kufikia Juni, 2017 Mfuko unatarajia kusajili jumla ya wanachama 33,007 na kukusanya michango yenye thamani ya shilingi bilioni 81.64. Kadhalika, mapato yatokanayo na uwekezaji yanatarajiwa kuongezeka hadi kufikia Shilingi bilioni 56.90 ifikapo Juni, 2017. Thamani ya Mfuko hadi kufikia Juni, 2017 inatarajiwa kuwa shilingi bilioni 697,217.72.

### (iii) Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma – PPF

**161. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka 2016/17, thamani ya Mfuko inategemea kukua hadi kufikia shilingi trilioni 2.9. Ukuaji huu utatokana na kufikiwa kwa malengo yatakayowekwa katika kukusanya michango kutoka kwa wanachama ya kiasi cha shilingi bilioni 420, kuongezeka kwa uwekezaji utakaoupatia Mfuko mapato yatakayotokana na uwekezaji yanayotarajiwa kufikia shilingi bilioni 260 ifikapo Juni, 2017. Aidha, katika mwaka 2016/17, Mfuko unategemea kuandikisha jumla ya wanachama wapya 66,660 kutoka katika sekta ya umma na binafsi.

#### **4.2.3 Rufani za Kodi.**

**162. Mheshimiwa Spika,** Bodi na Baraza kwa mwaka 2016/17 zitaendelea kusikiliza na kutolea maamuzi rufaa za kodi zitakazowasilishwa ili kuhakikisha kuwa haki inapatikana kwa wakati.

#### **4.2.4 Huduma za Bima**

##### **(i) Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima – TIRA**

**163. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2016/17, Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima imepanga kuanza kutekeleza Sera mpya ya Bima. Sera hii itafungua milango ya uwekaji bima za kilimo na mifugo, bima kwa ajili ya watu wa kipato cha chini ikiwa ni pamoja na kupata huduma za bima kupitia mabenki. Lengo ni kuongeza mchango wa Bima kwenye pato la Taifa kutoka asilimi 0.9 za sasa hadi asilimia 3 ifikapo mwaka 2019.

**164. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imepanga pia kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Elimu ya Bima kwa Umma kwa lengo la kuhakikisha ifikapo mwaka 2017 asilimia 25 ya Watanzania wote wawe wamefikiwa na huduma za bima. Aidha, Mamlaka kwa mwaka 2016/17 imepanga kufanya marejeo ya Sheria ya Bima, Namba 10 ya 2009 ili kuvutia uwekezaji mkubwa katika biashara ya bima wenye lengo la kukidhi mahitaji ya sasa ya soko la bima ndani ya nchi hususan bima za gesi na mafuta.

##### **(ii) Shirika la Bima la Taifa – NIC**

**165. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Shirika litaendelea na mkakati wa kujitangaza zaidi ili kuongeza biashara kwa kubuni bima mpya zitakazokidhi mahitaji ya wananchi, ikiwa ni pamoja na kutumia teknolojia ya mawasiliano kupitia mitandao ya simu za mkononi. Shirika pia litaendelea kutoa elimu ya bima kwa wananchi kupitia njia mbalimbali, kwa mfano redio, luinga na vipeperushi. Pia kukamilisha mipango yote kama ilivyocainishwa kwenye Mpango Mkakati wa Shirika.

#### **4.2.5 Mitaji na Dhamana**

##### **(i) Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana – CMSA**

**166. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Mamlaka ya Masoko na Mitaji imepanga kutayarisha Mpango Mkuu wa Kitaifa wa Maendeleo ya Masoko ya Mitaji (National Capital Market Master Plan); Kukamilisha hatua za kuanzishwa kwa biashara katika Soko la Bidhaa (Tanzania Mercantile Exchange -TMX) ambalo litaanzishwa kwa ubia wa sekta ya umma na binafsi; Kuendelea kuboresha uongozi wa Soko la Hisa la Dar es Salaam ili

kulifanya soko lijiendeshe kibiashara (Exchange Demutualization) na kuondokana na utegemezi kwa Serikali; Kuanzisha misingi ya kusimamia masoko kwa kuzingatia uzito wa athari (risk based supervision) ambapo mahitaji tofauti yatabainishwa kwa taasisi tofauti kulingana na kazi zao; na Kuendelea kushawishi kampuni za umma zinazofanya vizuri kuorodhesha hisa zake katika soko la hisa.

## **(ii) Soko la Hisa la Dar Es Salaam – DSE**

**167. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2016/17, Soko la Hisa la Dar Es Salaam limepanga kuongeza idadi ya kampuni katika Soko la Hisa kwa ushawishi na kuzishauri Serikali na sekta binafsi kuuza hisa zao kupitia soko la hisa; Kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Serikali kuweka mazingira yatakayoweza kampuni za sekta muhimu kama madini na mawasiliano ya simu kuorodheshwa sokoni; Kuanzisha aina mpya za Dhamana za muda mrefu kama hatifungani za Serikali za mitaa na miundo mbinu; Kuongeza ufanisi wa shughuli za minada kwa njia ya simu na mtandao wa intaneti; Kuendelea na juhudi mbalimbali zinazolenga kuongeza ufahamu wa masuala ya masoko ya mitaji kwa umma; na Kuendelea kutoa nafasi kwa wajasiriamali wadogo na wa-kati ili waweze kunufaika na dirisha dogo la DSE la EGM katika kufanikisha malengo yao ya kuanzisha biashara au kuendeleza biashara.

## **4.2.6 Dhamana za Uwekezaji Tanzania**

### **(i) Taasisi ya Huduma za Fedha na Mikopo Tanzania - UTT MFI**

**168. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Taasisi ya Huduma za Fedha na Mikopo Tanzania inatarajia kutoa mikopo kwa wafanyakazi wa umma, wafanyabiashara, na wakulima wapatao 64,715 yenye thamani jumla ya shilingi 43,000,000,000; Kuomba leseni ya kupokea akiba toka kwa wanachama kutoka Benki Kuu ili kupata mitaji wa kujiendesha na kutoa mikopo yenye gharama nafuu kwa wataanzania walio na kipato cha chini; na kufungua matawi mengine manne ili kuwafikishia huduma wananchi wengi zaidi.

### **(ii) Kampuni ya Usimamizi wa Rasilimali za Uwekezaji - UTT AMIS**

**169. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Kampuni ya Usimamizi wa Rasilimali za Uwekezaji itaendelea na jitihada za kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa Mifuko ili kuongeza thamani ya Mifuko na ukuaji wa thamani kwa kila kipande kinachowekezwa. Aidha, kampuni pia itafanya jitihada za kutoa elimu kwa umma ili wananchi waelewe fursa zinazotolewa na mifuko ya uwekezaji wa pamoja na kufanya jitihada ili kuwafikia wataanzania wengi zaidi kwa kutumia teknolojia ya kisasa ili waweze kupata huduma zinazotolewa na UTT AMIS kwa urahisi zaidi.

**(iii) Taasisi ya Miradi na Maendeleo ya Miundombinu - UTT PID**

**170. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2016/17, Taasisi ya Miradi na Maendeleo ya Miundombinu imejiwekea malengo ya kuhakikisha inakuza mtaji kutokana na shughuli zake; Inapanua wigo wa shughuli zake ili kuwafikia wateja wengi zaidi na kuongeza mapato ya taasisi; na kuboresha miundombinu ya taasisi ili iweze kusaidia kumudu changamoto zilizopo.

**4.2.7 Taasisi za Mafunzo**

**(i) Chuo cha Usimamizi wa Fedha – IFM**

**171. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Chuo cha Usimamizi wa Fedha kinatajaria kudahili wanafunzi 8000 katika fani mbali mbali. Chuo kitaendelea kuboresha shughuli zake za utafiti, kutoa machapisho na huduma kwa jamii (research, publication and consultancy). Jumla ya taffiti 9 zinategemewa kufanyika na kukamilika. Kwa upande wa huduma kwa jamii, Chuo kinatarajia kushinda kandarasi 8, pamoja na kuendesha kozi fupi na warsha zisizopungua 20 kwa mwaka 2016/17.

**172. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa ajira mpya na uboreshaji rasilimali watu, Chuo kinatarajia kuajiri watumishi wapya 16, watumishi 10 wanategemewa kupandishwa vyeo, na watumishi 20 wanategemewa kupata nafasi za kuendelea na masomo ya muda mrefu katika mafunzo ya Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu.

**173. Mheshimiwa Spika,** Chuo kitatenga fedha ambazo zitatumika katika kuliendeleza eneo lililopo katika vijiji vya Msata na Kihangaiko Wilayani Bagamoyo Mkoani Pwani kwa awamu ndogo ndogo kwa kadiri hali ya fedha itakavyoruhusu. Aidha, Chuo kimeazimia kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma zake kuu kwa wadau wa ndani na wa nje ya chuo. Huduma hizi ni pamoja na mafunzo kwa wanachuo kuanzia ngazi ya cheti mpaka Shahada ya Uzamili, utafiti na huduma ya utaalum shauri kwa jamii.

**174. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Chuo kinategemea kuanzisha kozi tatu za Shahada za Uzamili ambazo ni “Masters of Science in Insurance and Actuarial Sciences”, “Masters of Science in Social Protection, Planning and Policy” na “Masters of Science in Tax Administration”.

**(ii) Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini – IRDP**

**175. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini kitaendelea kuboresha miundombinu katika Kampasi zake za Dodoma na Mwanza. Miundombinu hiyo itajumuisha ujenzi wa jengo la tatu la mafunzo katika kituo cha Kanda ya Ziwa jijini

Mwanza na kukamilisha ujenzi wa jengo la pili la mafunzo katika Kampasi kuu Dodoma. Aidha, Chuo kinalenga kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi 4622 waliodahiliwa mwaka wa masomo 2015/16 hadi kufikia wanafunzi 5000 mwaka wa masomo 2016/17. Chuo kitaendelea na mkakati wake wa kuendeleza ujuzi na uwezo kwa rasilimali watu katika viwango mbalimbali vya kitaaluma ili kuwawezesha watumishi kutekeleza majukumu yao kwa weledi mkubwa. Vilevile, Chuo kimejipanga kusaidia Serikali za Mitaa na Serikali Kuu kupeleka Madaraka kwa Wananchi kwa kuweka mkakati wa kutoa mafunzo ya Muda Mfupi ya kujenga uwezo kwa watendaji namna ya kupanga, na kusimamia mipango ya mandeleo kwenye maeneo yao ya kazi.

### **(iii) Taasisi ya Uhasibu Arusha – IAA**

**176. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2016/17 Taasisi ya Uhasibu Arusha kinatarajia kuwasilisha mitaala mipya kwa ajili ya kupata ithibati kutoka NACTE. Mitaala hiyo itaainisha kozi katika ngazi ya uzamili zinazotarajiwa kutolewa na Chuo kwa kushirikiana na chuo cha TAMALE POLYTECHNIC cha nchini Ghana. Kozi hizo ni Shahada ya Uzamili ya Biashara, Stashahada ya Uzamili ya Fedha na Uwekezaji na Shahada ya Uhasibu na Ualimu.

### **(iv) Taasisi ya Uhasibu Tanzania – TIA**

**177. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Taasisi ya Uhasibu Tanzania imepanga kukamilisha taratibu za kuanzisha kozi nne mpya ikiwemo ile ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma katika ngazi ya cheti, diploma na shahada ili kutoa wahitimu wenye sifa za kufanya kazi katika Serikali kuu, Serikali za Mitaa na mashirika yasiyo ya Kiserikali. Aidha, Taasisi imepanga kuanza kutoa mafunzo ya shahada ya kwanza katika Kampasi ya Singida na Mwanza ili Watanzania waishio katika mikoa hiyo na ya jirani waweze kupata nafasi ya kujiendeleza kielimu. Taasisi imepanga kuendelea na uboreshaji wa miundo mbinu kwa kuendelea na ujenzi wa majengo mbali mbali katika kampasi ya Mbeya na Dar es Salaam ili kujiweka katika viwango vya taasisi za elimu ya juu.

### **(v) Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika – EASTC**

**178. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2016/17, Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrikakimepanga kuendelea kutoa mafunzo ya takwimu katika ngazi ya cheti cha awali cha takwimu rasmi, Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamili katika takwimu rasmi kwa watumiaji wa Chuo. Aidha, Chuo kinatarajia kutoa mafunzo ya Uzamili katika eneo la Utawala na Biashara. Mafunzo hayo yataendeshwa kwa ushirikiano na Chuo kikuu cha Nargajuma kilichopo nchini India. Vilevile, Chuo kitaendelea kutoa

mafunzo ya awali kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa takwimu wanafunzi waliomaliza elimu za Sekondari kidato cha nne.

**179. Mheshimiwa Spika,** mbali na mafunzo ya muda mrefu, Chuo kitaendelea kujijengea uwezo wake wa ndani katika kusimamia majukumu yake. Maeneo yaliyopewa kipaumbele ni mafunzo kwa wakufunzi, vitendea kazi na upanuzi wa Chuo kupitia Mpango Mkakati wake. Katika kukabiliana na changamoto za ukosefu wa vyumba vya madarasa, kumbi za mikutano na vyumba vya maktaba, katika bajeti ya 2016/17 Chuo kimeandaa bajeti ya miundombinu ya kiasi cha shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kumaliza ujenzi wa jengo la utawala, maktaba, vyumba vya madarasa na mabweni ya wanafunzi.

**180. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika kitaendelea kuzisaidia Wizara, Idara za Serikali, Mashirika ya umma na Makampuni binafsi katika kujenga mifumo ya kukusanya na kuchambua takwimu kwa njia ya mtandao. Mpango huu una lengo la kuhamasisha matumizi ya takwimu sahihi zilizoandaliwa kwa wakati hivyo kuziwezesha Wizara, Idara za Serikali, Mashirika ya umma na Makampuni binafsi kusimamia vema mipango yake ya maendeleo.

#### **4.2.8 Taasisi za Kitaalam na Huduma Nyinginezo**

##### **(i) Mamlaka ya Mapato Tanzania – TRA**

**181. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Mamlaka ya Mapato Tanzania imeweka lengo la kukusanya shilingi bilioni 14,139.016 sawa na ongezeko la asilimia 14.9 ikilinganishwa na matarajio ya makusanyo ya mwaka 2015/16. Aidha, kwa upande wa Zanzibar Mamlaka inategemea kukusanya jumla ya shilingi bilioni 209.21 sawa na ongezeko la asilimia 14.3 ikilinganishwa na matarajio ya mwaka 2015/16.

**182. Mheshimiwa Spika,** ili kudhibiti udanganyifu katika ukadiriaji, Mamlaka kwa mwaka 2016/17 imepanga kutumia njia mbalimbali zikiwemo, ushirikiano na mamlaka nyingine za mapato za nchi jirani katika kubadilishana uzoefu na kupashana habari, kuendelea kuboresha programu za ukaguzi hasa kwa kodi ambazo ukusanyaji wake unaenda kwa misingi ya ukaguzi, kama VAT, kudhibiti usimamizi wa bidhaa zinazopitia hapa nchini kwa ajili ya matumizi ya nchi jirani (*transit cargo*) hasa bidhaa za petrol na kuboresha taaluma kwa wafanyakazi.

**183. Mheshimiwa Spika,** ili kuimarisha mapato kwenye ushuru wa forodha na bidhaa, Mamlaka itaendelea kutekeleza mikakati ifuatayo:- Kutumia mfumo ulioimarishwa wa, *Import Export Commodity Database* (IECD) kwa lengo la



kuboresha na kuimarisha uthamini wa mizigo iingiyayo nchini kutoka nje; Kuimarisha matumizi ya mfumo wa TANCIS kwa lengo la kuboresha makusanyo ya ushuru wa forodha; Kudhibiti usimamizi wa bidhaa zinazopitia hapa nchini kwa ajili ya matumizi ya nchi jirani (*transit*), kuboresha shughuli za ukaguzi baada ya mizigo kutoka bandarini (*Post Clearance*), na kuimarisha ukaguzi wa mizigo gatini Dar es salaam (Dar Wharf); na kuboresha usimamizi wa Mfumo wa Kieletronic wa kufuatilia Mizigo (*Electronic Cargo Tracking System*).

**184. Mheshimiwa Spika,** mikakati mingine itakayotekelezwa na Mamlaka ni pamoja na kufuatilia kwa karibu ulipaji wa kodi kwa mizigo iliyokwisha kadirwa kulipiwa kodi na waagizaji wenyewe wa mizigo hiyo na kuhakikiwa na maafisa wa Forodha lakini Malipo yake bado hayajafanywa; Kuboresha usimamiaji wa bidhaa za mafuta ya petroli zinazolingizwa nchini; Kudhibiti biashara ya magendo katika bahari ya Hindi, mipaka na njia sizzo rasmi kati yetu na nchi za jirani; Kufanya ukaguzi wa ziada kwenye maeneo yenye viashiria vya uvujaji wa mapato, kutambua mapingamizi (*objection*) na kuyapatia ufumbuzi mapema kisheria, na kuboresha vifaa vya kufanyia kazi; na kuendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kusimamia kodi na kudhibiti vitendo vya rushwa kwa kupunguza umuhimu wa mlipakodi kukutana ana kwa ana na msimamizi wa kodi.

## (ii) Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)

**185. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2016/17, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imepanga kuendelea kukusanya, kuchambua, kutunza na kuwasilisha takwimu rasmi zinazohitajika katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii kwa wakati; Kufanya taffiti mbalimbali kama zilivyocainishwa katika Mpango Mkakati ili kukidhi mahitaji yaliyopo; Kuendelea kuchambua takwimu na taarifa mbalimbali zinazotokana na sensa na taffiti za kiuchumi na kijamii zinazofanywa na ofisi sambamba na uchambuzi na utoaji wa machapisho yenye takwimu mbalimbali; na kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar itaendelea na uelimishaji na uhamasishaji wa matumizi ya takwimu rasmi zinazotolewa na Ofisi hizi katika kupanga, kutunga Sera na kufanya maamuzi.

## (iii) Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha – SELF Microfinance Fund

**186. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2016/2017, Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha unakusudia kutoa mikopo ya thamani ya Shilingi bilioni 13.0 huku ikijita katika kuboresha kiwango cha urejeshaji kufikia angalau asilimia 95; Kufungua ofisi ya kanda katika mikoa ya Kaskazini; na kutoa mafunzo kwa viongozi na watendaji wa asasi zipatazo 30, mafunzo ya ujasiriamali kwa walengwa wapao 300 na pia kwa maafisa ushirika wa mikoa 10.



**(iv) Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi – NBAA**

**187. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi imepanga kuendelea kufanya usajili wa watahiniwa, wanachama na makampuni ya uhasibu na ukaguzi; Kufanya ukaguzi na kusimamia ubora wa kazi za ukaguzi; Kutoa miongozo ya viwango vya uhasibu na ukaguzi; Kuendeleza taaluma ya uhasibu; Kutoa mafunzo endelevu kwa wanataaluma na wadau wengine; Kusimamia mradi wa maboresha ya Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu; Kukamilisha ujenzi wa kituo cha wahasibu; Kusimamia uanzishaji wa mitaala mipya katika kuendesha mitihani ya Uhasibu; Kuendelea kushirikiana na mamlaka nyingine za udhibiti kama TRA, BRELA na BoT katika kuhamasisha wadau kuweza kuelewa na kutumia viwango uhasibu na ukaguzi wa hesabu vinavyokubalika.

**(v) Bodi ya Michezo ya Kubahatisha - Gaming Board**

**188. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2016/17, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha inatarajia kukusanya kodi itakayofikia shilingi bilioni 34.72, sawa na ongezeko la asilimia 26.35 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 27.48 inayotarajiwa kukusanywa katika mwaka wa 2015/16. Aidha, Bodi imejipanga kuendelea kusimamia vema sekta ya michezo ya kubahatisha nchini na kuhakikisha kwamba inaendelea kuendeshwa kwa mujibu wa sheria. Bodi inatarajia kuchangia kiasi cha Shilingi bilioni 2.17 kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina katika mwaka 2016/17 hii ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 50.69 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 1.44 ya mwaka wa 2015/16.

**5.1 MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA 2016/17**

**5.2 MAKADIRIO YA MAPATO**

**189. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara inakadiria kukusanya maduhuli kiasi cha shilingi **449,699,727,503** kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mauzo ya nyaraka za zabuni, kodi za pango, mauzo ya leseni za minada na mishahara isiyolipwa, gawio, marejesho ya mikopo na michango kutoka katika taasisi na mashirika ya umma.

**5.3 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2016/17**

**190. Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2016/17 kupitia mafungu yote tisa ya kibajeti inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 8,716,493,400,510 (bilioni 8,716.49)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 45,454,478,000 (bilioni 45.45)** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 8,671,038,922,510 (bilioni**

**8,671.04)** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Kwa upande wa fedha za maendeleo, Wizara ya Fedha na Mipango inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 791,998,424,268 (bilioni 791.99)**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 723,150,000,000 (bilioni 723.15)** ni Fedha za Ndani na **Shilingi 68,848,424,268 (bilioni 68.85)** ni Fedha za Nje. Mchanganuo kwa kila fungu ni kama ifuatavyo:-

## 5.2.1 FUNGU 50 – WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

**191. Mheshimiwa Spika**, katika Fungu hili kwa mwaka 2016/17, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

- (a)** Matumizi ya kawaida - **Shilingi 50,716,878,000 (bilioni 50.72)**. Kati ya hizo:
  - (i)** Mishahara - **Shilingi 6,984,801,000 (bilioni 6.98)**
  - (ii)** Matumizi Mengineyo – **Shilingi 43,732,077,000 (bilioni 43.73)**
- (b)** Miradi ya Maendeleo - **Shilingi 26,035,591,500 (bilioni 26.03)**. Kati ya hizo:
  - (i)** Fedha za Ndani - **Shilingi 9,000,000,000 (bilioni 9.00)**.
  - (ii)** Fedha za Nje - **Shilingi 17,035,591,500 (bilioni 17.03)**.

## 5.2.2 FUNGU 21 – HAZINA

**192. Mheshimiwa Spika**, katika Fungu hili kwa mwaka 2016/17, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

- (a)** Matumizi ya Kawaida - **Shilingi 411,279,240,510 (bilioni 411.28)**. Kati ya hizo:
  - (i)** Mishahara ya fungu hili - **Shilingi 4,474,752,000 (bilioni 4.47)**.
  - (ii)** Matumizi Mengineyo - **Shilingi 406,804,488,510 (bilioni 406.8)** ambazo ni kwa ajili ya matumizi ya idara, taasisi zilizo chini ya Fungu hili, pamoja na matumizi maalum.
- (b)** Miradi ya maendeleo - **Shilingi 740,155,523,400 (bilioni 740.15)**. Kati ya hizo:
  - (i)** Fedha za Ndani - **Shilingi 699,500,000,000 (bilioni 699.5)**

- (ii) Fedha za Nje - **Shilingi 40,655,523,400 (bilioni 40.65)**

### 5.2.3 FUNGU 22- DENI LA TAIFA.

**193. Mheshimiwa Spika**, katika Fungu hili kwa mwaka 2016/17, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

- (a) Matumizi ya Kawaida - **Shilingi 8,009,341,187,000 (bilioni 8,009.34)**. Kati ya hizo:

- (i) Mishahara - **Shilingi 9,340,716,000 (bilioni 9.34)**
- (ii) Matumizi Mengineyo - **Shilingi 8,000,000,471,000 (bilioni 8,000)**

### 5.2.4 FUNGU 23 – MHASIBU MKUU WA SERIKALI

**194. Mheshimiwa Spika**, katika Fungu hili kwa mwaka 2016/17, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

- (a) Matumizi ya Kawaida - **Shilingi 45,585,865,000 (bilioni 45.58)**. Kati ya hizo:-

- (i) Mishahara - **Shilingi 6,784,116,000 (bilioni 6.78)**
- (ii) Matumizi Mengineyo - **Shilingi 38,801,749,000 (bilioni 38.8)**.

- (b) Miradi ya Maendeleo – **Shilingi 4,493,750,000 (bilioni 4.49)** Kati ya hizo:

- (i) Fedha za Ndani - **Shilingi 2,000,000,000 (bilioni 2)**.
- (ii) Fedha za Nje - **Shilingi 2,493,750,000 (bilioni 2.49)**.

### 5.2.5 FUNGU 7 – OFISI YA MSAJILI WA HAZINA

**195. Mheshimiwa Spika**, katika Fungu hili kwa mwaka 2016/17, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

- (a) Matumizi ya Kawaida – **Shilingi 160,181,000,000 (bilioni 160.18)**. Kati ya hizo:-

- (i) Mishahara - **Shilingi 1,974,355,000 (bilioni 1.97)**
- (ii) Matumizi Mengineyo - **Shilingi 158,206,645,000 (bilioni 158.21)**.

(b) Miradi ya Maendeleo – **Shilingi 3,228,540,000 (bilioni 3.23)** Kati ya hizo:

(i) Fedha za Ndani – **Shilingi 650,000,000 (bilioni 0.65).**

(ii) Fedha za Nje – **Shilingi 2,578,540,000 (bilioni 2.58).**

#### **5.2.6 FUNGU 10 – TUME YA PAMOJA YA FEDHA**

**196. Mheshimiwa Spika**, katika Fungu hili kwa mwaka 2016/17, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya Kawaida - **Shilingi 1,374,270,000 (bilioni 1.37).** Kati ya hizo:-

(i) Mishahara - **Shilingi 464,472,000 (bilioni 0.46)**

(ii) Matumizi Mengineyo- **Shilingi 909,798,000 (bilioni 0.91).**

#### **5.2.7 FUNGU 13 – KITENGO CHA UDHIBITI WA FEDHA HARAMU**

**197. Mheshimiwa Spika**, katika Fungu hili kwa mwaka 2016/17, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kwa Matumizi ya Kawaida - **Shilingi 1,603,081,000 (bilioni 1.6).**

#### **5.2.8 FUNGU 45 – OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**

**198. Mheshimiwa Spika**, katika Fungu hili kwa mwaka 2016/17, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

(a) Matumizi ya Kawaida **Shilingi 32,373,096,000 (bilioni 32.37).** Kati ya hizo:-

(i) Mishahara ni **Shilingi 13,870,774,000 (bilioni 13.87)**

(ii) Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 18,502,322,000 (bilioni 18.50)**

(b) Miradi ya Maendeleo Fedha za Nje ni **Shilingi 12,285,427,368 (bilioni 12.28).**

(i) Fedha za Ndani – **Shilingi 8,000,000,000 (bilioni 8.00)**

(ii) Fedha za Nje – **Shilingi 4,285,427,368 (bilioni 4.28)**

## 5.2.9 FUNGU 66 – TUME YA MIPANGO

**199. Mheshimiwa Spika**, katika Fungu hili kwa mwaka 2016/17, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

- (a) Matumizi ya kawaida - **Shilingi 4,038,783,000 (bilioni 4.04)**. Kati ya hizo:
  - (i) Mishahara - **Shilingi 1,560,492,000 (bilioni 1.56)**
  - (ii) Matumizi Mengineyo - **Shilingi 2,478,291,000 (bilioni 2.48)**
- b) Miradi ya Maendeleo – **Shilingi 5,799,592,000 (bilioni 5.79)**. Kati ya hizo:
  - (i) Fedha za Ndani - **Shilingi 4,000,000,000 (bilioni 4)**.
  - (ii) Fedha za Nje - **Shilingi 1,799,592,000 (bilioni 1.79)**.

**200. Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maombi ya fedha kwa mafungu Tisa niliyoyataja katika aya ya 190 ya kitabu cha hotuba yangu, nichukue fursa hii pia kuwasilisha maombi ya fedha kwa mwaka 2016/17 kwa ajili ya Mfuko wa Mahakama (Fungu 40) na Mfuko wa Bunge (Fungu 42). Maombi haya ni kwa mujibu wa marekebisho yaliyofanyika kwenye kifungu cha 59 kifungu kidogo cha 3 cha Sheria ya Utawala wa Mahakama Sura 237 na kifungu cha 29 kifungu kidogo cha 3 cha Sheria ya Utawala wa Bunge, Sura 115, kupitia Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015. Sheria hizi zinampa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kuwasilisha Bungeni maombi ya fedha za matumizi ya mifuko hii.

**201. Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia sheria hii, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishhe jumla ya **Shilingi 230,693,160,000 (bilioni 230.69)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa mafungu haya mawili. Kati ya hizo, **Shilingi 176,931,426,000 (bilioni 176.93)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 53,761,734,000 (bilioni 53.76)** ni kwa ajili ya miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:-

## 5.2.10 FUNGU 40 – MFUKO WA MAHAKAMA

**202. Mheshimiwa Spika**, katika Fungu hili kwa mwaka 2016/17, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

- (a) Matumizi ya kawaida - **Shilingi 84,865,309,000 (bilioni 84.86)**. Kati ya hizo:-
  - (i) Mishahara - **Shilingi 50,345,775,000 (bilioni 50.35)**

(ii) Matumizi Mengineyo – **Shilingi 34,519,534,000 (bilioni 34.52)**

**(b)** Miradi ya Maendeleo - **Shilingi 46,761,734,000 (bilioni 46.76)**.  
Kati ya hizo:-

(i) Fedha za Ndani - **Shilingi 24,000,000,000 (bilioni 24.00)**.

(ii) Fedha za Nje - **Shilingi 22,761,734,000 (bilioni 22.76)**.

#### **5.2.11 FUNGU 42 – MFUKO WA BUNGE**

**203. Mheshimiwa Spika**, katika Fungu hili kwa mwaka 2016/17, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

**(a)** Matumizi ya kawaida - **Shilingi 92,066,117,000 (bilioni 92.07)**. Kati ya hizo:-

(i) Mishahara - **Shilingi 23,798,609,000 (bilioni 23.80)**

(ii) Matumizi Mengineyo – **Shilingi 68,267,508,000 (bilioni 68.27)**

**(b)** Miradi ya Maendeleo Fedha za Ndani - **Shilingi 7,000,000,000 (bilioni 7.00)**.

#### **5.3 SHUKRANI**

**204. Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie nafasi hii kuzishukuru nchi na mashirika mbalimbali ya kimataifa ambayo kwa namna moja ama nyingine yamesaidia katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara. Kwanza napenda kuzishukuru nchi za Finland, Uingereza kupitia shirika la DFD, Canada, Denmark kupitia shirika la DANIDA, Ireland, Japan kupitia shirika la JICA, Marekani, Norway, Sweden, Uholanzi na Ujerumani. Pia taasisi mbalimbali za kimataifa ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia, Global Fund, Umoja wa Ulaya, na Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya UNFPA na UNDP.

**205. Mheshimiwa Spika**, Napenda pia kuwashukuru sana wafanyakazi na wananchi wote ambao wameendelea kulipa kodi kwa hiari na pia kushiriki katika ujenzi wa Taifa letu. Ni imani yangu kuwa juhudi hizi zinazochukuliwa na Serikali yetu na wananchi zitatuwezesha kufikia malengo yetu ya kukuza uchumi na kupambana na umaskini.

**206. Mheshimiwa Spika**, mwisho kabisa napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara ([www.mof.go.tz](http://www.mof.go.tz)).

**207. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:**Hoja imeungwa mkono sasa tutamsikiliza Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Wakati Mwenyekiti wa Bajeti akija kwenye sehemu ya kuzungumzia kuna mgeni mmoja nimeletewa tangazo hapa hakuwa ameorodheshwa kwenye orodha iliyopita na huyu ni Profesa Mussa Assad, Mhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambaye ameambatana na Maafisa waandamizi kutoka kwenye ofisi yake, karibuni sana. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana awali ya yote naomba nishukuru fursa niliyojaliwa na Mwenyezi Mungu kusimama mbele yako na kusoma taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 99(7) na (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2015/2016 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Ambayo inajumuisha Fungu 50 - Wizara ya Fedha, Fungu 21 - Hazina, Fungu 22 - Deni la Taifa, Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali, Fungu 13 - Kitengo cha Udhhibiti na Utakatishaji wa Fedha Haramu, Fungu 66 - Tume ya Mipango, Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha na Fungu 7 - Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 kinaipa mamlaka Kamati ya Bajeti kupitia na kuridhia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama, Bunge na Ofisi ya Mkaguzi na Mhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. Sheria inaitaka Kamati ya Bajeti kufanya mashauriano na Serikali na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama- Fungu 40, Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi - Fungu 45 na Mfuko wa Bunge - Fungu 42 na baada ya mashauriano Waziri wa Fedha atawasilisha Bungeni kwa ajili ya kupitishwa. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Toleo la Januari 2016 Nyongeza ya Nane Sehemu ya (3)(9)(a) inaipa Kamati ya Bajeti jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha unaofuata na kulishauri Bunge ipasavyo kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilikutana mwezi Aprili, 2016 jijini Dar es Salaam na kupokea taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2015/2016 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara na mafungu yake kwa mwaka 2016/2017.



Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Bajeti za mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2015/2016. Hotuba iliyotolewa na Waziri wa Fedha na Mipango inatoa taswira halisi ya utekelezaji wa bajeti ya mafungu yake kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Kamati imefanya tathmini katika mafungu nane yaliyo chini ya Wizara hii na kuona yapo baadhi ya mafungu ya Wizara yamepata fedha ya kutosha na hivyo kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, yapo mafungu ambayo hayajapatiwa fedha za kutosha na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu yao, rejea jedwali namba nne lililopo kwenye taarifa yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa utekelezaji wa bajeti ya mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango unatia shaka ukizingatia kwamba kati ya mafungu nane, ni mafungu mawili tu Fungu 22 - Deni la Taifa na Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali ndio aliyopokea zaidi ya asilimia 70 ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge hadi kufikia mwezi Machi, 2016. Mafungu mengine sita yamepokea fedha chini ya asilimia 50 ya fedha iliyoidhinishwa, hivyo ni dhahiri kwamba utekelezaji wa shughuli nyingi za Wizara umeathirika kwa kiasi kikubwa.

Kwa kuzingatia mgawanyo wa majukumu na wajibu wa Serikali, *Government Instrument of 2016*, Wizara hii ina jukumu la kusimamia Sera ya Fedha (*Monetary Policy*) pamoja na Matumizi (*Fiscal Policy*) pamoja na kusimamia kanuni na taratibu za fedha nchini, Kamati inaona kuwa mwenendo huu wa utolewaji wa fedha uliopo ndani ya mafungu ya Wizara ya Fedha hautoi tija kwa mafungu haya kutekeleza majukumu yao ya msingi kwa kuzingatia sheria. Mfano mzuri tunauona kwenye Ofisi ya Msajili wa Hazina ambaye ndiye msimamizi mkuu wa mashirika ya umma imepokea asilimia nane tu ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako. Hapa Kamati inajiuliza kwa kiasi hiki cha fedha ofisi hii itatimizaje malengo yake? Hali kadhalika sura hii tunaona kwa Fungu 10, 13, 21 na 66.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango ijitathmini na kujitambua kuwa ndio Wizara Mama na inatakiwa kuwa mfano wa kuigwa katika kuhakikisha inasimamia na kutekeleza majukumu yake ya msingi hasa katika kutoa fedha kwa mafungu yake na mengine. Endapo mwenendo wa utoaji fedha utabaki kama ilivyo utaathiri kwa kiasi kikubwa utendaji kazi wa mafungu mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maombi ya Fedha kwa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Fedha na Mipango katika mwaka wa fedha 2016/2017 inakadiriwa kutumia jumla ya shilingi 9,383,606,520,094 kwa mafungu yote nane; katika fedha hizo, shilingi 31,583,704,480 ni kwa ajili ya

mishahara, shilingi 8,640,642,740,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengine (OC) ambayo yanajumuisha malipo ya Deni la Taifa la jumla ya shilingi 8,000,000,471,000 na matumizi ya kawaida shilingi 640,242,269,000 na shilingi 711,780,075,615 kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo ambapo fedha za ndani ni shilingi 659,650,000,000 na fedha za nje ni shilingi 52,130,075,614.

Aidha, Wizara imepanga kukusanya jumla ya shilingi 449,694,722,509 kutoka katika vyanzo vya ndani vya mapato ikiwa ni pamoja na mauzo ya nyaraka za zabuni, kodi za pango, mauzo ya leseni, minada, mishahara isiyolipwa, gawio, marejesho ya mikopo na michango kutoka katika taasisi za mashirika ya umma. Mchanganuo wa maombi ya fedha umeanishwa katika jedwali la pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa bajeti ya Mifuko ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Mahakama na Bunge kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Pamoja na kwamba utekelezaji wa Bajeti ya Mifuko ya Mahakama na Bunge kuwasilishwa katika utekelezaji wa Bajeti za kisekta husika, Kamati imeona ni vyema ikatoa picha ya utekelezaji wa Bajeti za Mifuko yote mitatu ili kutoa picha ya utekelezaji kabla ya kuwasilisha maombi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi; katika mwaka wa fedha 2015/2016 Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi iliidhinishiwa jumla ya shilingi 82,819,486,000 kati ya fedha hizo shilingi 14,209,421,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 57,942,949,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 10,667,116,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2016, Ofisi ya Taifa Ukaguzi ilikuwa imepokea shilingi 37,484,851,182 sawa na asilimia 45.3 ya bajeti iliyokuwa imeidhinishiwa. Kati ya fedha hizo shilingi 10,059,558,616 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi 25,608,736,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 1,818,556,966 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo ni fedha zote kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ilipanga kukusanya kiasi cha shilingi 8,638,120,000 hadi kufikia mwezi Machi 2016, ilikuwa umekusanya kiasi cha shilingi 7,374,747,484 sawa na asilimia 85.4 ya matarajio kwa mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Mfuko wa Mahakama uliidhinishiwa jumla ya shilingi 150,241,280,000 kati ya fedha hizo shilingi 86,435,365,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, shilingi 51,485,099,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 12,320,414,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2016, Mfuko wa Mahakama ulikuwa umepokea jumla ya shilingi 91,682,915,307 sawa na asilimia 61 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu; kati ya fedha hizo shilingi 35,543,784,998 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi 43,889,130,376 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida

na shilingi 12,300,000,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo ni fedha zote za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa jumla ya shilingi 173,768,567,000 kati ya fedha hizo shilingi 19,413,630,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 177,354,937,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 7,000,000,000 ni fedha kwa ajili ya maendeleo. Hadi kufika mwezi Machi, 2016, Mfuko wa Bunge uliweza kupata shilingi 86,257,667,730 sawa na asilimia 49.6 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako, kati ya fedha hizo shilingi 10,934,993,610 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi 68,322,774,120 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 7,000,000,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo ni fedha zote zinatoka ndani. Mchanganuo unajionyesha kwenye jedwali la tatu kwenye taarifa yangu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maombi ya fedha kwa Mfuko wa Mahakama, Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Bajeti Namba 11 ya mwaka 2015, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilijadili na kufanya mashauriano na Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Watendaji Wakuu wa Mfuko wa Mahakama, Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (*National Audit*) pamoja na Mfuko wa Bunge kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya mifuko hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mifuko tajwa iliwasilisha kwenye Kamati mapendekezo ya awali kuhusu bajeti zao zilizozingatia uzoefu wa miaka mingi katika uendeshaji wa taasisi hizo pamoja na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi husika. Kufuatia azma ya Serikali ya kupunguza asilimia 60 ya bajeti ya matumizi mengineyo yaani OC ya mafungu yote ili fedha hizo ziende kwenye miradi ya maendeleo, hatua hiyo ilisababisha mifuko hiyo kupewa ukomo wa Bajeti mdogo ukilinganisha na fedha halisi zilizoombwa na mifuko husika. Kamati ya Bajeti iliona hili na kufanya mashauriano na Wizara ya Fedha pamoja na mifuko husika na kwa kuzingatia mahitaji ya msingi ya mifuko na kukubaliana mifuko hiyo izingatie ukomo wa Bajeti iliyotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasisitiza bado kuna umuhimu wa kuhakikisha mifuko husika inapatiwa fedha za kutosha ili iweze kuendeshwa kwa ufanisi na tija kama kifungu cha 23(4) cha Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 kinavyoelekeza. Kamati itahakikisha inafanya mapitio ya nusu mwaka ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2017 yaani *mid year review* kama ilivyo elekezwa kwenye Sheria ya Bajeti kifungu 9(1) kipengele (h) ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya mifuko hii kwa kipindi cha nusu mwaka na hatimaye kulishauri Bunge ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liridhie maombi ya shilingi 131,627,043,000 kwa ajili ya Fungu 40 ambao ni Mfuko wa Mahakama na shilingi 99,066,117,000 kwa ajili ya Fungu 42 ambao ni Mfuko wa Bunge na shilingi 44,658,523,368 kwa ajili ya Fungu 45 - Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Mifuko hiyo kiufanisi na kuleta tija inayokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Kamati kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2015/2016 pamoja na maombi ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2016/2017; Kamati inapendekeza kutoa maoni na mapendekezo yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa utolewaji wa fedha kwa mafungu yaliyo chini ya Wizara ya Fedha pamoja na Mifuko kama ilivyo idhinishwa na Bunge. Kamati imefanya tathmini ya ujumla ya mwenendo wa utolewaji wa fedha za utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2015/16 kwa mafungu yaliyo chini ya Wizara ya Fedha na kuona haukuwa wa kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Machi 2016, kati ya mafungu nane ya Wizara hii na Mifuko mitatu ni mafungu mawili tu yaani Fungu 22 - Deni la Taifa na Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali yaliweza kupata fedha zaidi ya asilimia 70 ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka 2015/2016. Kwa mwenendo huu inaonyesha kuwa jukumu la Wizara ya Fedha ambaye ndiye msimamizi na mtoaji wa fedha kwa Wizara nyingine litakuwa limeathirika kwa kiwango kikubwa na hivyo kupelekea kushindwa kutekeleza jukumu hili kwa Wizara nyingine. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujidhihirishia hili, mfano mzuri tunauona kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kwamba kati ya mafungu 62 ya Serikali Kuu, mafungu 33 yamebainika kupewa asilimia chini ya 50, mafungu 29 yamepewa zaidi ya asilimia 50 na mafungu matatu yamepewa zaidi ya asilimia 100 ya fedha zote za matumizi kama ilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inataka Wizara ya Fedha na Mipango izingatie majukumu ya mafungu yake sambamba na kutoa fedha iliyobakia kwa mafungu yake kama ilivyoidhinishwa na Bunge ili yaweze kusimamia utekelezaji wa kibajeti kwa mafungu mengine ya Wizara na Idara za Serikali, hii tunasisitiza katika hiki kipindi ambacho kimebaki ni vizuri Wizara ya Fedha ikahakikisha kwamba inamalizia kutoa pesa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha. Kamati inatambua jukumu la Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ni kusimamia Sheria ya fedha ya mwaka 2001 yaani (*Public Finance Act*)

na utayarishaji na usimamizi wa Hesabu za Serikali. Pia Kamati inatambua juhudi za Idara hii katika kuboresha mifumo mbalimbali ya malipo ya kielektroniki yenye viwango vya kimataifa vya uhasibu kama vile *EPICOR-IFMs* na *TISS*, pamoja na uboreshaji wa utayarishaji wa hesabu kwa viwango vya kimataifa (*IPSAS Accrual*). Hatua hizi, zimewezesha kuimarisha usimamizi wa fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo Kamati inaona bado kuna changamoto kubwa zifuatazo ambazo Serikali inabidi izifanyie kazi haraka ili kuongeza ubora wa usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma:-

(i) Kuharakisha usambazaji wa Mkongo wa Taifa ili kupata mawasiliano ya kimtandao (*internet*) kwa Wizara, Idara za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuongeza ufanisi wa malipo kwa wakati.

(ii) Serikali ihakikishe inahaulisha mifumo mbalimbali ya taarifa za watumishi pamoja na mapato na matumizi ya Serikali kwa ufanisi. Mfano *kazi data* yaani *LAWSON* hauingiliani na mfumo wa *IFMS*.

(iii) Serikali ihakikishe inaongeza ukusanyaji wa mapato ili kufikia malengo ya ukusanyaji kila mwaka na hatimaye kuondokana na utaratibu wa *Cash Budget* na kwenda kwenye utaratibu wa *Accrual Budget*. (*Makofi*)

(iv) Kuhakikisha Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaboresha utayarishaji wa hesabu kwa viwango vya kimataifa (*IPSAS Accrual*) ili kuboresha uwazi zaidi katika mapato na matumizi ya fedha za umma.

(v) Kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Msajili wa Hazina ina jukumu la kusimamia uwekezaji wa Serikali katika Mitaji ya Mashirika na Taasisi za Umma na makampuni binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza hatua ya Serikali kutenga kiasi cha shilingi 169,017,000,000 kwa mwaka 2015/2016; kwa ajili ya kulipia madeni na kurekebisha mashirika yenye matatizo ya mitaji. Pamoja na hatua hii nzuri, hadi kufikia mwezi Machi, 2016 Serikali imetoa kiasi cha shilingi bilioni 10.03 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua ufinyu wa Bajeti uliopo hata hivyo ni vema Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ikawa inajipanga katika kukamilisha vipaumbele vyake. Uimarishaji na usimamizi mzuri wa mashirika ya umma kama yale ya *ATCL*, *TTCL*, *TRL* na mengine utatoa fursa ya

upatikanaji wa mapato yatakayosaidia Serikali kugharamia kikamilifu Bajeti yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Ofisi ya Msajili wa hazina ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi 342,530,000,000 kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato yasiyo ya kodi. Kati ya fedha hizo shilingi 142,530,000,000 zinatokana na gawio, michango ya asilimia 15 na makusanyo ya mapato yatokanayo na makusanyo ya Mtambo wa Udhambi wa Mawasiliano unaojulikana kama *Telecommunication Traffic Monitoring Systems (TTMS)* na shilingi 200,000,000,000 zinatokana na mauzo ya hisa zake asilimia 4 kutoka Kampuni ya Bia (*TBL*) na asilimia 2.5 katika Kampuni ya Sigara (*TCC*).

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi mwezi Februari, 2016 Ofisi ya Msajili ilikuwa imekusanya shilingi 344,470,000,000 sawa na asilimia 114.78 ya makadirio yote. Pamoja na nia njema ya Serikali kuuza hisa zake katika makampuni hayo ili kuchangamsha soko la hisa na kuwawezesha wananchi kushiriki katika uchumi bado kuna haja ya Serikali kuendelea kuwekeza kwenye makampuni mbalimbali kama vile makampuni ya gesi na madini ili kupanua wigo wa vyanzo vya mapato ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Tano kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina inaendelea na zoezi la kufanya uperembaji na ufuatiliaji kwa Mashirika na Makampuni yaliyobinafsishwa kwa lengo la kuangalia endapo....

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa yangu yote iingie kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge (*Hansard*). Dakika ngapi bado?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Tano kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina inaendelea na zoezi la kufanya uperembaji na ufuatiliaji kwa Mashirika na Makampuni yaliyobinafsishwa kwa lengo la kuangalia endapo kwa lengo la kuangalia endapo yatafanya kazi iliyokusudiwa. Kamati inaona kuwa hatua hii itaiwezesha kuyarudisha Serikalini Mashirika ambayo yamekiuka masharti ya kimkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, Kamati inashauri Serikali kuwa makini inapotekeleza jambo hili kwa kuzingatia sheria na mikataba ambayo Serikali iliingia wakati wa uuzaji, kinyume na hapo tunaweza kuliingiza Taifa katika hasara kubwa kwa kuwalipa wawekezaji ambao mikataba yao itavunjwa bila kufuata taratibu husika. Aidha, zoezi hili likamilike haraka iwezekanavyo ili kutimiza malengo ambayo Serikali imekusudia katika kutekeleza suala hili.



Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa upande wa Soko la Mitaji; Tanzania imekwisha kuchukua hatua za awali za kufungua soko la mitaji Tanzania (*Liberalization of Capital Market*). Inaeleweka kwamba umiliki wa hisa ni aina mojawapo ya uwezesaji wananchi kiuchumi kwa mataifa mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuendeleza juhudi za makusudi za kuboresha mazingira ya mfumo wa Soko la Mitaji ili liweze kukidhi mahitaji ya Watanzania. Muda umefika sasa kwa Mamlaka ya Soko la Mitaji (*Capital Market and Securities Authority*) kuanza kuhakikisha makampuni makubwa ya ndani na nje yanawekeza kwenye Soko la Mitaji la hapa nchini (*DSE*) ikiwa pamoja na kuhamasisha kuuza baadhi ya hisa zao kwa Watanzania. Hatua hii ni muhimu sana katika kuwawezesha Watanzania kumiliki uchumi wao na kuwezesha kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya eneo ambalo Serikali ina changamoto kubwa ya kulitua ni eneo linalohusu madeni ya mifuko ya jamii ambayo kwa pamoja yanaidai Serikali zaidi ya shilingi trilioni sita. Pamoja na kuwa Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ilionyesha nia njema (*commitment*) ya kulipa madeni haya likiwemo lile kubwa la *PSPF*, bado utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano katika mwaka wa fedha 2015/2016, Serikali iliahidi kutoa kiasi cha shilingi bilioni 150 pamoja na kutoa *non cash bond* ya kiasi cha shilingi trilioni 2.6 ili kulipia deni la *PSPF*. Hadi sasa ni shilingi bilioni 83 tu zilizotolewa na hakuna *non cash bond* yoyote iliyotolewa. Kamati inaona kuwa madeni haya ni fishio kubwa linaloathiri utekelezaji wa majukumu ya mifuko husika hasa la ulipaji wa pensheni ya wastaafu wanaongezeka kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja ya kwamba kwa mwaka huu wa fedha 2016/2017, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 157 kulipa malimbikizo ya deni hilo, Kamati inaitaka Serikali kuongeza kasi ya ulipaji madeni ya Mifuko ya Jamii pamoja na kutimiza ahadi yake ya kutoa *non cash bond* ya trilioni 2.6 kwa Mfuko wa *PSPF* ili uweze kuweza kupunguza mzigo mkubwa wa malipo ya wastaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa *Village Empowerment* maarufu kama milioni 50 kwa kila kijiji. Mradi huu wa *Village Empowerment* maarufu kama milioni 50 kwa kila kijiji. Mradi huu unalenga kutenga kiasi cha milioni 50 kwa kila kijiji kwa ajili ya kukopesha vikundi vya ujasiriamali kupitia Ushirika wa Kuweka na Kukopa (*SACCOS*) katika vijiji husika.



Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kwamba Tanzania bara ina jumla ya vijiji 19,600 ambavyo vinahitaji jumla ya shilingi bilioni 980 ili kila kijiji kupata shilingi milioni 50. Fedha iliyotengwa chini ya Fungu 21- Idara ya Bajeti ya Serikali chini ya mradi uitwao *Village Empowerment* ni shilingi 59,500,000,000 ambazo ni sawa na asilimia sita tu ya fedha zote zinazohitajika ili kuweza kuhudumia vijiji hivyo na hii inaweza kuchukua vijiji 1,190.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala hili ni mradi wa maendeleo na linahitajika kutekelezeka ndani ya miaka mitano; Kamati ya Bajeti inaishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

(i) kuongeza fedha hizi mpaka kufikia shilingi 196,000,000,000 sawa na asilimia 20 ya fedha zote zinazohitajika ili mradi ukamilike ndani ya miaka mitano.

(ii) kufanya utafiti wa kutosha kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi (*National Economic Empowerment Council*) ambao ndio wasimamizi na wawezeshaji ili kuwanda wananchi katika vijiji na kuhakiki utendaji na ufanisi wa SACCOS na Ushirika katika utoaji wa mikopo.

(iii) Wakati taratibu zinakamilika utoaji wa mikopo hii zikiendelea fedha za mradi huu ziwekwe katika Benki ya Kilimo na kuandaa dirisha maalum litakaloshughulikia mikopo hii. Aidha, utaratibu wa utoaji wa mikopo hii uwe shirikishi katika ngazi zote za kiutawala. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa angalizo hili ili kuepuka mradi huu kutofikia malengo yake kama ilivyokuwa kwa Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kukuza Ajira - maarufu kama Mabilioni ya JK ambao wajanja wachache wasiostahili walifaidika na kuwaacha vijana wakilalamikia utaratibu uliokuwa umelenga kuwakopesha wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya maeneo yaliyosababisha Serikali kupoteza kiasi kikubwa cha fedha ni uwepo wa watumishi hewa. Kulingana na taarifa iliyotolewa na Mheshimiwa Rais siku ya wafanyakazi tarehe 01 Mei, 2016 ni kwamba Serikali imebaini watumishi hewa 10,295, kati ya hao watumishi 8,373 wanatoka Serikali za Mitaa na watumishi 1,922 wanatoka Serikali Kuu. Watumishi hao wamekuwa wakilipwa shilingi bilioni 11...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa yote iingie kwenye *Hansard* na naunga mkono hoja. (Makofi)

**TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16 PAMOJA NA MAKADIRIO YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) na (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2015/16 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2016/17 ambayo hujumuisha Fungu 50 - Wizara ya Fedha, Fungu 21- Hazina, Fungu 22 - Deni la Taifa, Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali; Fungu 13 - Kitengo cha Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha haramu; Fungu 66 - Tume ya Mipango; Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha na Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 9 (1), (c) Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 kinaipa mamlaka Kamati ya Bajeti ya kupitia na kuridhia makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama, Bunge na Ofisi ya Mkaguzi na Mdhambi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Sheria inaitaka Kamati ya Bajeti kufanya mashauriano na Serikali na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama (Fungu 40), Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (Fungu 45) na Mfuko wa Bunge (Fungu 42) na baada ya mashauriano Waziri wa fedha atawasilisha Bungeni kwa ajili ya kupitishwa. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge toleo la Januari 2016 nyongeza ya Nane, Sehemu ya tatu 9 (a) inaipa Kamati ya Bajeti jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha unaofuata na kulishauri Bunge ipasavyo kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana mwezi Aprili, 2016 jijini Dar es Salaam na kupokea Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2015/16 pamoja na makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara na mafungu yake kwa Mwaka wa Fedha 2016/17.

**2.0 MAPITIO YA UJUMLA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MAJUKUMU YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa Fedha 2015/16, Wizara ya Fedha na Mipango kwa mafungu yote manane (8) iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 8,328,509,387,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 72,659,909,000** kwa ajili ya Mishahara (PE), **Shilingi 6,390,465,067,000** ni kwa ajili ya kulipia deni la Taifa na **Shilingi 844,292,763,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC). Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi**

**1,021,091,648,000** ambapo fedha za ndani zilikuwa **Shilingi 370,354,448,000** na fedha za nje zilikuwa **Shilingi 650,737,200,000**. Wizara ilikadiriwa kukusanya maduhuli ya **Shilingi 145,060,000,000** kutokana na mauzo ya nyaraka za zabuni, kodi za pango, mauzo ya leseni za minada, mishahara isiyolipwa, gawio kutokana na hisa za Serikali, marejesho ya mikopo na michango kutoka katika Taasisi na Mashirika ya Umma.

**Mheshimiwa Spika**, Mwenendo wa matumizi unaonyesha kuwa, hadi kufikia mwezi Machi, 2016 jumla ya **Shilingi 4,984,790,506,028.08** zilipokelewa; Kati ya fedha hizo **Shilingi 74,419,273,435** zilitumika kwa ajili ya mishahara (sawa na asilimia 102.4 ya fedha zilizoidhinishwa hii imetokana na mishahara ya wafanyakazi wa TRA kuingizwa kwenye kifungu cha mishahara cha fungu 21, ambapo awali ilikuwa chini ya kifungu cha matumizi mengineyo); na kiasi cha **Shilingi 4,886,279,533,417** kilipokelewa na kutumika kwa ajili ya matumizi mengineyo (sawa na asilimia 67.7 ya fedha iliyoidhinishwa). Miradi ya maendeleo hadi kufikia mwezi Machi 2016 ilipokea jumla ya **Shilingi 24,091,699,176** (sawa na asilimia 2 ya fedha zote zilizoidhinishwa). Kati ya fedha hizo **Shilingi 21,413,499,176** zilikuwa fedha za nje na **Shilingi 2,678,200,000.00** zilikuwa fedha za ndani. Aidha, Maduhuli yaliyokuwa yamekusanywa hadi kufikia Mwezi Machi 2016, yalifikia Shilingi **129,920,000,000** sawa na asilimia 90 ya makadirio.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango hasa ya kusimamia Sera ya Uchumi jumla; Kusimamia mapato na matumizi ya fedha za Umma; Kuboresha usimamizi wa ukusanyaji maduhuli katika Taasisi za Serikali Kuu na Serikali za mitaa; Kuimarisha thamani ya Shilingi kwa lengo la kuwa na sarafu imara; Kuendelea kuhakikisha uchumi unakuwa kwa kasi; na Kuongeza mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi wa kibajeti. Aidha, Kamati imeendelea kutoa ushauri, maoni na mapendekezo mbalimbali kwa Wizara ya Fedha na Mipango yenye lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu yake ya msingi.

### **3.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA MAFUNGU YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16 .**

**Mheshimiwa Spika**, hotuba iliyotolewa na Waziri wa Fedha na Mipango imetoa taswira halisi ya utekelezaji wa bajeti ya Mafungu yake kwa mwaka wa fedha 2015/16. Kamati imefanya tathmini katika mafungu Nane yaliyo chini ya Wizara hii na kuona yapo baadhi ya mafungu ya Wizara yamepata fedha za kutosha na hivyo kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, yapo mafungu ambayo hayajapatiwa fedha za kutosha na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu yao. (Rejea Jedwali Namba 1).

**Mheshimiwa Spika**, tathmini inaonyesha hadi kufikia mwezi Machi 2016, **Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango** lilipokea jumla ya Shilingi **48,496,535,452** sawa na asilimia 11.41 ya fedha zilizoidhinishwa; **Fungu 21 - Hazina** lilipokea jumla ya Shilingi **189,346,624,336** sawa na asilimia 15.20 ya fedha zilizoidhinishwa; **Fungu 22 - Deni la Taifa** lilipokea jumla ya Shilingi **4,651,741,834,652.08** sawa na asilimia 72.79 ya Bajeti iliyoidhinishwa; **Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali** lilipokea jumla ya Shilingi **76,250,462,743** sawa na asilimia 95.52 ya fedha zilizoidhinishwa; **Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina** lilipokea jumla ya Shilingi **14,196,328,053** sawa na asilimia 8.06 ya fedha zilizoidhinishwa; **Fungu 13 - Kitengo cha Udhhibiti wa Fedha Haramu** lilipokea jumla ya Shilingi **481,289,614** kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 49.91 ya fedha zilizoidhinishwa na hakukuwa na fedha zozote za maendeleo zilizotolewa kwa fungu hili. Pia, **Fungu 66 – Tume ya Mipango** lilipokea jumla ya Shilingi **3,618,995,527** sawa na asilimia 42.25 ya fedha zilizoidhinishwa; **Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha** lilipokea jumla ya Shilingi **658,435,651** sawa na asilimia 35.92 ya fedha zilizoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo wa utekelezaji wa Bajeti ya Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango unatia shaka ukizingatia kwamba kati ya mafungu nane (8), ni mafungu mawili (2) tu (*Fungu 22 - Deni la Taifa na Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali*) ndio yaliyopokea zaidi ya asilimia 70 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge hadi kufikia mwezi Machi 2016. Mafungu mengine sita yamepokea fedha chini ya asilimia 50 ya fedha zilizoidhinishwa, hivyo ni dhahiri kwamba utekelezaji wa shughuli nyingi za Wizara umeathirika kwa kiasi kikubwa. Kwa kuzingatia mgawanyo wa majukumu na wajibu wa Serikali (*Government Instrument of 2016*), Wizara hii ina jukumu la kusimamia Sera ya Fedha (*Monetary Policy*) na Mapato na Matumizi (*Fiscal Policy*) pamoja na kusimamia Kanuni na Taratibu za Fedha nchini. Kamati inaona kuwa mwenendo huu wa utolewaji wa fedha uliopo ndani ya mafungu ya Wizara ya Fedha hautoi tija kwa mafungu haya kutekeleza majukumu yao ya msingi kwa mujibu wa sheria. Mfano mzuri tunauona kwenye Ofisi ya Msajili wa Hazina ambaye ndiye msimamizi Mkuu wa Mashirika ya Umma imepokea asilimia 8 tu ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Hapa Kamati inajiuliza kwa kiasi hiki cha fedha ofisi hii itatimizaje malengo yake? Hali kadhalika sura hii tunaiona kwa Fungu 10, 13, 21 na 66. Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango ijitathmini na kujitambua kuwa ndio Wizara Mama inatakiwa kuwa mfano wa kuigwa katika kuhakikisha inasimamia na kutekeleza majukumu yake ya msingi hasa katika kutoa fedha kwa mafungu yake na mengine. Endapo mwenendo wa utoaji fedha utabaki kama ilivyo utaathiri kwa kiasi kikubwa utendaji kazi wa mafungu mengine.

## Jedwali Namba 1: Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Taasisi zilizo chini yake hadi mwezi Machi 2016

Jedwali 1: Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango na Taasisi zilizo Chini yake hadi mwezi Machi, 2016.							
N a	FUNGU	MISHAHARA	OC	MAENDELEO	JUMLA YA FEDHA ZILIZOPOKELEWA	FEDHA ZILIZOIDHINISH WA	ASILIMIA YA UTEKELEZAJI
1.	Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango	25,511,060,481	14,892,981,595	8,092,493,376	48,496,535,452	425,066,289,000	11.41
2.	Fungu 21 Hazina	34,646,049,200	143,504,986,502	11,195,588,634	189,346,624,336	1,245,739,430,000	15.20
3.	Fungu 22 Deni la Taifa	6,363,673,244.35	4,645,378,161,407.73		4,651,741,834,652.08	6,390,465,067,000	72.79
4.	Fungu 23 Mhasibu Mkuu wa Serikali	4,784,723,500	67,944,932,577	3,520,806,666	76,250,462,743	79,826,246,000	95.52
5.	Fungu 7 Ofisi ya Msajili Wa Hazina	1,450,095,010	12,396,348,543	349,884,500	14,196,328,053	176,048,903,000	8.06
6.	Fungu 13 Kitengo Cha Udhambi wa Fedha Haramu	-	481,289,614	-	481,289,614	964,233,000	49.91
7.	Fungu 66 Tume Ya Mipango	1,321,748,000	1,364,321,527	932,926,000	3,618,995,527	8,565,962,000	42.25
8.	Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha	341,924,000	316,511,651	-	658,435,651	1,833,257,000	35.92

## 4.0 MAOMBI YA FEDHA KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17.

### 4.1 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/17.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Fedha na Mipango katika Mwaka wa Fedha 2016/17 imekadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi 9,383,606,520,094** kwa mafungu yote nane. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 31,583,704,480** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi 8,640,242,740,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) ambayo yanajumuisha malipo ya deni la Taifa Shilingi **8,000,000,471,000** na matumizi ya kawaida **Shilingi 640,242,269,000** na **Shilingi 711,780,075,614** kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo ambapo fedha za ndani ni **Shilingi 659,650,000,000** na fedha za nje ni **Shilingi 52,130,075,614**. Aidha, Wizara imepanga kukusanya jumla ya **Shilingi 449,699,727,509** kutoka katika vyanzo vya ndani vya mapato ikiwa ni pamoja na mauzo ya nyaraka za zabuni, kodi za pango, mauzo ya leseni za minada na mishahara isiyolipwa, gawio, marejesho ya mikopo na michango kutoka katika Taasisi na Mashirika ya Umma. Mchanganuo wa Maombi ya Fedha umeanishwa katika Jedwali Na.2

**Jedwali Namba 2: Maombi ya Fedha kwa Mafungu Mbalimbali yaliyoko chini ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa Fedha 2016/17.**

Na	FUNGU	MISHAHARA	OC	MAENDELEO	JUMLA
1.	Fungu 50 Wizara ya Fedha na Mipango	6,984,801,480	43,676,411,000	26,000,000,000	<b>76,661,212,480</b>
2.	Fungu 21 Hazina	4,474,752,000	396,461,294,000	672,248,446,614	<b>1,073,184,492,614</b>
3.	Fungu 22 Deni la Taifa	9,340,716,000	8,000,000,471,000	-	<b>8,009,341,187,000</b>
4.	Fungu 23 Mhasibu Mkuu wa Serikali	6,784,116,000	38,801,749,000	4,869,465,000	<b>50,455,330,000</b>
5.	Fungu 7 Ofisi ya Msajili Wa Hazina	1,974,355,000	158,206,645,000	3,458,680,000	<b>163,639,680,000</b>
6.	Fungu 13 Kifengo Cha Udhhibiti wa Fedha Haramu	Inapitia Fungu 50 na Wizara nyingine	1,103,081,000	Hawana Fedha za Maendeleo	<b>1,103,081,000</b>
7.	Fungu 66 Tume Ya Mipango	1,560,492,000	1,583,291,000	5,203,484,000	<b>8,347,267,000</b>
8.	Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha	464,472,000	409,798,000		<b>874,270,000</b>
	<b>Jumla</b>	<b>31,583,704,480</b>	<b>8,640,242,740,000</b>	<b>711,780,075,614</b>	<b>9,383,606,520,094</b>

**Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango**

**4.2 Majukumu ya Msingi yaliyopangwa kutekelezwa na Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2016/17**

**Mheshimiwa Spika**, Waziri wa Fedha na Mipango katika hotuba yake ameeleza kwa kina majukumu yaliyopangwa kutekelezwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/17. Hata hivyo, Kamati ya Bajeti bado inasisitiza kuwa Wizara ya Fedha na Mipango ihakikishe inasimamia kikamilifu tatizo la mianya ya uvujaji wa mapato na ukwepaji wa kodi; ukusanyaji hafifu wa maduhuli; kuongezeka kwa Deni la Taifa pamoja na kushuka kwa thamani ya shilingi. Aidha, Wizara iendeleo kusimamia Sheria ya Bajeti ili kuhakikisha Bajeti zinazopitishwa na Bunge zinatekelezwa kama ziliyoidhinishwa pamoja; na kuboresha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma na uwajibikaji.

**5.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MIFUKO YA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI, MAHAKAMA NA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16**

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kwamba utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama na Bunge kuwasilishwa katika utekelezaji wa Bajeti za Sekta husika, Kamati imeona ni vyema ikatoa picha ya utekelezaji wa Bajeti za mifuko yote mitatu ili kutoa picha ya utekelezaji kabla ya kuwasilisha maombi.

**5.1. Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi:**

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2015/16 Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ulidhinishwa jumla ya Shilingi **82,819,486,000** kati ya fedha hizo **Shilingi 14,209,421,000** ni kwa ajili ya Mishahara, na **Shilingi 57,942,949,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 10,667,116,000** ni kwa ajili ya miradi ya



maendeleo. Hadi kufikia machi 2016, Ofisi ya Taifa Ukaguzi ilikuwa imepokea **Shilingi 37,484,851,182** sawa na asilimia 45.3 ya bajeti iliyoidhinishiwa, kati ya fedha hizo **Shilingi 10,059,558,216** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 25,608,736,000** ni matumizi ya kawaida na **Shilingi 1,816,556,966** ni kwa ajili ya miradi ya Maendeleo ambapo ni fedha zote za nje. Aidha, Ofisi hiyo kwa mwaka 2015/16 ilipanga kukusanya kiasi cha **Shilingi 8,638,120,000** hadi kufikia Machi 2016, ilikusanya **Shilingi 7,374,747,484** sawa na asilimia 85.4 ya matarajio kwa mwaka 2015/16.

## 5.2. Mfuko wa Mahakama.

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2015/16 Mfuko wa Mahakama uliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 150,241,280,000** kati ya fedha hizo **Shilingi 86,435,367,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, **Shilingi 51,485,099,000** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 12,320,814,000** ni kwa ajili ya miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia machi 2016, Mfuko wa Mahakama ulipokea jumla ya **Shilingi 91,682,915,307** sawa na asilimia 61 ya bajeti iliyoidhinishiwa, kati ya fedha hizo **Shilingi 35,543,784,998** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 43,839,130,376** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 12,300,000,000** ni kwa ajili ya miradi ya Maendeleo ambapo ni fedha zote ni za ndani.

## 5.3. Mfuko wa Bunge

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2015/16 Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 173,768,567,000** kati ya fedha hizo **Shilingi 19,413,630,000** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 147,354,937,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 7,000,000,000** miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia machi 2016, Mfuko wa Bunge **Shilingi 86,257,667,730** sawa na asilimia 49.6 ya bajeti iliyoidhinishiwa, kati ya fedha hizo **Shilingi 10,934,893,610** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 68,322,774,120** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 7,000,000,000** ni kwa ajili ya miradi ya Maendeleo ambapo ni fedha zote ni za ndani.

### Jedwali Na. 3 Utekelezaji wa Bajeti ya Mifuko ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Mahakama na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2015/16

MFUKO	FEDHA ZILIZO IDHINISHWA	FEDHA ZILIZOPOKELEWA HADI MWEZI MACHI	ASILIMIA YA UTEKELEZAJI
Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali	82,819,486,000	37,484,851,182	45.3%
Mahakama	150,241,280,000	91,682,915,307	61%
Bunge	173,768,567,000	86,257,667,730	49.6%

**Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango**



## 6.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MFUKO WA MAHAKAMA, MFUKO WA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI (NAOT) NA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilijadili na kufanya mashauriano na Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Watendaji Wakuu wa Mfuko wa Mahakama, Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) pamoja na Mfuko wa Bunge kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Mifuko hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/17.

**Mheshimiwa Spika**, Mifuko tajwa iliwasilisha kwenye Kamati mapendekezo ya awali kuhusu bajeti zao yaliyozingatia uzoefu wa miaka mingi katika uendeshaji wa Taasisi hizo pamoja na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Taasisi husika. Kufuatia azma ya Serikali ya kupunguza asilimia 60 ya bajeti ya matumizi mengineyo (OC) ya Mafungu yote ili fedha hizo ziende kwenye miradi ya maendeleo, hatua hiyo ilisababisha Mifuko hiyo kupewa Ukomo wa Bajeti mdogo ikilinganishwa na fedha halisi zilizombwa na Mifuko husika. Kamati ya Bajeti iliona hili na kufanya mashauriano na Wizara ya Fedha pamoja na Mifuko husika na kwa kuzingatia mahitaji ya msingi ya Mifuko na kukubaliana Mifuko hii izingatie ukomo wa Bajeti iliyotolewa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inasisitiza bado kuna umuhimu wa kuhakikisha Mifuko husika inapatiwa fedha za kutosha ili iweze kuendeshwa kwa ufanisi na tija kama Kifungu cha 23(4) cha Sheria ya Bajeti (2015) kinavyoelekeza. Kamati itahakikisha inafanya mapitio ya nusu mwaka ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/17 (Mid Year Review) kama ilivyo elekezwa kwenye Sheria ya Bajeti kifungu 9 (1) kipengele (h) ikiwa pamoja na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Mifuko hii kwa kipindi cha nusu mwaka na hatimaye kulishauri Bunge ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti inaliomba Bunge lako liidhinishhe makadirio ya Bajeti ya Mifuko hiyo kwa mwaka 2016/17 kama ilivyoanishwa kwenye jedwali lifuatalo:-

**Jedwali Namba 4: Fedha iliyoidhinishwa kwa Mfuko wa Mahakama, Mfuko wa Bunge na Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT).**

MAKADIRIO YA BAJETI YA MIFUKO KWA MWAKA 2016/17		MFUKO WA MAHAKAMA (FUNGU 40)	MFUKO WA BUNGE (FUNGU 42)	MFUKO WA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI (NAOT) (FUNGU 45)
Bajeti iliyopitishwa	PE	50,345,775,000	23,798,609,000	13,874,793,000
	OC	34,519,534,000	68,267,508,000	18,498,303,000
	DEV	46,761,734,000	7,000,000,000	12,285,427,368
Jumla ya Bajeti (OC, Mishahara na Maendeleo)		131,627,043,000	99,066,117,000	44,658,523,368

**Chanzo:Wizara ya Fedha na Mipango**

**Mheshimiwa Spika**, hivyo, Kamati inaliomba Bunge lako tukufu lilidhie maombi Shilingi 131,627,043,000 kwa ajili ya Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama; Shilingi 99,066,117,000 kwa ajili ya Fungu 42 – Mfuko wa Bunge; na Shilingi 44,658,523,368 kwa ajili ya Fungu 45 – Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi; ili kufanikisha utekelezaji wa m ajukumu ya Mifuko hiyo kiufanisi na kuleta tija inayokusudiwa

**7.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya Kamati kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2015/16 pamoja na maombi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2016/17; Kamati inapenda kutoa maoni na mapendekezo yake kama ifuatavyo:-

**7.1.1 Mwenendo wa Utolewaji wa Fedha kwa Mafungu yaliyo chini ya Wizara ya Fedha pamoja na Mifuko kama ilivyo idhinishwa na Bunge.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya tathmini ya ujumla ya mwenendo wa utolewaji wa fedha za utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2015/16 kwa mafungu yaliyochini ya Wizara ya Fedha na kuona haukuwa wa kuridhisha. Hadi kufikia mwezi Machi 2016, Kati ya mafungu Nane (8) ya Wizara hii na Mifuko Mitatu (3) ni mafungu mawili tu (Fungu 22-Deni la Taifa na Fungu 23-Mhasibu Mkuu wa Serikali) yamepata fedha zaidi ya asilimia 70 ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka 2015/16. Kwa mwenendo huu inaonyesha kuwa jukumu la Wizara ya Fedha ambaye ndiye msimamizi na mtoaji wa fedha kwa Wizara nyingine litakuwa limeathirika kwa kiwango kikubwa na hivyo kupelekea kushindwa kutekeleza jukumu hili kwa Wizara nyingine. Katika kudhihirisha hili, mfano mzuri tunauona kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kwamba; Kati ya mafungu 62 ya Serikali Kuu, mafungu 33 yamebainika kupewa asilimia chini ya 50, mafungu 26 yamepewa zaidi ya asilimia 50 na mafungu 3 yamepewa zaidi

ya asilimia 100 ya fedha zote za matumizi mengineyo kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Kamati inataka Wizara ya Fedha na Mipango izingatie majukumu ya mafungu yake sambamba na kutoa fedha iliyobakia kwa mafungu yake kama ilivyoidhinishwa na Bunge ili yaweze kusimamia utekelezaji wa kibajeti kwa mafungu mengine ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali.

### 7.1.2 Usimamizi na udhibiti wa matumizi ya Fedha za Umma

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua jukumu la Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ni kusimamia Sheria ya fedha ya mwaka 2001 (PFA) na utayarishaji wa na usimamizi wa Hesabu za Serikali. Pia inatambua juhudi za Idara hii katika kuboresha mifumo mbalimbali ya malipo ya kielektroniki yenye viwango vya kimataifa vya uhasibu kama vile *EPICOR-IFMs* na *TISS*, pamoja na uboreshaji wa utayarishaji wa hesabu kwa viwango vya kimataifa (*IPSAS Accrual*). Hatua hizi, zimewezesha kuimarisha usimamizi wa Fedha za Umma. Hata hivyo Kamati inaona bado kuna changamoto kubwa zifuatazo ambazo Serikali inabidi izifanyie kazi haraka ili kuongeza ubora wa usimamizi na udhibiti wa matumizi ya Fedha za umma:

- (i) Kuharakisha usambazaji wa Mkongo wa Taifa ili kupata mawasiliano ya kimtandao (*internet*) kwa Wizara, Idara za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuongeza ufanisi wa malipo kwa wakati;
- (ii) Serikali ihakikishe ina haulisha mifumo mbalimbali ya taarifa za watumishi pamoja na mapato na matumizi ya Serikali kwa ufanisi. Mfano kanzi data ya *LAWSON* hauingiliani na mfumo wa *IFMS*;
- (iii) Serikali ihakikishe inaongeza ukusanyaji wa mapato ili kufikia malengo ya ukusanyaji kila mwaka na hatimaye kuondokana na utaratibu wa 'Cash Budget' na kwenda kwenye utaratibu wa 'Accrual Budget';
- (iv) Kuhakikisha Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaboresha utayarishaji wa hesabu kwa viwango vya kimataifa (*IPSAS Accrual*) ili kuboresha uwazi zaidi katika mapato na matumizi ya Fedha za Umma;
- (v) Kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za matumizi ya fedha za umma.

### 7.1.3 Usimamizi wa Mashirika ya Umma na Soko la Mitaji

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Msajili wa Hazina ina jukumu la Kusimamia uwekezaji wa Serikali katika Mitaji ya Mashirika na Taasisi za Umma na makampuni Binafsi. Kamati inaipongeza hatua ya Serikali kutenga kiasi cha Shilingi 169,017,000,000 kwa mwaka 2015/16; kwa ajili ya kulipia madeni na kurekebisha mashirika yenye matatizo ya mitaji. Pamoja na hatua hii nzuri, hadi kufikia mwezi Machi 2016, Serikali imetoa kiasi cha Shilingi bilioni 10.038 tu. Kamati inatambua ufinyu wa Bajeti uliopo hata hivyo ni vema Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango

ikawa inajipanga katika kukamilisha vipaumbele vyake. Uimarishaji na usimamizi mzuri wa mashirika ya umma kama yale ya ATCL, TTCL, TRL na mengine utatoa fursa ya upatikanaji wa mapato yatakayosaidia Serikali kugharamia kikamilifu Bajeti yake.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2015/16 Ofisi ya Msajili wa hazina ilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi 342,530,000,000 kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato yasio ya kodi. Kati ya fedha hizo Shilingi 142,530,000,000 zinatokana na Gawio, Michango ya asilimia 15 na Makusanyo ya mapato yatokanayo na makusanyo ya Mtambo wa udhibiti wa Mawasiliano unaojulikana kama *Telecommunication Traffic Monitoring Systems (TTMS)* na Shilingi 200,000,000,000 zitatokana na mauzo ya hisa zake asilimia 4 kutoka Kampuni ya Bia (TBL) na asilimia 2.5 katika kampuni ya sigara (TCC). Hadi mwezi Februari, 2016 Ofisi ya msajili ilikuwa imekusanya shilingi 344,470,000,000 sawa na asilimia 114.78 ya makusanyo yote. Pamoja na nia njema ya Serikali kuuza hisa zake katika makampuni hayo ili kuchangamsha soko la hisa na kuwawezesha wananchi kushiriki katika uchumi bado kuna haja ya Serikali kuendelea kuwekeza kwenye makampuni mbalimbali kama vile makampuni ya gesi na madini ili kupanua wigo wa vyanzo vya mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Awamu ya Tano kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina inaendelea na zoezi la kufanya uperembaji na ufuatiliaji kwa Mashirika na Makampuni yaliyobinafsishwa kwa lengo la kuangalia endapo yanafanya kazi iliyokusudiwa. Kamati inaona kuwa, hatua hii itawezesha kuyarudisha Serikalini mashirika ambayo yamekiuka masharti ya kimkataba. Hivyo basi, inashauri Serikali kuwa makini inapotekeleza jambo hili kwa kuzingatia Sheria na Mikataba ambayo Serikali iliingia wakati wa uuzaji, kinyume na hapo tunaweza kuliingiza Taifa katika hasara kubwa kwa kuwalipa wawekezaji ambao mikataba yao itavunjwa bila kufuata taratibu husika. Aidha, zoezi hili likamilike haraka iwezekanavyo ili kutimiza malengo ambayo Serikali imekusudia katika kutekeleza suala hili.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, kwa upande wa Soko la Mitaji; Tanzania imekwisha chukua hatua za awali za kufungua soko la mitaji Tanzania (*Liberalization of Capital Market*). Inaeleweka kwamba umiliki wa hisa ni aina moja wapo ya uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa mataifa mbalimbali duniani. Kamati inaishauri Serikali kuendeleza juhudi za makusudi za kuboresha mazingira ya mfumo wa Soko la Mitaji ili liweze kukidhi mahitaji ya Watanzania. Muda umefika sasa kwa Mamlaka ya Soko la Mitaji (*Capital Market and Securities Authority*) kuanza kuhakikisha makampuni makubwa ya ndani na nje yanawekeza kwenye Soko la Mitaji la hapa nchini (DSE) ikiwa pamoja na kuhamasisha kuuza baadhi ya hisa zao kwa Watanzania. Hatua hii ni muhimu sana katika kuwawezesha Watanzania kumiliki uchumi wao na kuwezesha kiuchumi.

## 7.2 Ulipaji wa madeni ya Mifuko ya jamii

**Mheshimiwa Spika**, moja ya eneo ambalo Serikali ina changamoto kubwa ya kulitatua ni eneo linalohusu madeni ya mifuko ya jamii ambayo kwa pamoja yanaidai Serikali zaidi ya shilingi trilioni sita (6). Pamoja na kuwa Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ilionyesha nia njema (*commitment*) ya kulipa madeni haya likiwemo lile kubwa la PSPF, bado utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua. Mfano katika mwaka wa Fedha 2015/16, Serikali iliahidi kutoa kiasi cha shilingi bilioni 150 pamoja na kutoa *Non Cash Bond* ya kiasi cha shilingi trilioni 2.6 ili kulipia deni la PSPF. Hadi sasa ni shilingi bilioni 83 tu zilizotolewa na hakuna *Non Cash Bond* yoyote iliyotolewa. Kamati inaona kuwa madeni haya ni tishio kubwa linaloathiri utekelezaji wa majukumu ya mifuko husika hasa la ulipaji wa pensheni ya wastaafu wanaongezeka kila mwaka. Pamoja ya kwamba kwa mwaka huu wa fedha 2016/17, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 157 kulipa malimbikizo ya deni hilo; Kamati inaitaka Serikali kuongeza kasi ya ulipaji madeni ya Mifuko ya Jamii pamoja na kutimiza ahadi yake ya kutoa *Non Cash Bond* ya trilioni 2.6 kwa Mfuko wa PSPF ili uweze kupunguza mzigo mkubwa wa malipo ya wastaafu.

## 7.3 Mradi wa *Village Empowerment* maarufu kama Milioni 50 kwa kila Kijiji. (Fungu 21)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Village Empowerment maarufu kama Milioni 50 kwa kila Kijiji. Mradi huu unalenga “Kutenga Kiasi cha Milioni 50 kwa Kila Kijiji kwa ajili ya kukopesha Vikundi vya Ujasiriamali kupitia Ushirika wa Kuweka na Kukopa (SACCOS) katika vijiji husika”. **Kamati imebaini kwamba**, Tanzania bara ina jumla ya vijiji 19,600 ambavyo vinahitaji jumla ya Shilingi 980,000,000,000 ili kila kijiji kipewe Shilingi milioni 50. Fedha iliyotengwa chini ya Fungu 21 - Idara ya Bajeti ya Serikali chini ya mradi uitwao “Village Empowerment” ni Shilingi 59,500,000,000 ambazo ni sawa na asilimia 6 tu ya fedha zote zinazohitajika, inaweza kuhudumia vijiji 1,190.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa suala hili ni mradi wa maendeleo na linahitajika kutekelezeka ndani ya miaka mitano; Kamati ya Bajeti inaishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

**Kwanza**, kuongeza fedha hizi mpaka kufikia Shilingi 196,000,000,000 sawa na asilimia 20 ya fedha zote zinazohitajika ili mradi ukamilike ndani ya miaka mitano;

**Pili**, kufanya utafiti wa kutosha kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi (*National Economic Empowerment Council*), ambao ndio wasimamizi wa uwezeshaji huu ili kuwanda wananchi katika vijiji na kuhakiki utendaji na ufanisi wa SACCOS na Ushirika katika utoaji wa Mikopo.

**Tatu,** Wakati taratibu za ukamilishaji utoaji wa mikopo hii zikiendelea fedha za mradi huu ziwekwe katika Benki ya Kilimo na kuandaa dirisha maalumu litakaloshughulikia mikopo hii. Aidha, utaratibu wa utoaji wa Mikopo hii uwe shirikishi katika ngazi zote za kiutawala.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatoa angalizo hili ili kuepuka mradi huu kutofikia malengo yake kama ilivyokuwa kwa **“Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kukuza Ajira”** - maarufu kama Mabilioni ya JK; ambao wajanja wachache wasiostahili walifaidika na kuwaacha vijana wakilalamikia utaratibu uliotumika kukopesha fedha hizo.

#### **7.4 Watumishi hewa**

**Mheshimiwa Spika,** Moja ya maeneo yaliyosababisha Serikali kupoteza kiasi kikubwa cha fedha ni uwepo wa Watumishi hewa. Kulingana na taarifa iliyotolewa na Mheshimiwa Rais siku ya wafanyakazi tarehe 1 Mei, 2016 ni kwamba Serikali imebaini watumishi hewa 10,295, kati ya hao watumishi 8,373 wanatoka Serikali za mitaa na Watumishi 1,922 wanatoka Serikali kuu. Watumishi hao wamekuwa wakilipwa Shilingi 11,603,273,799.41 kwa mwezi na shilingi 696,196,427,964.60 katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Kamati inaamini suala la watumishi hewa na mishahara hewa ni suala lenye mtandao mpana kuanzia wakati wa kuajiri, kuingiza majina hewa kwenye mfumo na utaratibu mzima wa kufanya malipo ya mishahara na wanaochukua mishahara hiyo washiriki wao. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kufuatilia mtandao huo na kuwawajibisha watumishi wote wasio waaminifu watakaobainika kuhusika katika suala hili.

#### **7.5 Matumizi ya Mashine za Kielektroniki katika Ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa, moja ya changamoto kubwa iliyojitokeza katika ukusanyaji wa maduhuli ni baadhi ya Taasisi, wakala na Mashirika ya Umma kutotumia Mashine za kielektroniki (EFDs) katika ukusanyaji wa maduhuli. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha Wizara, Idara na Taasisi zote za Serikali zinatumia mashine za Ki-elektroniki katika ukusanyaji wa maduhuli ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato kama inavyohamasishwa kwa Sekta Binafsi nchini kutumia mashine hizo. Hivyo, Wizara, Idara na Taasisi yoyote itakayoshindwa kutekeleza agizo hili ichukuliwe hatua za kisheria na kinidhamu.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Mamlaka ya Mapato Tanzania iliagizwa kununua mashine za EFD na kuzigawa bure kwa wafanyabiashara wanaostahili bure. Hadi sasa mamlaka imekwisha nunua mashine za EFDs 5000 ambazo ni sawa na asilimia 2.5 ya mahitaji ya mashine za EFDs 200,000 zinazohitajika nchi nzima kwa wafanyabiashara walioandikishwa. Kamati inashauri Serikali ihakikishe kwamba



kila mfanyabiashara anaestahili kutumia mashine hizo anapewa na kuanza kuitumia kabla ya ifikapo mwaka 2018 ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato nchini.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kusisitiza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuongeza juhudi ya kukusanya mapato zaidi, ni vyema Serikali ikaboresha mazingira yao ya kufanya kazi kwani Kamati imebaini kuwa Makamishna wa Taasisi hii ukimuondoa Kamishna Mkuu bado wanakaimu katika nafasi zao. Hii inapunguza motisha wa kufanya kazi hasa ukizingatia hawajathibitishwa katika nafasi hizo. Kamati inaishauri Serikali kuwathibitisha wale ambao wameonyesha uwezo wa kuzimudu nafasi zao na kuwaondoa wale ambao wameshindwa kutekelezwa kutekeleza majukumu yao na kuwateuwa wale ambao wanastahili.

## **7.6 Maduhuli yasiyorejeshwa na Mawakala na yasiopolekwa Benki.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Agizo Na. 110 la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1997 imeainisha kuwa, makusanyo yote ya Halmashauri yawasilishwe kwa watunza fedha wa Halmashauri husika kwa usalama. Aidha, Agizo la 38 (3) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 2009 inazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa zitakozoamua kutumia wakala kukusanya mapato, zimtake wakala huyo kuweka amana sawa na malipo ya miezi mitatu, dhamana ya benki au aina yeyote ya dhamana ambayo Mamlaka ya Serikali za Mitaa itaona inafaa. Maagizo hayo yamekuwa hayatekelezwi kikamilifu na hivyo mawakala kukusanya Fedha na kutoziwasilisha kwenye Halmashauri husika. Kwa mujibu wa Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kati ya mwaka 2010 - 2015 Serikali imepoteza jumla ya **Shilingi 19,352,218,982**. Upotevu huu umetokana na Serikali kutosimamia kikamilifu ukusanyaji wa mapato ya Serikali za Mitaa chini ya utaratibu uliowekwa kisheria. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuimarisha na kusimamia mfumo na nidhamu ya makusanyo ya fedha kwa Mamlaka za Serikali za kama ilivyoidhinishwa Mitaa ili kuepusha upotevu wa mapato kwa mawakala wasio waaminifu.

## **7.7 Ufuatiliaji na Tathmini ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwa, Tume ya Mipango ndiye Msimamizi Mkuu wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hata hivyo, kwa mwaka wa fedha 2016/17, Tume hii imetengewa kiasi cha takribani Shilingi milioni 141 tu kwa ajili ya shughuli zote za kusafiri ndani ya nchi kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, Mafungu mengine ya Wizara, Idara na Taasisi hayana fedha kabisa za kufanya tathmini na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo. Pamoja na nia njema ya Serikali ya kupunguza matumizi yasio ya lazima ili kupeleka fedha kwenye miradi ya



maendeleo kwa asilimia 40; Kamati inaona kuwa bila kutengwa fedha za kutosha kwajili ya usimamizi na ufuatiliaji, miradi mingi haitaweza kukamilika. Kamati inaishauri Serikali kuongeza fedha ya usimamizi na ufuatiliaji kwa Fungu 66 – Tume ya Mipango ili kuhakikisha malengo ya miradi ya maendeleo yanatekelezwa kama ilivyokusudiwa.

## 7.8 Tatizo la Takwimu Sahihi za Serikali

**Mheshimiwa Spika**, kuwepo kwa takwimu sahihi katika kutoa taarifa zinazohitajika ni muhimu katika kuwezesha taarifa hizo kutumiwa pale inapobidi. Kamati imebaini uwepo wa tatizo la Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali kutoa takwimu zinazotofautiana juu ya suala moja. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuweka utaratibu mahususi wa kuzingatia inaitumia ipasavyo Tume ya Taifa ya Takwimu (*National Bureau of Statistics*) katika kutoa taarifa zenye takwimu sahihi kwa kuwa ndiyo yenye jukumu la kuandaa kanzi data (*Data Base*) ya Serikali kwa ajili ya matumizi ya umma. Aidha, bado kuna umuhimu mkubwa wa takwimu zote za masuala ya fedha kuhakikiwa na kuoanishwa na Hazina kabla ya kuziweka wazi kwa ajili ya matumizi ya umma.

## 7.9 Uhakiki wa Madeni ya Watumishi na Watoa Huduma

**Mheshimiwa Spika**, Suala la madeni ya watumishi, wakandarasi na wazabuni limekuwa ni tatizo la muda mrefu na kuisababishia Serikali hasara kwa sababu kila mwaka mpya wa fedha Wizara, Idara na Taasisi hubeba mzigo wa madeni ya mwaka wa fedha uliopita. Aidha, Serikali imeonyesha nia ya kuhakikisha inalipa madeni ya watumishi na watoa huduma kupitia Wizara ya Fedha. Pamoja na hatua hii nzuri, Kamati inaendelea kushauri kuwa zoezi la uhakiki lizingatiwe ipasavyo kabla madeni hayo hayajalipwa.

## 7.10 Udhibiti wa utakasishaji wa Fedha Haramu.

**Mheshimiwa Spika**, Kitengo cha Udhibiti wa Utakasishaji Fedha Haramu kinatekeleza na kusimamia Sheria ya Udhibiti wa Utakatishaji wa Fedha Haramu ya mwaka 2006, sura ya 423 na Sheria ya udhibiti wa utakatishaji wa Fedha Haramu na Mali Athirika ya Zanzibar ya mwaka 2010. Kamati imebaini kwa mwaka 2015/16, kitengo hiki kimepokea asilimia 44.68 tu ya fedha ya Matumizi ya Kawaida zilizoidhinishwa na Bunge na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu yake. Hivyo, Kamati inasisitiza Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha kitengo hiki kinaimarishwa na kupewa fedha za kutosha ili kiweze kuimarisha mfumo wa udhibiti wa utakasishaji wa fedha haramu unaokidhi viwango vya kimataifa utakao imarisha mfumo wa fedha na kudumisha haki na amani kwa jamii, kuleta utulivu wa kisiasa na kukua kwa uchumi endelevu.

## 8.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati, ambao wametoa maoni na mapendekezo mbalimbali yaliyowezesha kuboresha taarifa hii hatimaye kuletwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, naomba nitumie nafasi hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Hamida Mohamedi Abdallah, Mb
4. Mhe. Jerome Bwanausi, Mb
5. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
6. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
7. Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
8. Mhe. Susan Peter Maselle, Mb
9. Mhe. Agustino Manyanda Masele, Mb
10. Mhe. Janet Zebedayo Mbene, Mb
11. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
12. Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb
13. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
14. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb
15. Mhe. Salma Mohamed Mwassa, Mb
16. Mhe. Susana Chogidasi Mgonukulima, Mb
17. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb
18. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb
19. Mhe. Ali Hassan Omari, Mb
20. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
21. Mhe. David Ernest Silinde, Mb
22. Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb

Aidha, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt Philip Mpango Mb, Naibu Waziri Mhe. Dkt Ashatu K. Kijaji Mb, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu, Kamishna wa Bajeti pamoja na wataalamu wao kwa kuwa tayari kutoa ufafanuzi na kupokea maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati yangu wakati wote wa mjadala wa makadirio haya. Aidha, Kamati inatoa shukrani kwa Taasisi na Idara zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano waliutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nimalizie kwa kukushukuru wewe binafsi na Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg.

Lina Kitosi, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Mathew Kileo pamoja na Sekretarieti ya Kamati Ndg. Michael Kadebe (Kiongozi), Ndg. Godfrey Godwin, Ndg. Emmanuel F Rhobi, Ndg. Ruva Tunze, Ndg. Maombi Kakozi, Ndg. Lilian Masabala, na Ndg. Wilson E Machaine kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na hatimaye kuweza kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja.

Josephat Sinkamba Kandege (Mb)

**M/MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**

1 Juni, 2016

**NAIBU SPIKA.** Sasa tutamsikia Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Fedha na Mipango. *(Makofi)*

**MHE. DAVID E. SILINDE- NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:** Kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani naomba kuwasilisha hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bunge katika Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu Mpango wa Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na ninaomba hotuba yote iingie kwenye *Hansard* ya Bunge lako Tukufu ili iwe faida kwa Watanzania wote na kizazi kijacho.

Ila sitaisoma hotuba kwa sababu haturidhishwi na mwenendo wa namna wewe Naibu Spika, unavyoliendesha Bunge hususani kwetu sisi Wabunge wa Upinzani kama watoto wa shule ya msingi, naomba kuwasilisha.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KUHUSUMPANGO WA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2016*

---

## **1. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunilinda na kunipa nguvu na maarifa zaidi ya kusonga mbele na kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Momba. Aidha, napenda kumshukuru KUB Mhe. Freeman A. Mbowe (Mb) kwa kuiteua kuwa Naibu Msemaji Mkuu wa wizara hii muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu,

pia natoa ahadi kwake nakwa chama changu CHADEMA, na wananchi wote wapenda mageuzi kwamba, nitaitumikia nafasi hii kwa uadilifu mkubwa na kwa moyo wangu wote.

**Mheshimiwa Spika**, hali kadhalika nitumie fursa hii kwa namna ya pekee kumshukuru Mheshimiwa Halima James Mdee (Mb) Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara hii kwa kazi kubwa tulioifanya ya kuandaa hotuba hii, pia nitoe pongezi na kuwatia moyo Makamanda wote waliotolewa Bungeni kwa hila, ninasema mapambano yanaendelea na tuko pamoja. Aidha niwashukuru waheshimiwa wabunge wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa ushirikiano na umoja wetu.

## **2. WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO-Fungu 50**

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya fedha na Mipango ndio yenye mamlaka makubwa zaidi katika uchumi wa Tanzania. Wizara hii;

- i) Kubuni na kusimamia utekelezaji wa sera za uchumi jumla
- ii) Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani na nje ya nchi pamoja na matumizi yake (kwa mantiki hiyo wizara ambazo hazikupata fedha kwa kadiri zilivyopitishwa na Bunge, maelezo yake ni kuwa hazikupata fedha hizo kutoka wizara ya fedha )
- iii) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali
- iv) Kufuatilia utekelezaji wa mipango ya kupunguza umasikini katika sekta mbali mbali
- v) Kusimamia deni la Taifa
- vi) Kusimamia upatikanaji wa rasilimali fedha zinazopatikana katika miradi ya ubia baina ya serikali na sekta binafsi
- vii) Kusimamia sera, sheria ,kanuni na taratibu za uhasibu, ukaguzi wa ndani na ununuzi wa Umma,
- viii) Kusimamia Mali za serikali, taasisi na mashirika ya Umma (treasurer registrar)
- ix) Kusimamia masuala ya Tume ya Pamoja ya fedha
- x) Kuandaa na kulipa mishahara watumishi serikalini
- xi) Kusimamia ulipaji wa mafao na pensheni ya wastaafu nakudhibiti biashara ya fedha haramu pamoja na ufadhili wa ugaidi. Hivyo bajeti ya wizara hii inatakiwa kutekeleza majukumu haya ya wizara.

**Mheshimiwa Spika**, kwa majukumu hayo ya wizara, ni dhahiri kwamba uendeshaji wa nchi hii uko chini ya wizara hii ya fedha, hivyo kuporomoka au kupanda kwa uchumi ni jukumu la wizara ya fedha. Ile **“kauli mbiu ya Serikali”** ya kuwa na uchumi wa viwanda wakati inaelewa kabisa kuwa jambo hilo kwa miaka ya hivi karibuni haiwezekani kabisa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani imetumia neno kauli mbiu kwa ukweli kwamba mpango huo hauna tofauti na zile kauli mbiu za siasa ni kilimo, kilimo ni uti wa mgongo n.k na mwisho kauli mbiu hizo zilishindwa kutekelezeka na kuzaa matunda kutokana na kukosekana kwa uwekezaji kwa mipango hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, jambo hilo la uchumi wa viwanda ni sawa kabisa na pale baba mwenye nyuma kuwa na mboga na kutegemea kupata ugali au wali kutoka kwa jirani. Na tukumbuke kwamba kila mkataba wa fedha kwa kila mradi wa aina yoyote utakaotekelezwa hapa nchini ni lazima upitie na kuidhinishwa na hazina.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya fedha inaelewa vizuri kwamba kutokana na hali halisi ya Tanzania na upatikanaji wa fedha za ndani na za nje itakuwa ni vigumu kwa nchi yetu kutoa elimu bora na ya bure. Kwani, ukweli ni kwamba kizuri ni gharama na hivyo hutoaji wa elimu iliyo bora ni lazima kufanya uwekezaji mkubwa na sio kubabaisha na mwisho kuishia njiani bila ya kutimiza lengo.

**Mheshimiwa Spika**, ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara hii, kuhakikisha inatoa ushauri sahihi kwa Mheshimiwa Rais, badala ya ushauri usio na tija kwa taifa kama suala la sukari nchini na namna ya utekelezaji wa kutoa elimu bure. Mambo ambayo mpaka sasa yanaonekana kuishinda serikali ya awamu ya tano.

## 2.1. JUKUMU LA KUSIMAMIA UTEKELEZAJI WA BAJETI 2015/16

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ina jukumu la msingi la kupanga bajeti, na kusimamia utekelezaji wake. Ili kupima ufanisi wa Wizara hii ni lazima kufanya uchambuzi wa nini kilipangwa?nini kilipatikana na utekelezaji wake. Uchambuzi huu utatupa dira ya kujua uwezo wetu wa makusanyo na hatimaye kuwa na bajeti zinazotekelezeka!

**Mheshimiwa Spika**,wizara ya fedha imekuwa na jukumu la kupeleka fedha zote zilizopangwa kwenye bajeti kwa kila wizara lakini mpaka sasa utekelezaji wake ni hafifu na inaonyesha wizara kushindwa kabisa kusimamia jukumu hili. Mifano ya wizara ambazo wizara ya fedha na mipango imeshindwa kupeleka fedha ni pamoja na;-

**Wizara ya mambo ya ndani**, Kati ya fedha zote zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi ya Wizara, mishahara ilikuwa 52%, matumizi mengineyo ilikuwa 47% na kwa upande wa bajeti ya maendeleo ni 1% tu.<sup>1</sup>

---

<sup>1</sup> Taafira ya Kamati ya Bunge ya mambo ya nje , ulinzi n usalama, 2016/17, pg. 8

**Wizara ya afya:** bajeti ya maendeleo iliyotengwa 2015/16, hadi robo ya tatu ya mwaka hakuna fungu hata moja ambalo wizara hiyo ilikuwa imepata zilizoidhinishwa na Bunge kwa angalau 50%,halikadhalika Fungu 52 – Idara kuu Afya hadi kufikia tarehe 31 March 2016 kiasi cha fedha kilichopokelewa ni 31% tu ya Bajeti, **Wizara ya kilimo** katika kipindi cha mwaka 2015/16, hadi mwezi March, fedha za maendeleo zilizokuwa zimepatikana ni bilioni 5.1 ambazo ni sawa na 15.9% ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, hii ni mifano michache tu, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema Wizara ya Fedha inawafanyia wataanzania mchezo wa kuigiza kwa kutayarisha kile kinachoitwa “**nominal budget**” badala ya kutayarisha “**real budget**”. Kwa mazingira hayo ya upatikanaji wa fedha za maendeleo ambapo utekelezaji wa bajeti za maendeleo unakuwa chini ya asilimia 50, inawezekanaje serikali kufikia **uchumi wa viwanda** chini ya usimamizi wa wizara hii ambayo imekuwa ikishindwa kutekeleza majukumu yake ya kutoa fedha kama zilivyopangwa?

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inarudia tena kuwa wizara hii inajukumu kubwa hivyo inatakiwa itekeleze majukumu yake kwa uadilifu na uhakika, kinyume cha hapo mipango yote itakuwa ni ngonjera tu na miaka inazidi kupita na Tanzania badala ya kwenda mbele inarudi nyuma.

### 3. KITENGO CHA KUDHIBITI UTAKATISHAJI WA FEDHA HARAMU- (FIU) -Fungu 13

**Mheshimiwa Spika**,Benki Kuu ya Tanzania ni benki ya kitaifa inayosimamia masuala ya kibenki na kifedha. Kati ya majukumu yake ni utoaji wa fedha za Tanzania, [Shilingi yaTanzania](#). Benki Kuu ya Tanzania iliundwa na [Sheria ya Benki ya Tanzania 1965](#). Mwaka 1995, baada ya kuonekana kuwa benki hii ina majukumu mengi kuzidi uwezo wake,[Sheria ya Benki ya Tanzania 1995](#) ilipitishwa na kuipa benki hii jukumu moja ambalo ni kusimamia sera ya fedha nchini.

#### 3.1. Udhaifu wa Muundo wa Financial Intelligence Unit (FIU)

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatilia mashaka uwezo na dhamira ya Benki Kuu kufanya ujasusi wa Miamala ya fedha katika kuzuia utakatishaji wa fedha sambamba na uwezo mdogo wa Kitengo cha Financial Intelligence Unit, kitengo ambacho kinazuia utakatishaji wa fedha haramu.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeunda kitengo cha Financial Intelligence Unit (FIU) ambacho kina mamlaka ya kiutawala pekee na huishia kufanya uchambuzi wa taarifa za miamala ya fedha na kuziwasilisha ama Jeshi la Polisi au PCCB, wakati huo huo PCCB inalazimika kupitia kwa Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP) ili atoe ruhusa ya kufungua mashitaka.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo yake ni kuwa FIU haina uwezo wa kufanya uchunguzi, wala kuendesha mashitaka dhidi ya utakatishaji wa fedha haramu jambo ambalo ni mwanya unaotumiwa na watu waovu na mafisadi kama ilivyokuwa katika wizi wa Mabilioni ya Rada, wizi wa fedha kwenye akaunti ya Tegeta Escrow na wizi wa fedha katika Mkopo wa Serikali dola milioni 600 kutoka Stanbic Bank.

**Mheshimiwa Spika**, Mfumo wa FIU ya Tanzania ni “administrative model” wakati mfumo imara zaidi ni ule wa “Judicial Model” ambao unakiongezea nguvu kitengo hicho cha kuzuia miamala ya biashara haramu za kutakatisha fedha.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa “Egmont<sup>2</sup> Group of Financial Intelligence Units” Judicial Model of FIU inamaanisha kuwa; *“The Judicial Model is established within the judicial branch of government wherein “disclosures” of suspicious financial activity are received by the investigative agencies of a country from its financial sector such that the judiciary powers can be brought into play e.g. seizing funds, freezing accounts, conducting interrogations, detaining people, conducting searches, etc.”*

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Ungeni inaishauri Serikali kuimarisha kitengo cha FIU kwa kukiundia Mfumo wa Judicial Model ili kuepuka aibu ambayo Taifa letu imekuwa ikiipata kutokana na **Serious Fraud Office** ya Uingereza kuwana na uwezo wa kurudisha fedha za zilizoibiwa kwa njia ya kifisadi wakati kazi kama hiyo ingeweza kufanywa na vyombo vya hapa nchini endapo vingemarishwa kama ambavyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inavyoshauri kuimarisha kitengo cha FIU.

#### 4. OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI- Fungu 45

##### 4.1 Kupunguzwa kwa Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilianzishwa chini ya Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, na kufafanuliwa na sharia ya Ukaguzi ya umma, Na.11 ya mwaka 2008(kama ilivyorejewa) na kufafanuliwa na kanuni za Ukaguzi wa umma za mwaka 2009.

**Mheshimiwa Spika**, Lengo kuu la Ofisi hii ni kutoa huduma bora za ukaguzi zenye kuleta tija kwa nia ya kuimarisha uwajibikaji unaozingatia thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.

<sup>2</sup><http://www.egmontgroup.org/about/financial-intelligence-units-fius>  
retrieved at Egmont Group on 28.05.2016, Financial Intelligence Units



**Mheshimiwa Spika**, ili ofisi hii iweze kutimiza malengo yake kwa ubora, uadilifu na ubunifu wa hali ya juu inahitaji rasilimali fedha za kutekeleza hayo yote. Kwa mwaka wa fedha 2016/17 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilikuwa imeomba Shilingi **69.839 Bilioni** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi **8.0 Bilioni** kwa matumizi ya maendeleo, lakini Kiasi hicho kilipunguzwa na Serikali hadi na kuiwekea ukomo wa Shilingi **28.3 Bilioni** kwa matumizi ya kawaida na Shilingi 4.0 Bilioni, matumizi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, ni ukweli usio nashaka kwamba Ofisi hii kwa kiwango kikubwa imesaidia kuokoa mabilioni ya fedha ambazo zilikuwa zinatumiwa nje ya malengo na pia kugundua wizi na ukwepaji wa kodi ambao ulikuwa ni **donda ndugu** katika utumishi wa umma au kwa maneno mengine walivunja mtandao wa wizi uliokuwa unaelekea kuota mizizi kati ya watendaji Serikali na wafanyabiashara wasio waaminifu. Hivyo basi kitendo chochote cha kupunguza bajeti yao ya kufanyia kazi maana yake ni kuwafanya watendaji wasiwe na uwezo wa kutenda kazi zao kwa kiwango kilichowekwa na ofisi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, CAG amekiri kuwa “Hatua ya kushusha ukomo wa bajeti ya Fungu 45 itasababisha kupungua kwa uwezo wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika kutekeleza jukumu lake la kukagua na kudhibiti matumizi ya rasilimali za umma” Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaiona hatua hii kuwa ni dhamira ya Serikali ya CCM ya awamu ya tano kukwepa kuwajibishwa na kuua kabisa dhima nzima ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kama taasisi ya kusimamia uwajibikaji wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, CAG amekiri kuwa ukomo wa bajeti uliowekwa na Serikali utaathiri kabisa ukaguzi wa hesabu za Serikali katika maeneo 9, ambayo ni;

- (i) Ukaguzi wa Serikali Kuu
- (ii) Ukaguzi wa Hazina ikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania na Deni la Taifa
- (iii) Ukaguzi wa Serikali za Mitaa ambapo fedha nyingi zinaelekezwa katika ngazi za kata na vijiji
- (iv) Ukaguzi wa Mashirika ya Umma, Wakala za Serikali
- (v) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo
- (vi) Ukaguzi wa Ofisi za Balozi za Tanzania nje ya nchi;
- (vii) Maboresho katika Ukaguzi;
- (viii) Ujengaji uwezo wa Wakaguzi; na
- (ix) Uendeshaji wa Ofisi za Ukaguzi zilizopo Katika Mikoa yote ya Tanzania Bara.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaliomba bunge lako tukufu na wabunge wote kwa ujumla bila kujali itikadi zetu za siasa, kupitia Kamati ya Bunge ya Bajeti kupitisha azimio la kuongeza ukomo wa fedha za fungu 45 la Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kufikia Shilingi **69.839 Bilioni** kwa kuzingatia

Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015, kifungu cha 8 (e) kinacholipa bunge mamlaka ya kuishauri Serikali kuhusiana na vifungu vya bajeti.

**Aidha, Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaliomba Bunge kuangalia uwezekano wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, vitabu vyake vya hesabu na maombi ya fedha kufanyiwa kazi na kamati ya kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), badala ya ilivyo sasa ambapo inasimamiwa na Kamati ya Bajeti.

## 5. DENI LA TAIFA-Fungu 22

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya fedha ya fedha ina jukumu pia la kusimamia deni la Taifa, Deni la Taifa limeendelea kuwa changamoto kubwa sana kwa uchumi wetu. Hakuna ubishi kwamba kukua kwa deni la Taifa kunaisababishia serikali kuendelea kuwa tegemezi na hivyo kushindwa kutatua kero za kiuchumi za wananchi. Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha serikali imeendelea kukopa mikopo mikubwa yenye masharti ya kibiashara hali ambayo inazidi kufanya hali ya maisha kwa wananchi iendeleo kuwa ngumu kwa kuwa serikali inatumia fedha nyingi kulipa madeni **badala ya kuzitumia fedha hizo kugharamia miradi ya maendeleo. Tutarajie deni hili kuongezeka kwa kiwango kikubwa sana kwa kuwa kwa mwaka huu pekee tunatarajia kukopa mkopo wa biashara (wa ndani na nje) wenye thamani ya shilingi trillion 7.4**

**Mheshimiwa Spika**, Kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2016/17, kilichotolewa na wizara ya fedha na Mipango, **April 2016**, kinaeleza kwamba hadi kufikia **Januari 2016, deni la taifa limefikia dola za kimarekani 19.521** (sawa na shilingi trillion 42.9) na kwa nyongeza ya shilingi shilingi trillion 7.4 kwa mwaka ujao wa fedha (2017/18) deni la taifa litafikia trillion kati ya trillion 48- 50! Ikumbukwe ni mwaka 2008 (miaka 8 tu iliyopita) deni la Taifa lilikuwa shilingi Trillion 7.8!! kasi ya ukopaji wa mikopo mikubwa yenye masharti ya kibiashara ina athari kubwa kwenye uhimilivu wa deni.

**Mheshimiwa Spika**, Licha ya kwamba Serikali ya CCM inajinasibu kuwa inakopa fedha hizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo, takwimu za utekelezaji wa mpango wa Taifa wa miaka 5 tulizozainisha hapo juu, zinadhihirisha kwamba mikopo hii haijasaidia kubadilisha hali ya maisha ya wananchi! Na mbaya Zaidi wananchi hawa hawa ndio wanawajibika kulipa deni kwa njia mbali mbali ikiwemo kodi!

**Mheshimiwa Spika**, ikumbukwe kwamba deni hili halijajumuisha madeni ya mifuko ya hifadhi ya jamii, mikopo ya halmashauri na madeni mbalimbali ambayo yameingizwa kimakosa ofisi ya msajili wa hazina.

## 5.1. ATHARI ZA DENI LA TAIFA KATIKA UTEKELEZAJI BAJETI

**Mheshimiwa Spika, Mwenendo wa matumizi unaonyesha kwamba,** Hadi kufikia Machi 2016 serikali imetoa mgao wa matumizi (Exchequer issues) wenye thamani ya shilingi bilioni 15,271 kwenda kwenye mafungu mbali mbali kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti. **Kati ya kiasi kilichotolewa shilingi bilioni 12,247 zilikuwa ni za matumizi ya kawaida** na ikijumuisha shilingi **bilioni 4,744.6 kwa ajili ya mishahara** na shilingi bilioni 2,350.1 kwa ajili ya matumizi mengineyo (ambapo matumizi ya Halmashauri yanayotokana na mapato ya ndani shilingi bilioni 117.7) . **Shilingi bilioni 5,035 zilitolewa kwa ajili ya kugharamia Mfuko Mkuu wa serikali.**

Mchanganuo wa shilingi bilioni 5,035 za mfuko mkuu wa hazina:

- i) Malipo ya riba kwa madeni ya ndani na nje – bilioni 992.3
- ii) Matumizi 'mengine' ya mfuko Mkuu (CFS others) – bilioni 760.7 (nimatumizi gani ya kiasi hicho cha fedha?)
- iii) Malipo ya Mkopo (Principal payment)-bilioni 3,282.3
- iv) Malipo ya mkopo wa nje – bilioni 448.3
- v) Malipo ya dhamana na amana za serikali zilizoiva bilioni 2,834.0

**Mheshimiwa Spika,** Katika bajeti yote ya 2015/16 ya shilingi bilioni 22,495, fedha iliyotolewa kwa ajili ya matumizi yamaendeleo nishilingi bilioni 3,023 tu! Ambapo shilingi bilioni 2,645 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 378.9 ni fedha za nje. Wakati huo fedha iliyotumika kulipa deni ni shilingi bilioni 7,552( trillion 7.5)<sup>3</sup>

## 5.2. UHIMILIVU WA DENI LA TAIFA

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa muda mrefu imekuwa ikiitaka serikali ipunguze au iachane kabisa na mikopo yenye masharti ya kibiashara ambayo inazidi kuliongeza deni la Taifa. Hata hivyo serikali ya CCM imeendelea kupuuza mawazo haya mazuri kwa kisingizio kwamba deni husika ni himilivu. Na kwamba nchi yetu inakidhi vigezo vya kimataifa vya kukopesheka!

---

<sup>3</sup> Maelezo ya waziri wa fedha na Mipango kwenye Kamati ya kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2015/16 kwa kipindi cha Julai 2015 hadi Machi, 2016 na mwelekeo hadi Juni, 2016. Mei 2016 uk. 9 na 10.

**Mheshimiwa Spika**, Ripoti ya Tathmini ya kina ya Mpango wa Taifa wa miaka 5<sup>4</sup> inaeleza kwamba japokuwa thamani ya sasa ya deni kwa pato la Taifa ni 24.83% ,ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 50%. Ripoti husika inatoa tahadhari kwamba kiwango hiki kimekuwa kikiongezeka kwa kasi toka mwaka 2010. (2011 - 14.9% ya pato la Taifa, 2012- 18% ya Pato la Taifa na 2013- 24.83% ya Pato la Taifa).**Na kwamba ongezeko hili ni kiashiria cha uwezo mdogo wa kiuchumi kulipa deni** . Inasikitisha sana pale ambapo kuna kuwa na upotoshaji kwa upande wa serikali pale tunapohoji kuhusiana na deni la Taifa na uhimilivu wake.

**Mheshimiwa Spika**,Ikumbukwe madeni tunayoyazungumzia hapo juu hayajajumuisha madeni yanayotokana na 'Malimbikizo ya Madai' ambayo watoa huduma mbalimbali wanadai serikali. Hadi kufikia desemba 2015 Serikali ilikuwa imepokea madai mbalimbali yenye jumla ya shilingi bilioni 2.753. Kati ya hizo watoa huduma na bidhaa (goods and services) shilingi bilioni 1,182/-, madai ya umeme, maji na simu shilingi bilioni 137.2, madai ya pango la ofisi shilingi bilioni 53.4, wakandarasi mbalimbali (Construction work) shilingi bil. 1,247 na madai ya watumishi yasiyo ya kimsharara sh bn 133...<sup>5</sup>

**Mheshimiwa Spika**, Kambi rasmi ya upinzani inarudia tena hoja yake iliyotolewa kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, ili kujiridhisha kwamba deni la Taifa ni **'HIMILIVU'** kamainavyodaiwa:

Tunaitaka ofisi ya mthibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za serikali afanye ukaguzi maalum (Special Audit) katika kitengo cha deni la Taifa (Fungu 22) ili tuweze kujua mikopo tunayoichukua kila mwaka inatumika kufanyia nini, atoe taarifa ya miradi iliyotekelezwa kutokana na mikopo hiyo kama ni ya miradi ya kipaumbele kwa mujibu wa mpango wa Taifa wa Maendeleo. Halikadhalika ukaguzi huu maalum utatuwezesha kama Taifa kujua kiwango halisi cha deni la Taifa ambalo tunadaiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itenganishe deni halisi la Taifa na matumizi mengineyo yanayohusu Mfuko Mkuu wa Hazina ili kuziba mianya ya ubadhirifu au matumizi mabaya ya fedha za umma kwa kisingizio cha Deni la Taifa.

<sup>4</sup> The United Republic of Tanzania, Comprehensive Review Report for Tanzania Five Year Development Plan 2011/2012-2015/16.

<sup>5</sup> Maelezo ya waziri wa fedha na Mpango Mhe. Dk. Philip I Mpango (MB) kwenye kamati ya kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu tathmini ya hali ya uchumi na mwenendo wa utekelezaji wa Bajeti ya 2015/16 kwa kipindi cha julai hadi Desemba 2015 na mwelekeo hadi juni 2016, Machi 2016

**Mheshimiwa Spika**, takwimu zinaonesha kuwa kwa mwaka 2015 deni la taifa lilikuwa ni shilingi bilioni 33,539.8 na Pato halisi la taifa kwa kipindi hicho lilikuwa ni shilingi trilioni 44.1. Kwa mujibu wa mahesabu ya uhimilivu wa deni kwamba Deni la Taifa kwa Pato la Taifa ili liwe na uhimilivu ukomo wake uwe asilimia 50.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mahesabu hayo inaonekana kuwa asilimia ya uhimilivu kwa sasa ni asilimia 76. Kwa kuweka Kumbukumbu sahihi wakati wa Mheshimiwa Saada Mkuya Salum (Mb) akiwa Naibu Waziri wa Fedha alisema ukomo wa uhimilivu wa deni ni 50%. Hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa ufafanuzi wa uhimilivu wa deni letu.

## **6. OFISI YA MSAJILI WA HAZINA – Fungu 7**

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Msajili wa Hazina iliyo chini ya wizara ya fedha ina jukumu la kusimamia uwekezaji na maslahi ya serikali katika mashirika ya umma na taasisi nyingine.<sup>6</sup> Ofisi hii imepewa jukumu la kudumu la kusimamia uendeshaji wa biashara na mambo ya watumishi wa bodi ambapo msajili wa hazina ana maslahi nako ama anamiliki. Ofisi hii inasimamia mashirika/taasisi za umma zipatazo 216. Serikali ina umiliki wenye thamani ya shilingi bilioni 22,678.16 hadi tarehe 30 Juni 2015.

### **6.1. USIMAMIZI USIORIDHISHA WAUWEKEZAJI NA MASLAHI MENGINE YA TAIFA**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa serikali imebainisha kwamba wakati wa ukaguzi amebaini Kupungua kwa uwekezajiwa serikali katika mashirika na taasisi nyingine na wakati mwingine kupungua kwa hisa zake ,kutokana na serikali kushindwa kuongeza mtaji wakati ulipohitajika kwenye mashirika na taasisi ilizowezeza kupitia fursa ya haki ya kununua hisa za ziada na mpya.

Hali hii husababisha nguvu ya serikali katika kufanya maamuzi kupungua , na hatimaye kupungua kwa uwezo wa serikali kupata gawio. Licha ya umuhimu wa ofisi hii, katika mwaka wa fedha 2015/16 ofisi ya msajili wa hazina ilitengewa shilingi **169,017,000,000 (Bilioni 169)** kwa ajili ya kulipia madeni na kurekebisha mashirika yenye matatizo ya mitaji. Serikali ya CCM iliishia kutoa shilingi **bilioni 10** tu! Ni uwendawazimu kupongeza mgao wa fedha, pasipo kuangalia kiasi kilichotolewa!

<sup>6</sup> Ilianzishwa kwa Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu) Sura 370 ya mwaka 2002 na marekebisho yake mwaka 2010

**Mheshimiwa Spika**,Kumekuwa na udhaifu mkubwa sana wa ushiriki wa Ofisi ya Msajili wa Hazina katika Mikutano Mikuu wa mwaka katika taasisi ambazo kuna uwekezaji wa serikali,hii inatokana na msajili wa hazina kutegemea ruzuku kutoka serikalini ambayo haikidhi mahitaji ya kuweza kusimamia mashirika ya umma na binafsi ambayo serikali ina hisa.Ofisi ya msajili wa Hazina hukusanya gawio, mapato mengineyo na michango kutoka katika makampuni wanayoyasimamia.Fedha zote zinazokusanywa na msajili wa hazina hupelekwa serikalini kwa sababu Msajili wa hazina hayupo kwenye mpango wa bakizo (retention scheme). Hivyo uwezo wa msajili kuhudumia au kusimamia mashirika yaliyochini yake ni duni sana.

**Mheshimiwa Spika**,Katika taarifa ya Msajili wa hazina ya 30<sup>th</sup> June 2012 shirika hili halikuwemo katika listi ya Mashirika ya Umma. Na hakuna uthibitisho wowote wa uhalali wa kuondolewa. Utapeli huo huo umetokea kwenye shirika la UDA(ambao sasa hivi wanakumbatiwa na serikali ya CCM katika uendeshaji wa mabasi ya mwendo kasi).<sup>7</sup>UKAWA ambao tumepewa jukumu la kuongoza jiji la Dar es salaam, tutapambana usiku na mchana kuhakikisha udhalimu huu wa uporaji wa shirika la wakazi wa jiji la Dar es salaam haufanikiwa. Ni Imani yetu nia hii njema ya UKAWA itaungwa mkono na Mhe. John Pombe Magufuli.

## 6.2 MASHIRIKA /MAKAMPUNI YASIYOTOA GAWIO SERIKALINI

**Mheshimiwa Spika**,Wakati serikali ikilalama juu ya ukosefu wa fedha, taarifa ya Msajili wa hazina <sup>8</sup> inabainisha kwamba kuna kampuni ambazo serikali ina ubia lakini haitoi gawio.HususanKampuni za kibiashara ambazo serikali ina hisa chini ya 50%. Kuna Kampuni 33 (kama zilivyoinishwa hapa chini) ambazo ambazo serikali ina hisa na Licha ya kwamba yanatakiwa kutoa gawio serikalini, Ni kampuni 'chache' ambazo zinatoa gawio kutokana na faida zinazopatikana.

### KAMPUNI

### HISA

- |   |        |
|---|--------|
| 1. Abood seed Oil Industries Limited / abood soap | 20%    |
| 2. Airtel Tanzania                                | 40%    |
| 3. Aluminium Africa Ltd (ALAF)                    | 24%    |
| 4. Datel Tanzania Limited                         | 35%    |
| 5. East African Cables (Tanzania) Ltd             | 29%    |
| 6. Friendship Textile Co.                         | 49%    |
| 7. Industrial Promotion services ( Tanzania) ltd  | 18.16% |

<sup>7</sup> The United Republic of Tanzania, National Audit Office, Annual General Report of the controller and auditor General, on the Audit of Public Authorities and other Bodies for the financial Year 2014/15, pg 12-16

<sup>8</sup> Ibid

8. Inflight Catering services co/LGS Skychef	20%
9. Kariakoo Market Corporation	49%
10.Keko Pharmaceuticals Industries(1997) Ltd.	40%
11.Kilombero sugar Co.	25%
12.Mbeya Cement Co. Ltd	25%
13.Mbinga Coffee Curing	43%
14.Mbozi Coffee Curing	32%
15.Moshi Leather	25%
16.Mwananchi Engineering and Construction Co.	25%
17.National Bank of Commerce (NBC)	30%
18.National Microfinance Bank (NMB)	30%
19.New Africa Hotel	23%
20.Tanelec Limited	30%
21.Tanganyika Planting Co. (TPC)	25%
22.TANICA	7.67%
23.TANSCAN TIMBER CO. LTD	49%
24.Tanzania Breweries Ltd	4%
25.Tanzania Cigarette co. Ltd	2.5%
26.Tanzania development Finance Ltd	32.1%
27.Tanzania Nationa Re-Insurance Corporation 1 Golden share	
28.Tanzania Oxygen Ltd	9.59%
29.Tanzania Pharmaceutical Ltd	40%
30.Tanzania Pipeline Ltd	33%
31.TLL Printing &Packaging Limited	25%
32.Usafiri Dar es salaam	49%
33.Williamson Diamond Limited	25%

**Mheshimiwa Spika**,Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni,inaitaka serikali ilieleze Bunge hili tukufu , kati ya kampuni tajwa hapo juu, ambazo zinatuhumiwa na Msajili wa hazina kutokutoa gawio(kwa lugha nyingine yanawaibia watanzania),zipi zinazotoa gawio serikalini, na zinatoa kiasi gani? Na zipi hazitoi gawio na kwa sababu gani?

### 6.3. UWEKEZAJI WA TAASISI/MASHIRIKA YA UMMA USIO NA TIJA

**Mheshimiwa Spika**,Taasisi/ Mashirika mengi ya serikali yameingia katika uwekezaji wa majengo na makazi ya kibiashara ambao unatumia fedha nyingi na unachukua kipindi kirefu na mapato yanayotokana na uwekezaji kuwa kiduchu hivyo kusababisha taasisi hizo kutokupata faida inayostahiki.Na mbaya zaidi Taasisi nyingi zimekuwa zikiwekeza katika eneo moja na kumlenga mteja mmoja hivyo kusababisha majengo mengi kukosa wapangaji. Taasisi za mifuko ya hifadhi ya jamii ya PPF, PSPF, NSSF , LAPF na GEPF zimekuwa zikitumia michango ya wanachama wao katika uwekezaji huo , hali hii inahatarisha usalama wa fedha za wanachama pichi zinapohitajika na wahusika .



**Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa NSSF pekee, kwa uchache tu umewekeza fedha za wanachama zipatazo shilingi trilion 1.381. Fedha hizi ni mbali na fedha ambazo wameikopesha Serikali kujenga majengo mbalimbali kama vile Mchinga Complex, Chuo kikuu cha Udom, ujenziwa daraja la Kigamboni n.k.

Mifano michache ya miradiya nyumba za NSSF;

- i. Nyumba 300 za Mtoni Kijichi (PHASE I & II) – Nyumba hizo zilikwisha uzwa tayari
- ii. Nyumba 800-Flats 500 na Villas 300 (PHASE III) ambao umegharimu shilingi bilioni 137.
- iii. Mradi wa AZIMIO SATELITE -Kigamboni wenye Nyumba 7160 (Flats & Villas) – Utagharimu shilingi bilioni 871
- iv. Mradi wa Dungu Farm-Kigamboni (Flats 568) Utagharimu shilingi bilioni 140
- v. Mradi wa MZIZIMA TOWER nyumba ya Ghorofa 32 unaotarajiwa kumalizika Juni 2017, ambao utagharimu shilingi bilioni 233.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika hotuba yake ya wizara ya kazi na ajira iliongelea uwekezaji wenye mashaka uliofanywa na Mfuko wa hifadhi ya jamii wa NSSF. Lakini majibu ya waziri aliyekuwa na dhamana yalikuwa ya kisiasa mno badala ya kuangalia ukweli wa kitaalam wa uwekezaji huo kwa kulingana na uwekezaji uliopo na thamani halisi ya ardhi kwa wakati ambao mfuko ulinunua ardhi husika.

#### **6.4. MFUKO WA PENSHE NI KWA WATUMISHI WA UMMA**

**Mheshimiwa Spika**, Kuna mfuko wa pensheni kwa watumishi wa Umma (PSPF) mfuko huu wa hifadhi ulianzishwa kwa sheria Namba 2 ya Mafao ya Hitimisho la Utumishi wa Umma ya mwaka 1999, ikiwa imechukua nafasi ya sheria ya Pensheni Sura 371 ya mwaka 1954, na mfuko ukaanza rasmi shughuli zake Julai 1, 1999.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa kumbukumbu za nyaraka zinaonesha kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2015 **mfuko unaidai Serikali kiasi cha shilingi bilioni 533.238** zikiwa ni udhamini wa Serikali katika ujenzi wa majengo ya taasisi kadhaa za Serikali, pamoja na mkopo kwa bodi ya mikopo ya elimu ya Juu. **Mbali na fedha hizo Mfuko unaidai Serikali fedha za michango ya wanachama na tozo kwa kipindi cha kuanzia mwezi Agosti 2015** hadi Februari 2016, **kiasi cha shilingi bilioni 305.30. Hiyo ni mbali na deni la** shilingi trillion 6, kutokana na kuwahudumia wastaafu wa zamani ambao hawakuwa katika mfumo wa pensheni.

**Mheshimiwa Spika**, Jambo lingine la kuonesha kuwa hii mifuko kushindwa kusimamiwa, ni kuwa PSPF ilinunua jengo la Quality Plaza(kwa bei ghali tofauti na uhalisia wa jengo) na sasa linaitwa PSPF Plaza kwa shilingi bilioni 36 na mfuko ukafanya ukarabati kwa gharama ya shilingi bilioni 1.27 lakini mpangaji wake mkuu akawa ni **Yule aliyewauzia jengo hilo,Bwana Yusuph Manji** ,ambaye mpaka anadaiwa shilingi bilioni 13.31 na mkataba wake wa kupanga umeisha lakini bado anaendelea kukaa na amegoma kulipa kodi.

#### **6.5. MFUKO WA MAFAO YA KUSTAAFU-GEPF**

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko huu kama ilivyo mifuko mingine ya hifadhi za jamii, mfuko umejikita katika uwekezaji wa majengo, hisa za makampuni yanayoorodheshwa katika soko la mitaji, amana za Serikali, mikopo serikalini n.k.

**Mheshimiwa Spika**, Takwimu zinaonesha kuwa hadi Juni,2015 uwekezaji katika majengo na ardhi ulifikia kiasi cha shilingi bilioni 25.789. Uwekezaji uliofanywa kwenye ununuzi wa viwanja:

- a. Kiwanja na 2401 Kitalu M- kilichopo eneo la Forest –Mbeya chenye ukubwa wa mita za mraba 48,588 kilinunuliwa kwa gharama ya shilingi bilioni 1.6 sawa na kununua mita moja ya mraba kwa shilingi 32,929/-
- b. Kiwanja namba 8 Kitalu E-kilichopo Ilemela Mwanza chenye ukubwa wa mita za mraba 8,191 kilinunuliwa kwa shilingi bilioni 2 sawa na kununua mita moja ya mraba kwa shilingi 244,170.43/-.
- c. Kiwanja na. 206 Kitalu H kilichopo Raha Leo Mtwara chenye ukubwa wa mita za mraba 1,428 kilichonunuliwa kwa shilingi milioni 225, sawa na kununua mita ya mraba kwa shilingi 157,563/-.
- d. Kiwanja Na 207, Kitalu H, mita za mraba 1,424, gharama za kiwanja shilingi 225,000,000/-, gharama kwa mita moja 158,005. Kiwanja kipo Raha Leo Mtwara.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa sheria ya SSRA, Benki Kuu ndio mamlaka ya kuhakikisha mifuko inafanya uwekezaji makini, je kwa uwekezaji huu ambao taarifa ya CAG ilisema kuwa unauweka mfuko katika hali ya kuweza kufilisika na hivyo wanachama kukosa mafao, serikali inatoa majibu gani? Tukumbuke kuwa mfuko huu unaendeshwa na watumishi wengi ambaoni wa kada ya chini na ambao kila mara wamekuwa wakilalamikia mishahara midogo kama walimu na manesi na watumishi wengine wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Mifuko ya hifadhi ya jamii ni chombo ambacho kama kikisimamiwa vyema katika uwekezaji wake na pia kuwepo kwa nidhamu ya matumizi ya fedha za wanachama ingeweza kutekeleza miradi mingi mikubwa kama vile miradi ya umeme na mradi wa reli badala ya kutafuta mwekezaji kutoka nje ya nchi. Miradi hii ni dhahiri ingeweza kurejesha gharama za uwekezaji haraka, badala yake uwekezaji unafanyika mkubwa unafanyika kwenye miradi ya majengo miradi ambayo urejeshwaji wa gharama za uwekezaji sio wa haraka.

**Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni** inaitaka serikali kumuagiza Mdhidhi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali (CAG) kufanya ukaguzi maalum kwenye mifuko yote ya hifadhi ya jamii na kuangalia kama mikataba na uwekezaji ambao ulifanywa na mashirika haya una tija kwa mashirika yenyewe, Wanachama wa mifuko hiyo na taifa kwa ujumla .

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia kwa mdhibiti wa mifuko ya hifadhi ya jamii (SSRA) itoe tathmini **square meter** moja ya ardhi yaliyojengwa majengo yaliyojengwa na mifuko katika maeneo mbalimbali hapa nchini ilinunuliwa kwa shilingi ngapi?

#### **6.6. FAO LA KUJITOA (WITHDRAWAL BENEFIT)**

**Mheshimiwa Spika**, katika Bunge la 10, mwaka 2012 kulitokea mtafaruku mkubwa sana kwa wafanyakazi hasa wale wanafanyakazi kwenye migodi, kutokana na ukweli kwamba masharti yaliyowekwa kwa wanaotakiwa kunufaika na pensheni (fao la uzeeni) ni lazima uwe umechangia mfuko kwa kipindi cha miezi 180 au miaka 16 na pia awe ametimiza umri wa miaka 55.

**Mheshimiwa Spika**, Mbunge wa Kisarawe wakati alipewa kazi na Bunge kukutana na wadau na kutoa mapendekezo ni kwa jinsi gani kanuni na sharia zitaweza kurekebisha ili kuondoa usumbufu kwa fao hilo la kujitoka, na wadau walitoa ushauri na maoni. Na kwa bahati mbaya tarehe 23 mei, 2016, Msemaji wa PPF alitangaza kuwa fao hilo la kujitoka limefutwa.

**Mheshimiwa Spika**, mazingira yanaonesha kuwa wastani miaka ya kufanyakazi katika sekta ya migodi ni miaka 5, na wastani wa umri wa watumishi katika sekta hiyo ni miaka 35. Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba watumishi wengi ambao ni wa mkataba na wanachangia lakini hawana uwezo wa kuchangia katika mifuko kwa kipindi cha miaka 15 na pia wengine inawalazimu wakae miaka zaidi ya 15 au 20 ndipo wafikishe umri wa miaka 55.

**Mheshimiwa Spika**, hoja ni kuwa fedha hizo hata kama ni milioni kadhaa ziko katika mifuko ya hifadhi, kwa kuwa vigezo havikutimia hadi unafikisha miaka hiyo ya kisheria bado fedha utakazolipwa ni zile zile, na kutokana na mazingira ya kiuchumi ni dhahiri thamani ya shilingi kwa dolla ikashuka sana. Kambi Rasmi

ya Upinzani inamtaka waziri wa Fedha kuliangalia suala hili vizuri ili kuepusha madhara makubwa yanayoweza kuwapa wahusika wakuu ambao ni watumishi wa mikataba na migodini.

## 7. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kama ambavyo tumejadili kuhusu umuhimu wa wizara ya fedha katika mustakabali mzima wa uchumi wanchi yetu na pia ni wizara hiyo hiyo inayohusika na masuala ya yote ya kodi za bidhaa na huduma.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa wizara hii inachangamoto nyingi na kubwa katika kutekeleza majukumu yake, lakini hilo haliondoi ukweli kwamba ni jukumu lake la msingi ya kuhakikisha watanzania wanaishi katika nchi yao wakiwa na utulivu wa akili **“peace of mind”**. Kwa maana kuwa watanzania wanaweza kuishi katika kiwango kinachokubalika na kuweza kutekeleza majukumu ya msingi ya kifamilia, kwani uchumi wa mtanzania kukua ni lazima uakisi katika maisha binafsi ya watanzania.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

.....  
**David Ernest Silinde (Mb)**  
**Naibu Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-**  
**Wizara ya Fedha na Mipango**  
**1<sup>st</sup> Juni, 2016**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea ninayo orodha ya wachangiaji tutaanza na Mheshimiwa Peter Selukamba atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Elias Kwandikwa ajiandae.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitachangia maeneo matatu ambayo Waziri ameyasema kwenye kitabu chake. La kwanza amesema page ya 11 kusimamia Deni la Taifa, la pili kusimamia Taasisi za Mashirika ya Umma na la tatu Kusimamia Sera ya Ubia Kati ya Serikali na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Deni la Taifa ni jambo ambalo lazima tuingaike nalo vizuri sana, tusipohangaika nalo tunaweza tukajikuta juhudi zote zinazofanywa na TRA kukusanya kodi nyingi zisionekane kwa kiasi kikubwa

katika kupeleka maendeleo kwa watu wetu. Katika kuangalia suala la Deni la Taifa, naomba nijikite kwenye suala la *interest* ambazo tunalipa kwenye madeno haya tunayoyachukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, na nitaomba Waziri atakaponijibu aniambie wanampango gani. *Interest* ni *risk management*, *risk management* inahitaji kila siku tuangalie kinachoendelea kwenye uchumi wa dunia. Sisi tunakopa dola, so kitakachotokea kwenye uchumi wa Marekani wale watu woote wanaokopa dola lazima kiwa-affect, sasa tunafanyaje? Ukienda kwenye mikataba yetu yote ya Wizara ya fedha ambayo tumekopa pesa kwa ajili ya kuendesha bajeti jambo jema, *interest* zetu zote ni *liable fructuate* ni *floating interest*, uki-float *interest* maana yake nini? Unapofanya *floating interest* maana yake uchumi wa Marekani uki-tilt kwenda juu au kwenda chini utaku-affect kwa sababu kwanza unakopa kwa dola lakini kwa maana nyingi ni kwamba haijawahi kutokea ishuke sana kwamba ile uliyo-float wewe uta-benefit mara nyingi sisi tunapoteza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano tumewahi kuchukua kwenye *Swiss Credit*, ukiangalia *interest* ya mwezi wa kwanza ni 1.3% lakini ukienda nayo mpaka unamaliza inafika mpaka *five percent* unafanyaje, ukimuuliza leo Waziri wa fedha mwezi kesho utakapokuwa unalipa ile mshahara, ile *first charge* ambayo ni *interest* atuambie ni shilingi ngapi atalipa kama *interest* Waziri wa Fedha hajui, kwa sababu itategemea *situation* ya *economy* ya wakati ule anataka kulipa tunafanyaje sasa kama nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshauri Waziri wa Fedha umefika wakati watu wa Idara ya Madeni waangalie *trend* za *interest* zinaendaje. Wanachofanya wenzetu kuna kitu kinaitwa *swapping*, una-swap *interest rate* unazi-swap ili uzi-fix ukifanya *fixed rate* maana yake unaweza uka-determine *cash flow* yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo wakati unapanga unajua mwezi ujao mshahara kiasi fulani, sijui majeshi kiasi fulani, *interest* kiasi fulani kwa sababu unajua una uhakika kwa hiyo, ni rahisi katika ku-manage *budget* ya Serikali, lakini ukiruhusu tukaenda kwenye *floating* ambayo ukienda kuangalia inavyo *fructuate by the end of the year* itafika 0.894 maana yake ni nini, Kidata atakusanya pesa nyingi sana, zile fedha zikija nyingi zinakwenda kwenye kulipa madeni mpaka tutaanza kuulizana mbona makusanyo yameongezeka lakini mbona hela haziendi nyingi kwenye Halmashauri, ni kwa sababu hatu-manage *interest rate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Waziri wa Fedha aje ani-critisize hapa kwamba tunafanyaje kwenye suala la ku-budget *interest rate* ili ku-manage *budget* ya nchi, ku-manage *cash flow* zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nataka kuchangia ni suala la *PPP*. Waziri wa fedha anasema kwenye kitabu chake page ya 11, kusimamia sera ya ubia kati ya Serikali na sekta binafsi maana yake ni *PPP*. Ukienda page ya 29, Waziri wa fedha huyo huyo anasema, kwenye suala la kuchukua madeni anasema masharti nafuu ambayo inakopa kwa uangalifu kutumika kwenye miradi yenye vichocheo vya ukuaji wa uchumi ikiwemo ujenzi wa miundombinu, barabara, reli, ujenzi wa mitambo ya kufua umeme, ujenzi wa viwanja vya ndege pamoja na bandari na kadhalika. Maana yake ni nini? Huku unasema unataka ku-*embrace PPP*, huku unasema nataka nikope kujenga miundombinu, niambieni ni nchi gani Waziri wa Fedha atuambie unaweza ukaleta *PPP* kama siyo kwenye miundombinu? *Tell us? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli kama Serikali kwa nini leo uweke hela kwenda kununua majenereta wakati ukitangaza wako watu wengi sana watanunua majenereta halafu ile fedha ambayo ungenunua majenereta peleka kwenye elimu, peleka kwenye maji, peleka kwenye shule, peleka kwenye kulipa wanajeshi, lipa mapolisi wetu, hii ndiyo *management* ya *economy*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la *PPP* naomba tujifunze kwenye *aspect* moja na Wabunge nataka mnisikilize kwenye suala la simu. Leo vijijini kwetu nani anayeuliza simu hii ni ya nani? Si kila mtu anataka kuwa na simu? Nani anauliza simu hii ni ya Serikali au ni ya nani? Leo tumeweka *legal frame work* yenye *clarity* watu wameweka fedha, wamefanya nini leo simu ziko mpaka vijijini, tunapata ajira, tunapata kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kwenye mambo mengine tunaona wagumu kweli kuleta watu wa nje ama kuleta *PPP* na ukiamua ili u-*benefit* watu wako Waziri wa Fedha, kama nia ni kusaidia *private sector* ya Tanzania hii ndilo eneo la kusaidia watu. Waambie unataka kujenga bandari, siwezi kukupa kujenga bandari mpaka uwe na Mtanzania, unataka kufungua umeme mpaka uwe na Mtanzania hii ndiyo namna tutaweza kuukuza huu uchumi na ikatusaidia kwa maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukidhani Serikali inaweza ikafanya kila kitu, Serikali hii tutaichosha. Tutashindwa kununua dawa hospitalini, tutashindwa kupeleka hela kwenye *education* kwa sababu leo hii tunasema elimu bure maana yake ni nini, watoto wengi sana wana-access watakuwa wengi tutahitaji kujenga madarasa, tutajenga kila kitu, hii ni hatari sana kwenye *economy*. Nikuombe Waziri wa Fedha, tulipitisha sheria ya *PPP* mwaka 2009, tuanze kuitekeleza sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine nilitaka kulizungumzia ni suala la Mashirika ya Serikali. Taasisi za umma, naombeni Waziri wa Fedha na hii kazi ya



Waziri wa fedha pamoja na kukusanya kodi lazima ufanye jukumu la kukuza uchumi wa nchi. Utaukuza uchumi wa nchi kama tuta-embrace biashara. Kama bandari wanafanyabiashara waacheni kuwaingilia, waacheni wafanye kazi za biashara. Kama TANESCO wanafanya biashara waambieni wafanye maamuzi ya kibiashara, ninyi kazi yenu mwisho wa siku muwaulize tu *though TR tunaomba dividend* mwisho wa mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Serikali kuna baadhi ya maeneo tuna-share. Kwa mfano nitasema PUMA Serikali ina asilimia 50 lakini Waziri wa fedha naomba nikwambie kwenye *bulk procurement* hamjawahi kutumia Kampuni yenu ya PUMA hata siku moja. Kwenye kununua mafuta mnanunua kwa watu wengine hii ni nini? Huku mna-share, mnapata *dividend* lakini mnapoanza kununua mnanunua kwa watu wengine, hivi nani asiyejipenda? Ukienda *South Africa* leo hakuna mfanyakazi wa Serikali ambaye hapandi Ndege ya *South African Airways*. Leo tunaingiza pesa, tunajenga ndege kitakachotokea kwenye *ticket* mtapanda Emirates, maana tunaaulizana maswali hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunataka mashirika haya na taasisi za Serikali yachangie kwenye uchumi wa nchi tuyaache yafanye kazi kibiashara. Naombeni sana bila kufanya hivyo hatutokwenda, naombeni tuanze kazi ya kuamini wafanyabiashara nao ni watu na niombe Waziri wa Fedha, tuache kufikiria wafanyabiashara ni wezi. Tuweke mazingira ya kuzuia wasikwepe kodi lakini tujue ni watu tunaowahitaji kwa maendeleo ya Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalotaka kusema ni suala la bei ya mafuta, *again* narudi kwenye *interest* pale pale, bei ya mafuta duniani imeshuka weee, imefika mpaka *barrel* kwa pipa shilingi dola 29, leo imefika dola 50. Maana yake ni nini kwenye uchumi? Sisi tumekaa tunasubiri tu dunia iamue mafuta yakipanda sawa yakishuka sawa. Kazi ya Waziri wa Fedha, Idara yako hiyo ya Sera na ya Madeni ni kuangalia vitu hivi kinachotokea kwenye uchumi kila siku. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tulichotakiwa tufanye, tungefanya *oil hedging* baada ya mafuta tulivyoona yanaanza kurudi, yameanza kufika ishirini na tisa, thelathini tunge-hedge tukasema mafuta yetu ya miezi sita tuta hedge kwa dola 30 *per barrel*. Na uki-hedge wanafanya watu wote, kama watu binafsi wanafanya, watu binafsi wanapata *interest* ndogo, kwa nini Serikali tusipate? Ni kwa sababu tunataka kufikirie vilevile tulivyozoea. Uki-hedge Waziri wa Fedha, maana ukiacha, mafuta yakiendelea kupanda maana yake bajeti yako inakuwa *tilted*, yale uliyoyapanga kununua mafuta haitawezekana, itabidi ubane. Rais amekuja na jambo zuri sana, Rais ameweka *austerity measure* kubwa, ana-manage economy, anapunguza matumizi, sasa tumsaidie. (Makofi)



**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Tumsaidie kwa kuangalia *trend* za market kwenye dunia. Leo mafuta mwaka jana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea, Mheshimiwa Peter Serukamba muda wako umekwisha. Mheshimiwa Elias Kwandikwa atafuatiwa na Mheshimiwa Almasi Maige.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kunipa nafasi na ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ameniwezesha kusimama kwenye Bunge lako hili. Pia nishukuru kwa dhati Wizara hii ni Wizara ambayo mimi nimefanya kazi nikitumika katika Ofisi ya Taifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa hiyo, kufika kwangu hapa kwa moyo wa dhati naamini uko mchango mkubwa wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwamba Wizara hii inasimamia mafungu mengi na kama tulivyoona kwenye *report* hii kuna mambo mengi ambayo ameyaonyesha Mheshimiwa Waziri niwashukuru kwa kazi nzuri ambayo inaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niende moja kwa moja kwenye kuchangia hoja hii. La kwanza nilitaka nijue tu Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Rais hapa aliahidi kwamba Sheria ya Manunuzi italetwa katika Bunge hili. Nilikuwa nikipitia *report*, sijaona kwamba tumejiandaa namna gani ili sheria hii ambayo ni mwiba inakuja kwenye Bunge hili ili tuweze kuipitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nilitaka nizungumze juu ya hizi idara chache tu ambazo ziko chini ya Wizara hii nikianza na hii ya Ofisi ya Msajili wa Hazina. Utaona kabisa kwamba inalo jukumu kubwa sana la kusimamia taasisi nyingi ambazo ziko chini yake na hizi taasisi tunategemea zikisimamiwa vizuri ili ziweze kutoa mchango mkubwa wa mapato katika Serikali. Niko kwenye Kamati ya Uwekezaji ya Mitaji ya Umma, utaona kabisa kwamba mashirika yaliyoko huko na taasisi ziko 215 lakini tunahitaji tuwe na watumishi wengi sasa utaona kabisa hata bajeti ta *TR* iko ndogo sana na bado tumeona hapa,

tumesikia kutoka kwenye taarifa ya Kamati wamepata asilimia nane ya kilichokuwa kimebajetiwa kipindi kilichopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji kuangalia mambo mengi sana katika taasisi hizi ili ziweze kutoa mchango mkubwa kwenye mfuko mkuu wa Serikali. *Capital structure* ya mashirika haya haiko vizuri, lakini utaona mashirika yaliyo mengi hata *investment plan* hayana, kwa hiyo, utaona tunahitaji watu wenye weledi tofauti katika ofisi ya TR ili iweze kuweka msukumo mzuri na mwisho wa safari tuone mchango mkubwa unakwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ukiangalia kwenye kiasi ambacho kitachangiwa na *non-tax revenue* bado kiasi hiki ni kidogo lakini ukienda kuangalia kwa undani kabisa nafasi ipo kama tutasimamia vizuri Mashirika haya naamini kwamba mchango mkubwa utakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nilitaka nichangie tu kwenye hii Wizara, kwamba nilikuwa nafikiria Mheshimiwa Waziri atasema hii kada ya wahasibu. Kada ya wahasibu bado inatoa tu taarifa, msukumo haujawekwa vizuri nilikuwa nafikiria labda tungeweza kuzipandisha hadhi angalau ziwe katika hadhi ya Ukurugenzi ili waweze kutoa mchango mkubwa wa uchambuzi lakini pia kushiriki katika maamuzi kwenye Wizara. Kwa hiyo, utaona tumeendelea kuwa na *unit*, lakini umeona kabisa katika Wizara kuna fedha nyingi sana ambazo Wahasibu wanasimamia nilikuwa nafikiri Mheshimiwa Waziri alitazame. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine nilitaka nizungumze juu ya uandaaji wa hesabu. Serikali imefanya uamuzi mzuri utayarishaji wa hesabu kwa viwango hivi vya Kimataifa kwenye *Accrual Basis*, utaona sasa karibu kile kipindi cha mpito karibu kinakwisha, hatutakuja kuwa na hesabu nzuri. Tunahitaji tupate hesabu ambazo zitaonyesha ile *National Wealth* tuone majengo yanaonekana kwenye hesabu, jumuifu tuone madaraja gharama zake, tuone ardhi, tuone madeni na mali mbalimbali, utaona sasa tangu tulivyoingia kwenye mfumo huu ikifika mwaka 2017 itakuwa kile kipindi cha mpito kinaisha, tutategemea kuwa na hesabu ambazo zinaweza zisipate hati safi kama ilivyokuwa kwenye Halmashauri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa liko jambo la kufanya Mheshimiwa Waziri, uliangalie hili, kikubwa zaidi kwenye kufanya uthamini wa mali utaona kwamba hata Kwenye Halmashauri za kwetu tunao ma-*valuer* lakini hawafanyi kazi ya kutathmini mali hizi za Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nafikiri nimshauri Mheshimiwa Waziri kwamba hili suala la kuthamini mali lichukuliwe kama ni *National issue* ili tuwe na

*frame work* nzuri ya kuhakikisha kwamba tuna muda wa haraka kukamilisha uthamini wa mali ili hesabu zetu siku za usoni ziweze kuwa nzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niliombe kupitia Wizara yako Mheshimiwa Waziri, mafunzo ya *IPSAS* kwa sababu *update* zipo kila wakati, tuweke msukumo ili tuweze kuwa na hesabu nzuri ambazo zitatusaidia kufanya maamuzi mbalimbali tunahitaji kuwa na kuhasibu *oil and gas*, tunahitaji kuhasibu *shares* na *investment*, kwa hiyo kila wakati kuna *update* zinakuja nilikuwa najaribu kuangalia kwenye bajeti ninaona kwamba saa nyingine upande wa mafunzo bado kidogo tunahitaji tuweze kusukuma tuweze kuweka mafungu ya kutosha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nilitaka nizungumze juu ya *accountability* (uwajibikaji). Nilikuwa najaribu kuzitazama hizi ofisi za *Internal Auditor General* lakini naangalia pia na ofisi ya CAG. Nilivyokuwa nikiangalia kule naona kwamba tutakuwa na shida kubwa kwa sababu pamoja na kuwa kulikuwa na utaratibu ule wa kupunguza matumizi kwenye OC lakini utakuja kuona kabisa kuna kazi hazitafanyika. Mheshimiwa Waziri alitazame hili, *Internal Auditor General* ofisi yake ikiwezesha, itamuwezesha CAG iwe nyepesi na saa nyingine hata gharama za ukaguzi zinaweza zikapungua lakini bado naona hapa msukumo upo mdogo, hivi kwa nini Mheshimiwa Waziri ofisi ya *Internal Auditor General* isipewe *full vote* ili uwajibikaji uweze kuongezeka? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia bajeti ya CAG imepungua sana na ukija kuiangalia kwa undani nilikuwa naangalia kitabu *Volume II*, utaona kabisa kwamba hizi kaguzi kwenye Serikali za Mitaa hazitafanyika Mheshimiwa Waziri hebu litazame kwa sababu utaona kwamba imetengewa kwenye ule upande tu wa kwenda kutembelea Halmashauri, kwa mfano, ziko shilingi milioni 332 kwenye kile kifungu ukiangalia. Sasa hii ni wastani tu labda wa mtu mmoja siku 20 kila Halmashauri ataenda kufanya kazi haitawezekana, kwa hiyo utaona kabisa kwamba hii *funding* iliyokuwepo kwenye ofisi hii Mheshimiwa Waziri itazame vizuri lakini vinginevyo hatutategemea kuwa na *report* nyingi kama ulivyozyonyesha kwenye *report* hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *report* nyingi sana mwaka huu tumezipokea, kwa hiyo tategemee siku za usoni hatutakuwa na *report* za ukaguzi nyingi kama ilivyokuwa kwa sababu hali iliyopo hapa siyo nzuri. Utaona kabisa sehemu ambayo ilikuwa imetengewa kwa mwaka uliotangulia shilingi bilioni 2.3 kwa ajili ya ukaguzi wa Wizara, ziko shilingi milioni 280, sasa hii inatuonyesha nini? Inaonyesha kwamba hii kazi ya ukaguzi haijapewa msukumo wa kutosha ili kuhakikisha kwamba tunapata *report* lakini mwisho wa safari tunaweza kufanya maamuzi mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka pia nimalizie kwa kutoa ushauri tu kwamba kama tulivyosikia kwenye *report* ya Kamati pia kwamba kiasi ambacho kilikuwa kimetengewa kwenye bajeti ni kiasi kidogo, kwa hiyo, wakati msukumo mkubwa unakwenda kufanya makusanyo ya kutosha basi tuhakikishe kwamba kiasi ambacho kinatengwa kwenye Bunge lako hili Tukufu kinapelekwa na kwa wakati ili kama kiasi chote kitatolewa basi itakuwa ni wakati mzuri wa miradi mbalimbali ya maendeleo kuweza kutekelezwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wakati huo huo tuendeleo kuangalia maeneo mengine ambayo yataweza kuongeza mapato ya Serikali na hasa hasa hii *non-tax revenue* yako maeneo mengi ambayo tukiweza kuweka msukumo mkubwa tutaweza kuona kwamba tunapata fedha za kutosha na mwisho wa safari utaona kwamba angalau hata ule mtiririko wa fedha kwenda kwenye Halmashauri utakuwa unakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusisitiza tena suala la *asset valuation* ni suala muhimu sana ili *national accounts* ziweze kuficha vizuri ili mali zetu kwenye Halmashauri zetu ziweze kuonekana vizuri, lakini pia hati safi ziweze kuongezeka. Utakuja kuona kwamba kwenye Halmashauri zetu kwa mwaka huu uliokwisha saa nyingine tunaweza tusiwe tumefanya vizuri sana lakini kutokana na hili tatizo kubwa la *asset evaluation* imekuwa ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru sana kwa nafasi hii naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Almasi Maige atafuatiwa na Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma ajiandae. Mheshimiwa Almasi Maige naona ametoka kidogo, Mheshimiwa Oran Manase Njeza atafuatiwa na Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma, Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu ajiandae.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuchangia kwenye hoja ya Wizara muhimu, Wizara ya fedha. Nianze kwanza kwa kuipongeza Wizara, Waziri pamoja na timu yake kwa kufanya kazi zao vizuri sana na kwa hotuba nzuri na pia kwa kutupa muelekeo ni kwa namna gani wamejipanga kuhakikisha kuwa yale malengo ambayo walikuwa wametupa mwanzoni yatatimia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo nilitaka na mimi nijaribu kushauri mambo machache. La kwanza ni suala zima la ukusanyaji wa mapato. Naona kwa muda mrefu sana tumetegemea mapato yetu kupitia TRA. Sidhani kama tukiendelea namna hiyo itakuwa *sustainable* ili tuweze kufikia hayo malengo na kukiangalia ni namna gani kipindi chote kilichopita tulikuwa tunazungumzia kuhusu miradi mbalimbali na Wabunge wengi tumezungumzia

kuhusu namna ya kutumia pesa, hatukupata muda namna gani hizo pesa tutakazotumia zitatoka wapi na zitakusanywa wapi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kiasi kikubwa naona nchi yetu ina uwezo mkubwa wa kujitegemea na bila hata kutegemea misaada kutoka nje. Tukiweza kujipanga vizuri, tukaangalia zile fursa tulizonazo ambazo ni nje ya zile za kodi ambazo tulikuwa tumezizoea nafikiri malengo yetu yanaweza kutimia kwa haraka sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, angalia ofisi ya TR, tunashukuru kwanza imeimarishwa sasa hivi kuna timu nzuri. Nafikiri tukiendelea kuimarisha hii timu, kuna nafasi ya kukusanya pesa nyingi kutoka kwenye mashirika yetu. Tuangalie ni kiasi gani ambacho Serikali imewekeza mitaji kwenye hayo mashirika. Je, haya mashirika yamepewa malengo ya kurudisha kiasi gani Serikalini? Mabilioni na mabilioni yapo huko lakini ukisoma kwenye *report* ya Waziri anaangalia ni namna gani ya kuyasaidia haya mashirika yalipe madeni, nafikiri hilo Waziri jaribu kuangalia, dunia ya leo ni dunia ambayo inaangalia zaidi tuende Kibiashara zaidi. Tuongeze *capacity* kwenye mashirika yetu, tuwe na *management* zinazoeleweka, tuangalie mifano ya mashirika yanayofanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalia Shirika kama NMB, benki kama NMB ilivyokuwa? Ilikuwa imefilisika lakini leo inafanya kazi vizuri sana. Sababu yake kubwa ni nini? Ni kwa sababu Serikali ilihakikisha kuwa inaweka *management* nzuri na leo hii ukilinganisha NMB na NBC ninaimani NMB inafanya vizuri zaidi. Angalia Shirika la Nyumba lilivyokuwa hoi lakini baada ya kuweka *management* nzuri, Shirika la Nyumba sasa hivi linafanya vizuri sana. Kwa hiyo, na haya mashirika mengine naomba mpe uwezo mkubwa sana TR aweze kuangalia hata vilevile *management* zitakazokuwepo pale na bodi zitakazokuwepo pale, hilo lizingatiwe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nilichokuwa namuomba Waziri aangalie ni Benki ya Wakulima. Naona kwenye repoti ya Kamati wametoa mawazo mazuri sana ya milioni 59 zile ambazo zililengwa kwenda kwa ajili ya Mfuko wa Vijiji zipelekwe kwenye Benki ya Wakulima na mimi hilo naungana nao. Hizi zitasaidia sana ili zilete chachu huko vijijini, wakulima waweze kupata mikopo kirahisi lakini pia na zile pesa ziweze kusimamiwa kitaalamu. Lakini vilevile milioni 59 ni kidogo mno, naomba ziongezwe zifikie hiyo bilioni 196 ambayo ni asilimia 20 ya bilioni 980.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa zaidi Wizara iliangalie; ushiriki wa mabanki kwenye uchumi wa nchi yetu. Riba za mabanki ni kubwa sana ukilinganisha tofauti ya riba anayolipwa anayeweka pesa (*depositor*) na anayekopa ni kubwa kupita kiasi na tumeona kwa muda mrefu

haya mabenki yanatengeneza pesa nyingi sana, lakini ni namna gani hizi pesa wanazozitengeneza ambazo zimetokana wakati mwingine na amana za walalahoi zimeweza kurudisha kwa wale watu ambao ni *depositors*. Nafikiri hili nilijaribu kuliangalia, hizi riba za asilimia 20, asilimia 18 ni kubwa mno. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine; unapoangalia amana nafikiri Mheshimiwa Waziri aangalie pesa zinazozunguka kwenye miamala ya *M-pesa or mobile money*, ni kubwa mno. Hizi tumeziangalia vipi ya kwamba nazo zinawezakusaidia kwenye uchumi wa nchi hii? Zinasimamiwa vipi? Nafikiri hilo tuendeleo kuliangalia vizuri. Ukiangalia katika hotuba ya Wizara hapa, hajaiona hiyo kama ni sehemu mojawapo ya amana tulizonazo nchi hii ambazo zinaweza kusaidia katika uchumi wa nchi yetu. Amana inayozunguka kwa mwezi mmoja ni zaidi ya trilioni 4.5, hizo ni nyingi mno. Chukulia kidogo tu, ya kwamba unaweza kuchukuklia hata 0.5 zirudi kwenye uchumi wetu, utapata bilioni zaidi ya 270. Naomba na hilo liangaliwe kwa karibu, tuweke mfumo vilevile wa kuzilinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ningependekeza tuangalie vilevile ni namna gani tuweke usimamizi wa hizi pesa ambazo Wizara zinakwenda kwenye miradi yetu. Nafikiri hapa kuna tatizo kubwa kwa sababu kama Wizara itapeleka pesa kwenye Halmashauri au kwenye miradi asilimia yote ile ikaliwa hiyo mojawapo ni kwamba yale mapato tunakuwa tumeyapoteza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunakuwa hatuna sababu ya kuzungumzia kutafuta mapato wakati tunashindwa kusimamia vizuri matumizi ya hayo mapato. Ukichukulia mfano, kwenye Halmashauri ya kwangu kuna bilioni zaidi ya two point five zimepelekwa kwa ajili ya miradi ya maji lakini mpaka leo unashindwa kuuliza ni nani ambaye anasimamia zile pesa. Maji hayatoki, miradi huioni! Makandarasi huwaoni!

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hizo ni pesa za wananchi, ni pesa za kodi, nani anazisimamia? Zimetoka Wizara ya Fedha labda zimekwenda Wizara ya Maji na zimekwenda Halmashauri, msimamizi ni nani hapo katikati? Na hili nafikiri ni tatizo kubwa, nafikiri tuweke *coordination* kati ya hizi Wizara zinazohusika ili tuweze kusimamia hii miradi yetu vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Sika, baada ya kusema hayo ningependa kwa kumalizia kuipongeza hii Wizara na pia suala zima la *commodity exchange* ingawa nimeongelea kwa kiasi kidogo sana lakini nafikiri hiki ni chombo muhimu sana hasa kwa wakulima. Tuiangalie kianzishwe haraka ili kiweze na wakulima wakafaidika na mazao hayo ambayo kwa sasa hivi tunapovuna, mahindi bei inakuwa kidogo sana lakini baada ya muda mfupi bei zinapanda. Kwa hiyo, kama kukiwa na chombo kama hiki kinaweza kusaidia ili wakulima waweze kufaidika.



Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma, Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu ajiandae na Mheshimiwa Asha Abdullah Juma atafuata.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na pia namshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye anaendelea kunijaalia afya njema ili na mimi niweze kuendelea kutoa michango yangu katika Bunge lako Tukufu hasa katika Wizara hii ya Fedha na Mipango. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba niipongeze Wizara ya Fedha kwa sababu imekuja na mpango ambao wananchi sasa wanaanza kuwa na imani kwamba kama mpango huu utatekelezwa basi wananchi wote wataenda kufaidika na nchi yao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze katika michango yangu. Kwanza kabisa naomba kuchangia suala zima la Deni la Taifa. Ukiangalia Deni la Taifa, faida zake kubwa sana ni katika kusaidia kuchangia katika maendeleo ya Taifa hususan katika kuendeleza miundombinu kama vile barabara, viwanja vya ndege, reli na hata kwenye afya pia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha kusikitisha sana ni kwamba Deni la Taifa limekuwa likiongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, ninazo data kidogo hapa; mwaka 2005 hadi mwaka 2010 Deni la Taifa lilikuwa yapata trilioni 10; mwaka 2010 hadi mwaka 2012 Deni la Taifa liliongezeka hadi kufikia trilioni 14, lakini mwaka 2015 hadi sasa Deni la Taifa sasa limefikia trilioni 41; hii inasikitisha sana. Kwa sababu gani nasema inasikitisha? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Deni la Taifa linaongezeka lakini wananchi bado hali inazidi kuwa ni ngumu. Swali langu sasa kwa Waziri, na naomba Waziri atakapokuja anisaidie walau kunipa majibu lakini si mimi peke yangu wala Bunge lako hili Tukufu bali hata wananchi wote wanaonisikiliza sasa hivi, kwamba; ni kwa sababu gani deni hili lime-shoot kutoka trilioni 14 mwaka 2012 hadi kufikia trilioni 41 kwa mwaka 2015. Ninaomba Waziri atakapokuja basi aje na ufafanuzi utakaoweza kuwasaidia wananchi wa Tanzania kuelewa ni kwa nini deni hili linazidi kuongezeka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia na Wabunge wenzangu deni hili linapokuwa linazidi kuongezeka ni kwamba kila Mtanzania katika nchi yetu anazidi kuwa na ongezeko la kulipa deni hili. Kwa mahesabu, bahati mbaya hesabu nilipata "F" kwa hiyo, sijui namna ya kupiga deni hili kwa kila Mtanzania lakini mtanisaidia pamoja na Waziri, kwamba hivi deni hili ni lini basi litaweza kuwafaidisha wananchi wa Tanzania. Deni linaongezeka, barabara bado ni



mbovu, kila Mbunge akisimama hapa wakati wa kipindi cha maswali na majibu hata wakati wa maswali ya nyongeza utasikia kila mtu analalamika kuhusiana na suala zima la barabara lakini hata hivyo, masuala ya maji, kila Mbunge anasimama hapa akiwakilisha wananchi wake kwa kulalamikia suala la maji. Hivi kwa nini Deni la Taifa linazidi kuongezeka? Ninaomba na ninamtaka Waziri atakapokuja anieleze tu ni kwa nini Deni la Tafa linazidi kuongezeka na wakati wananchi bado wana maisha ya chini au la sivyo naomba nitoe taarifa kabisa kwamba nitashika shilingi ya Mheshimiwa Waziri itakapofika muda wake, kama hatakuja na majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wanasema mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Nampongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa sababu amesaidia. Tunaona kabisa ongezeko la mapato hapa nchini sasa limeongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna changamoto ambazo zipo. Kwa mfano, baada ya kuongezeka kwa mapato haya, Halmashauri zetu hazifaidiki na ongezeko la Pato la Taifa. Nasema hivyo kwa sababu kwenye Halmashauri zetu kuna kero mbalimbali ambazo zimefutwa ambazo zimekuwa zikiwakera wananchi, na hata Mheshimiwa Rais nae pia amekuwa akiziongelea kero hizi. Baada ya kero hizi kufutwa hakuna mbadala wa mapato ambao umekuwapo katika Halmashauri zetu na ndiyo maana unakuta kwamba hata Halmashauri inapotenga fedha kwa ajili ya kuondoa changamoto za barabara, maji hata afya, hawawezi kufikia malengo yao kwa sababu ongezeko la pato katika Halmashauri zetu – mapato yanapokuwa yanakusanywa malengo ya Halmashauri yanakuwa ni makubwa kiasi cha kwamba Halmashauri zinashindwa hata ku-prioritize kwamba tuanze na lipi na tumalizie na lipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi ninaishauri Serikali walau katika Wizara hii kwa sababu Wizara hii ndiyo Wizara ambayo inakusanya mapato ya Taifa kwa ukubwa kabisa. Wizara hii naweza nikaisema kama ni Wizara nono, Wizara ambayo imeshiba, basi tunaomba kwamba Wizara ya Fedha iweze kupeleka fedha ziwafikie wananchi hasa katika Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano mdogo tu; katika Halmashauri zetu tuna mpango mzuri sana ambao tumeuweka wakuzitenga asilimia 10 ambayo asilimia tano inatakiwa kwenda kwa wanawake na asilimia tano iende kwa vijana. Lakini ukiangalia Halmashauri nyingi kwa tathmini ya haraka haraka zimekuwa hazitengi fedha hizi na si kwa sababu wanafanya makusudi kutokutenga fedha hizi iliziweze kuwafikia wananchi, lakini ni kwa sababu ya kulemewa na mzigo wa mipango ambayo wanakuwa nayo kiasi cha kwamba ile fedha hata kama inakuwa imetengwa matokeo yake inakuja kufanya dharura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano; nikiongelea katika Jimbo la Ilemela ambalo ni Jimbo la Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi Mama Angelina Mabula, kule tumekuwa na mipango mizuri sana, kila mwaka wamekuwa wakitenga fedha hizi lakini inapofika wakati kwamba sasa fedha hizi ziweze kugawiwa kwa wananchi hasa wanawake na vijana unakuta fedha hizi zinatumika katika kutengeneza barabara. Ukiangalia katika Wilaya ya Ilemela, ni Wilaya ambayo bado Halmashauri yetu ni changa. Ninaitaka na ninaiomba Serikali kwa unyenyekevu mkubwa sana kwamba iweze kuangalia Halmashauri zetu ili basi waweze kuongezewa fedha walau ziweze kuwasaidia wanawake hususan akina mama kama vile mama lishe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mzunguko wa fedha umekuwa ukionekana kama unaishia huku juu tu, yaani unaishia kwenye sehemu za juu, yaani wananchi wa hali ya juu ndiyo ambao wanafaidika na pesa. Sasa unapoongelea Pato la Taifa limeongezeka wakati mwananchi wa chini bado fedha haijamfikia ni masikitiko makubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ninamuomba Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake anisaidie tu kuja na mikakati kwamba Serikali imejiwekea mikakati gani ya kuziba mianya ya fedha ambazo imekuwa ikipoteza, kwa sababu inawezekana tukakusanya pesa nyingi lakini wako watu ambao kazi yao wamekaa kuchungulia hizi pesa na kuweza kujinufaisha wao wenyewe matokeo yake wananchi hawafaidiki na fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niongelee suala la shilingi milioni 50 kila kijiji. Tulipokuwa tukizunguka katika kampeni zetu za mwaka huu. Kila mwananchi anakuuliza kuhusiana na suala la shilingi milioni 50 kwa kila kijiji. Swali kwa Waziri ni kwamba, je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba kila mwananchi ananufaika na pesa. Ukiangalia kwa mfano katika ukurasa wa 24 Maoni ya Kamati au Uchambuzi wa Kamati, unaonesha kwamba Tanzania tunavyo vijiji 19,600, tunahitaji shilingi bilioni 980. Serikali imetenga asilimia sita tu ambayo ni shilingi bilioni 59 na milioni 500. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata nisipoendee kusoma taarifa hii ya Kamati lakini utaona kabisa kwamba tunayo changamoto ambayo bado ni kubwa sana kwa sababu inaonesha wazi sasa ni vijiji vichache sana, yapata vijiji 1,000 ndiyo ambavyo vitafaidika na hii shilingi milioni 50. Ni masikitiko makubwa sana. Hivi tunaenda kurudi vipi kule kwa wananchi? Tutawaeleza nini wananchi wetu kuhusiana na suala la shilingi milioni 50 kwa kila kijiji? Naiomba Serikali ifuate ushauri ambao umetolewa na Kamati ya Bajeti kwamba waongeze pesa walau ifikie asilimia 20 japokuwa na fedha hii bado ni ndogo sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba Sheria ya Manunuzi iletwe...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umeisha Mheshimiwa Kiteto. Mheshimiwa Dalaly Peter Kafumu

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (Makofi)

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu mdogo. Kwanza nimshukuru Mungu tena kwa kunipa nafasi hii kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu nichangie kama Wabunge wengine. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri kwa *speech* lakini pia nampongeza kwa kazi ngumu aliyonayo mbele yake. Tunajua yeye ni mtaalam ataweza kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie mambo mawili tu, na kama nitakuwa na la tatu basi nitachangia. La kwanza, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 31 kifungu 3.4.10 anasema katika mwaka wa 2015/2016 Wizara imepitia Sheria ya Manunuzi ya Umma namba saba ya mwaka 2011 na kupendekeza marekebisho ya Sheria hiyo. Napenda niseme kati ya vichaka au sehemu ambazo zinatumiwa kumaliza fedha ya Taifa hili ni Sheria ya Manunuzi. Bei za *tender* za Serikali huwa ni za ajabu kweli, ni kwa sababu ya sheria hii. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali kwa kweli sheria hii iletwe kwenye Bunge hili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma sheria ambazo mmetupa tuangalie za marekebisho *miscellaneous*, hii sheria siioni, mtaileta nini? Maana yake ndiko huko fedha zinakopotelea. Tunaomba kama mnaweza kuileta hata kwa hati ya dharura tutashukuru kwa sababu matumizi ya Serikali yanatumika vibaya kulingana na sheria hii ya mwaka 2011. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nataka kusema ni juu ya kazi ya BOT (Benki Kuu ya Tanzania) na hili jambo niliwahi kusema na narudia tena, labda baadaye litaeleweka. Ni vizuri kusema sema hata kama ni jambo la uongo linaweza kuwa la kweli. Sisi tunachimba dhahabu katika nchi yetu, tuna migodi minne sasa inayotoa dhahabu. Kazi ya BOT ni kutunza fedha za kigeni lakini kutunza dhahabu safi na dhahabu ina *represent* utajiri wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati tulijaribu kununua dhahabu tukapata hasara kwa sababu tulinunua dhahabu, tulivyoipeleka kwenye *smelting* ikaonekana ni makapi lakini sasa tuna nafasi nzuri ya kupata dhahabu safi kwa kuwaambia makampuni watulipe nusu ya mrabaha katika dhahabu

safi, hatuna tatizo. Hivi tunashindwa nini kuchukua dhahabu safi tukalipwa, tukaitunza ili baadae watoto wetu tutakapokufa tunawaambia bwana dhahabu hiyo mnaona mashimo hayo, ipo pale tani 200, 300 zimekaa. Uzuri wa kuwa na dhahabu kwenye *reserve* yetu tunaweza kurekebisaha hata thamani ya shilingi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, thamani ya shilingi ikiteremka tuna-release kidogo inakuwa nzuri. Kwa hiyo, tuna wajibu sasa hivi kutunza dhahabu. Najua niliuliza swali mwaka jana, Serikali ikapiga chenga lakini nasema hatuna sababu ya kutokutunza dhahabu kwenye benki yetu. Nchi zingine kama Marekani wana tani 8,000 kwenye *reserve* yao. Ujerumani wana tani zaidi ya tani 3,000 hata Libya nchi inayopigana ina dhahabu 116 tani. Na nchi nyingi ambazo unazona ni tajiri zote zina dhahabu kwenye *reserve* yao. Kwa nini tusifanye hivyo, kwa vile na sisi tunachimba dhahabu. Nchi za Afrika, iko *South Africa*, ina tani zaidi ya 100 kwenye *reserve* yao, sisi tuna shida gani? Sisi zero! Kwanini? Kwa hiyo naomba sana Serikali mtafakari jambo hili. Tafuteni wataalam waangalie namna tunavyoweza kufanya jambo hili tukapata dhahabu. (Makofi)

Jambo la tatu, ni matumizi holela ya dola katika nchi yetu. Dola inatumika mahali popote. Ukienda leo mahali popote hata Karikao unaweza ukatoa dola ukanunua, hata *salon* umekwenda kutengeneza nywele ukanunua kwa dola. Dola zetu zinapotea. Haziingii kwenye mfumo halali wa nchi, kwa hiyo dola zinaibiwa, zinapotezwa, zinabebwa kwa sababu tumeruhusu hili jambo. Ukienda *South Africa* ninyi mashahidi, huwezi kulipa hata hoteli ya kitalii kama huna dola, lazima ukatafute hela yaki-*South Africa*. Nenda nchi za Ulaya, hivyo hivyo, nenda Thailand, kila mahali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuna ruhusu kila mahali dola inatumika, tunapoteza fedha. Serikali tunaomba tena, nilishawahi kuuliza swali mkapiga piga chenga, mimi naomba jamani uchumi wetu unaharibika kwa sababu tuna mifumo ambayo haisimamimii fedha zetu vizuri. Hili ni jambo sio zuri sana. Tunaomba Serikali msimamie jambo hili tungeni sheria. Tungeni sharia tuko tayari sisi Wabunge tutunge sheria ili fedha za kigeni ziweze kubaki kwenye *reserve* ya Taifa letu vinginevyo tuna kazi kubwa kweli. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Ubelgiji huwezi ukatumia hela ya nje lazima uibadilishe iwe *Euro* sasa sisi tuna shida gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne na la mwisho, naomba nisipigiwe kengele, leo niko *very smart*. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuelimishwa kidogo, la kwanza ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ya shilingi milioni 50. Amesema mama yangu pale, kwenye bajeti huko kote nimeangalia sioni, hivi tumeiwekea bajeti wapi?

Inawezekana nimeisoma vibaya, kwenye vitabu vyote nimeangalia hakuna mahali ambapo tumeweka fedha kwa ajili ya kutekeleza ile ahadi ya Rais, basi nielimisheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ni MCC. MCC tuliachia ikaondoka hatuna mradi wa MCC tena, labda kama kuna mazungumzo mapya. Hata hivyo, bado kuna *subvote* 1007 inasema imeweka hela shilingi milioni 500 kwa ajili ya MCC, ni kitu gani hicho?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma atafuatiwa na Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba kama muda utakuwa bado upo Mheshimiwa Subira Mgalu ajiandae. Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

**MBUNGE FULANI:** Mtera.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba.

**MBUNGE FULANI:** Mtera.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Umbulla, muda kama utakuwa bado upo Mheshimiwa Mashimba Ndaki ajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia Wizara hii ya Fedha. Kwanza namshukuru Mungu kwa kuniamsha salama na kusimama ndani ya Bunge lako na naanza kwa kusema kwamba naunga mkono hoja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza na jambo la msingi lililozungumzwa na Waheshimiwa wachache waliopita juu ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011. Najielekeza kwenye Sheria ya Manunuzi ya Umma kutokana na ahadi ya Mheshimiwa Rais kupitia hotuba yake ndani ya Bunge hili lakini kutokana pia na mwelekeo wa bajeti ya mwaka 2016/2017 ambapo asilimia 40 inatarajiwa kutumika kwenye miradi ya maendeleo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tunatambua wakati ule ilipokuwa chini ya asilimia 40, kwenye asilimia 22 na kuendelea tuliona changamoto kubwa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali, udhaifu wa taasisi mbalimbali katika usimamizi wa matumizi ya pesa za maendeleo na za kawaida. Leo tulipopokea taarifa ya *miscellaneous amendment* zinazotarajiwa kuwasilishwa Bungeni kutoonekana kwa Sheria ya Manunuzi ya Umma imetufanya baadhi ya Wabunge tupate mashaka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mashaka hayo nikaenda kuchukua taarifa ya PPRA ya mwaka 2014/2015; nikajaribu kupitia kwa kina upungufu uliobainishwa na taarifa hiyo. Pamoja na kwamba taarifa inaonesha masuala ya manunuzi ya umma katika taasisi mbalimbali za kiserikali *level of compliance* iko juu lakini ukaguzi wa mashirika haya, kwa mfano mwaka 2014/2015 wamekagua jumla ya taasisi za manunuzi 80 kati ya hizo 39 ni za Halmashauri, lakini tunazo Halmashauri 168. Kufanya maamuzi ya kuchelea kuleta marekebisho ya sheria kwa ripoti kwamba labda mambo siyo mabaya si sahihi kwa sababu hata ukaguzi unafanyika kwa taasisi chache.

Kwa hiyo, niombe Serikali iwasilishe Muswada huo tufanye marekebisho kwenye baadhi ya vipengele ili asilimia 40 ya fedha za maendeleo zilete tija na *value for money* na matumizi hayo yaonekane ili Watanzania wenzetu waweze kufaidika katika maeneo mbalimbali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo naungana na Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa mimi ni Mbunge wa Viti Maalum na kundi kubwa naloliwakilisha hapa ni wanawake na vijana; na wanawake na Watanzania wengi walikipigia kura chetu kwa matumaini ya ahadi ya shilingi milioni 50 kwa kila kijiji. Tunaamini ahadi hii ikitekeleza itakuwa chachu katika uibuaji wa miradi mbalimbali na pia itakuwa chachu ya mzunguko wa fedha katika maeneo yaliyokusudiwa. Naungana na maoni ya Kamati yangu, Serikali pamoja na changamoto iliyopo, lakini dhima ya kuinua uchumi wa watu wachache au kupitia vikundi vya SACCOS ni muhimu kwa sababu mwisho wa siku watalipa kodi kutokana na shughuli watakazozifanya na itaongeza mapato ya Serikali, huu ni mzunguko tu.

Kwa hiyo, niombe Serikali iongeze kwani asilimia sita haitoshi na wengine tumeshafanya ziara katika maeneo mbalimbali, wanawake wa Kibaha, Mafia, Mkuranga, Rufiji, Bagamoyo na Kisarawe pamoja na vijana na makundi mengine mbalimbali yanayohusiana na masuala haya ya asilimia 20 wako tayari. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nijielekeze kwenye suala zima la utekelezaji wa bajeti ya mifuko kwa 2015/2016. Tunaweza tukawa na bajeti nzuri, tunaweza tukatenga pesa nzuri kwa maendeleo na matumizi mengineyo lakini kama mifuko hii kwa mfano Mfuko wa NAOT mpaka mpaka Machi, 2016 una asilimia 45 tu. Ofisi hii Kikatiba imepewa dhima ya kukagua matumizi na mapato ya fedha za Serikali. Kwa dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kupambana na ufisadi, kupambana na ubadhirifu, kupambana na maovu mbalimbali na tumeona kasi yake, mchango mkubwa atasaidiwa na Ofisi ya Ukaguzi wa Serikali (*National Audit Office*). Kwanza niombe Wizara ijitahidi kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha iweze kuwawasilisha fedha ambazo hawajasilisha mpaka sasa, asilimia 45 mpaka Machi ni kiasi kidogo. (Makofi)



Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kuna Mifuko ya Mahakama pia asilimia 61, Mfuko wa Bunge asilimia 49 pamoja na *interest*. Nataka kusema dhima ya mifuko hii ina nafasi kuchangia katika ukuzaji wa uchumi. Kwa hiyo, napenda kuisitiza Serikali ilione hili kwa sababu kama Mfuko wa Ukaguzi utakuwa haufanyi kazi iliyokusudiwa hata uwepo wa Bunge hili katika kazi ya kuisimamia na kuishauri Serikali ambapo msaidizi wetu mkubwa ni Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inawezekana tukapata tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo nizungumzie Wizara zingine, kwa mfano mpaka mwezi Machi Wizara ya Kilimo ilikuwa haijapelekewa fedha ya maendeleo. Kama kweli tunataka kuongeza mapato ambapo tunategemea kilimo ndicho kitachangia katika mchango wa Taifa, Wizara hii mpaka Machi kuwa haijapelekewa fedha za ndani ni tatizo. Pia tunayo Wizara ya Afya asilimia 11 tu, hata Wizara yenyewe ya Fedha naomba niisemee pia asilimia sifuri. Wizara hii ina mchango mkubwa katika kusimamia uchumi wa Taifa letu kama ambavyo Wajumbe wengine wamesema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze kwenye masuala ya mishahara hewa. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ametoa maelekezo na kwa namna ambavyo kazi imefanyika vizuri na kwa namna ambavyo Serikali imeweza kubaini zaidi ya watumishi hewa 10,000. Hata hivyo, inawezekana kabisa tatizo kubwa ni mfumo. Kwa hiyo, naungana na maoni ya Kamati kwamba Serikali izidi kuangalia mifumo yake hasa LAWSON ambao unatumika katika mishahara, lakini pia EPICA, kuweza kuiunganisha kati ya EPICA9 na LAWSON na isisitize matumizi ya Mkongo wa Taifa. Nadhani kupitia Mkongo wa Taifa masuala ya TEHAMA itaweza kuziunganisha Halmashauri na Serikali Kuu katika mawasiliano ya namna ya kudhibiti watumishi hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tungependa kuona hatua za haraka zimechukuliwa kwa watu waliosababisha kuwa na watumishi hewa. Maana kama tumeshapata idadi ya watumishi hewa 10,000, kiasi cha shilingi bilioni 10 kwa mwaka kilikuwa kinatumika, tunatakiwa tuwajue kinagaubaga na waliohusika wachukuliwe hatua za kinidhamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa niopongeze Wizara ya Fedha, niendeleo kuwaomba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martha Umbulla.



**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie Wizara ya hii ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yamezungumzwa na wazungumzaji wamenifilisi kidogo lakini niendeleo kusisitiza kwamba kwanza naishukuru Serikali yangu kwa kuhakikisha kwamba bajeti ya mwaka asilimia 40 zinakwenda kwenye miradi ya maendeleo. Hii ni hatua ambayo imekuwepo kwa mara ya kwanza na kabla kabisa ya utekelezaji, kadri wenzangu walivyosisitiza tunaomba na kwa muda mrefu tumesisitiza kwamba Sheria ya Manunuzi iletwe haraka sana Bungeni tuweze kuifanyia marekebisho ili asilimia hiyo 40 iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo iweze kuwa na *impact* kwa bajeti hii ya mwaka 2016/2017. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kupanga matumizi ni jambo moja lakini kutekeleza yale yaliyokusudiwa ni jambo la pili na la muhimu zaidi. Nishauri Wizara kuhakikisha kuwa yale yote yaliyokusudiwa, yaliyopangiwa matumizi yaweze kutekelezwa jinsi ambavyo Bunge litapitisha na kuidhinisha matumizi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona hadi kufikia Machi 2016 fedha zile zilizokuwa zimepangwa kwa bajeti ya mwaka 2015/2016, kwa mfano mafungu 62 yale yaliyoko chini ya Serikali Kuu ni mafungu 33 yaliweza kupewa fedha kwa asilimia 50. Kwa hiyo, ni wazi kwamba bajeti hiyo haitakidhi matarajio yale ama matumizi yale ambayo yamepangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria ya bajeti ambayo ni ya 2015 mwaka jana tu, tunatarajia kwamba sheria hiyo italeti *impact* kwa bajeti ya mwaka huu. Kwa kuwa kuna sheria, tuna imani kwamba matumizi ya fedha ambazo zimepangwa kufikishwa katika miradi yetu yatasimamiwa na sheria hiyo. Zaidi sana kwa kuwa tuna *mid term review* ya bajeti yetu, tunaamini kwamba Sheria ya Bajeti itaisimamia kikamilifu kuhakikisha kwamba jinsi Bunge litakavyoidhinisha fedha hizo zitaweza kufikishwa jinsi zilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu spika, nizungumzie na mimi mradi wa *Village Empowerment* maarufu kama shilingi milioni 50 kwa kila kijiji. Kwanza ni-*declare interest* kwamba mimi nina utaalamu kiasi fulani wa *micro-finance* na kwa hiyo, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Rais wetu kwa kubuni mradi huu wa shilingi milioni 50 kila kijiji. Pia nieleze hofu yangu, sijajua vizuri kwamba hiyo shilingi milioni 50 ambazo zitatolewa kama mikopo kwa wajasiriamali ni pamoja na fedha zitakazotumika katika kuhamasisha wananchi ama zitakazotumika katika kuweka wataalamu watakaosimamia miradi hiyo ama ni fedha zitatangwa na bajeti nyingine ili kuweza kuhakikisha kwamba shilingi milioni 50 kwa kila kijiji inamfikia kila mwananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nieleze wasiwasi wangu pia kwamba je, shilingi milioni 50 zinavyokwenda kwenye kijiji ni kwa jinsi gani kila mwanakijiji atafikiwa na fedha hizo? Kama hivyo ndivyo ilivyo na nadhani ndiyo matarajio ya Rais wetu kwamba kila mtu atapaswa kupata mkopo hasa wale waliolengwa wanawake na vijana. Kwa hiyo, ni lazima kuwe na mkakati madhubuti kuhakikisha kwamba hizi fedha zinawafikia walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, fedha hizo zinawafikiaje? Mimi siamini utaratibu huu wa SACCOS, naamini zaidi utaratibu wa *revolving loan fund* ili fedha hizi zitakapotolewa kwa awamu ziweze kuzunguka zimfikie kila mwananchi. Kwa sababu tuna uzoefu tumeona kwamba katika mifuko mingine ambayo tumeahidiwa na viongozi wetu, kwa mfano mabilioni ya JK, bahati nzuri mimi nilikuwa mmoja wa walioteuliwa kati ya Wabunge saba kushauri katika ile *National Executive Empowerment Council* lakini tukaishia kupata barua na hatukuweza kuitwa hata siku moja na hatukujua hata yalikwendaje na yaliishia wapi. Kwa hiyo, tuna hofu kutokana na uzoefu wa kipindi kilichopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba fedha hizi za sasa zikiwekewa utaratibu madhubuti, zikawekewa na riba kwa sababu riba ni suala muhimu sana katika kukopesha wananchi, unapoweka riba inazalisha zaidi na kupunguza uzito kwa Serikali kwa sababu ile riba inaweza ikatumika katika kuhakikisha kwamba kunakuwepo na wataalamu watakaolipwa ili wasimamie kwa kikamilifu utoaji wa mikopo na urejeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilishikwa na wasiwasi kama Wajumbe wengine wa Kamati yangu, ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, kwa shilingi milioni 50 zinapaswa ziende shilingi bilioni 980 na zitafikia jumla ya vijiji 19,600. Hata hivyo, tunaona kwamba zimetengwa tu shilingi bilioni 59.5 ambazo hazitoshi kabisa. Kwa hiyo, naishauri Serikali yangu iongeze bajeti hiyo ili azma ya kufikia kila kijiji kwa shilingi milioni 50 iweze kutimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile fedha hizi ziwekewe utaratibu ili zisiweze kupotea kama ambavyo tunaona utaratibu wa mikopo ya Halmashauri inavyopotoea kwa sababu haina ufuatiliaji, haina riba, haina hata namna yoyote ili ya kufuatilia nani kapewa, nani karejesha na kwa muda gani urejeshaji ufanyike. Mkopo ni fedha unayompa mtu kwa matarajio ya kurejesha kwa hivyo ni lazima uwe na utaratibu madhubuti. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yamekwishasemwa lakini nashauri kwamba utaratibu huu wa *revolving loan fund* ni sawa unapompa mtu mwenye njaa samaki ukitarajia kwamba kesho atakuomba tena, lakini kumbe ni vizuri basi ukampa mtu vifaa vya kuvulia samaki ili aendelee kupata chakula badala ya kumpa samaki ambaye atakula leo tu na kesho atakuwa hana kitu. Kwa hivyo, mimi nashauri, *revolving loan fund* ndiyo utaratibu ambao utawezesha

kila mwananchi kufikiwa ndani ya kijiji na hatimaye mradi utakuwa endelevu, hata Rais atakapokuwa amemaliza muda wake wa miaka kumi, atakuwa ameacha *legacy* ya mikopo hii inaendelea ndani ya nchi yetu, wananchi wanaendelea kukopeshana na hatimaye tunapunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na haya machache mengine yamezungumziwa sina sababu ya kurudia, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa wachangiaji kwa kipindi hiki cha kwanza. Mchana Bunge litakaporejea wachangiaji watakuwa Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba, Mheshimiwa Mashimba Ndaki, Mheshimiwa Janet Mbene, Mheshimiwa Almas Maige, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud na Mheshimiwa Neema Mgaya.

Waheshimiwa Wabunge, kuna Mheshimiwa Mbunge amesahau funguo zake alipokuwa ameenda kumtembelea Mheshimiwa Toufiq. Kwa hiyo, funguo zake atazikuta kwa maaskari wa hili geti kubwa ukitoka hapa.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine, nataka kutoa ufafanuzi kidogo wa Kanuni kadhaa hapa, Kanuni ya 5(2) na ya (3). Fasili ya (2) inasema, nitasoma kwa sehemu sitasoma yote, inasema; *"Spika atawajibika kutilia nguvu kanuni zote za Bunge..."*

Fasili ya (3) inasema; *"Spika anaweza kumtaka Mbunge yeyote anayekiuka Kanuni hizi kujirekebisha mara moja."*

Kanuni ya 72 inasema; *"Spika atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa, utaratibu bora unafuatwa Bungeni, na uamuzi wa Spika kuhusu jambo lolote la utaratibu utakuwa ni wa mwisho."*

Waheshimiwa Wabunge, kwa Kanuni hizi na kwa kuzingatia mamlaka hayo aliyopewa Spika imetoa pia mwanya kwa kutambua kwamba Mheshimiwa Spika au yeyote anayekuwa anafanya kazi kwa niaba yake anaweza kufanya makosa imeweka Kanuni ya 5(4) nitasoma, inasema; *"(4) Mbunge yeyote ambaye hataridhika na uamuzi wa Spika anaweza kuwasilisha sababu za kutoridhika kwake kwa Katibu wa Bunge ambaye atawasilisha malalamiko hayo kwa Spika."*

*(5) Spika atawajibika kuitisha kikao cha Kamati ya Kanuni za Bunge na kulijulisha Bunge kuhusu uamuzi utakaotolewa na Kamati hiyo. (Makofi)*

*(6) Spika au Naibu Spika hatakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni za Bunge inapokaa kujadili uamuzi unaolalamikiwa, bali Wajumbe watachagua Mwenyekiti wa muda kwa asilimia 50 ya kura za siri."*

Waheshimiwa Wabunge, umekuwepo upotoshaji maeneo mbalimbali lakini niwashauri kwa sababu hizi Kanuni zimeweka utaratibu wa namna ya kuenenda ndani ya Bunge na pale inapoonekana utaratibu haufuatwi, Kanuni zimeweka nini cha kufanya. Kwa kutambua kwamba Kiti cha Spika kimepewa nguvu za maamuzi, Kanuni hizi hizi zinatoa fursa ya mtu kukatia rufaa maamuzi ya Kiti cha Spika.

Kwa hiyo, Mbunge yeyote asiyeridhika, Kanuni hizi zinamruhusu kukata rufaa na zinamueleza nini cha kufanya. Naomba tuelewane vizuri hilo na kama mtu hajaelewa vizuri atakuwa amezisikia hizi Kanuni kwa sababu wote tunazo akazisome sawasawa. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi jioni.

*(Saa 07.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Tukae. Katibu.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mwongozo wa Spika.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali  
kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 - Wizara ya Fedha na Mipango**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Mheshimiwa Keissy, miongozo nitachukua baadaye. Kipindi cha asubuhi nilitangaza majina ya watu watakaochangia mchana ambao ni Mheshimiwa Asha Abdullah Juma atafuatiwa na Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba na Mheshimiwa Mashimba Ndaki ajiandae.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Fedha. Kwa dhati

kabisa nakupongeza kwa umahiri na uhodari wako kwa jinsi unavyoliongoza Bunge hili na hivyo ndivyo tunavyotegemea, hutishwi wala hubabaishwi. Mimi ikiwezekana nataka ukae asubuhi na jioni uoneshe kama wewe uko *fit* kweli kweli. Maana hapa tuko katika sehemu ya kutunga sheria na kuondolea wananchi dhiki zao waliotutuma halafu tunakuja kufanya michezo ya kuigiza hapa kuingia na kutoka kama biharusi aliyekuwa hana kitu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo niseme kwanza naunga mkono hotuba hii ya Waziri wa Fedha kwa asilimia mia moja. Naamini kwa kupitisha bajeti hii basi yale mambo yote yaliyokuwa yanapata utatanishi au ugumu kidogo chini ya Mheshimiwa Dkt. Mpango yatakwenda sawa kwa sababu ni mchumi mahiri na anaweza kuongoza Wizara hii na naamini atafanya kazi nzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme katika kusimamia uchumi wa nchi yetu hii basi ni lazima uchumi huu uwe na udhibiti mkubwa, tutengeneze mikakati ya kudhibiti uchumi wetu. Kwa mfano, kwenye nchi hii sasa hivi mtu anatumia *currency* yoyote anayotaka na kwa sehemu yoyote anayotaka, hapa udhibiti unaonekana umekuwa hafifu. Unaenda sehemu saa nyingine unaambiwa ulipe kwa dola na wewe Mtanzania uko hapa, kwa nini? Kwa nini kule tunakokwenda kuwakilisha ukitaka kununua chochote kama kule *South Africa*, hata kama unayo hiyo dola au *Euro* unatakiwa ukanunue kwa pesa za kule ambazo ni *rand*. Sasa na sisi tuudhibiti uchumi wetu, Wizara ya Fedha ifanye kazi hiyo, shughuli ya kudhibiti *currency* yetu ifanywe kwa bidii zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ya maendeleo inasema kwamba uchumi wetu kama sikosei umekua kwa 7% lakini ni kwa kiasi gani mtu wa kawaida anaweza kupata *reflection* hiyo? Unamfaidia vipi au mtu wa kawaida anaonekana vipi hali yake kunyanyuka kiuchumi? Kwa sababu haya maelezo tunayopewa hapa ni ya kisomi zaidi lakini tunataka aje chini hata yule mtu wa chini ajue anafaidika nini na ukuaji wa uchumi huu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nalotaka kuzungumzia ni hili la ukusanyaji wa kodi. Tunapongeza hatua zilizofikiwa za kuweka mashine za *electronic* sehemu nyingi lakini bado kuna uvujaji katika ukusanyaji huo, hii *efficiency* iko kwa kiasi gani? Kwa mfano, inawezekana na imeshatokea unakamatwa na *traffic* njiani anakwambia mashine ya kutolea risiti haifanyi kazi, sasa unamlipa nani au ile pesa ukiitoa inakwenda kwa nani? Hapa inaonekana ni vema udhibiti uzidishwe pamoja na kwamba tunakuwa na *digital* lakini udhibiti kwenye hivi vifaa vya kukusanyia kodi uwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la kukuza sekta binafsi. Sekta binafsi tumeambiwa inachangia uchumi kwa kiasi kikubwa na tunaunga mkono,

jambo hili ni zuri. Hapa hapa inaonekana wadau wazalendo ambao wanashiriki kwenye hii sekta binafsi wanapata vikwazo kwa sababu wageni wanaleta bidhaa zao japokuwa hafifu, sisemi kama zote lakini nyingi ni hafifu, kwa bei ndogo ambayo wanaiuza hapa; mzawa na mwekezaji wa sekta binafsi anashindwa ku-compete. Hii binafsi na holela sana haifai, uwepo udhibiti wa bidhaa na tuwaunge mkono kweli kweli hawa wawekezaji wa binafsi ili waweze kushamiri. Kwa sababu nchi hii itajengwa na wenyewe wazawa, hao wengine wanakuja kuchuma kisha wanaenda zao. Itakuwa kama hii hadithi ya kudai mjusi, mjusi kachukuliwa tunadai hapa kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, naamini bado kuna kazi kubwa ambayo inatakiwa ifanywe na hii Wizara yetu ya Fedha na ninaamini itawezekana. Sina maneno zaidi kwa sababu mimi si mtaalamu wa fedha lakini kidogo mwanga ninao na naamini kwa kupitia Waziri wetu huyu kazi kubwa sana itafanyika. Nawapongeza wote na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba atafuatiwa na Mheshimiwa Mashimba Ndaki na Mheshimiwa Janet Mbene ajiandae.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nitoe mchango wangu katika Wizara hii muhimu ambayo ni ya Mipango na Fedha. Nichukue fursa hii pia kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kufika siku ya leo. Pia nitakuwa mnyimi wa fadhila kama sijampongeza Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mpango na timu yake kwa hotuba nzuri na mipango ambayo tunaiona Tanzania mpya iko mbioni kuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi. Nakupongeza kwa umahiri wako mkubwa, kwa weledi mkubwa na unavyoendesha Bunge hili la Kumi la Moja. Usitishike na hivi vitisho kutoka upande wa pili, simamia hapo kwa sababu ya kutenda haki. Walizoea kupindisha sheria, sasa wamekutana na nguli wa sheria ambaye ni wewe ndio maana wanagonga ukuta. Usivunjike moyo, sisi tuko nyuma yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba nijielekeze katika kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii hasa kwenye Benki ya Kilimo kwa sababu kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa hili. Serikali kwa kuliona hilo walianzisha Benki mahsusi ya Kilimo na Bunge hili la Kumi ambalo sisi hatukuwepo lakini tulikuwa tunasoma kwenye magazeti na taarifa mbalimbali lilipitisha sheria ya Serikali kuweka mtaji wa kutosha katika benki ile ili kutatua changamoto za wakulima wa nchi hii. Kwa sababu tatizo kubwa la nchi hii, sekta kubwa inayoajiri watu wengi ambayo ni kilimo imekuwa haikopesheki na niipongeze Serikali kwa kuliona hilo kwa kuanzisha benki hii. Walitenga zaidi ya shilingi bilioni 300 iwe kwenye Benki ya Kilimo, lakini mpaka sasa nasikitika Serikali wamepeleka shilingi bilioni 60 tu. Hizi shilingi bilioni 60 hazitoshi kutimiza malengo



na mipango ya Serikali iliyopanga kwa ajili ya kukwamua Watanzania walio wengi waliojijiri katika sekta ya kilimo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili limekuwa ni kubwa sasa matokeo yake benki hii badala ya kujielekeza katika lengo kuu la kuendeleza sekta ya kilimo hasa zile skimu za umwagiliaji na kuwakopesha wakulima, wanafanya kazi kama za benki za biashara, kutoa mikopo ya muda mfupi kwa sababu wanaogopa kupata *risk* kubwa. Wanaweza kutoa mikopo ya muda mrefu na pesa ikazama na wakakinzana na masharti ya Benki Kuu ya mtaji unaohitajika. Kwa dhamira hiyohiyo ambayo Serikali mliiona mwanzoni na mipango mizuri iliyokuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hii benki iongezewe fedha ili iweze kujitanua na kuwawezesha wakulima wengi kufaidika wakiwepo na sisi huku wa mikoani katika Jimbo langu la Morogoro Kusini Mashariki na Tanzania kwa ujumla, hii benki ndio mkombozi wa mkulima. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikiwezesha benki hii inaweza kufungua matawi yake na kuongeza rasilimali watu. Kwa sasa hivi ule mtaji waliopewa hawawezi kujitanua zaidi ya kuwa Dar es Salaam ambapo ndiyo makao makuu, lakini kama mnavyojua Dar es Salaam siyo wadau wakubwa sana wa kilimo, kilimo kiko mikoani, Morogoro na sehemu nyingine. Kwa hiyo, niombe sana Serikali yangu iongeze mtaji katika benki hii ili lengo na kusudio lililokusudiwa liweze kutimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa pili nijielekeze katika *Tanzania Commodity Exchange*. Ni wazo zuri kwa sababu utakuwa ndiyo muarobaini wa soko la uhakika la bidhaa zetu za kilimo hususan kwa wakulima wa Tanzania. Kwa sababu ni soko ambalo litatoa haki kwa wadau wote wa soko hili kuanzia mkulima, madalali, wafanyabiashara, mawakala lakini hata na wanunuzi wenyewe. Pia kutakuwa na uhakika wa ubora ambao unajulikana kwa sababu mambo yataenda kisheria na kimtandao, hawezi mtu yeyote kudanganywa, bei itakuwa wazi lakini hata na ubora utajulikana, ule udanganyifu mdogomdogo utaondoka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu tu katika hili na niombe Serikali kwa sababu katika utaratibu wa soko hili miongoni mwa wadau wakubwa watakuwa wale madalali wa hilo soko, madalali wa wanunuzi na wa wauzaji. Katika kitabu cha hotuba nimesoma anasema mpaka sasa hivi kuna makampuni matano ambayo yameshajiorodhesha katika soko hili. Kwa hiyo, niombe wakati anakuja kujumuisha angetutajia angalau makampuni haya ni yapi ili tuwe na uelewa mpana zaidi na tuone ni makampuni yale yale ya kiujanja ujanja yameshakamata fursa au sasa ni makampuni ya ukweli yako kwa ajili ya kumkomboa mkulima halisi wa Tanzania?



Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii ni pana sana na imeajiri watu wengi kwa maana ya wafanyabiashara wadogo, wafanyabiashara wa kati, mawakala, madalali, ajira zao kubwa ziko hapa. Kwa hiyo, naomba kuishauri Serikali pamoja na kwamba tunaenda kwenye utaratibu huu wa soko ambao ni mzuri sasa makundi haya ni vizuri tukayatambua katika ushirika wao mbalimbali. Kwa mfano pale Dar es Salaam kuna Chama cha Madalali cha Mazao ya Mahindi na Ufuta lakini Morogoro pia viko vyama vya madalali na mikoa mingi vipo. Kwa sababu mitaji yao ni midogo ni vizuri tukawatambua kisheria kwenye umoja wao huo tukaweka utaratibu wakaingia kwenye soko hili nao wakatumba kama ndio madalali wa wakulima au wa wazalishaji. Badala ya kuwaacha nje tukaachia makampuni makubwa ndiyo yashike kazi hiyo basi tujue tutakuwa na kundi kubwa la vijana wa Kitanzania watakosa ajira jambo ambalo ni hatari. Sisi lengo letu kubwa ni kutengeneza ajira kwa ajili ya kuongeza vipato kwa wananchi wetu wengi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu katika taratibu huu, Wizara hii ivitambue vikundi vyote au umoja wowote wa madalali Tanzania nzima. Kwa sababu kwanza itasaidia sana wakitambuliwa kisheria na kupewa leseni inaweza kuwa *tax base* nyingine kwa sababu nafahamu wanapata mapato makubwa hawa madalali wa mikoa mbalimbali. Suala la udalali mtu akienda kununua atatumia dalali na akiuza atatumia dalali. Wakitambuliwa kisheria na mapato yao yakijulikana watasaidia kuchangia katika pato la Taifa kwa maana ya kulipa kodi na kila kitu. Pia kama Serikali mkawatengenezea fursa ya kushiriki katika huu utaratibu mpya unaokuja ili tusiliache kundi kubwa nyuma baadaye tukaenda wachache. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo siyo kwa sababu ya umuhimu, hii Wizara ndiyo Wizara nyeti inayogawa mafungu ya fedha. Sisi kama Bunge hapa tunapitisha bajeti lakini kuna changamoto kubwa pesa haziendi kama tulivyopitisha na pia hazifiki kwa wakati. Nimuombe Waziri Mheshimiwa Dkt. Mpango, ni mpya kwenye Wizara hii na ndiyo maana sasa hivi hatuwezi kuchangia sana tunampa nafasi, changamoto zilizotokea huko nyuma tunaomba uzirekebishe ili pesa hizi tunazopitisha zifike kwa wakati na zifike kama tulivyopitisha ili zile shughuli za maendeleo tulizopanga katika Majimbo yetu na Wilayani kwetu ziende kama zilivyopangwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mmoja tu, suala la MKUKUTA katika Halmashauri yangu ya Morogoro Vijijini mwaka wa tatu huu haijafika hata senti tano. Hata ile miradi ambayo ilianzishwa imeishia palepale badala yake tumeelekeza nguvu kwamba wananchi wajichangie, wameshajichangisha tumeshamaliza vyumba vya madarasa zaidi ya miaka mitatu lakini mafungu hayapo. Kwa hiyo, nimuombe kwa niaba ya Serikali hiyo basi walete haya mafungu ili tuweze kumaliza miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja kwa 100% na nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mashimba Ndaki atafuatiwe na Mheshimiwa Janet Mbene na Mheshimiwa Almas Maige ajiandae.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nachukua nafasi hii kukushukuru kunipa nafasi tena ili na mimi niweze kutoa mawazo yangu juu ya Wizara hii ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea nataka mimi pia kama ambavyo amezungumza mzungumzaji aliyepita, nikutie moyo kwamba kazi unayofanya ni njema, hauna sababu za kunyong'onyea au kujisikia upweke, sisi tupo. Wote tumetumwa na wananchi ili kuja kuwasemea hapa Bungeni. Kwa hiyo, timiza wajibu wako kama ambavyo inakupasa kufanya na sisi tutakuwa pamoja na wewe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nijielekeze sasa kwenye kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri lakini nianze na ukurasa ule wa 40, Msajili wa Hazina. Msajili wa Hazina anayo kazi kubwa ya kusimamia rasilimali za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali kwa ujumla. Kazi yake hii ni kubwa na muhimu sana kwa Taifa, inabeba vitu vingi, mashirika na taasisi za Serikali uangalizi wake uko chini yake. Nilikuwa najaribu kujiuliza, je, huyu mtu ana wafanyakazi wa kutosha? Tena wawe wa kada mbalimbali kwa sababu, mashirika na taasisi hizi za Serikali ni nyingi lakini pia zina sekta mbalimbali tofauti-tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa najaribu kuangalia bajeti yake aliyowekewa na kulinganisha na ukubwa wa kazi ambayo amepewa, naona kama haitoshelezi. Mwanzoni niliona kama ni kubwa, iko shilingi 160,181,000,000 nikaona kama ni kubwa lakini nilipoingia kwa undani nikakuta ndani yake shilingi milioni kama 150 hivi ni kama *social responsibilities* kwa mashirika yaliyo chini ya huyu Msajili wa Hazina. Nikaona ukiondoa pesa za maendeleo anabaki na hela kidogo sana za uendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu hii imepewa kazi kubwa sana. Mheshimiwa Rais alipokuwa akihutubia Bunge hili alisema kuna mashirika ya umma yaliyouzwa ambayo tathmini yake inabidi ifanyike, mengine yarudishwe, mengine yaangaliwe kama yalipouzwa yanaendelea kufanya shughuli zile ambazo zilikuwa zimekusudiwa au la. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nimeona tu mashirika ambayo wameandika Kiswahili cha kileo, uperembaji ni kama 55 tu lakini pia hatujaona kwa kina kwamba haya 55 ndiyo yanayofanya kazi, ndiyo yaliyofilisika, ndiyo yaliyobadilisha matumizi au yana hali gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa najaribu kuangalia bajeti nikaona kwa sababu labda ya bajeti kuwa ndogo ndiyo maana Msajili wa Hazina hajaweza kufanya kazi yake ipasavyo kuweza kutupa taarifa zilizo kamili kama wananchi ili tuweze kufahamu. Kwa sababu kama ni ahadi ya Rais kwamba mashirika haya ya umma mengine yatarudishwa Serikali au yataangaliwa yauzwe upya au mengine yatafanyiwa mpango mwingine, tungetakiwa sisi kama wananchi kujua hatua iliyofikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Waziri anapohitimisha Wizara yake hii pengine tutapenda kujua kuna hali gani ya mashirika na mali za Serikali chini ya Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni ufuatiliaji na tathmini. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri pia nilipokuwa najaribu kuangalia ufuatiliaji na tathmini haujapewa uzito ule unaostahili. Asilimia 40 ya bajeti ya nchi yetu mwaka tunaouendea itakuwa ni bajeti ya maendeleo. Kama hatuna mkakati na mpango unaoeleweka juu ya ufuatiliaji na tathmini tunaweza kujikuta tuna miradi ambayo iko chini ya kiwango, haiko sawa na thamani ya fedha iliyopangiwa au haijakamilika sawasawa. Kwa hiyo, kipengele hiki cha ufuatiliaji na tathmini ni muhimu sana kikieleweka kwamba kipo na kwamba kinafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zetu huko tulikotoka miradi mingi inayotoka Serikali Kuu haina fedha ya ufuatiliaji na tathmini. Kwa hiyo, wanapoagizwa kufuatilia miradi hii ili waweze kutoa taarifa Serikalini wanashindwa kufanya hivyo kwa sababu hakuna bajeti mahsusi kwa ajili ya jambo hili kwa hiyo wanahangaika wanabaki tu sasa kujikusanyakusanya wenyewe kwa fedha yao lakini wana malalamiko makubwa. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri anapokuwa anahitimisha pia ajaribu kuangalia suala la ufuatiliaji na tathmini liwekewe uzito unastahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni uwezo wa mashirika chini ya Wizara hii, yapo mashirika chini ya Wizara hii lakini nizungumzie tu shirika moja la *TTCL*. *TTCL* bado inaendelea kupata ruzuku ya Serikali. Najiuliza *TTCL* ni Kampuni ya Simu kama ambavyo makampuni mengine ya simu yalivyo, inashindwaje kuingia kwenye ushindani kama yanavyoshindana makapuni mengine na yenyewe ikatupatia faida kama Shirika letu la Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukijaribu kuangalia taarifa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri unaona kabisa kwamba *TTCL* bado haijasimama pamoja na kutiwa nguvu na vitu vingine.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri anaposimama hapa kujibu hoja atuelezee mashirika yaliyo chini ya Wizara hii hasa yale ambayo ni mzigo kuna

sababu gani ya kuendelea nayo? Kwa nini mengine tusiyaache tukaendelea na mashirika ambayo yanaweza yakatoa faida kwa Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho kimezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengine ni Sheria ya Manunizi. Kweli kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri hajataja kitu chochote lakini sheria hii pia ilipigiwa kelele kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais alipokuwa anafungua Bunge hili. Tulitegemea kwamba tungepata majawabu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba hatua tulizonazo ni zipi sasa kuhusianana na sheria hii. Tunapeleka fedha nyingi kuanzia mwakani kwenye Halmashauri na sehemu zingine lakini Sheria ya Manunuzi imebaki ile ile inayotunyonya, ile ile inayolalamikiwa. Kwa hiyo, tungependa Mheshimiwa Waziri atueleze Sheria hii ya Manunuzi italetwa lini hapa Bungeni ili tuweze kuirekebisha na miradi itakayofanyika ifanyike kweli kuonesha *value for money* ambayo imetumika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze la mwisho juu ya Benki ya Wakulima ambayo imeundwa hivi karibuni. Benki hii imepewa shilingi 60,000,000,000 lakini bado wanalalamia wakati kuna benki nyingine wamepewa kama shilingi 20,000,000,000. Mfano *TIB Corporate* hata kwenye hotuba ya Waziri amesema hawa watu wameweza kuvuta amana zingine sasa hii *TADB* yenyewe imeshindwaje kuvuta amana zingine na inashindwaje hata kufika tu maeneo ambayo wakulima wapo? Kwa sababu ukijaribu kuangalia benki hii bado iko Dar es Salaam kama walivyozungumza wazungumzaji wengine, naona kama hatutaweka nguvu inayoeleweka mwelekeo wake hii pia inaweza ikawa benki tu ambayo ina jina la Benki ya Wakulima lakini wakulima haiwasaidii. (Makofi)

Kwa hiyo, naomba sana tuwasaidie wafanyakazi walioko kwenye benki hii ili kuweza kufikia maeneo yetu ya vijijini ili wawaguse wakulima kama lilivyo jina la benki yao. Vinginevyo tutakuwa tuna Benki ya Wakulima kama tulivyokuwa na Benki ya Wakulima Vijijini *CRDB* au *TRDB* zamani lakini isiweze kuwasaidia wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu yalikuwa ni hayo lakini Mheshimiwa Waziri atakaposimama kuhitimisha hoja yake basi naamini tutapata majibu na majawabu ya hoja hizi nilizozungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janet Mbene atafuatiwa na Mheshimiwa Almas Maige na Mheshimiwa George Malima Lubeleji ajiandae.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa lakini vilevile na mimi naomba niungane na wenzangu kukutia moyo kwa kazi nzuri unayoifanya humu ndani. Umekuwa unasimamia vizuri Kanuni

tulizojiwekea wenyewe Bungeni, umekuwa una misimamo mizuri ya kuhakikisha kuwa kazi za Bunge zinafanyika vizuri. Wale wanaokulalamikia ni kwa sababu wanataka kufanya kazi wanavyotaka wao wakati wakijua kabisa wana wajibu wa kutumikia wananchi. Sisi tuko nyuma yako, usitetereke wala usife moyo, kaza buti na kazi iendelee. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na mimi nimpungeze Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Naibu Waziri na Maafisa wake wote kwa hotuba nzuri iliyosheheni maelekezo mazuri sana lakini naomba nichangie machache. Kwanza kabisa, nataka kuzungumzia suala la Msajili wa Hazina. Naipongeza Serikali kwa kuitenganisha hii taasisi ikawa ya kujitegemea ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi mzuri zaidi. Nataka vilevile kuzungumzia kuwa Msajili wa Hazina sheria yake yeye na sheria za yale mashirika ambayo anayasimamia huenda kutakuwa na haja ya kuzipitia kuona kama kuna kusigana kwa aina yoyote.

Vilevile kazi ya Msajili wa Hazina ni kuhakikisha kuwa anasimamia vizuri uwekezaji wa Serikali katika mashirika mbalimbali. Katika kufanya hivyo anawajibika kuhakikisha kuwa haya mashirika yanaleta tija kwa Serikali na kwa nchi kwa ujumla. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na zoezi la muda mrefu kuangalia jinsi gani mashirika haya yamekuwa yaki-perform ili kuona kama yameshindwa kufanya kazi ambazo zililengwa tangu mwanzo basi itafutwe njia nyingine ya kuyamiliki au kuyaondoa kabisa. Kwa hiyo, hatutegemei mpaka sasa kuendelea kubeba mashirika ambayo ni mzigo. Tunataka kuona vilevile kuna uratibu fulani unafanywa kwa mashirika ambayo yalianza miaka mingi iliyopita na kwa wakati ule pengine yalionekana yanahitajika lakini sasa hivi kufuatana na maendeleo ambayo yamejitokeza katika uchumi duniani na nchini kwetu labda hayana tena umuhimu huo au yanafanya shughuli ambazo zinafanana basi yaunganishwe au yawe *harmonized* kwa njia ambayo italeta tija kwa Taifa, badala ya kuwa na mashirika ya umma mengi yanatulia fedha tu katika gharama za uendeshaji lakini faida yake kubwa haionekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia mashirika ambayo mengine yalikuwa ni ya *research* mbalimbali. Mengi yanafanana katika utendaji wao basi hebu tuyapitie tuangalie kama yanahitajika basi yaendeleo kuwepo, la sivyo, tuyavunje na tuyaweke katika mfumo ambao utaleta tija na zile sheria ambazo zilikuwa zimeunda mashirika yale zinaweza zikapitiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka kuipongeza Serikali hasa kwa kupitia Msajili wa Hazina kwa kuongeza mapato hasa ile asilimia 15 ya ule mfumo wa kuratibu mapato yanayotokana na mawasiliano, lakini vilevile zile hisa zetu kwa TCC na TBL. Napenda kuwahamasisha kuwa wapamue wigo wa

taasisi ambazo Serikali itawekeza tupate mapato zaidi. Mwenyekiti wa Kamati yangu alipokuwa akiwasilisha hapa amezungumzia kupanua wigo wa uwekezaji au hisa katika mashirika ya gesi, madini hata hayo hayo makampuni ya mawasiliano tungepaswa kuwa na hisa humo ndani. Mwelekeo uwe kuwa tunapoendelea sasa kila mwekezaji anayekuja hapa nchini Serikali au wananchi wa Tanzania wawe na hisa ndani ya kampuni hizo. Hii ndiyo njia pekee itakayoweza kuwafanya Watanzania wengi zaidi kushiriki katika uchumi wao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala zima la Sheria ya Manunuzi. Hatujafika kwenye vifungu lakini naomba niseme kabisa na naomba na Wabunge wenzangu mniunge mkono tushike shilingi ya Waziri leo mpaka atakapotuambia lini Sheria ya Manunuzi italetwa hapa Bungeni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumeongeza fedha nyingi sana za mfuko wa maendeleo kwa hiyo fedha nyingi sana ya miradi itakwenda Majimboni, Wilayani na Mikoani, itasimamiwa vipi kama Sheria mbovu kama hii ya Manunuzi bado ipo? Sielewi kwa nini miaka kumi inapita sasa sheria hii inalalamikiwa kila Bunge lakini hakuna kinachofanyika. Sijui ni kwa sababu kuna watu wana maslahi nayo au ina ugumu gani wa kuileta Bungeni. Naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tushinikize sheria hiyo ije hata kama ni kwa udharura. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile nizungumzie suala la zile mashine za kielektroniki za kuratibu mapato pamoja na kodi. Hili jambo limetuletea mizozo mingi sana hapa Bungeni na hata kwa wananchi lakini najua tumefika mahali pazuri Serikali imekubali sasa kununua zile mashine na kuzigawa kwa wale ambao wanastahiki kuzipata. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa hili jambo tusilifanyie siasa tena kwa sababu kwanza lina faida hata kwa wafanyabiashara wenyewe, lakini vilevile linatusaidia kupata mapato mengi zaidi kwa ajili ya uchumi wetu na kwa maendeleo ya nchi yetu. Naomba sasa Serikali ituambie ni lini mashine hizo zitapatikana zote kwa pamoja ili wafanyabiashara wanaohusika wazipate tuanze kupata hayo mapato. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kutakuwa na ukusanyaji mkubwa wa mapato, wigo wa ukusanyaji kodi uongezwe kwa maana ya kwenda kwenye sekta isiyokuwa rasmi. Kwa kuwa tutaanza kuwa tunapata mapato mengi kwa kupitia mashine hizi basi vilevile uangaliwe uwezekano wa kupunguza viwango vya kodi ili watu wengi zaidi wavutiwe kulipa kodi. Maana kodi inaeleweka kuwa ni mchango wa maendeleo siyo adhabu na kama siyo adhabu basi iwekwe katika kiwango ambacho wananchi wengi zaidi watahamasika kulipa kodi wakijua kabisa wanachangia maendeleo ya nchi yao. (Makofi)



Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia suala la Deni la Taifa na mimi nataka kujikita sana sana kwenye suala la *Eurobonds*. Nchi nyingi za kiafrika kwa kupitia Wizara zao za Fedha wameingia katika kununua madeni au kupata madeni kwa kupitia *Eurobond*. Wame-*float Eurobond* na wengi sasa hivi wako matatani. Ghana sasa hivi inatafuta kukwamuliwa na *IMF* kwa sababu wamefika mahali ambapo sasa uchumi umegoma hali kadhalika Mozambique, Namibia, Nigeria na Uganda. Sisi pia najua tumenunua *Eurobond*, je, tutegemee nini huko tunakokwenda maana nyingi karibu zinaanza kuiva na tayari chumi hizo ziko matatani. Najua kwa wakati ule mwaka 2008 kulikuwa kuna haja yakufanya hivyo kwa sababu ya uchumi ulikuwa umetetereka lakini na sisi tunavyojiingiza huko ni mkumbo au sisi tumejipanga vizuri zaidi kuwa hatutakuja kuathirika na hii *Eurobond* huko tunakokwenda? Ningependa kupata maelezo ya Mheshimiwa Waziri atuambie tunategemea kulipa nini, kwa vipindi vipi na itatuathiri au itatuletea faida kiasi gani? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ili kupunguza deni la Taifa kwa nini tusijiingize kwenye uwekezaji wa kutumia *PPP*? Mpaka sasa hivi tunazungumzia sheria, sheria imeshapatikana, tayari kuna wawekezaji wengi wanaotaka kuingia kuwekeza nchi kwetu katika mtindo huo lakini Serikali bado inaonekana kama ina mashaka ndiyo kwanza tunafikiria kukopa sisi wenyewe, hii itazidisha deni na tutashindwa kuhimili. Kwa nini sasa Serikali isiamue kujiingiza katika uwekezaji mkubwa kwa kupitia *PPP*? Nchi nyingi na wawekezaji wengi wana *interest*, wanatufuata hata sisi kuja kutuambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwa nini Serikali haifanyi biashara na taasisi zake yenyewe? Tunalalamikia *TTCL* lakini Serikali haiwapi biashara. Maofisi mangapi wana *land line* za kutosheleza ukilinganisha na simu za mkononi ambapo maafisa wao wote wanazo mikononi, mbili mbili au tatu tatu. Uchumi wetu utakuaje kama hatufanyi biashara na taasisi zetu wenyewe? Tunazungumzia mabenki, ni kiasi gani fedha ya Serikali iko kwenye mabenki ambayo sio ya Taifa ukilinganisha na yale ya kizalendo? Sisi wenyewe tunaanzisha taasisi halafu tunazikimbia, tunazikimbia zitafanya biashara na nani? Lazima tufanye biashara na taasisi zetu wenyewe. Nataka Serikali iweke mkakati na ije na agizo kabisa kuwa taasisi zake zote zitafanya kazi na Serikali, Serikali itakuwa mdau wa kwanza kwa taasisi za Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Almas Maige atafuatiwa na Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Ritta Kabati ajiandae ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa fursa ya kuchangia Wizara yetu hii ya Fedha. Kabla ya kuchangia mimi



niseme maneno machache sana, jambo usilolijua ni kama usiku wa giza. Watu ambao wanakukimbia wewe, wanatoka nje wanakuacha wewe hawakujui. Wewe unajua mimi nakujua sana kabla hujawa Naibu Spika, utendaji wako ulikotoka, chuoni, maisha yako yote, mwadilifu, mpole, msikivu, mtoto wa maskini, umesoma shule za kawaida, unajua mila za Kitanzania, wewe ni mzalendo, hawakuwa na sababu ya kutoka, wametoka hawa ni kama usiku wa giza. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, uwe na moyo, wale wote wanaokufahamu kule nje, wanayokwenda kuyasema watawazomea. Sisi tuliobaki humu ndani tunakufahamu fanya kazi, tuamini, tuko nyuma yako. Mimi nakupongeza sana, nampongeza pia Mheshimiwa Rais aliyekuteua kuwa Mbunge na baadaye ukagombea nafasi ya Naibu Spika. Nafasi ya Naibu Spika hajakupa Mheshimiwa Rais tumekupa sisi Wabunge kwa kukupigia kura. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kila jambo lina mwanzo wake, mwanzo wa wewe kuwa Naibu Spika ni sisi Wabunge humu ndani, walielewe hilo. Tunataka ufanye kazi na tunakuunga mkono sisi. Wote tuliobakia na walioko nje, raia, wananchi wa Tanzania wanakupenda, wanakuamini, fanya kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo sasa nichangie hoja iliyopo mezani na nitajikita katika mambo matatu.

La kwanza ningependa kuongelea ushiriki wa sekta binafsi hapa nchini na naomba ni-*declare interest* kwamba mimi ni mdau wa sekta binafsi. Serikali hii inaongelea kwamba uchumi huu injini yake ni sekta binafsi lakini Serikali hii haioneshi utatu ule unaotakiwa kwamba Serikali isaidie kuikuza kwanza na kuimarisha sekta binafsi ili yenyewe iwe injini kweli ya uchumi. Yapo mambo mengi, Serikali hii inaitoza kodi nyingi sana sekta binafsi, lakini ziko tozo ambazo hazina lazima kabisa. *SDL* tumeilalamikia kwa muda wa miaka mitano sasa kwamba ni kubwa kuliko kokote duniani. Asilimia 5 ya tozo ya *SDL* haina tija kwa waajiri ambao ndiyo waanzishaji wa ajira ambazo zitakuza uchumi. *SDL* wanasema inaenda kwenye *VETA*, kuna makampuni mengi hayana *interest* kabisa na *VETA*, hayatumii mafunzo ya *VETA*. Sekta ya ulinzi binafsi kwa mfano, hakuna kwata kule kwenye kozi ya *VETA*, u-nurse wanalipa hakuna kwata kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile yapo mambo mengine ambayo tunaona kwamba yanatubana sisi sekta binafsi. Ukitaka kuanzisha shughuli hapa Tanzania, utaenda nenda rudi, yanayosemwa kwamba *BRELA* wamepunguza ukiritimba si kweli. Wewe leo andika kwamba unataka kujua *status* ya kampuni yako, miezi sita na ukawaone watu mikononi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niongelee Sheria ya Kazi. Najua sana watu wengi tukiongelea Sheria ya Kazi wanaona kama ni jambo la Wizara

ya Sheria lakini ndani ya Sheria ya Kazi yako mambo ambayo yanaleta chokochoko ya watu kudharau kuajiriwa. Watu wanafanya mpango wa kutokwenda kazini na huwezi kuwafukuza kazi kwa sababu sheria inakubana na ukimfukuza utaanza mambo mengi na Serikali. Tumeomba sisi waajiri tuweze kuruhusiwa kubadilisha sheria ile lakini lazima tupite kwenye ukiritimba wa Wizara ya Kazi na kule kuna Baraza la *LESCO* halikutani, kwa hiyo sekta binafsi inadumaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala la kutokusikilizwa. Serikali inaamua mambo yake bila kufikiria utatu uliopo na ushoroba uliopo. Juzi hapa tumeshuhudia ndani ya Bunge lako sekta binafsi ya elimu imejieleza mpaka watu karibu walie humu ndani, Serikali imekaa na kujaribu kupanga ada elekezi bila kuwahusisha wahusika. Tunashukuru sana Serikali hii sikivu suala hilo limesitishwa na nafikiri watakapoanza kulifikiria tena wadau wote wa sekta ya elimu watakutana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka niliongelee ni Sheria ya sasa ya Manunuzi. Hapa pia naomba ni-*declare interest* kwa sababu ni Mkandarasi Daraja la Kwanza. Sheria hii ya Manunuzi imeanzisha vitengo vinaitwa *PMU* katika kila mnunuzi wa umma. Mashirika haya baada ya kuanzishwa vitengo hivi yamekuwa na mpango wa kutengeneza bei wao wenyewe. Kwa hiyo, badala ya kufanya kazi vizuri na sheria hii imekuwa chanzo cha rushwa katika makampuni ya umma yanayonunua manunuzi ya umma, lakini vilevile yametajirisha watu binafsi badala ya Serikali kupata manufaa ambayo yalikusudiwa na sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii imekuwa chanzo cha watu fulani kuingiza makandarasi kutoka nje kwa sababu wanataka kuhongwa dola. Pia wanataka safari za nje makampuni haya yakipewa *tender* wanataka kwenda kuangalia, wanasema wanafanya *due diligence* na huko ndiko wanapewa hela chungu mzima na imekuwa ndiyo kanuni. Kwa bahati mbaya sana nina mfano mzuri sana wa Shirika la Umma kubwa kabisa na naomba nilitaje kwa sababu nina ushahidi nalo. Benki Kuu ya Tanzania ndiyo shirika kubwa sana la umma linalovunja Sheria ya Manunuzi hapa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki hii au taasisi hii ya umma Mkurugenzi wake amefungwa jela miaka mitatu kuthibitisha kwamba kuna uvunjifu mkubwa wa Sheria ya Manunuzi ya Umma. Pia hapa mkononi nina hukumu ya *PPRA* ambako Benki Kuu wameshindwa kesi miaka kumi iliyopita na bado wanataka kumpa yule yule aliyefutiwa *tender* na *PPRA* na wamefanya hivyo na wamempa. Mbaya zaidi wako wafanyakazi wa Benki Kuu wamefungua kampuni zao wenyewe na wanachukua zabuni za mwajiri wao Benki Kuu. Nataka Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa aniambie wafanyakazi hawa

ambao wamefungua makampuni wanachukua zabuni za Benki Kuu na wao ni waajiriwa wa Benki Kuu amechukua hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo haya kwa watu wasiojua yanaonekana kama ni mzaha mzaha, hela nyingi sana Benki Kuu zinatoka nje ya nchi kwa sababu makandarasi walioletwa pale wanatoka nje ya nchi na ingawa sheria inasema kama hela ya Tanzania zinatumiwa zote 100%, ifanyike *local bidding*. Benki Kuu wameweza kutengeneza njama ya kumtafuta mtaalam kutoka nje aka-specify mitambo inayofanya kazi pale kwamba lazima itoke kwenye kampuni moja fulani. Kampuni hii ndiyo ilishtakiwa miaka kumi iliyopita na kufungiwa na *tender* ikarudiwa lakini sasa huyo ndiye msemaji mkuu wa zabuni tena za usalama wa Benki Kuu. Mimi naomba atakapokuja Mheshimiwa Waziri alieleze suala hili la Benki Kuu na zabuni kupewa wafanyakazi wa Benki Kuu pamoja na watu waliochongwa kwa ajili ya kufanya kazi za siri za Benki Kuu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu nichangie na naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Ritta Kabati ajiandae atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie machache kuhusu Wizara hii. Kwanza, niungane na Wabunge wenzangu, nakupongeza sana wewe binafsi na endelea na msimamo huo. Mimi nimo Bungeni humu sasa ni kipindi cha tano, Bunge ni mhimili, lazima uheshimike, Bunge si mkutano wa hadhara, siyo lazima kila hoja inakotoka kule, kwa mfano kuna tukio limetokea Mpwapwa sasa tuahirishe Bunge tujadili mambo ya Mpwapwa, sijawahi kuona kitu kama hicho mimi. Kwa hiyo, mimi nakuomba endelea asubuhi unakuja, jioni unakuja waendeleo kutoka tu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Waziri wa Fedha, Naibu Waziri wa Fedha, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nianze na TRA. Niwapongeze TRA wanafanya kazi nzuri sana ya kukusanya mapato lakini jiulize, kazi ya sisi Wabunge hapa ni kupitisha bajeti ya Serikali na tukishapitisha bajeti fedha zinagawanywa Wizara, Mikoa na Wilaya na mradi ukishapangiwa bajeti, kama ni barabara basi fedha yote ipelekwe. Nashangaa kwamba fedha zinapangwa, Bunge linapitisha bajeti lakini utakuta mwisho wa mwaka wa fedha karibu nusu ya fedha hazijaenda kwenye miradi.

Kwa hiyo, hii inatusababishia kuwa na viporo na vingi miradi mingi haikamiliki. Mheshimiwa Waziri hebu anieleze anayezuia/anayekata hizi fedha kule Hazina ni nani? Kwa sababu wenye madaraka ya kupitisha bajeti ni Wabunge, hakuna mtu mwingine ambaye anaweza kupunguza hizi fedha kwa ajili ya kazi nyingine. Kwa hiyo, naomba sana tukishapitisha bajeti basi Wilaya, Mikoa ipelekewe fedha zile ambazo Bunge limepitisha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nizungumzie kidogo Mfuko wa Mahakama, hili Fungu 40. Mahakama wanafanya kazi katika mazingira magumu sana hasa Mahakama za chini, tuna upungufu mkubwa sana wa mahakimu na wa mahakama. Kwa mfano, Wilaya ya Mpwapwa ina Mahakama za Mwanzo tatu tu na Kata ziko 33, kwa hiyo, wananchi wanasafiri mwendo wa kilometa zaidi ya 60-70 kufuata mahakama. Pamoja na ufinyu wa bajeti, naomba Serikali itenge fungu la kutosha kwa ajili ya kujenga Mahakama za Mwanzo na kuendelea kufundisha Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Tuna chuo chetu kile cha Lushoto, hebu tuongeze idadi ya wanafunzi. Nimekitebelea kile chuo mwaka juzi, mazingira yake hayaridhishi, tuongeze majengo ili wanafunzi wawe wengi tuweze kupata Mahakimu wengi wa Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niongelee jengo langu la Mahakama ya Mpwapwa. Nashukuru sana lile jengo la Mahakama ya Wilaya ya Mpwapwa ni jipya lakini halijakamilika bado. Hosteli ya Majaji hakuna, mgahawa hakuna, kama ilivyo kwenye majengo mengine mfano Kongwa. Kwa hiyo, naomba lile jengo likamilishwe ili Jaji akija asilale kwenye hoteli za kawaida, hapana, siyo vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu la 42, Mfuko wa Bunge, hapa nimeona fedha za miradi zilizotengwa ni shilingi bilioni saba na Wabunge wengi hawana Ofisi. Sasa labda nipate maelezo Mheshimiwa Waziri, hizi fedha ni pamoja na kujenga Ofisi za Wabunge au kwa shughuli zingine? Kwa sababu Wabunge wanalalamika hawana ofisi na zimetengwa fedha kidogo sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Sheria za Manunuzi, sheria hii inatumiza sana. Mimi nimewahi kuwa Mjumbe wa Bodi za aina mbalimbali, kwa mfano ukichukua shule ya sekondari ya bweni, dukani sukari unanunua shilingi 2000 au shilingi 2500 lakini mzabuni ananunua shilingi 3000 au shilingi 4000. Kwa hiyo, kwa kweli sheria hii inatumiza sana. Hivi kuna tatizo gani kuleta huu Muswada hapa Bungeni turekebishe hii sheria? Maana kila mwaka Serikali inasema italeti, italeti kwa nini msilete, watu wanaumia, fedha nyingi za Serikali zinaishia hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi yangu yalikuwa ni hayo machache lakini nisisitize sana ujenzi wa Mahakama hususani Mahakama za Mwanzo na

kuongeza mafunzo ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ili waweze kusambazwa kwenye Mahakama za Mwanzo. Nakushukuru na naunga mkono hoja hii lakini narudia tena uendeleo na msimamo wako huo huo, asubuhi na mchana uwepo waendeleo kutoka. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ritta Kabati atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud na Mheshimiwa Neema Mgaya ajiandae.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja hii ya Wizara Fedha. Vilevile na mimi nimuunge mkono mjumbe aliyepita kwamba Mheshimiwa Naibu Spika uzi ni huo huo, sheria ni msumeno. Lazima Bunge letu lifuate sheria na kanuni ambazo tumejitungia sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze sasa na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Waziri wake na watendaji wote wa Wizara kwa kutuletea hii bajeti ili tuweze kujadili. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais ambaye kwa kweli utumbuaji wake majipu umesaidia sana kuongeza kipato TRA na kwa kweli hakuna mtu ambaye hajui kwamba tumbuatumbua majipu imeweza kutuongezea kipato kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu naanza na kitabu cha Waziri ukurasa wa 59 kuhusu Shirika la Bima la Taifa (NIC). Kwa kweli nina masikitiko makubwa sana na inaniuma sana. Hili Shirika la Bima lilikuwa shirika ambalo lilisaidia sana nchi hii, wafanyakazi wengi waliweza kuajiriwa, lilikuwa na majengo mengi na mali nyingi sana ambazo leo hii lingeweza pia kuongeza pato kubwa sana katika nchi hii. Hata hivyo, bado Serikali haijawa na mpango haswa wa kuhakikisha kwamba hili shirika linafufuka ili liweze kuwa chanzo kikubwa sana cha mapato katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika bajeti iliyopita ya mwaka 2015/2016, aliyekuwa Waziri wa Fedha alipokuwa anasoma bajeti yake alituambia kwamba Serikali ina mpango wa kuongezea uwezo Shirika la Bima la Taifa kwa Serikali kukatia bima mali zake zote ikiwa ni pamoja na za taasisi na TAMISEMI kupitia shirika hili. Mbona sasa hakuna mpango wowote wa kuhakikisha kwamba haya mashirika yanakatiwa bima katika Shirika hili la Bima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kuamini mpaka sasa hivi hili shirika halina hata bodi ya wafanyakazi, shirika hili Mkurugenzi wake Mkuu na Wakurugenzi wengi sana wanakaimu tu, sasa kweli hili shirika litajiendeshaje kama bado halijajiwekewa mkakati kama huo? Tuna taasisi karibu 200 katika nchi yetu lakini katika kitabu hiki amesema taasisi 15 tu ndiyo ambazo zinatumiwa hili Shirika letu la Bima ya Taifa. Niipongeze sana Wizara ya Nishati kwamba imeweza kukata

bima katika bomba lake la gesi linalotoka Mtwara mpaka Kinyerezi. Najua ni mapato makubwa sana yanapatikana kwa kukatia bima kwenye Shirika letu la Bima la Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua siku zote huwa tunawasifia Wachina wanaongeza pato na sisi tulienda kweli tukaona Wachina jinsi walivyokuwa wazalendo. Kama nchi hii haitakuwa na uzalendo mashirika yetu mengi sana yatakufa. Kwa sababu ipo TTCL, Posta bado hatutumii mashirika yetu vizuri, tunaona mashirika na taasisi za Serikali zinaenda kukata bima sehemu nyingine. Unaona tu Wachina wamekuja hapa wamewekeza lakini wameleta pia mashirika yao ya bima, wameleta pia walinzi wao, wameleta kila kitu mpaka wafagiaji. Lazima iwepo sheria kwamba haya mashirika yetu ya bima yatumike pia ili kuongeza Pato la Taifa letu. Nitamuomba Waziri atakapokuwa anajibu angalau atupe mkakati kwamba ana mkakati gani wa kuyafufua haya mashirika na ni kwa nini mpaka leo hii hakuna hata bodi ya wafanyakazi kwenye hili shirika na Wakurugenzi bado wanaendelea kukaimu siku zote. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi pia niendeleo kuunga mkono kuhusiana na ile Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2011. Wabunge wengi sana siyo leo tu, siku zote tumekuwa tukiisema hii sharia, kwa nini haitetwi, kuna kitu gani kimejificha hapa nyuma? Kwa sababu hii sheria ingeletwa leo hii tusingekuwa tunalalamika, hii sheria ndiyo mkombozi. Naomba Mheshimiwa Waziri atujibu, tulipewa matumaini kwamba katika Bunge hili hii sheria ingekuwa tungeweza kuibadilisha, mbona hakuna chochote, kuna tatizo gani katika uletaji wa hii sheria hapa Bungeni?

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia kuhusu VICOBA, hakuna siri VICOBA ni mkombozi wa sisi wananchi hasa wanawake. VICOBA hii imetufichia mambo mengi sana, wanawake walikuwa wanadhalilika sana kwenye taasisi nyingine za fedha kwa kuchukuliwa mali zao lakini VICOBA imekuwa kama ndiyo mkombozi. Tuliambiwa kwamba VICOBA inaendeshwa bila kusimamiwa na sheria yoyote ya fedha na tuliambiwa sheria ingeletwa hapa ili tuweze kuipitisha lakini hakuna sheria iliyoletwa mpaka leo. Sasa wanatuambia nini kuhusiana na VICOBA kuendeshwa bila sheria yoyote ya fedha? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia kuhusu malipo ya wazabuni. Wazabuni wetu wanapata shida sana, ningepomba kujua ni lini Serikali italipa malipo wazabuni wanaozidai kwa muda mrefu sana Halmashauri na Wizara zetu. Wamekuwa wakizungushwa mno, wanaambiwa kwamba malipo yao yapo Hazina lakini wakienda Hazina bado hawalipwi, lakini hao wazabuni bado pia wanadaiwa kodi za Serikali. Sasa tutakusanyaje kodi kama hatuwalipi hawa wazabuni, watafanyaje biashara? Hawa wazabuni wamekuwa wakichukua mikopo kwenye benki, wanadaiwa riba, halafu TRA bado wanawatoza tena



kwa nini wamechelewesha kulipa kodi zao. Serikali hii imesema kwamba itawasaidia wafanyabiashara wadogo wadogo na wa kati, huko ndiyo kuwasaidia wazabuni? Kwa sababu wazabuni walio wengi ndiyo ambao wanatoa zabuni kwenye Halmashauri zetu na kwenye Wizara zetu. Ningeomba kwa kweli uwepo mkakati wa kushughulikia suala hili kwa sababu ni muda mrefu sana wazabuni wamekuwa wakipata matatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendeleo pia kuzungumzia kuhusu ucheleweshaji wa pesa za miradi katika Halmashauri na Wizara zetu. Huu ucheleweshaji siyo wa mara moja, siku zote pesa za maendeleo ya miradi zimekuwa zikicheleweshwa sana na ucheleweshaji huu wa miradi umekuwa ukisababisha miradi ile sasa inafanyika kwa gharama kubwa sana. Kwa mfano, katika Mkoa wetu wa Iringa kuna ule mradi wa machinjio wa kisasa, ulitakiwa tuujenge kwa pesa kidogo sana, lakini kadri fedha ambavyo zinacheleweshwa kuletwa ule mradi pia gharama zake zinaongezeka. Pia ule mradi kama tungekuwa tumeumaliza kwa wakati ungeweza kusaidia chanzo kikubwa cha mapato kwa sababu tunategemea kwamba tutapata mapato hata ya dola kwa sababu tutasafirisha zile ngozi nje ya nchi.

Vilevile tulikuwa tunategemea kuajiri wafanyakazi wengi sana katika Halmashauri yetu kupitia mradi ule. Sasa utaratibu gani huwa unatumika, ni kwa nini hizi pesa za miradi zinacheleweshwa sana? Karibu sehemu zote watu wanalalamika ucheleweshaji wa pesa katika miradi ya Halmashauri zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wengi sana wamezungumzia kuhusu riba kubwa inayotozwa na baadhi ya taasisi za fedha. Taasisi nyingi sana zimekuwa zikitoza riba kubwa sana na wananchi wengi sana wanashindwa kufanya biashara.

Wananchi wengi sana sasa hivi wakichukua mikopo benki mali zao zinauzwa, imesababisha wananchi wengi sana kupoteza maisha au kupata hata *pressure* kwa sababu mikopo halipiki dhamana zinachukuliwa. Ukichukua sasa hivi mikopo benki ujue kwamba wewe umeajiriwa na benki hupati chochote zaidi tu utafanya ile kazi, kama umechukua kwa ajili labda ya uzabuni basi utafanya kazi ya uzabuni, zabuni yenyewe wanakusumbua.

Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie upya hizi riba ambazo mabenki yetu yamekuwa yakitoza, ikae na ione ni kiasi gani ambacho kinaweza kikasaidia. Kwa sababu biashara ni ngumu sana, watu wanatozwa katika majengo, kuna tozo nyingi mno ambazo ukienda kuchukua mikopo unaona riba imekuwa kubwa sana. (Makofi)



Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nizungumzie kuhusu hizi mashine za EFDs. Wengi wamezungumzia suala hili, tulitegemea kwamba hizi mashine zingekuwa mkombozi, tungekusanya kodi nyingi sana. Tatizo utaona labda mtu mmoja au wawili ndiyo wana zile mashine wengine hawatumii, kwa hiyo, wengine wanalipa kodi wengine hawalipi, naomba hili suala liangaliwe. Pia Serikali ilisema ingetoa hizi mashine bure sijui zoezi hili limefikia wapi, ningependa kujua. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud atafuatiwa na Mheshimiwa Andrew John Chenge na Mheshimiwa Prosper Mbena ajiandae.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Na mimi napenda nikuunge mkono kwa kazi yako unayoifanya ya kusimamia sheria na kanuni zetu za Bunge. Endelea kusimamia sheria na kanuni za Bunge ili kulinda heshima ya Bunge letu. *(Makofi)*

Napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara ya Fedha, Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote wa Wizara hii kwa juhudi zao za kuhakikisha nchi yetu inapiga hatua za maendeleo. Naomba niwatie moyo, endeleeni na kazi, sisi tuko nyuma yenu kuwasaidia pale ambapo panahitajika kutoa msaada wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kutoa mchango wangu kwenye Tume ya Pamoja ya Fedha. Napenda tu kutoa msisitizo kwamba Tume hii ifanye kazi zake na kama kuna upungufu urekebishwe na kama kuna upungufu wa watendaji basi nafasi hizo zijazwe ili Tume hii ifanye kazi yake vizuri na kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kuhusu mashirika ya Serikali kama NIC na TTCL. Haya ni mashirika yetu ya Serikali lakini hali yake siyo nzuri kiutendaji na katika ukusanyaji wake wa mapato au kupata mapato. Ni vyema sasa taasisi za Serikali ikayatumia mashirika yetu ya Serikali ili kuongeza mtaji na fedha zaidi katika mashirika hayo. Mfano TTCL, taasisi zote za Serikali zikitumia mitandao hii ya TTCL nafikiri tutaweza kuwaongezea mtaji wa kuendesha shughuli zao na litaanza kunyanyuka pamoja na mashirika mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taasisi ambazo zinafanana katika shughuli zake za utendaji mfano TRL na RAHCO, TBS na Weights and Measures Agency. Hebu Serikali sasa iangalie taasisi za namna kama hiyo ambazo kazi zake

zinafanana au zinakaribiana iziunganishe ili zifanye kazi kwa pamoja na kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kuhusu ukusanyaji wa mapato katika bandari bubu. Ni kweli kabisa fedha nyingi zinapotea katika bandari bubu. Kwanza ni kuziorodhesha bandari zote bubu za Tanzania na baadaye kujua ni mbinu gani ambazo wanatumia katika kupitisha bidhaa. Kwa kufanya hivyo tutaweza kudhibiti upotevu wa mapato na bidhaa za magendo. Kwa kupitia bandari bubu si ukwepaji tu wa kodi uliopo huko bali pia zinatumia kupitisha bidhaa ambazo haziruhusiwi mfano nyara za Serikali zinapitishwa na zinakwenda katika maeneo mengine na zinasafirishwa. Mfano, zinaweza zikapitishwa bandari bubu za Tanga na Zanzibar na kusafirishwa huko zinakokwenda kama China na kwingineko. Kwa hivyo, ulinzi na ukaguzi madhubuti ufanyike katika bandari bubu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi natilia mkazo Sheria ya Manunuzi kama wenzangu walivyoiongelea, iletwe hapa ili ifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitilie mkazo kuongezewa mtaji Benki ya Kilimo kwa sababu benki hii kutokana na mpango kazi wake imejipanga kwenda katika mikoa yote ya Tanzania. Tatizo lao ni mtaji wa kufika na kufungua ofisi katika mikoa yote ya Tanzania. Kama itaongezewa mtaji itaweza kuwafikia wananchi wote huku waliko ili kuwasaidia wananchi katika miradi midogo midogo ya kilimo, uvuvi, ufugaji na mingineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine tutilie nguvu ukwepaji wa kodi, najua hili mnalifanyia kazi. Nataka kuuliza, kulikuwa na uwakala wa ukusanyaji wa VAT kati ya Tanzania Bara na Visiwani kila mmoja ni wakala wa mwenzake. Sasa sijui mpango huu mpaka sasa unaendelea au umesimama? Pia naomba tudhibiti mfumko wa bei, kila kukicha mfumko wa bei unakuwa mkubwa na unakuwa mzigo mkubwa kwa wananchi katika kununua bidhaa za kujikimu kimaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni hii Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Mifuko hii ni vema ikaangalia masharti ya wanachama wake ili kupunguza baadhi ya masharti ili isiwe mzigo kwa wanachama wa mifuko hii. Mfano umri wa kulipwa pensheni wakati wa kustaafu inamlazimisha mwanachama lazima afikishe miaka ile waliyoitaka wao na pengine kungekuwa na nafasi ya kustaafu mapema akalipwa haki zake angeweza kustaafu na nafasi zile zikajazwa na vijana wengine ambao wanataka kuajiriwa. Kwa kipengele hicho kinafanya mtu abakie tu kusubiri kulipwa pensheni kwa sababu kama hukufikisha umri huo huwezi kulipwa pensheni yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisisitize kuhusu ukusanyaji wa mapato kwa jumla. Naomba wafanyabiashara wahamasishwe zaidi kutumia hizi

mashine za kieletroniki na mashine hizi zisiwe kwa baadhi tu ya watu, ziwe kwa wafanyabiashara wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja, nawatakia kheri katika ufanisi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Andrew John Chenge atafuatiwa na Mheshimiwa Prosper Mbeni, Mheshimiwa Jitu Soni ajiandae, tutamalizia na Mheshimiwa Dkt. Mary Ngu.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge katika kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Nianze kwa kusema naiunga mkono hoja hii asilimia mia moja lakini mniwie radhi kwa sauti yangu kidogo leo haijakaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili na mimi niseme, haya yanayoendelea pamoja na kwamba ni michezo ya kisiasa lakini isitukwaze. Sisi kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Bunge, akidi ya maamuzi tunayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kama kuna kitu Mbunge amekereka kanuni zina utaratibu. Mimi nawasihi wenzangu hawa tutumie Kanuni zetu, huo ndiyo utaratibu wa Kibunge na siyo kwenda kufanya vikao kantini na maeneo mengine. Mimi siko nyuma yako, bali niko bega kwa bega na wewe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Deni la Taifa, nimesikiasikia hata kwenye hotuba ya wenzetu wanalisemea hili, ndiyo linakua lakini Tanzania ya leo siyo ile ya mwaka 1960, 1970, 1980. Taifa hili linakua na mahitaji yake yanazidi kuwa makubwa na lazima Serikali kupitia bajeti yake iweze kuwahudumia wananchi katika sura hii. Hoja siyo deni la nchi hii kukua, hoja ni kwamba tunapochukua mikopo hii iwe ni mikopo wa muda wa kati au muda mrefu tunazielekeza wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tukizielekeza kwenye *consumption* ndiyo inakuwa tatizo, lakini tukizielekeza katika maeneo ya uzalishaji yanayotujengea uwezo ya uchumi wetu kukua kwa haraka deni letu litaendelea kuwa himilivu. Tulielewe hilo lakini kusema kwamba tunagawanya deni hilo kwa *population* haiendi hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa mkakati wetu wa kusimamia Deni la Taifa na Sheria yetu ya Mikopo, Dhamana na Misaada labda Waziri angeweza kutusaidia tu tukajua huwa tunafanya tathmini ya Deni la Taifa

baada ya muda gani maana ni vizuri tukajua deni la kipindi cha muda wa kati au muda mrefu. Pia vile viashiria ambavyo vinatumika, maana ukichukua kwa mfano thamani ya sasa ya deni la Taifa uwiano wake na Pato la Taifa ni asilimia ngapi. Maana nadhani haya ndiyo yanapaswa sisi kama Wabunge Serikali iwe wazi ili kupunguza haya maneno. Unapolinganisha ukomo, ule ukomo ukisema ni asilimia 50 msingi wake ni nini au unaposema deni letu la Taifa kwa sasa thamani ni hii lakini ukilipima kwa mauzo yetu ya nje ya bidhaa zetu na huduma ni asilimia ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndiyo masuala ya msingi. Nadhani Waziri wa Fedha anapokuja kuhitimisha atusaidie katika kuyasema haya ili nchi na Wabunge tuweze kulipata hili suala vizuri. Naamini deni hili linahimilika na tutaendelea kuwa nalo na tutaendelea kukopa lakini tukope kwa misingi ambayo inajenga Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili amelisema kwa sura tofauti Mheshimiwa Janet Mbene, nataka niulize tu tumekuwa na hili zoezi la nchi yetu kufanyiwa tathmini ili iweze kukopesheka nje, ile *sovereign rating* imesemwa sana humu. Mara ya mwisho nakumbuka katika bajeti ya Serikali ya mwaka 2013/2014 Serikali ilisema wako *advanced* sana lakini sasa hivi hatusikii tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna faida zake kwenda *route* hiyo kwa sababu ndiyo unapata *access* kwa mikopo *from* masoko ya kimataifa ya masharti nafuu lakini pia na makampuni ya Kitanzania yanaweza pia na yenyewe kupata mitaji kutoka kwenye masoko ya Kimataifa. Sasa tungependa tueleze ni nini kimetukwamisha tena tunarudi nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ni hili la *Public Private Partnership*. Kusema kweli visingizio vimekuwa vingi. Naiomba Serikali ile miradi 125, maana mwanzoni tuliambiwa sheria haijakaa vizuri, ni kweli maana mtu anakuja hapa na pesa zake umuambie afuate Sheria ya Manunuzi kulikuwa na mgongano, tukasema tuunyooshe na Bunge likafanya kazi yake. Wakasema kuna *centers* nyingi sana za maamuzi na kadhalika tukanyoosha sheria. Wakasema sasa imeleta miradi 125 inafanyiwa uchambuzi ili kuona kama inakidhi kuingia katika mfumo huo mpaka leo hatuoni kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huu unachochea uwekezaji lakini pia unapunguza mzigo wa Serikali kwenye bajeti ili tuelekeze nguvu katika maeneo ya afya na maji lakini barabara, miundombinu ya reli, bandari na kadhalika tunashirikiana na *private sector* kwa misingi tuliyojiwekea na hili mimi nasema linawezekana na linafanyika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne limesemwa ni Benki ya Kilimo, inatia huruma sana kwa ahadi ya Serikali ya muda mrefu kutotekelezeka na mimi

nasema *there is more than one way of skinning a cat*. Benki ya Rasilimali ya Tanzania Serikali ilipoianzisha miaka 1970 na ile iliyokuwa *Tanzania Rural Development Bank* kabla ya kuwa CRDB, Serikali ilichukua *line of credit* kutoka AIDA, *European Investment Bank* na *Nordic Investment Bank* kuweza ku-*capitalize* hizi benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwe wabunifu tukienda na lugha hii, kwanza Benki ya Maendeleo kwa Sheria ya Mabenki na *Financial Institution* unahitaji upate leseni *minimum fifty billion, ten billion* ndiyo fedha za kwenda kukopesha halafu tunasema ikopeshe kwa masharti nafuu maana yake ifanye hasara tangu *day one* haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kweli kwa hili tu-*capitalize the bank* na tuone namna ya kufanya. Hizi hati fungani za mtaji zinawezekana zikatumika kwa sababu ukinitolea ni kama *I owe you money, interest* utakuwa unanilipa ndani ya miezi sita na *principal* mwisho wa mwezi, angalau una-*clean up balance sheet* yangu na wengine wanaoniangalia kama benki niweze kukopesheka, ndiyo tunaiomba Serikali ilione kwa mtazamo huo.

*I owe you money, interest* utakuwa unanilipa ndani ya miezi sita na *principle* mwisho wa mwezi ili kama benki niweze kukopesheka, ndiyo maana tunaiomba Serikali ilione kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho. Hii Mifuko ya Hifadhi kwa *principle* hiyo hiyo, najua Serikali ime-*underwrite* Mifuko hii hasa PSPF; lakini kwa vile tumechukua pesa na tumezitumia kwa maendeleo yetu, nadhani tuwe wakweli tu, tunapowasema tutatoa *a non cash bond* kweli tuitoe. Tukisema tutatoa bilioni 80 mwaka huu kwenye bajeti zionekane kuliko kuzidi kuididimiza Mifuko hii halafu wafanyakazi waliostaafu kama mimi unakuta hawalipwi kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mimi nilikaa kwa kipindi cha miezi saba silipwi pensheni na, ni kweli eeh, lakini ndiyo haya mambo tunayosema, Serikali wasikasirike maana tumezitumia pesa hizi kwa nia njema, lakini tuje sasa na utaratibu utakaotusaidia kuyajibu hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa, Waheshimiwa Wabunge Kanuni za Bunge zinawaruhusu wala tusionekane kuwa ni wanyonge; hii Sheria ya Manunuzi kama Serikali hawataileta sisi wenyewe; hata mimi mmoja wao kwa sababu najua kuandika hizi sheria, tutaleta *amendment* ya sheria humu! Eee! Hilo tusiogope maana fursa hizi zipo tunaweza kuyafanya haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, amelisema vizuri sana Mheshimiwa Ritha, kwenye Sheria ya *Micro-finance*. Mimi nilikuwa *consulted* kufanya kazi hiyo na tulifanya kazi kubwa na akina Dunstan Kitandula. Sasa kwa kuiheshimu

Serikali tukasema kwa sababu wanalifanya tukasema hebu waanze tutakuja ku-takeover baadaye, lakini naona sasa *again* halisemwi tena. Sasa tutayafanya hayo Waheshimiwa Wabunge tukitaka na ndio moja ya kazi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Prosper Mbena atafuatiwa na Mheshimiwa Jitu Soni na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu ajiandae.

**MHE. PROSPER J. MBENA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa maoni yangu au mchango wangu kwenye hotuba hii muhimu ya Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango. Kabla sijatoa maoni yangu na mimi niungane na wenzangu waliokupongeza wewe kwa msimamo sahihi, haki na kutokubali kuyumbishwa. Nadhani ni mmoja kati ya watu ambao tayari nilishakupongeza na uendeleo na msimamo huo. Ngingekuwa nina uwezo wa kukupangia basi ningesema umalize ngwe hii yote mpaka tutakapoondoka, nakushukuru sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie maeneo machache tu katika Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, nikianza na lile la mafanikio ya MKUKUTA II.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amesema vizuri kwamba mafanikio makubwa yameonekana katika MKUKUTA II na moja ya mafanikio hayo ni pale ambapo umaskini umepungua kwa karibu asilimia 6.2. Sasa tukiangalia mmoja mmoja kwenye Majimbo yetu basi ndipo tunapoonza kwamba kipimo kile kumbe sisi wengine bado hatujakifikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwangu mimi vijiji vyangu nikianza na pale nilipozaliwa Lugeni niende maeneo mengine ya Konde, Kisaki *Station*, Nyingwa ni ndoto ukisema kwamba umaskini umepungua; umaskini umeongezeka. Sasa hii maana yake ni kwamba mpango huu haukuwanufaisha wale waliolengwa na inawezekana sana Waheshimiwa Wabunge, Madiwani na watendaji wengine wa karibu na wananchi hawakuhusishwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe kwenye mpango mwingine unaokuja na matayarisho yake yaanze sasa, tuwe na takwimu sahihi ya hao walengwa, tuwe na utaratibu mzuri wa kuwafikia hawa walengwa, Wabunge wahusishwe kikamilifu, sisi ndiyo tunaojua watu wetu wanaohitaji msaada mkubwa, tunaojua umaskini umekaa wapi ili mafanikio haya yanayozungumzwa sehemu nyingine yaweze kufika kwenye maeneo yetu haya ambayo kwa bahati mbaya kwenye MKUKUTA II hatukuweza kunufaika.



Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia suala la hili la Sheria ya Manunuzi. Wenzangu wamesema na mimi niongeze tu sauti. Nashukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Chenge ametuonesha ukubali wake na utayari wake wa kulifanya hili kama Serikali itakuwa bado ina kigugumizi cha kuleta hapa mbele ya Bunge. Sidhani kama Serikali inaona ugumu; ninachojua kwa sababu nimetoka huko Serikalini, muda wote nilipokuwa pale Serikalini kilio ni hicho hicho kwamba sheria hii ni mbaya, itokee nafasi tuibadilishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nashangaa fursa hiyo tunaiacha inapita lakini hata Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alituahidi hapa Bungeni kwamba sheria hii italetwa ili tuweze kuibadilisha; nawaomba sana Serikali, Waziri wa Fedha, ashughulikie hili tulimalize. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu naomba nilizungumzie hili ambalo pia wenzangu wamelizungumza, pesa hii shilingi milioni 50 kwa kila Kijiji. Hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, Mkuu wa nchi, imetangazwa nchi nzima, dunia nzima inajua hakuna *shortcut* yake, ni utekelezaji tu unaotakiwa hapa. Mheshimiwa Waziri utafute hizi pesa tutengeneze utaratibu mzuri ili pasiwepo na ufujaji wa pesa hizi ili kwa kweli wananchi wetu maskini waweze kunufaika na mchango huu mkubwa uliotolewa na Mheshimiwa Rais. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo Wabunge wenzangu wawili wamezungumzia kuhusu mikopo ya benki za biashara. Mikopo hii inayotolewa kwa wananchi na kwa kweli mwananchi anapokwenda kukopa ni kwamba, ana shida, lakini mabenki haya yanatumia shida za hawa wananchi kuwabana. Dhamana wanayoweka ya nyumba, mikopo hii masharti yake ni magumu sana, utekelezaji wa mikopo huu ukijumlisha na riba, mikopo unakuwa ni mara mbili. Wapo wananchi wengi sana wamepoteza nyumba zao za kuishi, wengine wamejiua, wengine wamepata maradhi ya kusunoneka na wengine ndoa zao zimeharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, yote haya yameletwa kwa sababu nadhani Serikali haikuangalia sana. Faida zinazotengenezwa na benki hizi kutokana na mikopo hii, wote sisi ni mashahidi, baada ya mwaka utasikia wametengeneza bilioni 10 wanagawana; lakini wamefanya hivi kwa kumgandamiza huyu mwananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu Wizara ya Fedha ikishirikiana na Benki Kuu iangalie upya mwenendo wa benki hizi na mikopo yao kwa wananchi na hasa kama inawezekana, dhamana hii ya nyumba itolewe katika mpango mzima wa kuwakopesha watu. Kwa sababu kwa kusema ukweli tunawarudisha wananchi wetu kwenye umaskini mkubwa sana kwa ajili ya matatizo haya ya mikopo ya kibenki. (Makofi)



Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ametuelezea kuhusu ukusanyaji wa mapato ya Serikali, na katika hotuba yake ameeleza kwamba wafadhili kwa mwaka 2015/2016 wameweza kupunguza ahadi yao ya mchango kutoka Shilingi bilioni 660 hadi kufikia Shilingi bilioni 399, punguzo hilo ni karibuni asilimia 40. Hili jambo linanisikitisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa ni wafadhili ambao tuliona ni marafiki zetu, tumekaa nao katika meza, tumewaeleza mipango yetu na wao wala si kwa kushurutishwa wamekubali kuchangia hicho walichoahidi. Leo hii kwa sababu yoyote ile wanafika mahali wanajitoa anavuruga kabisa bajeti na mpango mzima wa maendeleo wa nchi yetu, haikubaliki. Serikali inatakiwa iwaeleze, Serikali inatakiwa ifike mahali ijulishe dunia kwamba hawa ni marafiki ambao wametuangusha katika nia yetu ya kufika mahali fulani kwenye maendeleo, haikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *na-declare interest*, nilikuwa Kamishna wa *External Finance* pale Wizara ya Fedha, nimefanya kazi kwa muda mrefu sana. Mahusiano ni muhimu lakini mahusiano hayo yana heshima ya nchi na nchi. Inapofika mahali dharau inaoneshwa namna hii ni juu ya Serikali kuonesha kwamba mwenendo huo hatukuupenda katika mahusiano yetu. Kwa hiyo, nawaomba sana Serikali hebu tusiwe wanyonge hivyo, dalili ninazoziona ni kwamba kuna unyonge unyonge hivi, ndiyo maana tunachezewa hivyo, ndiyo maana barabara nyingine sasa zimeachwa kwa sababu tu wafadhili fulani hawakutoa pesa ambazo waliahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Jitu Soni, tutamalizia na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nichukue nafasi hii kukupongeza kwa namna unavyoendesha Bunge hili na naamini kwamba kuanzia siku ya kwanza ingekuwa wote tunasimamia kanuni na utaratibu ambao tumejiwekea kisheria, haya mambo yote yasingetokea. Kwa hiyo, uendelea na msimamo huo kwa sababu bado huu ndiyo mwanzo. Kwa hiyo tukianza kuzoea kufuata taratibu, kanuni na sheria huko mbele ya safari tutakuwa tunakuja hapa na kulenga hoja mbalimbali katika kuishauri na kuisimamia Serikali, hizi siasa nyingine zote tutazifanya huko nje ya hapa. Kwa hiyo, nakupongeza sana na naomba uendelea na msimamo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Waziri wa Fedha, Naibu wake, Katibu Mkuu ambaye anaongoza na timu nzima ya wataalam kwa juhudi kubwa wanayofanya na wametuletea

Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Wizara yao, ambapo Wizara hii ndio Wizara mama inasimamia Wizara nyingine zote. Mafanikio yao ndiyo mafanikio ya Wizara nyingine zote. Kwa hiyo, nimpongeze Rais kwanza kwa kuwateua, lakini kwa uzoefu wake Waziri na timu yao na namna wanavyokubali ushauri, niwapongeze sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze kwenye masuala mawili muhimu. Moja, wenzangu wengi wamesema, ni Sheria ya Manunuzi. Naomba nisisitize kwa Wabunge wenzangu wote; kama itatokea kwamba sheria hii haijaletwa muda bado tunao wa siku 21 wa kuleta hoja binafsi ya kubadilisha baadhi ya vipengele ili fedha nyingi ambazo tutapeleka kwenye maendeleo, asilimia 40, zikatumike vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama itakuwa tupo nje ya muda basi nitaomba Wabunge wenzangu wote tukubaliane tutakapopitisha Bajeti Kuu ya Serikali tuweke kipengele kwamba pesa za maendeleo hata shilingi isitumike mpaka hapo hiyo sheria itakaporekebisha. Fedha ziwekwe kwenye akaunti maalum, sheria ije, ikipita ndipo fedha zitumike, kwa sababu hiki kimekuwa ni kilio cha miaka mingi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nizungumzie juu ya Sheria ya *Micro-Finance*. Serikali imekuja na mpango mzuri wa kupeleka milioni 50 kwa kila Kijiji. Kule ni masuala ya *Village Empowerment*, ile milioni 50 kama VICOBA haitakuwa kisheria ambapo inategemeana na Sheria hiyo ya *Micro-Finance* bado tutarudi pale pale. Kwa hiyo, ningeomba sheria ya *Micro-Finance* ni muhimu ije mapema ili zile fedha zikienda kule usimamizi wake uwe kisheria na uweze kusimamiwa vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mbali na hiyo pia ningeomba Wizara ya Fedha iishauri Serikali ingalie namna ya kuhakikisha kwamba tunapata sheria. Asilimia kubwa ya taasisi zetu za Serikali ambazo zinafanya huduma mbalimbali; kwa mfano huduma za simu na data za TTCL, lakini pia NIC. Hapa tumeoneshwa kwenye kitabu, Waziri ametaja baadhi ya mashirika ambayo yanafanya biashara na NIC; leo NIC haina mtaji mkubwa. Ningeshauri kazi zote za Serikali iwepo sheria kwamba zote ziende NIC. Mashirika mengi ya umma hayapeleki kazi huko, kwa hiyo taasisi zote za umma na Serikali zifanye kazi na TTCL, NIC, kazi nyingi ziende VETA, ziende Magereza. Taasisi za Serikali hakuna haja ya kuwapa fedha za kujiendesha wapewe biashara ili waweze kujiendesha wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ni vizuri Serikali ikaangalia namna ya kuangalia hizi *regulatory bodies* zote, zote ziunganishwe ziwe *regulatory body* moja na nyingine zote ziwe idara chini yake. Tuangalie sheria zilizounda hizo *regulatory bodies* ili zifanyiwe kazi na zote ziunganishwe na iwe moja; hii italeta

mazingira mazuri ya kufanyia biashara nchini. Wakati wanakwenda kwenye kukagua viwanda, biashara au shughuli yoyote basi ni taasisi moja inakwenda, tozo inakuwa moja ndogo, itakuwa mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara. Huko tunapotaka kuelekea, kwenye uchumi wa viwanda, hiyo body ikiwa moja tozo itapungua na ufanisi wa kazi pia utakuwa ni mzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ili kupunguza gharama za kuendesha hizi bodies mbalimbali za Serikali na taasisi zake tungeangalia namna ya kuziunganisha. Kwa mfano RAHCO na TRL zote shughuli ni moja, zingeunganishwa. Mfano mwingine ni kwenye TBS na Weight and Measurements; zingeunganishwa ili shughuli hizi zote zinazofanana zifanywe na moja ili gharama za usimamizi na management yote ipungue na OC nyingi zitapungua. Kwa hiyo, tuhakikishe kwamba tunaweza kufanya namna ya kuziunganisha taasisi nyingi hizi za Serikali ili kupunguza gharama. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, muhimu nyingine nitakayoendelea kuisisitiza ni kwamba Serikali iangalie na iwe na nidhamu yamatumizi ya fedha. Fedha ambazo ni ring-fenced Wizara ya Fedha ijitahidi isitumie sehemu yoyote nyingine. Pia katika hii Mifuko mitatu; Mfuko wa Bunge, Mfuko wa Mahakama na Mfuko wa CAG, fedha zile ziwe consistent ziende kwa wakati, hasa kwenye huu Mfuko wa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali; wao wanakwenda kwa calendar year na wanafuata ratiba. Tunawaomba muwape kipaumbele na zile fedha zihakikishwe kwamba zinaenda kwa wakati kufuatana na kalenda yao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tutakapokuja kwenye mid-year review; kwa sababu hawataweza kufanya kazi yao inavyopaswa, ni vizuri tuangalie ili waongezewe bajeti wanayoihitaji. Kwa sababu ya fedha za maendeleo tutazongeza, hiyo asilimia 40, ni muhimu sana watchdog, ambayo ni Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ipatiwe fedha za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la mid-term review naamini kwamba hiki kidogo ambacho Serikali inacho sasa hivi, basi tukisimamie vizuri na wote tuwe wavumilivu. Nina uhakika kutokana na uwazi na maoni na ushauri unaopokelewa na Wizara safari hii, naridhika kabisa kwamba najua huko tutafika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningeomba; Wizara ya Fedha kwenye Tume ya Mipango iwawezeshe sana, tena wewe mwenyewe Waziri ulikuwa huko kwa muda mrefu; tunaomba pawe na namna ya kuiunganisha Tume hiyo ifike mpaka ngazi ya Mkoa na Wilaya kwa sababu huko ndio tunakopanga mipango. Kwa sababu Halmashauri na Mikoa yetu ingekuwa na mipango mizuri basi na huku juu pia hii mipango itakuwa ni endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunaomba Tume hiyo ndiyo iwe inashauri. Kwa mfano, kwenye Halmashauri yangu na Halmashauri nyingi, Afisa Mipango ni mmoja hivyo ni ngumu sana kupanga mipango mingi. Hii mipango ikiwa *integrated*, yaani wakiwa wanafanya kazi kwa pamoja mafanikio ya Serikali yatakuwa yanaonekana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, muhimu nyingine ni suala la kuhakikisha kwamba tunaongeza mapato ya Serikali. Taasisi ambayo inakusanya mapato ya Serikali (TRA) tunawapongeza, lakini kwenye baadhi ya maeneo waendeleo kujirekebisha. Kwa mfano, suala la *uplifting* kwenye bidhaa ambazo zinaingizwa ni kero kubwa ambayo inawakatisha tamaa wafanyabishara. Lakini pia kuna kodi nyingine wanakusanya ambazo tayari sheria ilishafuta, sasa na hizo pia zifanyiwe kazi. Yale ambayo tunaongeza yaongezwe *immediately* lakini yaliyoondolewa pia yaondolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, muhimu ni kwamba kila Mtanzania ajitahidi kuwa na tabia ya kulipa kodi, bila kulipa kodi sisi wenyewe basi huko hatutaweza kufika na haya malengo ambayo tunajiwekea hatutayafikia. Kwa hiyo, pawe na *fair trade competition* kila mahali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine muhimu ni ile Tume ya *Fair Competition Commission*, tunaomba basi bodi yake iundwe mapema ili hizi shughuli nyingine ambazo zinakwama kutokana na shughuli ambayo inatakiwa kufanywa na hiyo *Commission* basi hizo ziweze kufanywa mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia sehemu nyingine muhimu ni kuhakikisha kwamba kodi na tozo zile ambazo ni kero katika biashara Wizara ya Fedha ingekuwa na timu maalum ambayo itakuwa inafanya uchunguzi, la si vyo hii ndoto yetu ya kufika kwenye uchumi wa viwanda hatutafikia na bado bidhaa za nje sisi hatutakuwa na uwezo wa kuwa kwenye ushindani nazo. Kwa hiyo, zile kodi na tozo ambazo ni kero ambazo zinafanya biashara hizo zisifanikiwe, basi ziondolewe na pawe na mazingira wezeshi ili wafanyabiashara wetu waweze kufanya biashara vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani kubwa na timu nzima ya Wizara ya Fedha na kuna masuala mengi ambayo wameweza kuweka wazi safari hii pia. Hata kile kitabu cha *volume one* tulipewa kabla ya muda wa bajeti, ambapo huko miaka ya nyuma huwa tunapewa siku ile ambapo Bajeti ya Serikali inasomwa, kwa hiyo hata mwelekeo wa namna ya makusanyo tayari tumeshaanza kuyajua. Muhimu tena naomba Benki hii ya Kilimo ipatiwe fedha ya kutosha ili uchumi uendeleo kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, naomba nishukuru na naunga mkono hoja mia kwa mia. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, atafuatiwa na Mheshimiwa Ngonyani, Naibu Waziri wa Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano, halafu Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali atafuata baada ya hapo.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nami niungane na wenzangu wote ambao wametangulia kusema kwamba tukitaka Bunge hili liweze kutekeleza wajibu wake na kwamba kila mtu awe na nafasi, lazima kanuni zisimamiwe humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiangalia toka ulipoanza umekuwa ukilikazania hilo, naomba uendeleo hivyo, kusitokee mtu anakukatisha tamaa kwa sababu ukikata tamaa maana yake ni kwamba uendeshaji wa Bunge hili hautakuwa na utaratibu ambao unategemewa kisheria. Nakupongeza sana, nakutia moyo na nina uhakika wale waliotaka kukutikisa au kulitikisa Bunge hili watarudi bila wewe kutikisika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Naibu wake na watendaji wote kwa kazi nzuri ambayo tayari wameshaionesha kwa hotuba hii ambayo ni nzuri. Baada ya pongezi hizo nipende kumshukuru na kumpongeza Rais kwa kumchagua Waziri anayeongoza Wizara hii. Waziri nimefanya naye kazi, na-*declare interest* kwamba nilikuwa Waziri wa Uwekezaji, na nilipohamia Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango ilikuwa chini yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo naomba niseme machache kuhusu PPP au ubia kati ya *Public Sector na Private Sector*. Hii ndiyo namna ya kuweza kuhimiza uwekezaji mkubwa ndani ya nchi hii. Huwezi ukaiachia sekta binafsi peke yake wala huwezi kuiachia Serikali peke yake. Tukitaka kujenga uchumi wa soko lazima Serikali na sekta binafsi washirikiane na hakuna namna ambavyo wanaweza kushirikiana ila katika ubia. Sera ipo, sheria ipo, ilifanyiwa marekebisho, kilichobaki ni utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ubia kitu ambacho kinatakiwa ni kuona *risk* ambayo kila mbia anabeba. Kuna athari (*risks*) nyingine ambazo sekta binafsi haziwezi kubeba, pale ambapo Serikali inahitajika iingie, lakini inapotokea mtaji unapotakiwa na upo kwenye sekta binafsi, Serikali ina uwezo mkubwa wa kuzuia mambo ambayo sekta binafsi wenyewe hawawezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ambalo lilikuwa limeisibu PPP ni urasimu ambao haukuwa na maana, au kutokuelewa vizuri sera na sheria ile. Wizara ya Fedha na Uwekezaji ndizo zilikuwa zina sera na sheria lakini utekelezaji uko kwenye *sector Ministries*. Kwa mfano, Wizara ya Ujenzi inaweza ikajenga barabara nyingi sana na katika muda mfupi kama ikipata sekta binafsi

ambayo inaweza ikaingia nayo ubia na kuna namna nyingi ya kuweza kuingia kwenye ubia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kuliongelea ni nafasi ya mabenki katika kujenga uchumi wa soko. Katika mambo ambayo yaliathiri sekta binafsi ni pale ambapo walipokuwa *crowded out* na Serikali yenyewe kupitia *treasury bills* au wakati mwingine hata *bonds*. Kwa sababu Serikali inapokopa kwenye mabenki, mabenki yatapendelea Serikali kwa sababu *risk* ya kukopesha Serikali ni ndogo sana au hakuna, kwa hiyo sekta binafsi haiwezi kupata nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Wizara ya Fedha kuamua kutoa fedha zake ambazo zinakopa, ambazo ni zake zenyewe na kuzirudisha Benki Kuu, sasa mabenki yameanza kuwahimiza watu wapeleke fedha benki. Kabla ilikuwa ni uchaguzi wao kupata fedha kutoka kwa watu binafsi, walikuwa wanategemea zile fedha za Serikali ambazo hatimaye Serikali inakopa. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo benki sasa zimeanza kuchacharika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, najua kwamba Serikali haiwezi kuacha kukopa, lakini mjaribu ku-*balance* ili sekta binafsi isikose nafasi. Huwezi kuwa na uchumi wa soko kama sekta binafsi haiko *active*. Kwa hiyo, naomba mliangalie suala la *treasury bills*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni riba. Katika uchumi wa soko huru faida haiwezi ikawa juu ya asilimia 10. Sasa kama riba ya benki inayotoza ni zaidi ya asilimia 10 maana yake yule ambaye yuko kwenye soko huru hawezi kwenda kukopa halafu apate faida ya chini. Hili ndilo limelikumba Taifa hili. Naomba muangalie suala hili la riba zinazotowwa na benki zetu. Kwa sababu mkitaka sekta binafsi ambayo ni *rational* ikakope benki lazima riba iwe chini ya faida ambayo inapatikana kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia hilo, naomba niongelee VICOBA. Kuna fedha nyingi sana ndani ya VICOBA, na fedha zile haziendi benki, tujiulize kwa nini? Ni kwa sababu hakuna sera na sheria. Kuna watu ambao wamesemea hapa, naomba Benki Kuu iangalie sera ambayo itafaa VICOBA viwe rasmi na vinufaishe watu kama inavyohitajika. Vijijini kuna VICOBA vingi sana na sioni namna ambayo soko huru linaweza kwenda vijijini bila VICOBA hivi kutumika. Naomba sana tuone watu walio wengi ambao hawatataka kukopa hela nyingi lakini kwa wingi wao wakikopa kidogo kidogo italeti *impact* kubwa ndani ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kuliongea kwa ufupi ni Benki ya Kilimo. Nimesikia na Ushirika unataka kuanzisha benki na Serikali ndiyo itakayochangia benki hizo mbili. Tukianza tena kuzindua Benki ya Ushirika



maana yake Benki ya Kilimo itasimama kwa sababu hatuna hela za kuchangia benki hizo zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Wizara na Benki Kuu kwamba tukazanie Benki ya Kilimo, hatimaye kama Benki ya Ushirika inaanza tuondokane na Benki ya Kilimo lakini hatuwezi kuwa na benki zote mbili na zianze kwa wakati mmoja. Tukiruhusu benki zote mbili zianze kwa pamoja tutatawanyanya nguvu zetu na hakutakuwa na *impact* kwenye kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima ndio watakaoikomboa nchi hii, mazao ya kilimo ndiyo yatakayokuwa malighafi ya kiwanda. Mazao ya kiwanda ndicho kitakachokuwa chakula cha wale wanaofanyakazi viwandani na kilimo ndio uti wa mgongo ambao watu wangu wanategemea. Kwa hiyo, tusipokazania benki hii, najua kwamba suala hili liko kwenye bajeti tutakayojadili, lakini kwa leo nataka nisisitize kwamba hatutakuwa tumetenda haki kwenye Benki ya Kilimo kama tutaanzisha Benki ya Ushirika wakati hii ya kilimo bado haijapewa mtaji wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Najua kuwa suala la *sovereign ratings* ni muhimu sana ili nchi hii ionekane kwamba inaweza kukopa kwenye masoko ya nje, lakini hilo tuliangalie kwa sababu kuna nchi ambazo zimefanya hivyo zikaingia kwenye matatizo. Tusiiachie nchi yetu ikaingia kwenye matatizo. Nchi hii tunapata fedha kidogo sana kwenye *investment* kutoka nje. Kiasi cha *investment* inayokuja Tanzania ni 0.03 percent, ni hela kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana Waziri wa Mambo ya Nje alivyokuwa anaongelea *issue* ya *Economic Diplomacy*; tunachopigania ni kwamba *investments* zaidi zije na *share* yetu ya *international markets* iwe kubwa; hilo ndilo matokeo mazuri ya *Economic Diplomacy* ambayo ni nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiisimamia Benki Kuu na Benki nyingine na sekta binafsi nina hakika tutapiga hatua kubwa kwenye kujenga uchumi wetu na sioni pengine ambapo kazi hii inafanyika isipokuwa kwenye Wizara yetu ya Fedha na Mipango. Nawaombea Mwenyezi Mungu awape afya njema muweze kusimamia. Waziri Mpango ana uwezo, Naibu Waziri ana uwezo, Watendaji wana uwezo, nina hakika Wizara hii itasimamia uchumi wetu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naomba usikate tamaa. Wewe ni mtoto wetu, sisi tuko hapa kuona kwamba kazi ambazo zinanufaisha Bunge hili unaendelea kuzifanya na usitetereke sisi tuko na wewe. Ahsante sana. (Makofi)



**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ngonyani, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano atafuatiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, halafu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii. Kwa kweli kazi uliyoifanya umeliletea heshima Bunge hili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nieleze tu eneo moja dogo. Kwa kawaida wenzetu wa upande wa pili wanapochangia, hata wakisema maneno mabaya kiasi gani upande huu wanakaa kimya. Tunapochangia sisi wanaanza kutuzomea hata michango yetu haisikiki. Naomba na hili nalo tulidhibiti. Tukilidhibiti hilo Bunge hili litakuwa zuri kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Dkt. Philip Mpango kwa mipango yake kabambe na hasa katika miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujibu maswali machache ambayo Waheshimiwa Wabunge wamechangia. Moja, kuhusiana na bandari bubu. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, Serikali imejipanga kudhibiti bandari bubu. Kama mtakumbuka hivi karibuni nilijibu swali moja la Mheshimiwa Mbunge wa Mtwara; kwamba tuna vikao vinavyoshirikisha Serikali za Mwambao pamoja na Zanzibar kuhakikisha tunazitambua bandari zote bubu na hatimaye kudhibiti mapato yanayopotea kupitia hizo bandari bubu. Tutaendeleza na katika Maziwa Makuu. Kazi hiyo tutaifanya kwa kasi, mwaka huu ujao wa fedha hiyo kazi lazima ikamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee *TTCL*. *TTCL* naomba niwaote wasiwasi. Tulivyojipanga Wizarani na ndani ya Serikali *TTCL* mnayoiona sasa, *TTCL* mliyoizoea kuanzia mwezi wa Tisa itakuwa ni *TTCL* tofauti kabisa. *TTCL* hii itaingia kwenye kusambaza teknolojia za simu na mitandao ya 2G, 3G na 4G kuanzia Dar es Salaam na mikoa mingine tisa mpaka mwezi Desemba mwaka huu na miaka inayofuata tutasambaza Tanzania nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanya hilo, na kwa sababu Mkongo wa Taifa uko chini yetu hatutakuwa na mshindani. Tutashindana kibiashara na sisi tutaingia katika mashindano ya kutoa vifurushi, kwa sasa hatujaanza kutoa. Nawahakikishia *TTCL* hii itakuwa tofauti kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wa Fedha alivyoniahidi, madeni yote ya *TTCL* yatalipwa na baada ya hapo tunaiwezesha *TTCL* si kwa mtaji, kwa namna tulivyojipanga sasa wala hawahitaji mtaji tena, wanaingia kwenye biashara za ushindani na tuna makamanda pale. Baadhi tutawaondoa ili tuhakikishe kile tunachokikusudia katika *TTCL*

kinapatikana katika muda mfupi na hatimaye Serikali nzima itatumia huduma za TTCL.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee TEMESA nayo. Nayo tuna mipango kabambe ya kuibadilisha. Zile tabia za ajabu ajabu za kudhani TEMESA haina mwenyewe zitakwisha. Masuala ya kuvuruga vuruga, mtu analeta gari zima linatoka bovu mwisho wao ni mwaka huu, baada ya mwaka huu hali itabadilika na Serikali itapunguza matumizi kwa kutumia huduma za TEMESA.

Mheshimiwa Naibu Spika, TRL na RAHCO. Waheshimiwa Wabunge wengi wameongelea kuhusu kuunganisha TRL na RAHCO. Wametoa maelezo marefu, Serikali imeyachukua. Lakini, upande wa pili hawauongelei sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tuna mpango wa kujenga reli kutoka Tanga hadi Musoma, tuna mpango wa kujenga reli kutoka Mtwara hadi Mbamba Bay, tuna reli ya TAZARA, tuna reli ya Kati na matawi yake yote. Hapa ni wajibu wa Serikali na ushauri wenu tutauchukua, kuamua je miundombinu hiyo ya reli zote isimamiwe na TRL peke yake? Kuna faida lakini vile vile kuna hasara zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia upande wa hasara, ujenzi wa miundombinu unahitaji fedha nyingi sana na fedha hizo sehemu kubwa tutazipata kupitia mikopo. Mikopo hii ikikaa TRL kazi yao ya kutoa huduma inaweza ikakwamishwa kutokana na ukubwa wa madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tunadhani TRL ifanye kazi ya kutoa huduma halafu RAHCO kiwe ndicho chombo cha Serikali cha kuwekeza na tutakopa mikopo yote itaingia RAHCO ili TRL iweze ku-operate kibiashara. Kama nilivyosema, kupanga ni kuchagua, tumesikia maoni yenu, tutayajadili ndani ya Serikali na hatimaye uamuzi utatoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ATCL. Kuna baadhi walichangia kuhusu ATCL. Tutafanya kazi ya kuirekebisha ATCL, tutafanya kazi ya kuibadilisha ATCL. Tatizo kubwa la ATCL liko kwenye *mindset*. Tutafanya kazi ya kuondoa matatizo ya kwenye *mindset* ili tuwapate watu ambao wana fikra za kibiashara waweze kutusaidia tuweze kuinua na kuisimamisha ATCL iweze kutoa huduma za usafiri. Kwa kweli, ndege nyingi zinatumia sana fedha za Serikali na fedha za Serikali zinakwenda nje na tunalazimisha kulipa hela nyingi sana kwa gharama za usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiweza kuimarisha ATCL kwanza tutatoa ushindani kwa nchi, lakini vile vile tuta-save fedha nyingi sana zinazopotea sasa kutokana na gharama ambazo hawa wenzetu wachache wanajipangia kwa

namna wanavyotaka wao. Naomba tushirikiane tuifanye kazi ya kuibadilisha ATCL iweze kutusaidia kwa namna ambavyo tunataka.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nirudi tena kwenye TTCL. TTCL mnafahamu kwamba tulikuwa na *partnership* na *Bharti Airtel*. Hivi sasa tunaongelea tutaanza mwezi wa Tisa kwa sababu kwanza tunalitatu hili tatizo la *Bharti Airtel* na tuna uhakika itakapofika mwezi wa Saba tatizo hili litakuwa limekwisha, TTCL itamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100, ndipo tutakapoanza kuingiza hiyo mitaji na mitaji haitoki Serikalini, inatoka kama mkopo, TIB anafanya *Syndication* na makampuni yanayotoa Service kama vile *Alcatel*, ZT ya Japani pamoja na *Huawei*. Watu wa TIB wanatusaidia kufanya *Syndication* na ndiyo mtaji tutakauotumia kuibadilisha TTCL.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na hayo machache na nakuomba sana tena sana utusaidie kulirekebisha Bunge hili. Uwezo unao, umeanza vizuri na naamini hili eneo dogo lililobakia tukilikamilisha kulirekebisha, Bunge hili litakuwa na heshima inayostahili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja na ahsante sana kwa kunipa fursa. (Makofi)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kupata fursa ya kuchangia jioni hii kwenye hoja hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nikushukuru kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia. Nichukue fursa hii pia kukupongeza kwa kazi nzuri unayofanya ndani ya Bunge hili, ili kuwezesha chombo hiki muhimu ambacho kimepewa jukumu kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali kitekeleze majukumu yake ya Kikatiba ipasavyo, kiweze kufanya majukumu yake kwa kuzingatia Sheria, Katiba na Kanuni kilichojiwekea. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, siku moja niliwahi kushauri hapa kwamba, chombo kama hiki, ambacho kinafikia maamuzi yake kwa majadiliano ni lazima kiheshimu Katiba, Kanuni na Sheria zinazotawala katika uendeshaji wa shughuli za chombo hicho. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja iliyoko mbele ya meza yako Tukufu na nampongeza Mheshimiwa Waziri na Wizara nzima kwa kuleta hoja hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeombwa kuchangia ili kueleza mambo machache ya Kikatiba na Kisheria, ambayo yamejili katika michango ya

Waheshimiwa Wabunge, ambao nao nawapongeza kwa michango yao ya kuboresha Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni hili linalohusu Sheria za Mifuko ya Hifadhi za Jamii, kuhusu mapendekezo ya kurejesha au kuwa na fao la kujitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema tu kwamba, mafao ya wafanyakazi yanasimamiwa na Sheria za Mifuko ya Jamii na Sheria hizo ni Sheria ya Mfuko wa Mafao ya Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Sheria ya Mfuko wa Mafao ya Serikali za Mitaa (LAPF), Sheria ya Mfuko wa Mafao ya Mashirika ya Umma (PPF), Sheria ya Mfuko wa Mafao ya Utumishi wa Umma (PSPF) na Sheria ya Mfuko wa Mafao wa GEPF.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa msingi wa mafao haya ya watumishi wa umma ni katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ibara ya 11 ya Katiba hii, Mheshimiwa naomba uniruhusu niisome, hii ndiyo inaweka msingi wa mafao hayo ya watumishi wa umma na yenyewe inasema hivi:-

*Mamlaka ya Nchi itaweka utaratibu unaofaa kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa haki ya mtu kufanya kazi, haki ya kujipatia elimu na haki ya kupata msaada kutoka kwa jamii wakati wa uzee, maradhi au hali ya ulemavu na katika hali nyinginezo ambazo mtu huwa hajiwezi.*

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndio msingi wa mafao haya ya wafanyakazi hawa. Sasa sheria tulizonazo zimegawanyika kwenye makundi mawili; Sheria ya LAPF na Sheria ya PSPF, zenyewe bado zinalo fao la kujitoa, lakini Sheria ya NSSF, Sheria ya PPF na Sheria ya GEPF haina fao la kujitoa. Sasa kumekuwa na hoja kwamba, labda kama kuondolewa kwa fao hilo la kujitoa kunavunja Katiba ya nchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusema kwamba, kwanza hizi Sheria, ambazo hazina fao la kujitoa ndizo zinazozingatia matakwa ya Katiba ya nchi, lakini pia suala hili liliwahi kufikishwa mahakamani. Mahakama ya Rufaa katika shauri la rufaa namba 105 (*consolidated civil appeal*) namba 105 na 81 za mwaka 2006, kati ya Nassoro Athuman Gogo na James William Lugiana, wakiwakilisha wenzao 2,487 liliamua kwamba, Sheria ya PPF iliyokuwa haina fao hilo la kujitoa ilikuwa haivunji Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, huu ndiyo ushauri wangu, ndiyo msimamo wa Katiba, ndiyo msimamo wa Sheria kwenye masuala haya. Lakini Bunge linaweza kufanya maamuzi, maamuzi ambayo lakini pia linapoyafanya lazima lizingatie Katiba na maamuzi ya Mahakama ya Rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni hili ambalo limezungumzwa kuhusu suala la kampuni moja inaitwa *Quality Plaza*, kwa sababu nimeliona hapa, halikuzungumzwa hadharani. Mashauri yako mahakamani yanayohusu masuala haya na yameshasikilizwa na inasubiriwa tu sasa kutolewa hukumu. Kulikuwa na mashauri mengi na vyema niyataje tu mashauri haya, lakini sitaenda ndani kwa sababu suala liko mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kulikuwa na shauri namba 33 la mwaka 2009 Mahakama Kuu, shauri namba 40 la mwaka 2011 Mahakama Kuu, shauri namba 59 la mwaka 2012 Mahakama Kuu, shauri namba 77 la mwaka 2012 Mahakama Kuu. Hata hivyo, baadaye mashauri yote haya yaliunganishwa kwa pamoja yakawa *consolidated* kwamba ni shauri namba 33 la mwaka 2009 kwa sababu yote ni ya migogoro ya upangaji. Shauri hili limesikilizwa, linasubiriwa tu kutolewa hukumu na kwa sababu hiyo hatuwezi kulijadili hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata hivyo, *Quality Plaza* walifungua shauri namba 97 la mwaka 2015 walipotakiwa kuhama na liko mahakamani, hatuwezi kuyaongelea hapa. Kwa hiyo, ndiyo niliona kwamba, niyaseme hivi, lakini ukweli ni kwamba, *PSPF* imekuwa ikichukua hatua za kuhakikisha kwamba, inalinda maslahi kwenye pango hili isipokuwa kama tu kwa sababu ya *technicalities* za mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, ambalo naomba kuliongea ni hili suala la chombo kinachoitwa *Financial Intelligence Unit*. Naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, mwaka 2014 ndugu George Mcheche Masaju, wakati huo akiwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliiwakilisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Taasisi moja ya masuala ya kifedha duniani inaitwa *Financial Action Task Force*. Tanzania ilikuwa imekuwa *blacklisted for almost five years*, kwamba tuna mifumo dhaifu ya kupambana na utakatishaji wa fedha haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi Januari, mwaka 2014, nikatumwa Paris kwenye *Financial Action Tax Force*, nikaitetea wale wakubwa wakaridhika. Mwezi wa Nne wakaja kufanya *On site visit Inspection*, wajiridhishe na mifumo yetu ya Sheria, wakaridhika. Mwezi wa Saba, 2014, Tanzania ikaondolewa katika lile kundi la nchi ambazo zina mifumo dhaifu ya udhibiti wa fedha haramu na vitendo vya ugaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Tanzania ina mifumo imara ya kisheria ya kudhibiti vitendo vya utakatishaji wa fedha na ugaidi. Na ni kwa sababu hiyo pia, imejiunga na *Egmont Group*, ambayo ni jumuiya ya Taasisi hizi za *Financial Intelligence Unit*, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kumekuwa na hoja kwamba, *Financial Intelligence Unit* ya Tanzania ilipaswa iwe na mamlaka ya kuchunguza kama zilivyo mamlaka nyingine. Haiwezekani! Yenyewe hii, kuna makundi matatu ya hizi *Financial Intelligence Unit*.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ni *Administrative* kama ya kwetu hii, ya kiutawala. Yenyewe inapata taarifa hizi, inazipeleka kwenye vyombo vya uchunguzi kama Polisi, PCCB na Taasisi nyingine halafu na Vyombo vya mashtaka. Pia, kuna kundi la pili linaitwa *Investigative Financial Intelligence Unit*, hii inakuwa na mamlaka yenyewe ya kuchunguza, inachunguza tu, lakini inapeleka kwenye vyombo vingine vya mashtaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kundi la tatu ambalo ni *Hybrid* lenyewe linachunguza na kushtaki. Mifumo yote hii mitatu imekubaliwa katika kundi hili la *Egmont Group* na ndiyo maana sisi tulijiunga mwaka jana kwenye hii *Egmont Group* kwamba tuna sifa zote za kutekeleza hayo. Kinachozingatiwa zaidi kwenye hizi *financial intelligence* ni kwamba; je, hizi Taasisi ni huru? Hilo la kwanza. La pili, zina uwezo wa kuchunguza na kujiridhisha kufanya *focused investigation* ikiwa ni pamoja na kushirikiana na Taasisi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kushauri tu kwamba, hii Taasisi ya *Financial Intelligence Unit* iliyopo hapa kwetu, kwa sababu tu yenyewe haichunguzi au kwamba, haipeleki mashtaka mahakamani kwamba, basi ni dhaifu, hapana. Ndivyo ilivyo na ni utaratibu katika dunia kwa haya makundi matatu na sisi tunaingia kwenye kundi hilo, hakuna matatizo mengine yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niseme tu kwamba, naunga mkono hoja kama ambavyo nilishaongea tokea mwanzo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha hatua hii tuliyofika jioni hii ya leo kama Wizara na kama Serikali. Pili naomba nimshukuru na nimpungeze kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya katika kusogeza mbele gurudumu la maendeleo la Taifa letu. Pia naomba nikushukuru wewe mwenyewe Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujasiri wako, kwa kusimamia haki na kuhakikisha kwamba haki inasimama na nidhamu inarejea ndani ya Bunge letu Tukufu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia, niwashukuru Wabunge wote waliochangia hoja iliyowasilishwa mezani na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Michango yenu tumeichukua ni mingi, tunawashukuru sana na sina uhakika kama tutaweza kujibu yote hapa, tutajibu machache, lakini kiuhalisia tumechukua na tutawajibu kimaandishi, tunawashukuru sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache ya utangulizi, naomba sasa nichangie hoja chache ambazo zimejili katika majadiliano ya Waheshimiwa Wabunge katika kujadili na walioleta kwa maandishi pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza, ambayo ningependa kuichangia ni Ucheleweshaji wa Michango ya Mwajiri na nyongeza ya Pensheni kwa Wastaafu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kabisa, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango inawajibika sana kuwasilisha mchango wa mwajiri kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wote wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016, Serikali imefanya jitihada kubwa sana katika kuwasilisha michango hiyo. kwa mfano, mchango wa mwajiri uliotarajiwa kuwasilishwa ni Shilingi bilioni 797. 781, hadi kufikia Mei, 2016, Wizara imewasilisha Shilingi bilioni 529.932 kama mchango wa mwajiri kwa Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Wizara na kama Serikali, bakaa ya Shilingi bilioni 267.849 itawasilishwa kabla ya tarehe 1 Julai, 2016. Kwa hiyo, kama Serikali tunatoa *Commitment* mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba, michango yote hii ya waajiri tutaweza kuiwasilisha katika Mifuko yetu yote ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa mujibu wa kifungu namba 30(3) na (4) cha Sheria ya Mfuko wa PSPF namba Mbili ya mwaka 1999, Serikali inatakiwa kuwasilisha pia tofauti ya nyongeza ya pensheni kwenye Mfuko wa PSPF. Kuanzia Julai, 2015 hadi Aprili, 2016 Wizara imewasilisha PSPF kiasi cha Shilingi bilioni 75 kati ya Shilingi bilioni 94 zilizotakiwa kuwasilishwa. Pia tunatoa *commitment* ya Serikali yetu kwamba, bakaa la bilioni 18 tutaweza kuliwasilisha kabla ya tarehe 1 Julai, 2016 ili kuwezesha Mfuko wetu wa PSPF uweze kufanya kazi zake vizuri.



Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu Serikali yetu inafanya kazi kwa *Cash Budget*. Kwa hiyo, michango ambayo hatujamalizia ni kutokana na mapato, ambayo tumekuwa tukikusanya. Hata hivyo, sote sisi ni mashahidi, kupitia Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, tumeweza kuongeza mapato tangu Serikali yake ilipoingia madarakani na ndiyo maana tunatoa *commitment* hizi kwamba, tutamalizia bakaa zote zilizobaki katika michango ya hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niongelee hoja namba mbili, ambayo ni tatizo la Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali kutoa takwimu zinazotofautiana juu ya suala moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni kweli lipo, lakini kama Serikali hatujakaa kimya, tumeendelea kulifanyia kazi. Ofisi ya Taifa ya Takwimu, tunafahamu ndiyo yenye mamlaka kisheria kuratibu na kusimamia utoaji wa takwimu rasmi zinazotumiwa na Serikali na wadau wengine kwa ajili ya kupanga mipango ya maendeleo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kutoa takwimu zinazotofautiana, Serikali tumeona tatizo hili na hivyo ilitungwa Sheria ya takwimu ya mwaka 2002; kwa sababu ya kukosa nguvu kisheria ilibadilishwa mwaka jana mwaka 2015 na sasa hivi tunajipanga vizuri zaidi ili kuweza kufika na kuja na takwimu ambazo ni sahihi zitakazoweza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Sheria hii, ambayo imeanza kufanya kazi kuanzia mwezi Novemba 2015, Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika, imeanza kutengeneza Kanzidata ijulikanayo kama *e-population register*, ambayo itaandikisha watu wote katika Kaya na kuunganisha na masuala ya elimu, hali ya ulemavu, afya, kilimo, kazi na masuala mengine katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanzidata hii ni maelekezo ya kifungu cha 56 cha Sheria za Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982 pamoja na Kanuni ya Pili na ya Tano ya taratibu za kazi za Mwenyekiti wa Mtaa au Kitongoji ya mwaka 1993 pamoja na Tangazo la Serikali namba Tatu la tarehe 7 Januari, 1994; ambalo linasisitiza kila Mtaa, Kitongoji kuwa na *Register* ya wakazi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa kutambua umuhimu na Mamlaka yake Kisheria, imeanza kutekeleza kazi ya kutengeneza kanzidata ya Taifa, ambayo itasaidia Serikali kuwa *One Stop Centre* ya Takwimu Rasmi katika sekta zote za katika nchi yetu kwa kutumia takwimu za utawala (*Administrative Records*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi, mfumo huu unafanyiwa majaribio katika Kata ya Mapinga, Mkoani Pwani na baadaye tutaendelea nchi nzima. Kupitia Ofisi ya Takwimu ya Taifa, kazi ya kuimarisha takwimu za utawala, umetengewa jumla ya Shilingi bilioni 1.6 kwa nchi nzima kwa bajeti ya mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kuwaomba Wananchi wote kupitia sisi Wabunge wao kutoa ushirikiano wa kutosha kwenye zoezi hili kwa ajili ya Taifa letu. Pia Watendaji wa kata, vijiji, vitongoji na mitaa watoe ushirikiano wa kutosha ili tuweze kuwa sasa na takwimu zilizo sahihi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tatu, ambayo ningependa kuitolea ufafanuzi ni hoja iliyoletwa na Kambi Rasmi ya Upinzani, kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye ukaguzi maalum katika Kitengo cha Madeni na Uwekezaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali haina pingamizi na mapendekezo haya ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni juu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalum katika Kitengo cha Madeni na Uwekezaji wa Mifuko ya Hifadhi Jamii ili kujiridhisha na usahihi wa taarifa zilizopo. Ni wajibu wa CAG kufanya kazi hiyo na Serikali itampa ushirikiano wa kutosha ili kufanikisha kazi hiyo kwa wakati na kwa kadri Bunge litakavyoelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ushauri wa kutenganisha deni halisi la Taifa na Matumizi mengineyo yanayohusu Mfuko Mkuu wa Hazina pia tutaufanyia kazi kwa kadri itakavyowezezana. Ingawa hakuna ubadhirifu wowote ulioripotiwa katika Mfuko huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni fedha zilizoidhinishwa na Bunge hazitolewi kama zinavyoidhinishwa. Kama nilivyotangulia kusema, tunafahamu mfumo tunaoutumia kutoa fedha za utekelezaji wa bajeti yetu ni mfumo wa *Cash Budget*. Kwa mfumo wa *Cash Budget*, fedha za miradi ya maendeleo pamoja na matumizi ya kawaida hutolewa kulingana na mtiririko wa upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ni vyema ikaeleweka kuwa bajeti ni makadirio ya mapato na matumizi, hivyo ni muhimu lakini si lazima bajeti iliyopangwa au kuidhinishwa na Bunge ilingane na matumizi halisi kwa sababu inaangalia uhalisia wa mapato tutakayokusanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kama nilivyosema mwanzo, Serikali inaendelea na jitihada za kuboresha upatikanaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ili kuweza kutoa fedha kama zinavyoidhinishwa na Bunge. Tunatarajia

kabisa kwamba mapendekezo yetu ya bajeti yetu tutaweza kuyafikia kwa kiwango kikubwa kutokana na uboreshwaji wa mapato ambayo Taifa limeyafikia kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa inasema Serikali iruhusu kutumia fedha za maduhuli badala ya kupelekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Kama Serikali, tungependa kufanya hivyo, lakini utaratibu wa fedha za maduhuli kupelekwa Mfuko Mkuu unasaidia kuwepo kwa mgawanyo mzuri wa fedha kwa taasisi au Wizara ambazo hazikusanyi maduhuli, mfano Ofisi yetu ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kuruhusu maduhuli yatumike sehemu yanapokusanywa bila kupelekwa Mfuko Mkuu kuna hatari kubwa ya baadhi ya taasisi zetu kutopata fedha na kusababisha kushindwa kutekeleza majukumu yake. Serikali ina vyanzo mbalimbali vya fedha kwa ajili ya kutekeleza bajeti yake. Fedha za maduhuli ni mojawapo ya chanzo cha mapato ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiruhusu fedha hizi za maduhuli zisipelekwe kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, ipo hatari ya Wizara, taasisi na mikoa isiyokusanya kutopata fedha za kuendesha ofisi, kuendeleza shughuli za maendeleo na kulipa mishahara. Hivyo fedha za maduhuli zinapaswa kupelekwa Mfuko Mkuu ili ziweze kugawanywa katika mafungu mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza bajeti iliyoidhinishwa, ambapo makusanyo ya maduhuli ni asilimia 15 ya mapato yote ya ndani. Tunawaomba Waheshimiwa Wabunge mtuunge mkono katika hili ili tuweze kutekeleza bajeti yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa Serikali iwalipe wastaafu kwa wakati wanapostaafu, ikiwa ni pamoja na kuwalipa pensheni kwa kutumia viwango vyao vya mishahara wa mwisho. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba mishahara ya mwisho kwa watumishi wenye masharti ya ajira ya kudumu na malipo ya uzeeni ndiyo inayotumika kukokotoa kiinua mgongo na pensheni ya watumishi hao mara wanapostaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wastaafu ambao nyaraka zao za kustaafu zinawasilishwa kwa wakati, yaani angalau miezi mitatu kabla ya mtumishi husika kustaafu na zikiwa hazina kasoro yoyote, wamekuwa wanalipwa mafao yao kwa wakati. Ili kuhakikisha wastaafu wote wanalipwa kwa wakati, waajiri wanashauriwa kuwasilisha nyaraka zote ili tuweze kuwalipa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia napenda kuwaomba waajiri wote, upo mchezo ambao unafanyika mwajiriwa anapokaribia kustaafu, amebakiza miezi miwili kustaafu tayari ameshapeleka nyaraka zake mbalimbali katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, unakuta sasa mwajiriwa huyu ana-*collude* na mwajiri wake, anapandishwa cheo, kwa hiyo hii ndiyo inayoleta utata. Tayari nyaraka

zake zilishapelekwa, sasa inakuwa ni vigumu, umepandishwa cheo mwezi mmoja kabla ya kustaafu inakuwa ni changamoto kushughulikia mafao yako pale ambapo mwajiriwa huyu anapostaafu. Hivyo niwashajihishe waajiri kupeleka nyaraka zote pale miezi mitatu inapokaribia mstaafu huyu anatarajia kustaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyowasilishwa na ambayo napenda kuitolea maelezo ni kwamba mikopo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo haujasaidia kubadilisha hali ya maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kuna kipindi cha mpito kati ya kukua kwa deni la Taifa linalotokana na mikopo ya miradi ya maendeleo na ustawi wa maisha wa wananchi wetu. Tunafahamu wote ukikopa leo deni linaongezeka leo lakini utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo unachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kuna *lax period* ambayo lazima turuhusu miradi hii inapokuwa imeshatekelezwa, kama miradi mingi ya ujenzi wa barabara, *then* tutaweza kuona maisha ya wananchi wetu yanaendelea kubadilika. Naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba muda si mrefu maisha ya wananchi wetu yataendelea kubadilika na mpaka 2025 tutakuwa ni Taifa la kipato cha kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niongelee tatizo moja ambalo limeongelewa ambalo nalo nimeona Wabunge wengi wameliongelea. Nayo ni marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ambayo haijajumuishwa katika Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali uliogawiwa kwa Wabunge; wanaomba Serikali iwasilishe marekebisho ya Sheria hiyo haraka iwezekanavyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410, yatawasilishwa Bungeni kupitia Muswada wa Sheria unaojitegemea kuhusu marekebisho ya sheria hii. Serikali imejipanga kuwasilisha Muswada huu katika Bunge hili la Bajeti linaloendelea sasa hivi. Kwa hiyo, naomba niwape *comfort* Waheshimiwa Wabunge, marekebisho hayo yatakuja na sheria hii itafanyiwa marekebisho kabla Bunge hili halijafika mwisho. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba nirudie kusema naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Nakushukuru sana. (Makofi)

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikushukuru sana kwa kuliongoza vizuri sana Bunge toka asubuhi na

mchana huu. Niungane na waliotangulia kusema kwamba haya wanayofanya upande mwingine yasikukatishe tamaa. Chapa kazi, fanya kazi ambayo Bunge hili lilikuchagua kufanya na hakika Watanzania wanajua umahiri wako na matunda ya kazi yako njema. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango mizuri sana na ushauri wao na naahidi kabisa kwamba ushauri ambao mmetupatia tutaufanyia kazi na tutauzingatia katika kutekeleza bajeti ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 36 wamechangia hotuba yangu; waliochangia kwa kuzungumza ni 24 na waliochangia kwa maandishi ni 12. Kwa kuwa baadhi ya michango ni ushauri lakini hata hoja hizi si haba, kwa muda ambao ninao sitaweza kujibu zote, lakini naomba kuliahidi Bunge lako Tukufu kwamba tutawasilisha majibu ya hoja zote kwa maandishi ili Bunge liwe na rejea na kumbukumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo machache ya utangulizi, basi naomba nitoe maelezo kwa baadhi ya hoja ambazo zimejitokeza wakati Waheshimiwa Wabunge wakijadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango na taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nianze na hoja ambayo ilijielekeza kusema kwamba ni vizuri kama Serikali tuangalie tutakavyoweza kuzuia athari zinazoweza kujitokeza katika kukopa na kutumia *instrument* mbalimbali za masoko ya fedha kama vile *hedging* na *swaps*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hili labda tu niseme kwamba, Wizara ya Fedha na Mipango katika ukopaji tunazingatia Mkakati wa Kati wa Usimamizi wa Madeni, kwa Kiingereza inaitwa *Medium Term Debt Strategy*, lakini pia Sheria ya Madeni. Mkakati huu unaelekeza tukope wapi, sarafu zipi, riba gani, kama ni *fixed rates* au *variable rates*, lakini kubwa ni kwamba tuhakikishe Serikali inakopa kwa gharama nafuu na zenye athari ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika ukopaji wa deni la nje kuna athari nyingi ambazo zinaweza kujitokeza ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya riba (*Interest Rate Risk*) lakini pia mabadiliko ya viwango vya kubadilisha fedha (*Exchange Rate Risk*). Tunaweza tukatumia vyombo mbalimbali ikiwa ni pamoja na *instruments* ambazo aliyetoa swali alipendekeza, ikiwa ni pamoja na *hedging* na *Interest Rate Swaps*. Hivi ni vyombo ambavyo hata hivyo vina gharama kuvitumia na pia vinahitaji utaalum wa hali ya juu katika kuotea viwango vya riba katika masoko ya fedha ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu kwamba, kimsingi hizi *instruments* kwa sasa zinatumiwa zaidi kwa nchi ambazo ziko kwenye mikopo ya kibiashara na ambazo zina viwango vya riba vinavyobadilika mara kwa mara, lakini mahali pia ambapo madeni yako katika sarafu moja. Kwa hiyo, tunavyoendelea huko mbele tutaangalia tukiongozwa na, kama nilivyosema, *Medium Term Debt Strategy* ili kuona polepole na sisi tunavyoweza kutumia hizi *instruments* zikatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nisemee kidogo suala la deni la Taifa na nimshukuru sana Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge kwa ufafanuzi wake mzuri alipolielezea kwa nini linaongezeka. Naomba tu nisisitize kwamba kwa kweli kwa Taifa kama letu ambalo lina mahitaji makubwa sana ya maendeleo, ni lazima tuendeleo kukopa na ukopa maana yake unaingia kwenye deni. Tuna mahitaji makubwa sana ya miundombinu, kwa hiyo lazima tukope. Kwa sasa hatuna vyanzo vya fedha vya kutosha kuweza kukidhi hayo mahitaji yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kikubwa Mheshimiwa Chenge amekieleza, ni kwamba tunakopa kwa masharti gani? Hili ni jambo la kuangalia. Kwa hiyo riba kiasi gani, tutalipa kwa muda gani, *grace period* na masharti mengine, haya lazima kuyachambua kwa umakini. La muhimu zaidi, tunakopa hizi fedha kufanyia nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mara huwa nasisitiza nchi inavyokopa haina tofauti na mtu binafsi. Kama unakopa ukaenda kustarehe ukalewea pombe na kadhalika basi unajua kabisa huo mkopo hauna faida kwako wewe na familia yako na Taifa ni hivyo hivyo. Kama unakopa na unazitumia kuongeza uwezo wako wa kuzalisha, unaongeza uwezo wako wa miundombinu bora ambayo inawasaidia wawekezaji na wananchi kuweza ku-move goods and services, hilo ndilo jambo jema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kinachotakiwa ni umakini, kwamba mikopo hiyo tunaifanyia jambo gani. Kwa nchi yetu, kikubwa tumeelekeza mikopo hiyo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu. Ni wazi kabisa miundombinu kama umeme Kinyerezi, barabara nyingi ambazo zimejengwa nchini, madaraja na kadhalika, yote haya kwa fedha za ndani peke yake tusingeweza, kwa hiyo ilitulazimu kwenda kukopa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa upande wa tathmini ya deni la Taifa, kwa kweli hapa tunafanya tathmini mara nyingi. Kila mwaka tunafanya tathmini chini ya ushirikiano wetu na Shirika la Fedha la Kimataifa na wao wanashiriki, hatufanyi peke yetu. Kwa hiyo hizi *estimates*, tunapoangalia uhimilivu wa deni la Taifa kulinganisha na vigezo vya Kimataifa, kwa kweli hakuna uchakachujaji. Kwa hiyo, moja tunatazama uwiano kati ya deni na pato la Taifa (*debt to GDP*)



*ratio*) na Kimataifa ni kwamba *debt to GDP ratio* inatakiwa isizidi asilimia 50, ndiyo viwango vya Kimataifa na kwa Tanzania hivi sasa tuko asilimia 19.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, kigezo kingine ni deni la nje kwa uwiano wake na uwezo wetu wa kuuza bidhaa nje (*export*) na hapa ulimwenguni ukomo wastani ni asilimia 200, Tanzania sasa hivi tuko asilimia 97.7. Pia tunaangalia uwiano kati ya deni la nje na mapato yetu ya ndani na ukomo wa Kimataifa ni asilimia 300, sisi bado tuko asilimia 145.3 kwa hiyo tunaangalia vigezo kama hivi na zaidi ya hapa na kimsingi vigezo vyote vinatunyesha kwamba deni letu ni himilivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kidogo kuhusu Serikali kutoa *non-cash bond*. Naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ilishaamua kutoa *cash bond* na tumechelewa kidogo kwa sababu tumekuja kupata taarifa kwamba baadhi ya madai ya Mifuko yana maswali mengi. Kwa hiyo, kwa maana kwamba sasa tunatoa *cash bond* kwa kuzingatia madai yapi ilikuwa ni tete na ilikuwa ni muhimu sana kufanya uhakiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ilashamuagiza *Internal Auditor General* kufanya uhakiki na bahati nzuri hivi ninavyozungumza amekamilisha uhakiki, anamalizia tu ku-polish ile ripoti yake ili tuweze kufanya uamuzi na kuendelea kutekeleza uamuzi wa Serikali wa kutoa *cash bond*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulishauriwa na nafikiri alikuwa Mheshimiwa Prosper Mbeni, kwamba tuangalie upya mwenendo wa benki kwa sababu kwa kweli hali ya *interest rates* si nzuri na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, nithibitisha tu kwamba Serikali tumeanza kufanya hivyo. Mtakumbuka kwamba katika kikao kilichopita cha Bunge lako nilieleza Bunge lako uamuzi wa Serikali, kwa mfano kuagiza kwamba fedha ambazo zinashikiliwa na Benki za Biashara, fedha za Serikali za taasisi ambazo zinashikiliwa kwenye benki za biashara zifunguliwe akaunti Benki Kuu ili tuweze kuona fedha hizo ni kiasi gani na zinatumiwa kufanya nini badala ya benki za biashara kuzitumia kufanya biashara, ikiwa ni pamoja na kufanya biashara za hati fungani za Serikali hiyo hiyo. Kwa hiyo hatua kama hii ni moja ya hatua ambayo inazilazimisha sasa hizi benki ziondoe *too focus* kwenye makampuni makubwa na kwenye miji ili sasa ziangalie na kwenda kutafuta wateja hata vijijini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunaangalia pia sababu nyingine ambazo zinasababisha *interest rate* katika benki kuwa kubwa na hii ni pamoja na kutoa elimu ili wananchi wa Tanzania wawe na hakika kabisa kwamba unapokwenda kukopa lazima urudishe na lazima utaratibu huu uendelee kujengwa siyo unakwenda kukopa halafu unaingia mitini.



Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lazima kuchukua hatua za makusudi kabisa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba Mtanzania anajulikana alipo anafanya shughuli gani, mali zake ni zipi ambazo amekopea na kadhalika. Hizi zote ndizo zinazochangia kwenye gharama za mikopo, kwa hiyo, lazima hizi tushughulike nazo ili riba hatimaye ziweze kuteremka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwepo hoja ya pia kwamba wafadhili kupunguza ahadi zao ni kweli haikubaliki na kwamba ni vizuri Serikali ijulishe dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tu kwamba kwenye hotuba yangu nimeeleza baadhi ya hatua ambazo tumechukua ili kukabiliana na tatizo hili. Moja kubwa ni kuendelea na mazungumzo na wadau wetu wa maendeleo. Kama nilivyoeleza asubuhi tumekwishafikia uamuzi kwamba tunatafuta, tumepata mtaalam elekezi ambaye ni *third part* na yeye ataangalia pande zote mbili ili kuona changamoto ambazo zinajitokeza (*concerns*) kwa pande zote ili tuweze sasa kuandaa utaratibu mzuri zaidi wa hii misaada ya wafadhili na kuhakikisha kwamba ahadi zao zinatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilitolewa *observation* kwamba pana upotevu mkubwa sana wa mapato bandarini ikiwa ni pamoja na bandari bubu. Hili halina ubishi na Serikali na Wizara inafanya jitihada za makusudi kabisa kuimarisha ulinzi na kuhakikisha kwamba tuna *patrol team* ambayo inakagua baadhi ya hizi bandari zikiwemo bubu na kufuatilia pale ambapo tunakuwa tumepata taarifa za kiintelijensia juu ya watu ambao kwa makusudi wanatumia bandari zetu kuikosesha Serikali mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli pia kwamba nchi yetu ni kubwa na mipaka yetu ni mirefu, kwa hiyo, njia za panya bado ni nyingi. Wito wangu kwa Watanzania ni kuendelea kutupatia taarifa kutoka sehemu mbalimbali za nchi yetu ili tuweze kwa kadri inavyoweze kadhhibiti mipaka yetu na bandari zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulishauriwa hapa kwamba Tume ya pamoja ya fedha ifanye kazi yake. Mheshimiwa Waziri anayesimamia masuala ya Muungano alieleza vizuri kwamba kwa kweli waraka ulishaandaliwa ambao ni pamoja na kuhakikisha kwamba, kwa mfano mgawanyo wa mapato baina ya Serikali zetu mbili, unafanyika vizuri na kwa makubaliano ya pande zote na tume ya pamoja ya fedha kwa kweli ni *interest* ya kila mtu kwamba ifanye kazi yake vizuri ili Muungano wetu uendelee kuimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulisemea ni hili la malipo ya wazabuni kwamba watalipwa lini? Niseme tu kwamba Wizara ya Fedha na Serikali kwa ujumla imedhamiria kuongeza kasi ya kumaliza

malimbikizo halali, nirudie tena malimbikizo halali ya madai ya wazabuni. Bahati nzuri kwa kuwa sasa makusanyo ya Serikali yanaimarika kwa kweli ni dhamira ya dhati kabisa ya Serikali kwamba tuyamalize haya mapema inavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nitumie nafasi hii kusisitiza kwa wazabuni, wote ni muhimu sana wanapowasilisha madai yao yakawa ni ya kweli. Pawepo uaminifu katika madai ambayo yanawasilishwa kwa sababu kila mara Ofisi ya *Internal Audit General* inapofanya kaguzi zake, inapofanya uhakiki tumegundua kuna madai mengi hewa. Kwa hiyo, nao watusaidie, ni sehemu ya kufanya machelewesho kwa sababu ni lazima tuhakikishe kwamba tunalipa madai halali na siyo kutumia fedha za umma isivyo sawasawa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokea maoni kwamba utumbuaji wa majipu mamlaka ya mapato umezaa mapato zaidi. Ni kweli na napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba kwa hili tutaendelea tutawatumbua Watumishi wasio waadilifu, tutawashughulikia kikamilifu. Wakati huo huo niwapongeze sana watumishi wema wa Mamlaka ya Mapato ambao wameendelea kufanya kazi yao nzuri sana na kwa sasa tuna zaidi ya trilioni moja kama mapato ya Serikali ya kodi kila mwaka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Bima la Taifa, kama mpango wa kulifufua na kuliongezea uwezo uko wapi? Hata bodi kwamba iko na walio wengi kwenye *management* wanakaimu. Napenda niseme tu kwamba, Wizara yangu imefikia hatua nzuri kuteua Wajumbe wa Bodi na ninavyozungumza Wajumbe wanaopendekezwa wanafanyiwa upekuzi na mara baada ya bodi kuundwa basi bodi hiyo nayo tutaielekeza mara moja ishughulikie suala la Maafisa Waandamizi ambao bado wanakaimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ndani ya Serikali tumekwishatoa maelekezo kwamba kwa kadri inavyowezekana Taasisi za Umma na Mashirika yake zitumie *National Insurance Corporation* ili tuweze kuhakikisha kwamba tunaliongezea mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja juu ya Mfuko wa Mahakama lakini pia ukweli kwamba kuna upungufu wa Mahakimu lakini hata hali yenyewe ya Mahakama zetu, Mahakama za Mwanzo hairidhishi na inahitaji kuboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo la msingi kabisa na Serikali inatambua hili, ndiyo maana mapema mwaka huu Mheshimiwa Rais, aliagiza Mfuko wa Mahakama uongezewe fedha na tulifanya hivyo, tuliwaongezea fedha za maendeleo Shilingi bilioni 12.6 na moja ya kazi ya fedha hizi ni kwa ajili ya kuhakikisha miundombinu ya Mahakama inajengwa na Serikali itaendelea kufanya hivyo kwa kuwa tunatambua umuhimu wa Mhimili wa Mahakama katika kutoa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nilisemee suala la tuhuma ambazo zimetolewa kuhusu Benki Kuu kufungua makampuni na watumishi wanachukua tenda za Benki Kuu ambazo zinajumuisha kazi za siri. Naomba tu nikiri hapa kwamba taarifa hii nimeisikia hapa mbele ya Bunge lako Tukufu na namwomba Mheshimiwa aliyetoa hoja hii atupatie taarifa kamili niko radhi kabisa tuzungumze tupate hizo taarifa na tutazifanyia kazi tuhuma hizi mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nilisemee hili la kwamba Serikali haijasaidia kukuza sekta binafsi na hususani baadhi ya kodi na sheria ambazo zinakuwa ni kero kwa Waajiri na pengine na baadhi yao hazina tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niseme kwamba namwomba Mheshimiwa Mbunge aliyetoa hoja hii asubiri na asikilize hotuba yangu ya bajeti ya Serikali Kuu Jumatano iliyayo kwa hamu baadhi ya mambo haya tutayashughulikia. Hata hivyo, niseme tu kwamba ni kweli baadhi ya vipengele vya sheria yetu ya kazi vimekuwa vinalalamikiwa na wawekezaji na kwamba pengine haitoi fursa kwa waajiri kuchukua hatua ingawa pia kuna upande mwingine kwamba baadhi ya waajiri nao wanawanyanyasa wafanyakazi wao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba Serikali ni sikivu, imesikia na inaendelea kusikia na ndiyo maana Mheshimiwa Rais, kati ya makundi ya kwanza aliyokutana nayo mara baada ya kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni wawakilishi wa wafanyabiashara na kusikiliza kero zao ili kuweza kuhakikisha kwamba mazingira ya kuwekeza na kufanya biashara ikiwa ni pamoja na marekebisho yanayotakiwa kwenye hizi sheria yanafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nilifuata hatua za Mheshimiwa Rais wetu na nimeshafanya mikutano na wafanyabiashara Dar es Salaam na Arusha lakini lengo ilikuwa ni hilo hilo, kwamba tuzielewe vizuri changamoto ambazo wanakabiliana nazo ili tuweze kuzifanyia kazi na kupata suluhisho mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisisitize kwamba wakati nawasilisha mpango wa maendeleo wa miaka mitano hapa nilisema wazi kabisa kwamba Serikali ya Awamu ya Tano moja ya msisitizo mkubwa ni kuhakikisha kwamba mazingira ya biashara na uwekezaji haya tutayawekea mkazo zaidi katika awamu hii maana hatutaweza kujenga viwanda katika nchi yetu kama mazingira ya wawekezaji na waajiri hayako sawasawa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja pia kwamba kwa nini Serikali isiingie katika uwekezaji mkubwa na hususan wa miundombinu kupitia PPP. Niseme tu kwamba kwa kweli hii ndiyo njia nzuri na njia mbadala ya kuhakikisha

kwamba nchi changa kama yetu basi itakuwa na uwezo wa kugharamia miradi mikubwa ya maendeleo na hasa ile ambayo inagharimu fedha nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba niseme mawili. Bahati mbaya ni kwamba *experience* ya nchi yetu katika *PPP* haikuwa nzuri sana. Mtakumbuka kwa mfano tulipopeleka utaratibu wa *PPP* kwenye sekta ya maji na kwenye sekta ya umeme matokeo yake yalikuwa si mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli pia ni kwamba *PPP* bado ni mfumo mgeni na unahitaji ujuzi ikiwa ni pamoja na *negotiation* katika kuingia ubia. Kwa hiyo tumeanza sasa, ndiyo maana tunacho kitengo pale ndani ya Wizara ya Fedha kwa ajili hii, ambacho bado kinajengwa. Tumeanza na miradi michache, ni matumaini yangu kwamba tutapiga hatua nzuri na kwa haraka kutumia mfumo huu kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nimalizie kwa kusema juu ya Ofisi ya Msajili wa Hazina. Ofisi ya Msajili wa Hazina ni chombo muhimu sana maana hili ndio hasa jicho la Serikali kwa ajili ya kumiliki mali ambazo tumewekeza kwenye taasisi mbalimbali za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba Ofisi hii imefanyiwa maboresho makubwa ikiwa ni pamoja na marekebisho ya sheria inayoongoza chombo hiki, lakini pia tumebadilisha uongozi ikiwa ni pamoja na kupata *Treasury Registrar* mpya ambaye ana uzoefu kutoka sekta binafsi lakini pia tunaendelea na jitihada za kuongezea taasisi hii watumishi wenye weledi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niseme tu kwamba uzuri katika kipindi kifupi ambacho mabadiliko haya yamefanyika tumeanza kuona matunda kwa maana ya kuongezeka kwa mapato, lakini *dividend* kutoka kwenye Mashirika haya. Kwa hiyo, nafikiri ni hatua nzuri, Waheshimiwa Wabunge naomba tuendeleo kuiunga mkono ofisi hii ili ifanye kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwezo wa Mashirika kama *TTCL* kwa nini nashindwa kuingia kwenye ushindani naomba niseme tu kwamba tumekuwa na changamoto toka tulipo anza kuingia kwenye ubinafsishaji na *management* ya *TTCL* kwa kweli bado ni mpya inaendelea kujipanga. Naamini ndani ya muda mfupi tutaona mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini haya Mashirika kwa kweli hatuwezi kusema tu kwamba kwa sababu kwa sasa hivi yanaonekana ni mzigo basi tuyatupe. Ni muhimu ni sisitize kwamba baadhi ya haya mashirika ikiwa ni pamoja na *TTCL* ni mashirika ambayo ni ya kimkakati, *very strategic* kwa ajili ya usalama wa nchi lakini pia kwa maana ya *contribution* yake kwenye uchumi

wa Taifa. Kwa hiyo, hatuwezi kuyatupa tu, ni lazima tuyafanyie kazi ili tuweze kuyafufua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa kumalizia nichukue nafasi hii kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri na ushauri wao. Kama nilivyosema naahidi kuwa ushauri mliotupatia tutaufanyia kazi na tutaazingatia vizuri kwa umakini katika utekelezaji wa bajeti hii na bajeti zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tutakapoingia kwenye hatua zinazofuata Waheshimiwa Wabunge waunge mkono hoja yangu ili tuweze kuendelea kutekeleza haya ambayo tumewaelezeni toka asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*  
*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono nitawahoji baadaye. Katibu!

## KAMATI YA MATUMIZI

### Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango

#### MATUMIZI YA KAWAIDA

Kif. 1001 - *Administration and HR Mgnt...* ...Sh. 7,551,731,000

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wajumbe ninayo orodha hapa ya wajumbe watakaosimama kwa ajili ya kutaka ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri kwenye kifungu hiki, tutaanza na Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na Mheshimiwa Waziri ninaposimama hapa ni kutafuta tu *clarification*, sidhani kama kutakuwepo na mambo makubwa. Naomba niseme kwamba hoja yangu Naibu Waziri ameijibu vizuri sana kwa sababu ilikuwa inahusu suala zima la kuhakikisha marekebisho ya Sheria ya Manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa wengi hapa wameshachangia na majibu kwa kweli yameridhisha kwa sababu hili ni suala la haraka na kama alivyokuwa amesema Mheshimiwa Chenge na wengine kwamba kama tungeona kwamba Serikali yetu hii ya hapa kazi tu ingechelewa, tulikuwa tayari kuja chini ya *program* ya kanuni ya 81 ambayo kimsingi tunaweza kuweka Muswada Binafsi au wa Kamati, lakini naona kwamba inatia moyo na hatutafika huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo naomba sana, kwa kuwa suala hili sasa umuhimu wake umetambuliwa na Serikali, Mheshimiwa Rais Magufuli alilizungumzia sana na wananchi wetu wengi wanategemea tulimalize ili kuondokana na huu udhaifu uliokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongezee hapo kumuuliza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri amejibu vizuri kuhusu tatizo la fedha kutotosha kwa ajili ya maendeleo, Waziri wa Fedha yeye ndiye anawawezesha Mawaziri wengine kufanya kazi zao; naomba ufafanuzi kuhusu mkakati mzima wa kutafuta fedha za kusukuma maendeleo yetu. Kutegemea mikopo peke yake, Mheshimiwa Waziri ni Mchumi mwenzangu, tunatoka Idara moja ya Chuo Kikuu unajua kabisa kwamba fedha ziko *equity*, kwa hiyo, unataka ufafanue mkakati wako wa *equity financing* kusudi madeni yasije yakatuzidi nguvu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tibaijuka muda wako umekwisha. Mheshimiwa Waziri mtoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Profesa Tibaijuka kwa kukubali majibu ya Serikali kuhusu suala la mabadiliko ya Sheria ya Ununuzi. Kwa kweli hili ni kero ya muda mrefu na kama nilivyosema ni ahadi ya Mheshimiwa Rais na kwa hiyo kama Serikali tumeliweka kwenye *fast track*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo hazitoshi, moja ya njia imekuwa ni mikopo, lakini tuna njia nyingine ambazo tumekuwa pia tunazitumia na Mheshimiwa Profesa anafahamu kwamba kwa ndani tunahangaika sana kupanua wigo wetu wa kodi na kutafuta vyanzo ambavyo ni tofauti na vile ambavyo vimezoeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa la kwanza ni kuhakikisha kwamba, mkakati wetu wa kujenga viwanda nchini unaongezeka maana huo hasa ndiyo wigo wetu wa kodi. Lazima tuhakikishe kwamba tunakuwa na viwanda vingi zaidi. Nilishasema katika vikao vya nyuma kwamba laiti kama tungekuwa na makampuni kama ishirini hivi ya size ya TBL hakika hizi kodi nyingine ndogondogo tungeachana nazo, hizi zingetusaia sana kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo; lakini tunaiangalia pia sekta isiyo rasmi kuona namna ambavyo nao tunaweza kuwaleta ndani ya uwigo wa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu analolisema ni muhimu sana, huko nje ziko *funds* mbalimbali ambazo tunaweza tuka-tape into na hili ni eneo ambalo tumejipanga sasa kwamba tunapoenda mbele *equity funds* mbalimbali tuweze kuzitumia ili tuweze kupata fedha zaidi kwa ajili ya maendeleo. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Profesa Tibaijuka kwamba

tunajua adha ya mikopo na changamoto zake, lakini mkakati wa Serikali ni ku-*diversify* vyanzo vyetu vya kupata fedha za kugharamia maendeleo.

**MWENYEKITI:** Profesa Anna Tibaijuka, nilidhani umeelewa tayari!

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri amejibu vizuri, lakini nimeona kwamba kuna umuhimu wa kuelewa zaidi na bila kuleta ukakasi mkubwa, kwamba suala la Dar es Salaam *Stock Exchange* na kazi ambayo inaweza ikapatikana katika kuisaidia Serikali, kutafuta fedha za miradi mikubwa ambayo ipo katika programu mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano tuna changamoto ya reli ya kati, ambayo Serikali imejipambanua imeweka trilioni moja, Mheshimiwa Waziri anajua kwamba anatafuta zaidi ya trilioni nane kama siyo tisa; Kwa hiyo, nafikiria kwamba nitalazimika kusema kwamba Mheshimiwa Waziri aniridhishe kabla sijachukua shilingi yake kwamba atatumiaje soko la ndani, hasa Dar es Salaam *Stock Exchange*, Watanzania sasa waanze kuchangia maendeleo ya nchi hii twende kwa kasi zaidi. Mheshimiwa Waziri anajua kwamba asilimia 70 ya fedha ziko mikononi mwa watu binafsi, kwa hiyo naomba kutoa hoja kwamba tujadili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tibaijuka, kwanza hoja yako ya pili ni tofauti na uliyokuwa umeitoa mwanzo na Kanuni zinataka uzungumzie jambo moja la kiseri. Kwa hivyo, kwa sababu ulielewa yale mazungumzo ya mwanzo ndiyo maana ukaleta hoja nyingine, basi tunaendelea na mchangiaji mwingine. Mheshimiwa Jitu V. Soni.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Tunataka kuiuliza Serikali, tunahitaji *commitment* ya uhakika, tuna taasisi nyingi za Serikali na Mashirika ya Umma ambayo yanafanya biashara zao na wanapeleka michango yao kwenye taasisi ambazo siyo za kiserikali, kwenye *private sector*, mfano mmoja pale Waziri alipoelezea kwamba tuitupe *TTCL*, sisi hatusemi tuitupe, tunasema *TTCL* ifufuliwe kwa nguvu zote na huhitaji kuweka mtaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika makampuni ambayo yanafanya biashara na Serikali, taasisi na mashirika ya umma yapo karibu 215, hapa yametajwa 15 tu ndiyo yanachangia *NIC*, yaani yanapeleka kazi *NIC*. Tunasema tuwe na mpango na tuwe na sheria kwamba angalau asilimia 80 au asilimia 100 kazi hizo zote ziende *NIC*, *TTCL*; kazi ambazo tunapeleka kwa mfano kutengeneza magari yaende *VETA* na kwingine kwenye taasisi za Serikali ili fedha ya Serikali irudi ndani na *private sector* huko nje, wakiona...



**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jitu Soni, nadhani muda wako umekwisha, kengele imegongwa hapa au Katibu ilikosewa kengele?

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Amegongewa.

**MWENYEKITI:** Imeshagonga kengele.

**MHE. JITU V. SONI:** Naomba kutoa hoja na kama nisipopata majibu ya kuridhisha basi tutazuia shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri mtoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA NA MPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Jitu Soni alinisikiliza vizuri, nimesema kwamba Serikali imekwishafanya uamuzi huo na yapo maelekezo kwamba kwa kadri inavyowezekana Serikali na Taasisi zake zitumie zaidi Mashirika haya kwenye huduma za bima, kadhalika kwa Shirika kama la *TTCL* kwa umuhimu na unyeti wake, kwa hiyo *commitment* ya Serikali ipo na naomba nimhakikishie kwamba *we are firm on this* na tutasimamia utekelezaji wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jitu sasa nadhani pia, ulitoa na ushauri na Mheshimiwa Waziri ameshakupa ahadi ya uhakika, bado unataka maelezo ya ziada?

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba tu kwamba mbali na hiyo ambayo tumetaja mbili ya mfano, lakini shughuli zile zingine ambazo zilikuwa kwa mfano kwenye *VETA* mikoa yote, kama kuna shughuli yoyote na kama kuna *VETA*, basi kazi angalau ipelekwe huko ili wanafunzi wetu wapate *experience*. Magereza na Taasisi zote zile ambazo ni za Serikali au vyyo vyetu ambavyo vinaweza kufanya hiyo kazi, basi kazi ya Serikali iende huko ili biashara ambayo wanapata *private sector* watateremsha bei na kutakuwa na *competition* ili na sisi Watanzania wa kawaida tunufaike na huduma hizo zingine. Kwa hiyo, naamini kabisa kutokana na kauli ya Waziri na siku zote anakuwa mkweli na kauli yake inakuwa imenyooka na naamini kwamba tutafanikiwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea, Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba Waziri anipe ufafanuzi kwenye eneo la Benki ya Kilimo. Serikali ina mpango gani wa kuongeza pesa kwenye benki hii ili iweze kupeleka matawi maeneo mbalimbali hasa Mikoa ya Pembezoni ambako ndiko

wakulima wako huko. Pesa niliyoiona hapa ni ndogo kwa maana ya bilioni 60, ni ndogo sana haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo kama maelezo ya Mheshimiwa Waziri hayataridhisha, basi nakusudia kuondoa shilingi kwenye eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri mtoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima namwomba sana Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani, asifikirie kabisa kuninyang'anya shilingi kwenye mshahara, maana haya yote niliyoyasema sasa itakuwa taabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu nimfahamishe Mheshimiwa Ngonyani kwamba, kwanza benki hii ni mpya, kwa hiyo kwa kweli kazi ya kujenga taasisi hii ndiyo kwanza imeanza na ni dhamira ya dhati kabisa ya Serikali kwamba tuendeleo kujenga mpaka tuhakikishe kwamba kilimo ambacho kwa muda mrefu tunalalamika kwamba uwekezaji katika kilimo ni mdogo hakuna mikopo iweze kufanyika hivyo. Maana kilimo ndiyo uti wa mgogo wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hatuwezi kutegemea fedha za bajeti peke yake, kwa hiyo, Mheshimiwa Ngonyani mkakati ambao tunao ni pamoja na kutumia sasa fedha ambazo tayari zimetengwa kwa ajili ya kuongeza mtaji wa Benki ya Kilimo ili ku-*leverage funds* kutoka kwenye taasisi zingine za kibenki kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu. Ni dhamira ya dhati kabisa ya Serikali kuhakikisha kwamba chombo hiki ambacho tumekianzisha kitakuwa ndiyo msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtakumbuka kwamba tulianza likiwa ni dirisha la kilimo pale *TIB* na baada ya kuona kwamba *demand* imeongezeka ndiyo tukasema hapana iwe benki inayojitegemea na iondoke Dar es Salaam. Kwa hiyo, polepole *in the medium term* hiyo ndiyo dhamira yetu, Mheshimiwa Ngonyani naomba kabisa usifikirie kutoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Nadhani Mheshimiwa Ngonyani ameelewa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Mheshimiwa Waziri, hayajaridhisha hata kidogo, kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri akumbuke kwamba nchi yetu tumejipanga kuhakikisha kwamba tunafikia uchumi wa kati. Ili tufikie uchumi wa kati ni wazi kwamba asilimia 75 ambayo tunaitegemea ili kuweza kuendesha viwanda vyetu viweze kufanya kazi vinatokana na malighafi

ambazo zinatokana na shughuli za kilimo, sasa endapo kama asilimia 75 ni ya wakulima ambao ndiyo watazalisha hizi malighafi, kama hatujawapelekea hii benki ikawa karibu yao ili waweze kukuza mitaji yao, kufanya shughuli zao za kilimo vizuri kuhakikisha kwamba tunapata malighafi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata mashaka kama kweli tunaweza tukafikia Mikoa ya Pembezoni ambayo ni Ruvuma, Rukwa, Katavi, Tabora na Mikoa yote ile ya pembezoni inayotegemea kilimo. Naomba kwenye eneo hili Waziri anieleze, ni kiasi gani cha pesa ambacho kinatarajiwa kuingizwa huku, sijaridhika na hii bilioni 60 ambayo itakuwa imetolewa toka mwaka jana na haitoshi..

**MWENYEKITI:** Muda tayari Mheshimiwa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nitoe shilingi ili na Waheshimiwa Wabunge wenzangu mniunge mkono tuweze kujadili, natoa hoja.

**MWENYEKITI:** Naomba uzime *microphone* yako. Hoja imeungwa mkono, naomba Waheshimiwa tukae nitachukua majina muda kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, tukumbushane hii Kanuni ya 103 kuhusu hoja ya kutoa shilingi, Fasili ya Tatu inasema hivi; madhumuni ya hoja na aina hiyo ni kumwezesha Mbunge aliyeitoa aweze kueleza kutoridhika kwake na utekelezaji wa jambo fulani mahsusi, ambalo dhahiri linahusika na kifungu hicho.

Mheshimiwa Waziri hapa ameeleza hii benki ni mpya, sasa kama tunashika shilingi kwa ajili ya hii benki ambayo tunahoji utekelezaji wake, tuangalie matakwa ya hii Kanuni. Hata hivyo hoja imeungwa mkono, kwa hivyo niwape fursa Wabunge watatu hivi tuijadili hiyo hoja, lakini tuzingatia hii Kanuni tunapotaka kutoa shilingi unazungumzia utekelezaji wa jambo fulani ambalo wewe hujaridhika nao.

Wajumbe waliokuwa wamesimama nilimwona Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Janeth Mbene, Mheshimiwa Albert Obama, halafu inabidi niendeleo kambi mbadala Mheshimiwa Anna Lupembe. Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, au ni nani niliyemwona?

**NDG. LAWRENCE MAKIGI-KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Shangazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Naomba niunge hoja ya Mheshimiwa Msongozi mkono, kwamba

pamoja na maelezo ya Waziri kwamba benki hii ni mpya, lakini tunataka kuona kwamba benki hii pamoja na benki nyinginezo zote zinaelekeza shughuli zao vijijini. Ni kweli kabisa nchi yetu inaelekea katika uchumi wa viwanda; viwanda hivi vinategemea mali ghafi za kilimo na kilimo chetu bado hakijawa cha kutengeneza tija ambayo inatokana na uzalishaji mkubwa kwenye mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri lazima tuhakikishe kwamba benki inatawanyika kwa haraka inavyowezekana, isiende kwa mwendo wa kinyonga kama ambavyo tumezoea kuona benki nyingine zinavyosuasua kuelekea vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janet Mbene.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani kuhusiana na Benki hii ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti hii benki imeanzishwa kwa madhumuni maalum. Madhumuni yake ni kuhakikisha kuwa inaharakisha kilimo cha kisasa chenye tija ili nchi hii ipate chakula cha kutosha lakini vilevile ipate malighafi kwa ajili ya viwanda kwa sababu sasa ndiyo tunajielekeza katika uchumi wa viwanda. Hatuwezi kusema tena tungoje mpaka lini tutumie huo mtaji mdogo tuliouweka kama *leverage*, tunajua kuwa sasa hivi mitaji ya kukopa nje siyo rahisi kiasi hicho lakini humu ndani tayari tunao uwezo wa kuzalisha au kutumia fedha zilizopo kuingiza katika benki hii kama mtaji wa kuanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunazungumzia fedha za Mfuko wa *Village Empowerment* milioni 50 kwa kila kijiji; hizo fedha kwa nini na zenyewe zisiingizwe katika benki hii zikawekewa *special window* zikatumika kwa ajili ya kukopesha wakulima, wavuvi na wafugaji. Hii ni njia mojawapo sasa tungependa Serikali ije na *commitment* badala ya kutuambia kwamba tuta-*leverage*, hicho ni kitu kiko jumla mno hakitupi sisi picha. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbene muda wako tayari. Mheshimiwa Obama!

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda tu nimwombe Mheshimiwa mwenzangu Ngonyani kwa wazo lake kwamba benki hii iweze kuongezewa mtaji, mawazo yangu yalikuwa yawe tofauti kidogo. Kwa kweli kama Mheshimiwa Waziri alivyosema benki hii bado ni mpya na imeanza 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia nzuri ya Serikali ambayo Serikali ilishatoa karibu bilioni 60; ni nia kubwa ambayo sasa hii benki bado kwanza inaweka

management yake iweze kukaa vizuri, bado ni changa na tumepata semina ya benki hii wiki iliyopita. Katika bilioni 60 walizonazo wameshakopesha bilioni 1.7, sasa kama Serikali ilishatoa bilioni 60 na wewe Mkurugenzi wa benki umeshatoa bilioni moja na milioni 700 tu, nahisi kwamba tuipe nafasi Serikali, hii benki yenyewe iendelee kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea kwamba benki hii katika bilioni 60 kama ingekuwa imeshatumia zaidi ya bilioni hata 15, ingekuwa imefanya vizuri, kwa hiyo nina mategemeo kwamba hiyo benki mtaji ilionao bado inatosha, kwa hiyo naunga hoja ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anna Lupembe.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Jacqueline kusema benki hii iweze kuongezewa pesa kwa sababu wananchi wetu wengi asilimia 80 ni wakulima na tunahitaji mazao mengi na vitu vingi tunahitaji kutoka kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutapenda sana sasa benki hii iweze kufanya kazi kwa haraka iweze kuwafikia wananchi vijijini na wananchi wetu wengi wa vijijini hawajui benki, sasa napo inatakiwa hii benki iweze kusambaa vijijini kwa haraka ili waweze kupata benki yao ili waweze kulima vizuri na kupata mazao ili tuweze kufaidika. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani malizia hoja, aah! Mheshimiwa Waziri una ufafanuzi?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tu kidogo kwamba nirudie tena dhamira ya Serikali kuongezea mtaji benki hii ni thabiti kabisa kinachogomba hapa ni kwa uharaka gani ambao tunaweza tukafanikisha dhamira hii ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichosema ni kwamba njia mojawapo ni kutumia hizi fedha ambazo tayari zimeshatolewa na Serikali kuweza kufanya leverage, kwa maana ya kuweza kupata taasisi nyingine ndani na nje ya nchi kuweza kupata mtaji zaidi kwa ajili ya benki hii na iweze kujitana kwenda vijijini kama wanavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala la kusema tutumie hizi milioni 50 za kila kijiji ambazo mwaka huu peke yake tumetenga bilioni 59 kwanza sijui kama *politically* kweli tunaweza tukarudi kwa wananchi na kuwaambia tumepeleka hizo bilioni 59 kwingine ambapo hatuna *guarantee* hapa kwamba kesho asubuhi zitakapohitajika kwenye vijiji basi tutaweza sasa kuzipeleka kule kwenye vijiji ipasavyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbua kwenye mjadala tayari hiyo bilioni 59 yenyewe anasema haitoshi iongezwe kwenda zaidi ya bilioni mia moja tisini. Kwa hiyo nadhani ni wazo zuri kulitafakari kwamba wapi tupate *funds* zaidi kuongeza uwezo wa TADB (Tanzania Agriculture Development Bank) kuweza kutufanyia kazi ambayo tumeiunda kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nazidi ku-*appeal* kwa Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani aniachie shilingi yangu nifanye kazi ya kusimamia chombo hiki kiweze kufanya kazi ya Watanzania ambayo wanaitarajia. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo mengi marefu na mazuri, namwonea huruma Mheshimiwa Waziri kwa sababu ni bajeti yake ya kwanza. Kwa hiyo, nairudisha shilingi lakini aangelie Ruvuma, kutoka Njombe kwenda Ruvuma pale katika mikoa ya mfano basi aingize na Ruvuma pale ni karibu tu pua na mdomo. Naomba kuwasilisha. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ameshakusikia. Mheshimiwa Maige.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nioneshe tutoridhika kwangu na hivyo kuomba maelezo ambayo ninaamini yataweza kuniridhisha kuhusu Fungu Na. 45 bajeti ya Ofisi ya Mkaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ezekiel Maige sasa hivi tupo; hatujafika kwenye hilo Fungu unalolisema nadhani tukifika hapo utasimama.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ni mmoja..

**MWENYEKITI:** Waziri ni mmoja lakini Fungu unalolisema kwa sababu tulilopo sasa hivi ni hili Fungu namba 50 na tunajadili kwenye mashahara wa Waziri.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo hivyo ninavyosema kwamba ninavyofahamu tunapojadili suala la kisera ambalo Waziri anawajibika tunashika na kuzungumzia kwenye mashahara wake itakapofika kwenye Fungu hilo ni ufafanuzi ambao hautakuwa kwenye dhana hii niliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kwa sababu ni Wizara moja...

**MWENYEKITI:** Basi naomba usilitaje Fungu wewe elezea basi hoja yako.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Concern hapa ni kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya ofisi hii. Ninavyofahamu ni kwamba kipindi hiki tulichonacho kila Mtanzania anafurahia na anapenda sana kuona uwajibikaji ukifanyika, ili kufanya kazi hii kwa ufanisi ni lazima jicho la Serikali liweze kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa. Kikatiba jicho la Serikali mamlaka yenye uwezo wa kukagua na kutoa taarifa kwamba hili eneo kumefanyika visivyo ni CAG. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa mfano kiasi cha fedha kilichokuwa kimetengwa mwaka jana kwa ajili ya ukaguzi wa Wizara ilikuwa ni kama bilioni nane, kimepunguzwa hadi bilioni nne, kiasi cha fedha kilichokuwa kimetengwa kwa ajili ya ukaguzi wa Halmashauri na Halmashauri zimeongezeka mwaka uliopita zilikuwa bilioni 17 sasa hivi zimeshukua hadi bilioni sita. Kwa vyovyote vile ukiangalia ofisi hii haitakuwa na uwezo wa kuweza kufanya kazi zake vizuri, kwa maana hiyo hatutaweza kufanya uwajibishaji unaotakiwa kwa watu ambao tunaamini hawasimamii vizuri ofisi hizi na fedha hizi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu lengo la Serikali kwa kweli ni kupeleka fedha nyingi iwezekanavyo kwa wananchi kupitia Halmashauri zetu, ili tuweze kusimamia na kukagua vizuri shughuli hizo nilifikiri ofisi hii ingeweza kuwa imetengewa fedha nyingi zaidi na wala siyo kupunguzwa. Sasa nataka tu kujua ofisi hii Waziri ana mpango gani au mkakati gani wa kuondoa wasiwasi huu. Niseme pia tu kwamba, nakusudia kuondoa shilingi endapo maelezo ya Waziri hayataridhisha. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri mtoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nisisitize kwa Mheshimiwa Ezekiel Maige kwamba kazi ya Waziri wa Fedha, kati ya Taasisi za Umma ambazo ni msingi mkubwa wa kazi yake ni ofisi hii ya Taifa ya Ukaguzi. Ofisi hii ndiyo inayonithibitishia kwamba fedha za wavuja jasho wa nchi hii inatumika ipasavyo, *there is value for money*. Kwa hiyo, kama ni mtu wa kuitetea ofisi hii, mtu wa kwanza kuitetea ofisi hii ni Waziri wa Fedha *unless* sijui kazi yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niseme kwamba namwomba sana Mheshimiwa Ezekiel Maige taasisi hii tutaiangalia kwa umakini kadri bajeti ya Serikali inavyotekelezwa na wakati wowote, hata kama itafika kabla ya mwezi December tunapo-review utekelezaji wa bajeti kama kutakuwa na kazi muhimu ya chombo hiki imekwama Wizara ya Fedha itachukua hatua mara moja za kurekebisha hali hiyo. (Makofi)



Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme kwamba ni muhimu vilevile dhamira ya Serikali ikaeleweka vizuri kwamba tumeamua kutokana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ilivyokuwa katika mwaka huu wa fedha unaoisha ambapo baadhi ya mafungu yamepata hela kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya uamuzi wa dhati kabisa kwamba tutenge fedha nyingi zaidi ya asilimia 40 ya bajeti yote iende kutekeleza miradi iliyokuwa imekwama na michache ambayo ni ya kimkakati kuli-move Taifa letu kwenda kuwa Taifa la Viwanda. Ndiyo dhamira iliyofanya baadhi ya fedha hasa kwa ajili ya matumizi ya kawaida zikawa chini. Hata hivyo, tunaelewa aina ya kazi ambazo CAG anafanya na ni *commitment* ya Serikali kwamba hatutaacha kazi yake ikwame hata kidogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ezekiel Maige.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nimemsikiliza Mheshimiwa Waziri na naamini Wabunge wenzangu tumemsikia. Anachokisema Mheshimiwa Waziri ni kwamba anajua kwamba ofisi haijatengewa fedha za kutosha na anasubiri ishindwe halafu ndiyo turekebishe. Nafikiri siyo vizuri, unajua gari ni bovu, unasema liingie barabarani kwanza, lisababishe ajali halafu ndiyo urekebishe! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ndiyo wakati wa bajeti na kuanzia kesho tutaanza majadiliano kabla ya bajeti kuu ya Serikali kupitishwa au kujadiliwa wiki ijayo na tuliweka hivyo ili kipindi hiki cha siku saba (7) mapendekezo haya tunayoyatoa yaweze kufanyiwa kazi na kufanyiwa marekebisho. Fedha zinazotakiwa hapa sidhani kama ni bilioni 20 kwa vyovyote vile haiwezi ikazidi bilioni 10 za nyongeza. Kwa hiyo, nafikiria kwamba kimsingi nimwombe Waziri akubali ili tusifike kwenye kuondoa shilingi ambayo ndiyo dhamira yangu, Waziri akubali aahidi kwamba katika hizi siku mbili anarekebisha, angalau kuwepo nyongeza ya fedha ili kufanya ofisi ifanye kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sijajua jibu la Waziri litakuwaje naomba ku-register nia yangu ya kutoa shilingi endapo hatatoa hiyo *commitment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maige nadhani hata wenzio sasa umewachanganya maana ukishaongea mara ya pili *either* unatoa shilingi ama unaiacha. Sasa wewe kama umeamua kutoa shilingi utuambie umetoa shilingi watu wachangie.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshatoa shilingi, labda ni suala tu la utaratibu. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Haya, Kambi mbadala Mheshimiwa Mwamoto, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Omari Kigua, Mheshimiwa Taska Mbogo na Mheshimiwa Elias Kwandikwa, wametoshia kwenye hoja ya Mheshimiwa Maige. Tutaanza na Mheshimiwa Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Maige. Ukiangalia kazi kubwa ambayo imefanyika ya ukusanyaji mapato kwenye Serikali yetu, ofisi ya CAG imefanya kazi kubwa sana na tunategemea wao ndiyo watakuwa wadhibiti wakubwa wa mapato kwa ukusanyaji. Sasa fedha hizo ambazo kweli zimetengwa zinakatisha tamaa. Kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Waziri wa Fedha bado ana nafasi kubwa ambayo anaweza kuifanya na tutamsaidia ili waongezewe fedha ili wafanye kazi kwa kujiamini na kukusanya mapato makubwa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Joseph Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkonohoja. Niseme kwamba katika eneo ambalo ni muhimu kwetu, katika Awamu hii ya Tano ambayo ina kauli mbiu ya 'Hapa Kazi Tu' ni hii ofisi ya CAG. Siyo siri wote mmeona ripoti ya CAG aliyotuletea ilivyosheheni mambo mazuri ambayo yanatakiwa kurekebisha. Sasa yeye amefika pale amekuta sahani ni tupu lakini anataka kufanya kazi na anaofanya nao kazi wanatakiwa kulipwa na pia anatakiwa kugharamiwa anapokwenda kila mahali, atatekeleza vipi kama hatapewa hela za kufanyia kazi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nisisitize hakuna ambavyo tutaondoka hivi bila kumwongezea hela huyu Mdhibiti Mkuu ili tuone kwamba kazi inafanyika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili niache tu na wengine weweze kuchangia nasisitiza na makofi haya..

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa Shally Rymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Omari Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Maige kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wote wanaamini kabisa kwamba suala la Serikali kupeleka asilimia 40 ya fedha za maendeleo imekuwa kama sherehe na kila mmoja amefurahia hilo. Hata hivyo, tunaamini wote kwamba jicho na mlinzi wa rasilimali za Serikali hii ni CAG. Sasa leo hii unapokuwa unamnyima fedha maana yake *performance audit* ya miradi ya Serikali ya maji na barabara yote haitaweza kufanywa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri yeye hatokuwa na wataalam wa kufuatilia mambo haya, mtu wa kutusaidia hili ni Mheshimiwa CAG, naomba tafadhali Mheshimiwa Waziri wa Fedha apeleke fedha kwa ajili ya CAG aweze kutufanyia kazi nzuri. Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza naomba kusema kwamba CAG hajatendewa haki. Kwa sababu unapofanya *audit* kwanza unakuwa na *audit scope* na kuna *audit procedures*. Kwa hiyo, kuna *time* tayari umeshazi-align pale, unajua watu wangu watakwenda vituo kadhaa, Halmashauri 181 watatumia muda kadhaa kwenye *areas* ambazo wale watu wamepangiwa. Kwa hii fedha ambayo imetengwa hapa hawata-meet target iliyopo. Kwa hiyo ni lazima Serikali iwaongezee fedha au la, Mheshimiwa Waziri atoe mwongozo kwamba, katikati ya kipindi fedha itapatikana wapi ili ofisi ya CAG iweze kufanya kazi. Kwa hiyo fedha haitoshi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kwandikwa.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Maige. Kwa kuwa, pia Mheshimiwa Waziri amezungumza kwenye hotuba yake kwamba anakubaliana na maazimio ya Kimataifa kama lile la Lima and Mexico Declaration ambalo kati ya mambo mengi linazungumza pia kuhusu *financial independence* ya CAG. Pia utakuja kuona *nature* ya kazi ya CAG ni kusafiri kwenda kufanya *audit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala la kupunguza kwa kufuata hiyo *percent* ni kuinyima kabisa zoezi la kazi nzima ya kwenda kufanya *audit*. Kwa hiyo, naunga mkono hoja kwamba suala hili lazima litazamwe, kiasi cha fedha kiongezwe vinginevyo labda Mheshimiwa Waziri akubali kwamba kazi haitafanyika. Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi au mapendekezo ya bajeti ya ofisi hii tuliyajadili kwa muda mrefu sana na Kamati ya Bajeti na nawashukuru sana Kamati ya Bajeti hatimaye walielewa changamoto ambazo tunakutana nazo. Kwa hiyo, niseme kwamba kwanza tulichowaomba ofisi hii ni kutambua kwamba bajeti ya Serikali ni *cash budget* siyo kwamba tuna fungu mahali limekaa Waziri wa Fedha nafungua natoa, ni lazima tukusanye kwanza tukishakusanya ndiyo tunaweza tukagawia Wizara na Idara mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ukomo tulionao ukiniambia leo niongeze bajeti ya CAG maana yake ni kwamba lazima nipunguze Fungu lingine. Kwa hiyo, nimefanya *commitment* hapa ya Serikali kwamba tunavyoendelea kutekeleza bajeti ya Serikali hapo ndiyo tutaona namna ambavyo tunaweza tukafanya. Kwa kawaida mwezi Disemba baada ya kutekeleza bajeti kwa miezi sita tunafanya *mid-year review* ambapo tunafanya *reallocations* na kuweza kupeleka fedha mahali ambapo tunaona kwamba kazi za msingi zimekwama. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kwa Serikali nzima ikiwemo Fungu hilo ambalo tunalijadili, tumesisitiza sana umuhimu wa kila Fungu kujiangalia kwa ndani kuangalia *efficiency gains* ambazo zinaweza zikafanyika. Mathalani kwa Fungu hili tulisisitiza sana kwanza waangalie posho ambazo zilikuwa zimewasilishwa hazina mchanganuo, vilevile tulisisitiza sana kwamba kuna tozo za ada za ukaguzi ambazo wanapata wanapokwenda ku-*audit* taasisi na mashirika mbalimbali. Pia kwa hali ilivyo tulishauri sana kwamba gharama za ujenzi wa ofisi kwa kila Mkoa ziangaliwe ili tuweze kuwa na utaratibu *sequencing* ambayo inaendana na upatikanaji wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nazidi kuomba tena Mheshimiwa Maige kwa *considerations* hizi na *commitment* ya Serikali kwamba tutaendelea ku-review utekelezaji na kadri makusanyo yanavyopatikana tuweze kuendelea kui-facilitate ofisi hii muhimu sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maige nadhani Mheshimiwa Waziri amejitahidi sana kueleza, nadhani Serikali nzima, ofisi zinaangalia namna ya kubana matumizi ili fedha zielekee kwenye fedha za maendeleo, malizia hoja yako.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na kwa kweli namshukuru pia hata Mheshimiwa Waziri. Kimsingi *commitment* ambayo nimeisikia na naikubali ni kwamba bajeti tutakayoipitisha ya CAG haitoshi, ni bajeti ambayo tunaamini itamfikisha mwezi Desemba na hivyo Waziri anaahidi kwamba mwezi wa Desemba kwenye *budget review* atafanya marekebisho. Kwa msingi huo, nakubaliana na hivyo naachia shilingi yake. Nashukuru. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maige japokuwa *Hansard* itarekodi kwamba, Waziri amesema CAG amalize hizo pesa by Disemba nadhani sicho Waziri alichosema, lakini nikushukuru kwa kurudisha shilingi. Waziri amesema katika utekelezaji wa shughuli za CAG akiona kuna mahali amekwama, basi atarudi kwa Waziri na watafanya utaratibu mzuri ili kazi ziendeele kufanyika. Mheshimiwa Leah Komanya.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kutoa hoja yangu. Hoja yangu ilikuwa sawa na hoja ya Mheshimiwa Maige kuhusu kutokuridhika na utekelezaji katika Ofisi ya CAG. Pamoja na majibu yaliyotolewa na Serikali naomba tu niweze kusisitiza kidogo. Kama CAG kwa mwaka wa fedha unaoanza hatapatiwa fedha za kutosha na itabaki bajeti hii atashindwa kukagua baadhi ya mafungu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Komanya samahani kidogo, kwa sababu hiyo hoja ndiyo tumetoka kuisemea sasa hivi au wewe unataka ushike shilingi mpaka mwisho?

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Hapana, naomba kusisitiza kidogo tu.

**MWENYEKITI:** Kwa sababu kama hilo siyo lengo, itakuwa ni hiyo ambayo imetolewa maelezo sasa hivi.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kusisitiza kidogo.

**MWENYEKITI:** Hakuna kusisitiza, unaelezea na wewe kutokuridhika kwako. Kwa hiyo, maana yake na wewe uanze upya.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitaridhika nakusudia kushika shilingi.

**MWENYEKITI:** Hauwezi kushika shilingi kwenye hoja ile ile, kwa sababu hakuna kitu kipyaa tutakachokisikia.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeridhika na majibu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Simba.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa muda huu. Nami nakusudia kumuuliza Mheshimiwa Waziri anifahamishe kuna tatizo gani kwenye mabenki yetu yanatoza *interest rate* kubwa wakati wa

kukopa ikilinganishwa na *rate* ambayo wanatoa kwa wale ambao wana-*deposit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo linawatia umaskini Watanzania. Mtanzania mara atakapokopa tu ujue ameshajitumbukiza kwenye umaskini. Tunasema tunaenda kwenye uchumi wa viwanda, kwa hali hiyo, kwa *interest rate* kubwa namna hiyo! Mheshimiwa Waziri sijui *Central Bank* inafanya kazi gani katika kusaidia jambo hili, kwa sababu imekuwa mbaya sana sasa mpaka kwenye *Community Bank* ambazo tunazianzisha wenyewe, unakuta *interest rate* inakuwa kubwa kwa visingizio ambavyo wanasema wanaagizwa, sijui wanaagizwa na nani! Nitashukuru kama Mheshimiwa Waziri atalielezea jambo hili na kama nikiridhika nitamuacha, kama sivyo itabidi nichukue shilingi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtoa hoja!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Mheshimiwa Sophia Simba kwa hoja yake aliyoisema ya riba kuwa kubwa, lakini naomba nimwambie Mheshimiwa Sophia Simba kwamba tangu mwaka 1991 tumeingia katika soko huria katika mabenki, Serikali ilijitoa moja kwa moja katika kupanga bei za benki zetu na huduma zao. Kwa hiyo, tukisema sasa turudi na kuanza kuzipangia itakuwa ni ngumu sana kwa sababu tayari tumeingia katika soko huria na sasa tunarejea tena nyuma, naona kuna ugumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *Community Banks* kama alivyosema nazo zinatoza riba kubwa, tunajua kwa nini *Community Bank* zinaanzishwa, zinapokuwa zimeanzishwa na zinapokuwa zipo kwenye soko huria na wao wanajikuta wanajisahau katika lengo la kwa nini benki za kijamii zimeanzishwa wanaanza na wao kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimwombe Mheshimiwa Sophia Simba kwamba tunafahamu tatizo hilo lipo, ni kubwa lakini Serikali ilishatoa mikono yake moja kwa moja katika hilo, imebaki tu kutengeneza mazingira mazuri ili benki zingine za kijamii, benki za kibiashara ziweze kuanzishwa ili sasa *competition* ikiwa kubwa basi riba zitaweza kushuka chini. Kwa mpango huo namwomba Mheshimiwa Sophia Simba asishike shilingi ya Mheshimiwa Waziri wangu, kwa sababu zipo kwa sheria tuliyoipitisha humu ndani ya Bunge tukaingia katika soko hilo. Naomba sana Mheshimiwa Sophia Simba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika na majibu hayo. Najua Serikali ina *role to play* katika kuhakikisha uchumi wa nchi hii. Kwa hali ilivyo na hizi *interest rate* hatuwezi tukawaachia! Hivi kweli tumesema tume-*liberalised* halafu tunawaachia inzi anaingia, nyuki anaingia, ndiyo hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja ya kutoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Naibu Waziri Joelson Mpina, Mheshimiwa Allan Kiula, Mheshimiwa Keissy naona unatajwa na wenzako kule nyuma, Mheshimiwa Musukuma na Mheshimiwa Massay. Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namuunga mkono Mheshimiwa Sophia Simba. Serikali leo inasema na inataka Wabunge tuamini, kwa sababu ya soko huria wamejitoe. Nataka Bunge lako leo liambiwe hivi hati fungani Serikali wana-*offer* kwa asilimia ngapi? Maana kinachopima kuhusu *interest* unaanza na hati fungani, ninyi hati fungani zetu zaidi ya *digit* mbili, sasa mnataka benki iende chini! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kama mnataka mmejitoa hati fungani wekeni zero na *interest* zitashuka, lakini mkituambia mmejitoa *role* ya *ku-manage economy* ni ya nani sasa? Na leo tunasema watu wanaweka fedha nje ya Tanzania ni kwa sababu hii, kwa sababu wakiweka pesa kule nje wanachukua *interest* wanakopa kwa *interest* ndogo ndiyo maana watu wote wanapeleka pesa nje, kwa sababu *interest* za hapa huwezi kufanya biashara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi viwanda tunavyoambiwa hapa, kwa *interest* hizi hakuna atakayejenga kiwanda Tanzania, asilimia 21, asilimia 18 inawezekanaje! Naomba tuambiwe tu jibu la ukweli, habari kwamba ni soko huria siyo kweli. Ahsante. (Makofi)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningemshawishi Mama yangu Sophia Simba amuachie Waziri hii shilingi kwa sababu zifuatazo:-

Kutokana na sababu ambazo Serikali imezichukua mpaka sasa hivi za kuhakikisha kwamba riba zinashuka moja ni hatua za Serikali za kuhakikisha mpango wa *sovereign rating* unakamilika. Pili, ni kuhakikisha madeni ya wazabuni yanalipwa. Tatu, ni kuhakikisha kwamba, Serikali inaondoa fedha katika mabenki. Nne, ni kuhakikisha kwamba, tunaanzisha benki zetu ambazo kwa vyovyote vile zitatoa riba ya chini kwa maana ya *TIB* pamoja na *TADB*.



Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hati fungani Waziri hapa alizungumza na Mheshimiwa Rais jana alisisitiza kwamba suala sasa la Serikali kukopa zaidi kwenye soko la ndani itaendelea kupunguza huo taratibu. Tukishapunguza huo utaratibu *automatic* tutakuwa tumepunguza riba ambazo ziko kwenye benki sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuangalia hizi hatua ambazo Serikali imezichukua nina uhakika, najua kwamba ni mambo ambayo hayawezi yakatokea siku moja, kwa sababu unapozunguza *intetrest rate* unazungumza uchumi mzima wa nchi na unapozungumza uchumi mzima wa nchi maana yake ni kwamba matokeo yake hayawezi kuonekana kwa siku moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hizi hatua tunazozichukua kwa mfano, ilikuwa inaongeza *risk* kubwa kwenye mabanki pale madeni yetu ya Wazabuni yalipokuwa makubwa na Wazabuni wetu wengi wakaonekana kwamba hawana uwezo wa kulipa benki na kuongeza *risk* kwenye benki. Kwa hiyo, haya tunayoyafanya yote yatapunguza sana riba zinazokuja na hili tatizo litaondoka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina ahsante. Mheshimiwa Allan Kiula.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi. Nami naungana na mtoa hoja aliyetoa shilingi, kwa sababu yako mambo ambayo inabidi tuyaangalie kwa jicho la karibu. Kwanza kauli ya Waziri ya kusema tangu mwaka 1991 tuingie soko huria Serikali kujitoa ni jambo la hatari. Ndiyo maana nikitoa mfano tofauti tumesema Sheria ya Manunuzi irudishwe tumeona kulikuwa na makosa, kwa hiyo kama kuna makosa lazima tuyarekebishe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuangalie *cost* kila benki na *cost structure* zake lakini kwa nini hizo *interest rate* zinakwenda zinarandana, ina maana hawa wana-*collude* na kama wana-*collude* suala hili haliwezi kuachiwa. Mheshimiwa Serukamba amesema kama hizi *interest rate* zitaenda kwa asilimia 18, asilimia 22, *refreshing rate* asilimia sita, ni biashara gani itakayofanyika hapa iweze kulipa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo hili linatakiwa liangaliwe kwa makini na litolewe uamuzi. Kwa hiyo naendelea kumshauri aliyeshika shilingi, ashike shilingi mpaka mwisho.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siungi hoja kwa sababu benki ni biashara. Watanzania karibu asilimia zaidi ya 50, kama wanakopa asilimia 100, asilimia 50 hawalipi, wanalipa *half*. Kwa hiyo, benki zetu tukipunguza riba walipaji wengi siyo waaminifu na ndiyo unaona nyumba zinapigwa mnada, benki zinapata hasara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukue mfano Benki ya Wanawake ndiyo yenye riba kubwa kuliko benki zote Tanzania. Kwa hiyo, namuunga mkono Waziri, naunga mkono benki tuendele kupambana na riba hiyo kwa sababu walipaji wengi siyo waaminifu. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami namuunga mkono Mheshimiwa Waziri kwa hoja yake na namuomba Mama yetu Sophia Simba aiachie hii shilingi kwa sababu kwanza Waziri huyu ni mpya na ana mawazo mazuri kabisa ameeleza hapa, wengine wamekuwemo kwenye Serikali hii miaka 20 mpaka tukafika kwenye hizi riba kubwa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kama alivyosema Mheshimiwa Keissy kwamba wakopaji wengi wa Tanzania siyo walipaji na mabenki haya hayatulazimishi hizo riba ni wewe mwenyewe na njaa zako unakubaliana unaenda unakopa kwa ile riba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nilichokuwa naomba, tumrudishie shilingi Mheshimiwa Waziri tupambane kwa sababu pia wakopaji wa Tanzania siyo walipaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nimuunge mkono Waziri, nasema haya kwa sababu moja tu, kwanza..

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, naomba usubiri kidogo. Kwa mujibu wa Kanuni ya 104 (1) naongeza nusu saa. Mheshimiwa Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na kwamba mimi ni Kambi Mbadala na nimeisikia sana *concern* ya Serikali na kwa sababu najua kabisa kwamba mabenki yamekuwa mara nyingi yakipewa pesa na Serikali na Serikali yenyewe wakati mwingine inakwenda benki kukopa, wakati huo mabenki yanaipiga Serikali kwa tozo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri sasa nimwombe Mama yangu Sophia akubali tu kurudisha ile shilingi ili tumuache sasa huyu ndugu yetu mzee Mpango kwa sababu ni baba aongeze mipango zaidi ili Serikali sasa ifike mahali iwe na nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, thamani ya shilingi yetu irudi pale pale, Watanzania maskini Mama yangu tunaumia kule nyumbani, hebu tuipe Serikali ya mwaka huu ya Awamu ya Tano iwe na nguvu, shilingi ipate uwezo wake.

Mama naomba nikuombe sana rudisha shilingi ili baba yetu apate kasi zaidi. (Makofi)

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikiri tu kwamba, ni kweli tatizo la riba kubwa ni tatizo kubwa ambalo halileti matumaini na hasa kwa wananchi wetu ambao ni maskini ambao wanatafuta mikopo midogo ili waweze kuwekeza na kuendeleza maisha yao. Kama mnakumbuka Mheshimiwa Rais Kikwete, Rais mstaafu alieleza bayana kwamba, benki siyo rafiki wa maskini, kwa hiyo ni *real problem*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nieleze kwamba, viwango vya riba vina sababu zake, kwa hiyo moja ya vitu ambavyo vinafikiriwa wakati wa kupanga viwango vya riba, limeshasemwa humu ndani ni gharama za uendeshaji katika mabanki, hata kutoa huo mkopo wenyewe maana yake una Ofisa wa Benki, una makaratasi na kadhalika ambayo yanachangia kwa sababu ni biashara ambayo lazima upate faida kama ilivyo biashara yoyote lazima uangalie gharama zako ili uweze kuona nitaweka bei gani ambaye itanipatia faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, kuna taarifa za wateja ndiyo maana kwa mfano, Bakhresa akienda kukopa mali zake nyingi zinafahamika, *balance sheet* yake iko vizuri, *audited*, lakini akienda Ndugu Mpango kwa mfano, hana *balance sheet* wala hana chochote ambacho anaonesha kwamba, hiyo shughuli yake inayomuingizia kipato kumwezesha kulipa basi iko pale, kwa hiyo benki zinaangalia pia taarifa kama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yameshasemwa pia hapa siyo mara moja wala mbili mtu anakopa halafu anatafuta janja ya kupotea. Sasa benki haziwezi kukaa zikasema basi hii ni fedha imepotea kuna utaratibu, lakini yote haya yanakuwa *considered* katika ku-*set interest rate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna *risk* mbalimbali kwa vile benki zenyewe zinakopa pia baadhi ya mitaji, kwa hiyo, ni lazima wai-*factor* hiyo katika ku-*determine* ile *interest rate* na faida yenyewe wanayoweza kukadiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, hili ni jambo ambalo linagusa wananchi wetu wengi na ni wajibu wa Serikali na Wizara yangu kuliangalia kwa umakini zaidi ili tuweze kuona ni hatua gani za ziada ambazo Serikali inaweza kuendelea kuchukua ili kusaidia ku-*influence*, siyo kuziamua *administratively interest rate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukachukua hatua ambazo zina-*influence interest rate* kuteremka ambazo nilieleza, tulishachukua hatua kuagiza fedha za umma ambazo ziko kwenye taasisi mbalimbali ambazo mabanki ya biashara walikuwa wanazitumia kwenda ku-*influence* soko la hati fungani sasa

ziende Benki Kuu ili sasa tuwe na *level plain field* na benki zingine nazo ziende kule kwa wananchi na *interest rate* zitateremka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali kupitia Benki Kuu ilianzisha utaratibu wa kuwa *credit reference bureau* ambayo inaweka taarifa juu ya wakopaji ili kuweza kuwapa *comfort* benki kwamba kwa mfano, Ndugu Philip Mpango anayeenda kukopa anajulikana ana kitu gani na kwamba *in case* hawezi kurudisha mkopo hiki ndicho kinaweza kufanyika. Tunatambua kwamba kunaweza kuwa na michezo ya benki ku-*collude* lakini hii ndiyo kazi ya Benki Kuu ku-*regulate* biashara na benki na kuziangalia siku kwa siku zinavyofanya biashara zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo Serikali ina *role* na tunavyokwenda mbele namuomba Mheshimiwa Sophia Simba atupatie nafasi ya kuliangalia suala hili, tunalifanyia kazi kwa uzito wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Simba, naona Serikali inasema inalifanyia kazi.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo Serikali kweli inasema inalifanyia kazi, wengine wanasema Serikali ni mpya. Mimi najua Serikali hii ni mpya Uongozi lakini Serikali ya Chama cha Mapinduzi inaendelea, kwa hiyo haijaja Serikali ya Chama kingine, ni Serikali yetu hii tunaijua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea sana Waziri atetee hili jambo, atuambie watafanya nini, pia nadhani wanaweza wakaanza kwenye hati fungani, wangeanza wao wenyewe kupunguza hati fungani, naamini zingeshuka na huko kwenye benki pia zingeshuka na hivyo kusaidia wananchi kupata *interest rate* ndogo na kukuza uchumi zaidi, kwa sababu wanachokipata siyo kikubwa sana ukilinganisha kama wananchi wengi wangechukua mikopo *at low interest* wa-*stimulate* uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado nashikilia shilingi yangu aweke *commitment* kwa hayo ambayo anayasema watayafanya ili ku-*regulate* hizi benki. Bado siamini kwamba tumeziacha ni sawa, umeajiri mfanyakazi nyumbani, unasema nimeshamruhusu anafanya kazi wale watoto wako huwashughulikii mwenyewe. Ninyi ndiyo baba zile benki zinapata leseni kutoka Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo bado nashikilia shilingi yangu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wajumbe nitawahoji.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kupata ufafanuzi kwa hoja yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu kwanza kabisa inahusiana na suala la VICOBA. Kwanza nimpongeze Mbunge mwenzetu ambaye alianzisha VICOBA vikaenea karibu nchi nzima Devatha Likokola. Kwa sasa VICOBA vimekuwa ndiyo mkombozi hasa kwa wanawake wa vijijini na wa mjini. Hivi VICOBA kwa kweli vimetusaidia hata katika kupata mikopo midogo midogo ambayo imekuwa ikisaidia uchumi wa mwanamke na uchumi kwa ujumla ambao umekuwa ukisaidia sana katika vijiji na mikoa yetu. Mpaka leo hii haijatambulika kisheria na masharti ya mikopo kila VICOBA imekuwa tu ikijiwekea chenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi kirefu sana Serikali imekuwa ikiahidi kuleta Muswada wa kisheria itakaosimamia shughuli za *microfinance* pamoja na hivi VICOBA. Sasa nilikuwa naomba....

**MWENYEKITI:** Malizia Mheshimiwa Kabati kengele imeshagonga.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Nauliza ni lini sasa huu Muswada utaletwa hapa Bungeni ili tuweze kuupitisha ili VICOBA viweze kujulikana kisheria vifanye kazi vizuri zaidi? (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mtoa hoja naona habari imekuja kwenye lini, nadhani kimsingi anataka kujua hiyo habari ya VICOBA kwa nini haijashughulikiwa mpaka sasa.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mheshimiwa Ritta Kabati kwa kuleta hii hoja ya VICOBA. Serikali tunafahamu hii ni taasisi muhimu sana kwa ajili ya uchumi wa Taifa letu na hasa akinamama. Siyo kwamba Serikali tumekaa kimya kwamba sheria hii haijaandaliwa, sheria tayari iko kwenye mchakato ambao ni Sheria ya *Microfinance Act* ambayo tuna uhakika mwaka huu 2016 itakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tayari sera ya huduma ndogo za fedha ya mwaka 2016 iko katika hatua za mwisho kabisa. Mwezi Februari, 2016 tayari ilizinduliwa pale Benki Kuu tuna uhakika sasa, naomba nimwambie siyo Bunge hili la Bajeti, Bunge lijalo, *Microfinance Act* tutaileta ili iweze kupitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali na kumshukuru Waziri kwa majibu yake. Naamini kabisa sheria hii itakapoletwa, sasa ujasiriamali utakua na tuna imani kwamba wajasiriamali hasa wanawake sasa nasi tutachangia pato kubwa na tutalipa kodi kama ambavyo inatakiwa. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ritta Kabati.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.1002- Finance and Accounts.....Sh. 880,288,000/=

Kif.1003- Policy and Planning.....Sh. 31,566,272,000/=

Kif.1004- Legal Service.....Sh.1,095,452,000/=

Kif.1005- Gvt. Comm. Unit.....Sh. 404,592,000/=

Kif.1006- Internal Audit Unit.....Sh. 519,791,000/=

Kif.1007- MCC Tanzania.....Sh. 500,000,000/=

Kif.1008- Procurement Mgt. Unit.....Sh. 707,652,000/=

Kif.1010- Information & Comm. Tech.....Sh. 930,720,000/=

Kif.3001-Internal Auditor General.....Sh. 1,906,204,000/=

Kif.5001- Gvt. Asset Mgt. Div.....Sh. 2,646,416,000/=

Kif.6001- Financial Mgt. Info. Syst. Div.....Sh. 2,007,760,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 07- Msajili wa Hazina**

Kif.1001-Admn. and HR Mgt.....Sh. 3,376,629,000/=

Kif.1002- Finance and Accounts.....Sh. 386,336,000/=

Kif.1003- Planning Unit.....Sh. 358,315,000/=

Kif.1004- Legal Services Unit.....Sh. 336,117,000/=

Kif.1005- Procurement Mgt. Unit.....Sh. 227,090,000/=

Kif.1006- Information & Comm. Tech.....Sh.409,265,000/=

Kif.1007- Info., Edu. & Comm. unit.....Sh. 232,226,000/=

Kif.1008- Internal Audit unit.....Sh.269,697,000/=

Kif. 2001- Public Investment Mgt Div.....Sh.152,868,929,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbogo unajua hiki kifungu tumeshahoji watu wamesema ndiyo, naomba ukumbuke kusimama haraka.

Kif.3001- *Privatisation and Monitoring*.....Sh. 863,316,000/=

Kif.4001- *Mgt. Service Division*.....Sh. 853,080,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)

### **Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha**

Kif. 1001 - *Administration & HR Mgt* .....Sh. 1,163,238,000/=

Kif. 1002 - *Internal Audit unit*.....Sh. 39,300,000/=

Kif. 2001 - *Technical Department*.....Sh. 87,600,000/=

Kif. 2002 - *Zanzibar Office*.....Sh. 84,132,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)

### **Fungu 13 – Kitengo cha Udhhibiti wa Fedha Haramu**

Kif. 1001 - *Admn. & HR. Mgt. Unit*..... Sh. 1,019,730,000/=

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo *subvote1001* katika 220900 - *Training Foreign*. Mwaka huu imewekewa fedha nyingi tofauti na miaka mingine iliyopita kwa nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtoa hoja umekiona hicho kifungu kidogo anachokiulizia?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kitengo hiki ni muhimu sana kikatusaidia kwenye maeneo ambayo bado utalaam wetu siyo mkubwa sana na inahitaji pia *interaction* na taasisi zingine ambazo zinafanya kama hizi katika nchi nyingine ambazo zina uzoefu. Kwa hiyo, ndiyo sababu ili kukiimarisha na tuweze kuendelea kupambana zaidi na ugaidi lakini pia kupata elimu kwa ajili ya fedha hizi za miamala ambazo ni haramu, ndiyo maana tumeongeza fedha hizi pamoja na ongezeko la idadi ya Watumishi kuweza kuhangaika na eneo hili ambalo kwa kweli bado ujuzi unahitajika sana, ndiyo sababu ya kukiongezea fedha.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif.1002- *Finance & Accounts unit*.....Sh. 30,819,000/=

Kif.1003- *Internal Audit Unit*.....Sh.5,250,000/=

Kif.1004- *Monitoring unit*.....Sh.89,240,000/=

Kif.1005- *Inspection unit*.....Sh.252,692,000/=

Kif.1006- *Procurement Mgt. unit*.....Sh.11,800,000/=



Kif.1007- Legal Service Unit.....Sh.80,870,000/=

Kif.1008- Mgt. Info. System Unit.....Sh.112,680,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)

### **Fungu 21 - Hazina**

Kif.1002- Finance and Accounts.....Sh. 721,862,000/=

Kif.1009- Public Procurement Policy Unit.....Sh. 867,880,000/=

Kif. 2001- Gvt. Budget division.....Sh.160,586,494,510/=

Kif. 2002- Policy Analysis division.....Sh.197,651,787,000/=

Kif. 4001- External Finance division.....Sh.49,599,507,000/=

Kif. 4002- Public Private Partnership Unit.....Sh.549,450,000/=

Kif.7001-Poverty Eradication & Empmt. ....Sh.1,302,260,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)

### **Fungu 22 - Deni la Taifa**

Kif.1001- Admn. and HR Mgt.....Sh. 8,009,341,187,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)

### **Fungu 23 -Mhasibu Mkuu wa Serikali**

Kif. 3001- Public Debt Mgt.....Sh. 97,650,000/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wajumbe kabla sijawahoji, ukurasa wa 86 lakini hizi tarakimu zimebadilishwa kidogo na taarifa ambayo meza imeletewa *andendum*. Kwa hiyo vifungu hivi tutakuwa tukisoma kwa kadri ilivyobadilishwa, kwa hiyo kuna mahali ambapo kutakuwa na tofauti kidogo. Tunaendelea katibu.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif.3002- Expenditure Mgt.....Sh. 5,202,900,000/=

Kif.3003- Financial Mgt.....Sh. 30,854,203,000/=

Kif.3004- Financial System.....Sh. 5,949,642,000/=

Kif.3005- Sub Treasury Arusha.....Sh 91,310,000/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wajumbe, inabidi tuitikie kwa sababu lazima tupitishwe hivi vifungu sasa inapofika kifungu hata mtu mmoja hasemi inakuwa taabu kidogo!

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3006- Sub Treasury Pwani.....	Sh. 84,180,000/=
Kif. 3007- Sub Treasury Dodoma.....	Sh. 239,620,000/=
Kif. 3008- Sub Treasury Iringa.....	Sh.107,755,000/=
Kif. 3009- Sub Treasury Kagera.....	Sh.104,395,000/=
Kif. 3010- Sub Treasury Kigoma.....	Sh.107,087,000/=
Kif. 3011- Sub Treasury Kilimanjaro.....	Sh.104,960,000/=
Kif. 3012- Sub Treasury Lindi.....	Sh.107,860,000/=
Kif. 3013- Sub Treasury Mara.....	Sh.154,450,000/=
Kif. 3014- Sub Treasury Mbeya.....	Sh. 202,360,000/=
Kif. 3015 - Sub Treasury Morogoro.....	Sh. 147,085,000/=
Kif. 3016 - Sub Treasury Mtwara.....	Sh. 102,260,000/=
Kif. 3017 - Sub Treasury Mwanza.....	Sh. 120,035,000/=
Kif. 3018 - Sub Treasury Rukwa .....	Sh. 109,435,000/=
Kif. 3019 - Sub Treasury Ruvuma .....	Sh. 114,725,000/=
Kif. 3020 - Sub Treasury Shinyanga.....	Sh. 93,730,000/=
Kif. 3021 - Sub Treasury Singida .....	Sh. 97,335,000/=
Kif. 3022 - Sub Treasury Tabora.....	Sh. 109,945,000/=
Kif. 3023 - Sub Treasury Tanga .....	Sh 117,310,000/=
Kif. 3024 - Sub Treasury Manyara .....	Sh 124,245,000/=
Kif. 3025 - Sub Treasury Njombe .....	Sh 139,810,000/=
Kif. 3026 - Sub Treasury Geita .....	Sh 119,040,000/=
Kif. 3027 - Sub Treasury Katavi .....	Sh. 108,485,000/=
Kif. 3028 - Sub Treasury Simiyu.....	Sh. 150,560,000/=
Kif. 4001 - Local Govt. Finances .....	Sh. 209,060,000/=
Kif. 7001 - Pension and Gratuity .....	Sh. 314,435,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaingia kwenye utaratibu wa kupitisha mafungu yote kwa sababu muda wetu umebaki dakika kumi.

#### **Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama**

Kif. 2002 Court of Appeal DSM.....	Sh. 84,865,309,000/=
------------------------------------	----------------------

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya*

*Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 42 – Mfuko wa Bunge**

Kif. 1001 - Admn. & HR Mgt.....	Sh. 7,019,376,000/=
Kif. 1002 - Library & Research Department....	Sh. 548,888,000/=
Kif. 1003 - Information Comm.& Tech. ....	Sh. 8,436,364,000/=
Kif. 2001 - Budget Department.....	Sh. 1,675,472,000/=
Kif. 2002 - Table Office Department .....	Sh. 64,951,445,000/=
Kif. 2003 - Parl. Committees Dep.....	Sh. 6,031,376,000/=
Kif. 2004 - Hansard Department .....	Sh. 828,164,000/=
Kif. 2005 - Legal Counsel Department....	Sh. 74,219,089,000/=
Kif. 3001 - Private Office of the Speaker.....	Sh. 595,984,000/=
Kif. 3002 - Private Office Deputy Speaker.....	Sh. 300,208,000/=
Kif. 3003 - Office Leader of Opposition .....	Sh. 376,184,000/=
Kif. 3004 - Private Office of The Clerk .....	Sh. 1,487,568,000/=
Kif. 3005 - Finance and Account Dep.....	Sh. 650,280,000/=
Kif. 3006 - IR & Protocol Department .....	Sh. 2,444,844,000/=
Kif. 3007 - Info. Edu.& Comm. ....	Sh. 267,580,000/=
Kif. 3008 - Internal Audit Unit .....	Sh. 223,212,000/=
Kif. 3009 - Procurement Mgt. Unit.....	Sh. 479,404,000/=
Kif. 3010 - Defense and Security Unit .....	Sh. 237,948,000/=
Kif. 3011 - Estate Mgt Unit .....	Sh. 2,075,156,000/=
Kif. 3012 - Zanzibar Directorate .....	Sh. 272,296,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

Kif. 1001 - Admn & HR Mgt. Div.....	Sh. 6,900,606,000/=
Kif. 1002 - Finance and accounts Unit .....	Sh. 1,050,884,000/=
Kif. 1003 - Internal Audit Unit .....	Sh. 701,345,000/=
Kif. 1004 - Ministerial Audit Division .....	Sh. 4,633,251,500/=
Kif. 1005 - Local Govt. Authorities Div.....	Sh. 6,581,292,000/=
Kif. 1006 - Performance Audits Div.....	Sh. 1,735,655,360/=
Kif. 1007 - National Account Divison .....	Sh. 3,152,782,000/=
Kif. 1008 - Tech. Support Service Unit .....	Sh. 1,194,861,000/=
Kif. 1009 - Public Authorities Audit Div.....	Sh. 1,520,008,000/=
Kif. 1010 - Plan., Monitoring & Evalu.Div.....	Sh.1,065,041,000/=
Kif. 1011 - Procurement Mgt. unit .....	Sh. 595,240,000/=
Kif. 1012 - Info. & Comm. Tech. Unit.....	Sh. 1,445,801,600/=
Kif. 1013 - Forensic Audit Unit .....	Sh. 536,112,940/=
Kif. 1014 - Quality Assurance Unit .....	Sh. 474,169,000/=

Kif. 1015 - Govt. Comm. Unit.....Sh. 245,156,200/=

Kif. 1016 - Risk Mgt. & Compliance Unit ..... Sh. 88,750,000/=

Kif. 1017 - Legal Service Unit.....Sh. 192,560,000/=

Kif. 1018 - Parliamentary Coordination Unit...Sh. 259,580,333/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 66 – Tume ya Mipango**

Kif. 1001 - Admn.& HR Mgt..... Sh. 1,141,604,000/=

Kif. 1002 - Finance and Accounts ..... Sh. 128,172,000/=

Kif. 1003 - Planning and Monitoring Div..... Sh. 127,800,000/=

Kif. 1004 - Gvt. Comm. Unit .....Sh. 101,192,000/=

Kif. 1005 - Internal Audit Unit..... Sh. 113,331,000/=

Kif. 1006 - Procurement Mgt. Unit ..... Sh. 101,660,000/=

Kif. 1007 - Library and Documentation Unit ... Sh. 86,976,000/=

Kif. 1008 - Mgt. Information System..... Sh. 158,284,000/=

Kif. 2001 - Macro Economy Cluster ..... Sh. 979,841,000/=

Kif. 2002 - Productive Sector Cluster .....Sh. 291,092,000/=

Kif. 2003 - Infrastructure & Services Cluster..... Sh. 258,800,000/=

Kif. 2004 - Social Service & Demog.Cluster.... Sh. 292,021,000/=

Kif. 2005 - Int. Trade & Econ. Relat. Cluster..Sh. 258,010,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

### **MIPANGO YA MAENDELEO**

### **Fungu 07 – Msajili wa Hazina**

Kif. 1001 - Admn. & Human Resources Mgt..... Sh 0

Kif. 1003 - Planning Unit ..... Sh. 229,500,000/=

Kif. 1004 - Legal Services Unit ..... Sh. 140,500,000/=

Kif. 1006 - Information and Comm. Tech... Sh. 1,985,000,000/=

Kif. 1007 - Information, Educ. & Comm. Unit...Sh. 75,000,000/=

Kif. 2001 - Public Investment Mgt. Div. ....Sh. 634,500,000/=

Kif. 3001 - Privatization and Monitoring .....Sh. 111,600,000/=

Kif. 4001 - Mgt. Service Division.....Sh. 52,440,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 21 – Hazina**

Kif. 1009 - *Public Procurement Policy Unit*...Sh. 1,525,525,000/=

Kif. 2001 - *Gvt. Budget Div.*.....Sh. 687,456,783,525/=

Kif. 2002 - *Policy Analysis Division* ..... Sh. 42,183,761,219/=

Kif. 4001 - *External Finance Div.*..... Sh. 3,148,443,656/=

Kif. 4002 - *Public Private Partnership Unit*... Sh. 5,000,000,000/=

Kif. 7001 - *Poverty Eradication & Empowmt*... Sh. 841,050,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 23 – Mhasibu Mkuu wa Serikali**

Kif. 3003 - *Financial Management* ..... Sh. 3,872,665,000/=

Kif. 3004 - *Financial Systems* ..... Sh. 513,600,000/=

Kif. 4001 - *Local Government Finances*.....Sh. 107,485,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama**

Kif. 1001 - *Admin. & HR Mgt* ..... Sh 200,000,000/=

Kif. 1003 - *Planning & Coordination Div.*.... Sh 46,561,734,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 42 – Mfuko wa Bunge**

Kif. 2001 - *Budget Department* ..... Sh. 0

Kif. 3011 - *Estate Mgt. Unit* ..... Sh. 7,000,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

Kif. 1001 - *Admin. & HR Mgt Division* ..... Sh. 6,051,600,000/=

Kif. 1010 - *Planning, Monitoring & Eval. Div.*..Sh. 6,233,827,368/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango**

Kif. 1001 - Admin. & HR Mgt..... Sh. 5,160,375,000/=

Kif. 1003 - Policy and Planning ..... Sh. 11,056,647,500/=

Kif. 1004 - Legal Services ..... Sh. 2,000,000,000/=

Kif. 1005 - Gvt. Comm.Unit ..... Sh. 322,500,000/=

Kif. 1007 - MCC Tanzania ..... Sh. 0

Kif. 3001 - Internal Auditor General ..... Sh. 2,734,191,000/=

Kif. 5001 - Gvt. Asset Mgt. Div..... Sh. 1,984,150,000/=

Kif. 6001 - Financial Mgt. Info. Sysys. Div..... Sh. 2,777,720,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 66 – Tume ya Mipango**

Kif. 2001 - Macro Economy Cluster ..... Sh. 700,000,000/=

Kif. 2002 - Productive Sector Cluster.....Sh. 913,752,000/=

Kif. 2004 - Social Serv.&Demo. Cluster .....Sh. 4,185,840,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja taarifa!

### **TAARIFA**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati ya Matumizi imepitia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango, Mfuko wa Bunge na Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2016/2017, kifungu kwa kifungu bila mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa  
Mwaka 2016/2017 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Nachukua fursa hii kutangaza kwamba makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango yamepitishwa na Bunge. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo nichukue fursa hii kuipongeza Wizara ya Fedha pamoja na Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wenu wote na niwatakie kila la kheri kwa niaba ya Wabunge hawa katika utekelezaji wa hii bajeti. Ni imani ya Bunge hili kwamba fedha mlizoomba na mmepeka mtaweza kutekeleza yale yote mliyotuahidi katika hii bajeti.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo niliahidi Mheshimiwa Keissy ningempa mwongozo mwishoni naomba uwe mwongozo mfupi kwa sababu muda wetu umekwenda.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba mwongozo wa vifungu Na. 64(7) isomeke pamoja na Kanuni ya 74, 75 na 76.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuongezea kwamba hii Serikali haitaki watumishi hewa, inaonesha Wabunge hapa tumekuwa kama watumishi hewa, tunakuja tuna-sign tunatoka. Je, Madaktari nao wakifanya namna hii, au Walimu wakifanya namna hii itakuwa ni haki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiba hela za Serikali. Kifungu cha 75 naomba nikisome hapa cha Kanuni kinasema:

“Mbunge aliyesimamishwa kazi, atatoka katika Bunge na hataingia tena katika Bunge sehemu yoyote ya Ukumbi wa Bunge na maeneo ya Bunge kwa muda wote atakapokuwa amesimamishwa na atalipwa nusu ya mshahara na nusu ya posho zinazoambatana na mshahara huo”.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hawa wanaoingia baada ya ku-sign wanaingia na kutoka, Serikali inawaona, Naibu Spika unawaona na Viongozi wanawaona, huu siyo utumishi hewa? *(Makofi)*



Mheshimiwa Naibu Spika, nataka mwongozo wako, kama siyo kuiibia Serikali. Je, sisi Wabunge wote tuje hapa tusaini na tutoke tukuache wewe na Makatibu wako itakuwa halali? Bunge litaendelea? Tuanze kesho kusaini na kutoka itawezekana?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka mwongozo wako. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Keissy amerejea Kanuni kadhaa hapo, lakini najua pia muda wetu umekimbia sana. Nitatoa huu mwongozo hapo baadaye, kwa hivyo Mheshimiwa Keissy vuta subira. Utapewa huo mwongozo kwa mujibu wa hiyo Kanuni ya 68(7) inayosema mwongozo unaweza kutolewa hapo hapo ama baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo ninayo matangazo machache. Tangazo la kwanza linahusu Wajumbe wa Kamati ya Uongozi kwamba kesho tarehe 2 Juni, saa saba mchana kutakuwa na kikao cha mashauriano baina ya Kamati ya Uongozi, Kamati ya Bajeti na Waziri wa Fedha na Mipango. Kikao hicho kitafanyika katika Ukumbi wa Spika, mnasisitizwa msikose Wajumbe wa Kamati ya Uongozi.

Tangazo lingine ni kwamba kesho kutakuwa na semina ya Wabunge wote mara baada ya kipindi cha maswali na semina hiyo itakuwa Ukumbi wa Pius Msekwa na itakuwa inatolewa na Taasisi ambayo inaitwa *Association of Certified Fraud Examiners*. Kwa hiyo, Wabunge mnasisitizwa kuhudhuria.

Waheshimiwa Wabunge, pia ninalo tangazo hapa kuhusu *Bunge Sports Club* kwamba wamepata uongozi mpya, nafasi ya Mwenyekiti imechukuliwa na Mheshimiwa William Mganga Ngeleja. Nafasi ya Makamu Mwenyekiti imechukuliwa na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko. Nafasi ya Meneja wa timu imechukuliwa na Mheshimiwa John Peter Kadutu na kuna nafasi tano za Wajumbe wengine ambao ni Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu na Mheshimiwa Cosato David Chumi. Kwa hiyo, hawa ndiyo viongozi wetu wa *Bunge Sports Club* na wanasisitiza Waheshimiwa Wabunge mjitahidi kwenda kwenye mazoezi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu.

*(Saa 2.30 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 2 Juni, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*